**22 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

____________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

____________

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 22 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa tunaendelea na Mkutano wa Tatu Kikao cha Kumi na Nne leo tarehe 22 Aprili, 2026.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MHE. DOTTO J. BAHEMU K.n.y. MWENYEKIYI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Fungu 58, Wizara ya Nishati, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ephraim kwa niaba ya Mwenyekiti.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, aulize swali lake.

Na. 159

**Kuanza Miradi ya *TACTIC* Halmashauri ya Mji wa Ifakara**

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA K.n.y. MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza Miradi ya *TACTIC* iliyopangwa kutekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Ifakara ni miongoni mwa halmashauri za miji 45 zinazotekeleza miradi ya *TACTIC* nchini. Halmashauri ya Mji wa Ifakara ipo kundi la tatu la

utekelezaji lenye jumla ya miji 18 ambayo imetengewa kiasi cha shilingi billioni 13.25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *TACTIC* umekamilisha usanifu wa miradi ya kundi hili la tatu ikiwemo Mji wa Ifakara wenye Barabara za *NBC* - Mangwale - Msikitini (km 1.29), Simba *Oil - Mark Guest* (mita 520), Uhuru *Roads* (km 1.08), Kilosa - Kalifornia (mita 70), Kituo cha Afya - *SACCOS* (mita 570), *Junction* - Katrini - Mlenge (mita 370), Vibaoni - Hospitali (mita 330), Stendi - Sokoni (mita 420).

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi zina urefu wa jumla ya km 4.65. Aidha, utekelezaji wa mradi huu utajumuisha mradi wa ujenzi wa stendi ya mabasi katika Kata ya Kibaoni na Soko Kuu katika Kata ya Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha usanifu wa miradi hii ya kundi la tatu, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea na taratibu za maandalizi ya kuanza utekelezaji wa miradi katika kundi hili ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Ifakara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wafanyabiashara hawa waliahidiwa soko hili kuanza tangu Julai, 2025 na mpaka sasa wanashindwa kufanya biashara zao kwa sababu hawajui hatima yao. Je, ni lini sasa Serikali inategemea kuanza mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tuna miradi kadhaa Mkoa wa Morogoro ambayo inatakiwa, iko chini ya *TACTIC*. Je, ni lini Serikali inajipanga kuanza kukamilisha kwa sababu mingi iliahidiwa tangu mwaka 2025?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inatekeleza miradi hii ya

*TACTIC;* tunayo makundi matatu. Kuna kundi la kwanza la miji 12, kundi la pili la miji 15 na kundi la tatu ambalo Ifakara imo ni miji 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeshaanza utekelezaji wa miradi hii katika makundi ya kwanza na ya pili na utekelezaji unaendelea. Ipo miradi iliyokamilika, ipo ambayo inaendelea na hatua mbalimbali. Baada ya kukamilisha usanifu wa miradi hii ya kundi la tatu, tutaanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Kilombero na Ifakara kwamba Serikali baada ya kukamilisha usanifu wake tutaanza mara moja utekelezaji wa mradi katika eneo la Ifakara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunafahamu kuwa iko miji kadhaa ambayo iko kundi la tatu, la kwanza na la pili ambayo inaendelea na utekelezaji wa miradi ya *TACTIC*. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ambavyo utekelezaji unaendelea, tutahakikisha inakamilika kwa wakati. Ile ambayo haijaanza, na ambayo iko *tier three* tutahakikisha nayo inaanza kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inatekelezwa kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Ally, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota, na Mheshimiwa Damas Ndumbaro ajiandae. Maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Mvomero kwenye Tarafa ya Turiani ambayo ni ya kimkakai ya kiuchumi haina miundombinu ya barabara wala masoko. Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuiweka miradi hii kwenye mpango wa miradi ya *TACTIC* ili kuongeza uchumi wa wananchi wa Turiani?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba Jimbo la Mvomero

Tarafa ya Turiani ni moja ya maeneo ambayo yanakua kwa kasi kwa kuwa na shughuli nyingi za kiuchumi na za kijamii na zinahitajika barabara, masoko, stendi na miundombinu mingine ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Sara Msafiri kwamba, kwa sasa mradi wa *TACTIC* unatekelezwa kwenye miradi ambayo ilishafanyiwa *design* kwenye miji 45. Kwa hiyo, tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya maeneo ambayo hayapo kwenye miradi ya *TACTIC,* ikiwemo Mvomero, kuhakikisha tunajenga barabara hizo kwa awamu, lakini pia kuhakikisha kwamba tunajenga miundombinu kama masoko ili wananchi wa Turiani na Mvomero kwa ujumla wapate huduma bora.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Nanyamba inatekeleza mradi wa *TACTIC* kwenye awamu ya tatu. Timu mbalimbali za TAMISEMI zikifika, kumekuwa na kubadilikabadilika kwa miradi itakayotekelezwa *phase one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna timu ilituambia tutaanza mradi wa kituo cha mabasi na barabara kilomita tano na kuna timu wanatuambia kuna barabara kilomita tano, stendi na soko. Je, Serikali itatamka rasmi sasa kwamba awamu ya kwanza Nanyamba tutafanya kitu gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wa Nanyamba, Mheshimiwa Chikota, kwamba Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ipo katika mradi wa *TACTIC* awamu ya tatu. Hivi sasa kazi ya usanifu iko hatua za mwisho kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule una *package* tofauti. Ninaomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya *session* hii ya maswali na majibu nitafuatilia nimpe hakika na awamu ya kwanza ni mradi ipi na awamu ya pili ni mradi ipi ili kusiwe na kubadilikabadilika kwa miradi ambayo itatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Songea Mjini ni mmoja kati ya maeneo ambayo miradi ya *TACTIC* inatekelezwa. Mradi wa ujenzi wa masoko ya Manzese A na B umechukua muda mrefu sana. Je, ni lini ujenzi huo utakamilika? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ndumbaro, Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini kwamba Serikali inafahamu kwamba utekelezaji wa mradi wa *TACTIC* katika Manispaa ya Songea unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya miradi haijakamilika kwa wakati. Tumeshachukua hatua kwa kukaa na mkandarasi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anaongeza kasi na kukamilisha ile miradi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tunafuatilia kwa karibu, na tutahakikisha kuwa miradi hiyo inakamilika ili iweze kuleta tija inayokusudiwa kwa wananchi wa Manispaa ya Songea.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Christina Solomon Mndeme, Mbunge wa Viti Maalum.

**22 APRILI, 2026**

Na. 160

**Uhitaji wa Mikopo kwa Wanawake - Tabora**

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME** aliuliza: -

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inawafikia Wanawake wote wenye uhitaji wa Mikopo katika Mkoa wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Majibu swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Solomon Mndeme, Mbunge wa viti maalumu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba wanawake wenye sifa katika Mkoa wa Tabora wanafikiwa na mikopo ya 10% kwa kuongeza fedha zinazotengwa kwa vikundi vya wanawake. Katika Mkoa wa Tabora, kiasi cha mikopo kwa wanawake kimeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.54 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 4.80 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii katika halmashauri za Mkoa wa Tabora Serikali inaendelea kuwasaidia wanawake kuunda na kusajili vikundi, kupata mafunzo ya ujasiriamali na kuandaa miradi yenye tija ili waweze kukidhi vigezo vya kupata mikopo. Kutokana na hatua hizo, vikundi vya wanawake vilivyosajiliwa na kupewa mikopo vimeongezeka kutoka vikundi 234 mwaka 2020/2021 hadi vikundi 532 mwaka 2024/2025, huku vikundi vilivyopatiwa mafunzo vikiongezeka kutoka 1,718 hadi 5,907 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaendelea kutumia mfumo wa WEZESHA *Portal* katika usajili na usimamizi wa mikopo.

Aidha, Serikali imezielekeza halmashauri zote kutangaza fursa hizo kwa uwazi kupitia mbao za matangazo, mikutano ya hadhara na vyombo vya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza uhamasishaji na kuwajengea uwezo wanawake wanufaike zaidi na mikopo hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa na mpango mzuri wa kuwawezesha wananchi kiuchumi na hususan wanawake wa Mkoa wa Tabora. Tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa mikopo hiyo imekuwa ikileta tija kwa wanawake wanaokopeshwa.

(a) Je, Serikali inapango gani wa kutoa elimu ya fedha na ujasiriamali kwa wanawake wanaopata mikopo kwa kuwafuata katika maeneo yao walipo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na mfumo mzuri wa ufuatiliaji wa matumizi ya mikopo hiyo ili kufahamu changamoto walizopitia na wanazopitia wanawake wakati wa kutumia mikopo hiyo ambayo inaweza kuathiri urejeshaji wa mikopo waliyochukua, na hasa wanawake wa Mkoa wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge Dkt. Christina Solomon Mndeme amesema, ni kweli kwamba mikopo hii imekuwa na tija kubwa sana kwa makundi maalumu, wakiwemo wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua kwamba wako wanawake ambao wako maeneo ya vijijini, na ambao

mara nyingine ni ngumu kufika katika Makao Makuu ya Halmashauri, tumeunda kamati za mikopo kuanzia ngazi za kata na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kuwafundisha Maafisa Watendaji wa Kata, na tunaendelea pia kuwafundisha Maafisa Watendaji wa Vijiji ili katika maeneo husika waweze kuwa msaada kwa kutoa elimu, hamasa na kuwezesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuandika maandiko sahihi ya kibiashara na waweze kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja hao, Maafisa Maendeleo ya Jamii wamekuwa mara kwa mara wakifanya huduma mkoba kwa kwenda kule maeneo ya vijijini na kukutana na vikundi hivi na kuendelea kuelimisha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huo unaendelea na Serikali itahakikisha inaendelea kufanya hivyo ili kuongeza uwezo wa vikundi kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, wakati tunafanya mafunzo hayo pia tunafanya tathmini ya ufanisi wa biashara ambazo vikundi hivyo vinaendesha kupitia mikopo ya 10% na kuona maeneo ambayo yana changamoto na kuwasaidia ili wawe na mafanikio na waweze kuwa na urejeshaji mzuri. Suala hili tutaendelea kulifanya ili kuhakikisha mikopo ya 10% inakuwa na ufanisi mkubwa zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninakushukuru. Kwa kuwa ni Sera ya Serikali ya Kuwainua Wanawake Kiuchumi kupitia mikopo ya 10%, je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha elimu juu ya mikopo yenye riba nafuu inayotolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa wanawake wa vijijini Mkoa wa Simiyu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasikia vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ni kuhusu mikopo ya wanawake Simiyu, majibu kwa ufupi.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kufikisha elimu ya mikopo yenye riba nafuu inayotolewa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa wanawake wa vijijini wa Mkoa wa Simiyu? Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii tunafanya kazi kwa pamoja katika maeneo ya makundi maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge Wizara ya Maendeleo ya Jamii inaendelea pia kuwafikia wanawake na makundi yale ambayo yanahitaji kupata mikopo hiyo kutoa elimu juu ya upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu. Kwa hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu tumelichukua hilo. Tutakaa kwa karibu zaidi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii ili kuendelea kuboresha mbinu za kuwafikia akina mama na kujua kwamba kuna fursa za mikopo hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Neema Majule.

**MHE. DKT. NEEMA W. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu ni hili hapa. Je, ni vipi na ni lini Serikali itafanya *impact assessment* kuona matokeo ya mikopo hii inayotolewa kwa wanawake inawa-*transform* kweli wanawake? Yaani inawabidisha kabisa wanawake; au tutakumbana na njia nyingine mbadala, labda badala ya kutoa hii mikopo kidogo kidogo kwa kila mwanamke labda tuje na kujenga viwanda ambavyo vitaweza kuajiri vijana wanawake na watu wenye ulemavu, ni lini itafanya *impact assessment* ili tuone matokeo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ni swali na ushauri hapo hapo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Neema ameongea jambo la muhimu sana la kufanya *impact assessment* kuona namna ambavyo mikopo hii imesaidia kuwakomboa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya tathmini, na tuna ushahidi wa maendeleo ya biashara hizi kwa baadhi ya vikundi. Viko vikundi ambavyo vilianza na mikopo ya milioni tano kwa mfano, lakini wakakuza biashara zao na kukopa shilingi milioni 50, shilingi milioni 60 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona kuna mwendelezo mzuri wa baadhi ya vikundi ku-*graduate* kutoka kukopa kidogo kidogo na kufanya biashara ndogo na baadaye wanaanzisha viwanda vya kuchakata bidhaa mbalimbali kama za kilimo na bidhaa nyingine. Kwa hiyo, tunaamini kwamba mikopo hii inaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kufanya *impact assessment* tumelichukua ili tujue, tufanye kwa ujumla wake tangu tumeanza mpaka sasa tuweze kuona mwelekeo wa tija katika mikopo hii na kuweka mipango mizuri zaidi ya kuboresha tunakoelekea mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Clayton Chipando Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na. 161

**Kuongeza Mtandao wa Barabara za Lami – Kigoma Mjini**

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mtandao wa Barabara za lami Kigoma Mjini kwa kuongeza bajeti?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji hadi mwaka wa fedha 2020/2021 ilikuwa inapokea Bajeti ya Matengenezo ya barabara na madaraja jumla ya shilingi bilioni 1.6 kwa mwaka. Kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 mpaka 2025/2026, bajeti iliongezeka hadi kufikia shilingi bilioni 3.2 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa *TACTIC* Awamu ya Kwanza inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Barabara za kilometa 9.4, Mitaro Mikubwa ya Maji ya Mvua kilometa 5.4, Soko kuu la Mwanga pamoja na Soko la Samaki la Katonga katika Manispaa ya Kigoma Ujiji. Utekelezaji wa mradi huu utaongeza mtandao wa Barabara za lami Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuujengea uwezo wa kibajeti wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini ili uweze kutekeleza Ujenzi wa Barabara za tabaka la lami kwa awamu kote nchini ikiwemo katika Manispaa ya Kigoma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Moja litakuwa swali, na lingine litakuwa ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Bwawa la Katubuka linazidi kuwaletea madhara makubwa sana wananchi wa Kata ya Katubuka na tayari kulikuwa na mkandarasi pale

anaendelea na kazi ya kutoa maji yale kwa kutengeneza mtaro mkubwa ambao ulikuwa unayapeleka maji Ziwa Tanganyika. Sasa hivi ameondoa vifaa katika eneo la *site*. Serikali ina mpango gani wa kumlipa yule mkandarasi ili aweze kumaliza kazi ya kuyaondoa yale maji na kuwaacha wananchi katika makazi yao wakiwa na amani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, nilikuwa ninaiomba Serikali, sisi Wabunge pamoja na kufanya maendeleo, lakini tunafanya siasa pia. Tulikuwa tunaomba, pale ambapo wanaleta fedha ya ujenzi wa barabara, basi wataalamu wetu waambiwe waje washauriane na sisi, ni barabara gani ambazo zikienda kujengwa zitatusaidia, na pia ndiyo kilio cha wananchi wetu katika Majimbo yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ukiwa uko huku Bungeni unaambiwa tu greda liko mtaani linafanya kazi, unaweza kukuta hiyo barabara inayojengwa ni barabara ambayo kwenye ahadi zako kwa wananchi wako haina umuhimu kama kuna barabara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa ruhusa yako naomba nimtajie barabara tano ambazo hata nikifa leo ninaomba zijengwe katika Jimbo la Kigoma Mjini. Barabara ya kutokea Uwanja la *Lake Tanganyika* kupita Bezebazeba Sokoni – Rusimbi, Kata ya Majengo pamoja na Kata ya Machinjioni. Barabara ya kutokea Kata ya Mwanga Kaskazini inaitwa Barabara ya Serengeti inayounganisha Kata ya Mwanga Kaskazini na Kata ya Gungu; Barabara ambayo inaunganisha Kata ya Buhanda na Kata ya Businde; Barabara ambayo inaanzia Shini – Vamia – Bega; Barabara ambayo inaanzia Madukani…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton ahsante. Ameshakuelewa kwa sababu hilo ni ombi, siyo swali. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshakuelewa, tunashukuru…

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri abaki na hizi barabara kichwani hata nikifa leo hayo ndiyo maombi ya wananchi wa Kigoma Mjini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, niaomba kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando, Mbunge wa Kigoma Mjini kwamba Bwawa la Katubuka ambalo limekuwa likisababisha mafuriko ya mara kwa mara kwa wananchi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji, Serikali inatambua kwamba kuna changamoto hiyo na ndiyo maana ilishapeleka mkandarasi pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshafanya *addendum* kwenye mkataba kuhakikisha kwamba mkandarasi analiingiza suala la ujenzi wa mfereji mkubwa wa kutoa maji kwenye maeneo hayo yanayosababishwa na mafuriko ya Bwawa la Katubuka kupeleka Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tuko hatua za mwisho za kufanya malipo kwa mkandarasi ili arejee, aendelee na ujenzi na hatimaye kuondoa kero hiyo ya mafuriko ya mara kwa mara kwa wananchi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kweli kwamba kuna fedha za ujenzi wa barabara ambazo zimeendelea kupelekwa kwenye Majimbo yote kote nchini likiwemo Jimbo la Kigoma Mjini. Hivi karibuni Jimbo la Kigoma Mjini limepelekewa jumla ya shilingi milioni 898 kwa ajili ya kujenga lami ya *Baptists* mita 800, lakini shilingi milioni 450 kwa ajili ya kujenga Barabara ya Zuru kiwango cha zege mita 420 na bajeti ya Kigoma Mjini imeongezeka kwa mwaka 2025/2026 kutoka bilioni 3.2 za mwaka uliopita mpaka shilingi bilioni 5.33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inathamini uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika Mji wa Kigoma, lakini nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwamba ni maelekezo ya Serikali kwamba fedha zozote

zinapoingia katika Majimbo yetu, lazima Waheshimiwa Wabunge wapewe taarifa rasmi ya mapokezi ya fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya utekelezaji iwe barabara au miundombinu mingine yoyote, lazima Waheshimiwa Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi katika Majimbo hayo washirikishwe ili tuwe na uelewa wa pamoja na maamuzi ya pamoja ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limetolewa maelekezo mara kadhaa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba tutafuatilia kwa karibu na tutachukua hatua kwa Wakurugenzi na Watendaji ambao hawatatekeleza maelekezo haya ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, swali la nyongeza.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Malinyi lina mtandao wa mita chache za lami. Je, ni lini sasa Serikali ina mpango wa kuongeza kupitia programu ya kuboresha Halmashauri za Wilaya au Makao Makuu ya Wilaya kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Mbunge wa Malinyi, Mheshimiwa Mecktridis amelifuatilia suala la Barabara za Malinyi mara kwa mara. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tunaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kujenga barabara kwa kiwango cha changarawe na pale inapowezekana kuendelea kujenga barabara kiwango cha lami na tutahakikisha kadri fedha zinapopatikana tunatoa kipaumbele cha juu kabisa kwa ajili ya Mji wa Malinyi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo aulize swali lake.

Na.162

**Taasisi ya *ZEMA* Kuwa Wakala wa *NEMC***

**MHE. MATTAR ALI SALUM** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kufanya *ZEMA* kuwa Wakala wa *NEMC* ili kuratibu na kusimamia kwa ufanisi Miradi inayotekelezwa upande wa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge kutoka Shaurimoyo Zanzibar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Sura 191 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Zanzibar ya mwaka 2015 zimeanzisha taasisi mbili za usimamizi wa masuala ya uhifadhi wa mazingira nchini. Taasisi hizo ni Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* kwa upande wa Tanzania Bara na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar *(ZEMA)* kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi hizi zimekuwa zikishirikiana kwa ufanisi katika kusimamia mazingira hususan katika masuala yafuatayo: kwanza, zimekuwa zikishirikiana kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo; pili, zimekuwa zikitafuta fedha za uhifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo; pamoja na kubadilishana utaalamu na uzoefu kuhusu masuala ya usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuimarisha ushirikiano pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa, taasisi hizi mbili zipo katika taratibu za kuanzisha makubaliano rasmi ya ushirikiano ambayo yanalenga kuimarisha usimamizi wa mazingira katika pande zote mbili za Muungano na nchi zetu kwa ujumla. Hivyo, kutokana na ushirikiano huo, Serikali za pande zote mbili hazioni haja ya kuifanya *ZEMA* kuwa Wakala wa *NEMC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar Ali Salum.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali kwa Mheshimiwa Waziri. Ninaomba kufahamu *commitment* ya Serikali, lini makubaliano haya yatakuwa yamekamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili pia, ninaomba *commitment* ya Serikali kwamba hii *NEMC* lini itakuwa Mamlaka kamili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijayajibu maswali ya Mheshimiwa Mattar nimshukuru sana na kumpongeza kwani amekuwa ni sehemu ya Wabunge kutoka Zanzibar, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ambavyo Wabunge wote wanaowakilisha Zanzibar kwenye Bunge hili, wamekuwa ni watu watetezi wazuri wa upande wa pili wa Muungano. Ametaka kujua ni lini makubaliano kati ya *ZEMA* na *NEMC* yatatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Serikali zote mbili na Mamlaka hizi mbili zimeshaandaa *MOU (Memorandum of Understanding)* ya namna gani wataweza kutekeleza majukumu kwa pamoja katika uhifadhi wa mazingira ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maana ya kushirikiana *ZEMA* kutoka Zanzibar na *NEMC* kutoka huku kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makubaliano haya yameshakamilika. Hivi sasa pande zote mbili zinayapitia ili kama kuna jambo la kuongeza ama la kupunguza waweze kukubaliana na baada ya hapo tutakwenda kwenye kusaini makubaliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza ametaka kujua, ni lini *NEMC* itakuwa mamlaka kamili? Mheshimiwa Waziri wetu wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa *Eng*. Masauni jana amesimama hapa, amesoma bajeti yetu ya Wizara na katika mambo ambayo yamesomwa kwenye bajeti ile ni jambo hili la *NEMC* kuwa Mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Hotuba ile tumeahidi hapa Bunge lijalo ambalo ni Bunge la Miswada ya Serikali, italetwa hapa Muswada ili Bunge hili liridhie *NEMC* kuwa Mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Wabunge. Tunaendelea sasa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo Mbunge wa Missenyi aulize swali lake.

Na. 163

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA* - Missenyi**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Chuo cha *VETA* Wilaya ya Missenyi utakamilika ikizingatiwa kuwa ujenzi huo umechukua muda mrefu sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali namba 163 la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Jimbo la Missenyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Missenyi ni sehemu ya mpango wa Serikali wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* 65 katika Wilaya 64 na Mkoa mmoja wa Songwe. Utekelezaji wa mpango huu unafanyika katika Wilaya na Mkoa ambao bado hauna Vyuo hivi. Lengo ni kuhakikisha fursa za mafunzo ya ufundi stadi zinasogezwa karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Missenyi ambacho kinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026. Hadi sasa, Serikali imeshatumia jumla ya shilingi bilioni 1.0 kati ya shilingi bilioni 1.6 zilizotengwa kwa ajili ya kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi huu. Ujenzi umefikia 65% ya utekelezaji wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo, zima mic hiyo hapo mbele mara moja. Tayari.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Missenyi nishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuifanya Missenyi ikawa miongoni mwa Wilaya 64 ambazo zinapata Miradi ya Chuo cha *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niupongeze Uongozi wa Wizara ya Elimu chini ya Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda na pia Naibu Waziri. Chuo hiki cha *VETA* kwa muda mrefu kilidorora katika ujenzi, lakini nikupongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, baada ya kwenda ofisini kwake na kueleza, aliwapigia simu wasaidizi wake; na nimhakikishie, hata vifaa wiki iliyopita *semi-trailer* imeshusha vifaa, ujenzi unaendelea kama alivyosema. Kwa hiyo, Wanamissenyi wana matarajio kwamba hii 65% na 60% ambayo unaisema, Chuo kitakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tunaona kwamba Chuo kinaenda kukamilika mwezi wa Saba, je, hatuwezi kuanza kufanya usaili wa wanafunzi ili chuo hicho kikikamilika wanafunzi waanze moja kwa moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kukamilika ujenzi bado tunahitaji vifaa na walimu, je, Serikali inatoa *commitment* gani kuhakikisha kwamba Chuo hicho kitaanza kutumika lini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimjibu maswali ya nyongeza Mheshimiwa Florent Kyombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyojibu katika swali langu la msingi kwamba chuo hiki kinatarajiwa kukamilika ifikapo Septemba, 2026 kwa awamu ya kwanza kwa kukamilisha majengo ya Utawala, Vyoo, Karakana, Mifumo ya Umeme na Maji, baada tu ya kukamilika Chuo hiki, basi kitaanza kutoa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kwamba kwa kawaida mafunzo ya *VETA* huanza kila mwezi Januari wa kila mwaka. Kwa hiyo, kwa kuwa Chuo kinamalizika Septemba, 2026 tunategemea kwamba mpaka Januari, 2027 Chuo kitaanza kutoa mafunzo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado Shaibu. Wengine wazime kidogo jamani tuweze kuendelea. Mheshimiwa Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Tunduru ni moja kati ya Wilaya ambazo hazina Vyuo vya *VETA*, na kwa kuwa ujenzi wa awamu ya kwanza wa Chuo cha *VETA*, Tunduru unaohusisha majengo tisa mpaka sasa bado unasuasua, kwani ulipaswa kukamilika mwaka 2024 lakini

mpaka sasa haujakamilika, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kukamilishwa kwa Chuo cha *VETA* Tunduru?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu kwenye swali la msingi, tunatarajia vyuo hivi kukamilika Septemba, 2026. Hata hivyo, ahadi ya Serikali ni kwamba baada ya Bunge hili nitafanya ziara mahususi ya kupitia Vyuo hivi na kuona maendeleo ya vyuo hivi ili tuone wapi tunakwamua, pale vyuo hivi vilipokwama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, Mbunge wa Viti Maalum.

Na.164

**Kuboresha Programu za Uanagenzi**

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuboresha Programu za Uanagenzi, Ufundi Stadi na Ubunifu ili kuwawezesha Vijana kujiajiri na kuondoa changamoto ya ajira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* imeendelea kueneza Mpango wa Mafunzo kwa Mfumo wa Uanagenzi Pacha *(Dual Apprenticeship Training System)* ambapo mafunzo yanatolewa kwa kushirikiana na viwanda. Mfumo huu unaendeshwa kwa utaratibu Ungwe

*(Block Release)* ambapo wanafunzi hujifunza kwa kubadilishana muda wa kuwa chuoni kisha viwandani na sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu unawawezesha wanafunzi kupata umahiri kwa haraka na fursa za ajira pindi wanapohitimu. Kwa sasa mfumo wa *DATS* unatumika kwa fani za kilimo, ukarimu, utalii, ufundi magari, ufundi umeme na programu za madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mikakati ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushirikiano na viwanda na waajiri; kujenga uelewa kwa wadau wa viwanda *(Industrial Mentors)* na kueneza mfumo wa *DATS* kwa kuongeza fani za mafunzo na Vyuo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Regina Christoper Malima.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza juhudi za Serikali katika kuboresha masuala ya vyuo na vyuo vikuu, na ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, hivyo sina swali la nyongeza, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, swali la Mheshimiwa Jesca John Magufuli, Mbunge wa Viti Maalum litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Dickson Lutevele Villa.

Na. 165

**Hitaji la Ujuzi Sahihi wa Akili Mnemba kwa Vijana**

**MHE. DICKSON N. KUTEVELE K.n.y. MHE. JESCA J. MAGUFULI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijana wanapata ujuzi sahihi na kunufaika kupitia Akili Mnemba *(AI)*?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca John Magufuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi na taasisi za Kimataifa kuhakikisha vijana wanajengewa ujuzi sahihi wa matumizi ya akili mnemba. Vilevile, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa matumizi salama ya Teknolojia ya akili mnemba unaolenga kukuza ujuzi kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi vyuo vikuu ili kujenga hazina ya wataalamu mahiri nchini. Aidha, Serikali kupitia Tume ya TEHAMA imepitia mitaala 110 ya vyuo vikuu 32 vyenye Mlengo wa TEHAMA ili kuhakikisha vyuo hivyo vinajumuisha Moduli za Akili Mnemba, hatua inayolenga kuendana na mahitaji ya soko la ajira pamoja na kuzalisha vijana wenye ujuzi wa teknolojia ya kisasa ikiwemo akili mnemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Akili Mnemba utahusisha uanzishwaji wa vituo vya ubunifu nchini katika Mikoa ya Lindi, Dodoma, Tanga, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, na Zanzibar. Sambamba na vyuo hivyo, Serikali inakamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijiti katika eneo la Nala – Jijini Dodoma, ambayo itajikita katika utoaji wa mafunzo kwa teknolojia zinazoibukia ikiwemo akili mnemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi yatakayochochea ubunifu, kuimarisha ushindani wa Kimataifa na kuhakikisha manufaa ya teknolojia ya akili mnemba na teknolojia nyingine zinawafikia wananchi wote kwa maendeleo jumuishi na endelevu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dickson Lutevele.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaomba

nimwulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa teknolojia hii ya *AI* ndiyo inayoongoza dunia kwa sasa, na mara nyingi fursa kama hizi zinawapata tu vijana wa mjini, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuhakikisha kwamba teknolojia hii mnazunguka hasa vijijini ikiwemo maeneo ya mikoani kama Mafinga kwa ajili ya kuwafundisha vijana wote ili waweze kupata fursa hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwafikia vijana katika maeneo ya mikoa mbalimbali, ndiyo sababu nimeeleza kwamba tumeanza utaratibu wa kujenga vitu vya ubunifu nchini. Tumeanzia na mikoa ambayo nimeitaja, Mikoa ya Lindi, Dodoma, Tanga, Dar es Salaam, Tanga, Arusha, Mwanza, Mbeya, na Zanzibar, na tutaendelea hatua kwa hatua kuwekeza katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali wa Kimataifa. Kwa mfano, tunashirikiana na *International Telecommunication Union (ITU),* wanafanya mradi na Tume ya TEHAMA. Huu mradi unaitwa *ITU IA For Good Sandbox*. Mradi huu unatekelezwa kwa vijana wote nchini bila kujali ni wa mjini au wa vijijini, kwa lengo la kuwapa uwezo wa kutengeneza mifumo ya *AI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inalitambua hilo, na pia inashirikiana na *UNESCO* kuwekeza katika maeneo haya. Hili litahusisha watumishi wote wa Serikali walio mjini na maeneo yote ya nchini, vijijini na kila sehemu kwa kuwajengea uwezo wa eneo hili la akili mnemba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula Magangila.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Sekta ya Elimu tumekuwa tukihangaika na walimu wengi kwa baadhi ya masomo kama Sayansi na Biashara, je, ni lini Serikali sasa itatumia teknolojia hii kutengeneza walimu ambao wataenda kufundisha masomo ambayo yana upungufu wa walimu watokanao na akili mnemba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimeeleza kwamba, Serikali kupitia Tume ya TEHAMA imepitia mitaala 111 ya vyuo vikuu 32 vyenye mlengo wa TEHAMA. Hivi vyuo vingine vinawafundisha walimu, kwa hiyo, hii mitaala ambayo tumeipitia itahakikisha kwamba tunatoa wataalamu wanaotumia akili mnemba wakiwemo walimu, ili waende kufundisha katika shule wanazozitumikia.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima, Mbunge wa Ikungi Mashariki.

Na. 166

**Mawasiliano ya Kimtandao katika Kila Kijiji Nchini**

**MHE. THOMAS M. KITIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itahakikisha kila kijiji nchini kinapata mawasiliano ya kimtandao na kuwepo kwa minara ili kurahisisha mawasiliano hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Mngoto Kitima, Mbunge wa Jimbo la ikungi Mashariki kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa huduma za mawasiliano ya uhakika katika kila kijiji nchini kama msingi wa kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hasa katika zama hizi za uchumi wa kidijiti. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na Sekta Binafsi, imeendelea kupanua miundombinu ya mawasiliano ikiwemo ujenzi wa minara ya simu,

hususan katika maeneo ya vijijini ambayo bado kuna changamoto ya mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa Mpango Mkakati Mahsusi wa Ujenzi wa Minara kwa Kipindi cha Miaka Mitano (2025 – 2030). Mpango huu unalenga kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 vijiji vyote nchini vinapata huduma za mawasiliano mbadala ili kuwezesha wananchi kupata huduma ya mawasiliano na kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mpango huu, mwezi Disemba, 2025 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, ilikamilisha Mradi wa Awamu ya Nane ya Ujenzi wa Minara 758 nchini. Utekelezaji wa awamu ya tisa ya ujenzi wa minara 636 unaendelea na utakamilika mwezi Disemba, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, *UCSAF* inaendelea na awamu ya 10 ya ujenzi wa minara 287 ambayo mikataba yake ilisainiwa Disemba, 2025. Hatua hii inalenga kuongeza upatikanaji wa huduma za Mawasiliano katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na kuboresha huduma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Kitima.

**MHE. THOMAS M. KITIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. kwa kuwa karibia kata nyingi hazina mawasiliano, Mfano vijiji katika Kata ya Mang'onyi, Ntuntu, Misuhaa, Kikio ambapo kuna maeneo kama Mnane, Kundi, pamoja na Makumi, ambao hawana kabisa mawasiliano; na hata mimi nikienda kwenye ziara huwa nikifika huko ni kama nipo gizani, au nimepotea na siwezi kupatikana; je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuwapatia hawa watu mawasiliano kwa kuwajengea minara, hasa hasa katika maeneo yenye huduma za kijamii kama shule ili yawepo mawasiliano na iweze kufanya miradi ya Kitaifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kijiji ninachotoka kinaitwa Siuyi na nikiwa kijijini huwa ninalazimika kwenda kijiji cha jirani ambacho kinaitwa Makiungu, ili tu nipate mawasiliano. Mara

nyingine huwa ninalazimika kutokufika kijijini, nilale mjini ili mradi tu nisikose taarifa za Kitaifa. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais ana jambo la Kitaifa, kwa hiyo, ninalazimika kukaa mjini ili tu niweze kupata mawasiliano, kwa kuwa kijiji ninachotoka hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaona umuhimu hiki Kijiji cha Siuyi kipate mawasiliano ya kutosha? Kwa kuwa mimi Mbunge wao ninatoka pale, wakiona hata Mbunge hana mawasiliano, itakuwa siyo jambo zuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara tumepokea changamoto ya Mheshimiwa Mbunge. Ninaomba nimwelekeze Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* aende jimboni kwa Mheshimiwa kufanya tathmini ya kina kuhusu tatizo hili la mawasiliano na kuchukua hatua za dharura kulifanyia utatuzi kwa kadri itakavyowezekana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa aulize swali lake.

Na.167

**Ujenzi wa Vihenge vya Kisasa (Maghala)**
**Eneo la *TAZARA* Isangu Mbozi**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa vihenge vya Kisasa (maghala) vya kutunzia mazao vilivyopo eneo la *TAZARA* Isangi Mbozi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Vihenge vya Kisasa (maghala) vya kutunzia mazao vilivyopo eneo la *TAZARA* Isangi Mbozi ni mojawapo ya miradi ya ujenzi wa vihenge na maghala ya kisasa unaotekelezwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa vihenge hivyo ulikuwa ukitekelezwa na Kampuni ya *Feerum S. A.* ambayo ilishindwa kukamilisha kazi hiyo kwa wakati na hatimaye Serikali ilisitisha mkataba wake ukiwa umefikia 74% ya utekelezaji mnamo Oktoba, 2024. Baada ya hatua hiyo, mkandarasi mpya *Unia Araj* amepatikana na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo ifikapo Juni, 2027.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na yenye matumaini. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa sasa mkataba mpya wa Kampuni hii ya *Unia Araj* umeshasainiwa, je, una thamani ya shilingi ngapi ili mradi huo uweze kukamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa ujenzi huu umechukua muda mrefu sana na ulikuwa unatekelezwa kama ulivyosema na Kampuni ya *Feerum*, ambayo toka mwaka wa 2021 ilitangaza kwamba imefilisika na ikaacha kutekeleza miradi yote mitano katika maeneo ya mikoa mbalimbali, na sababu zilizotolewa ilikuwa ni kwamba anadai fedha zilizobaki hazitoshi kukamilisha mradi huo, sasa swali langu, je, Serikali imeshapata fedha za ziada kutoka wapi ili ziweze kutumika kukamilisha mradi huo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi kwa maswali ya msingi, na kiukweli amekuwa akipigania jambo hili Mbunge wa Vwawa Mheshimiwa Hasunga kuhakikisha kwamba Mradi huu wa Vihenge unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ambalo ninataka nimhakikishie, moja, thamani ya mradi ambao sasa kwa sababu ni vihenge vyote ambavyo vilikuwa chini ya *Feerum,* tumesaini mkataba mpya wa dola milioni 38, ambao sasa utakamilisha vikiwemo hivi vya Mbozi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha, tunayo, kwa sababu *NFRA* wamekuwa wakifanya biashara ya mahindi na wewe unafahamu, na ndiyo maana wamenithibitishia. Nimeongea na Mkurugenzi mimi mwenyewe akaniambia vitakamilika kama ambavyo tumesaini katika huu mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sasa hivi fedha ipo na mradi ule utakamilika kama ambavyo sisi Serikali tumepanga. Kwa hiyo, niwathibitishie tu wananchi wa Vwawa na Mkoa wa Songwe kwamba, Vihenge vile vitakamilika kwa wakati na watafanya biashara yao kwa uhakika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Johannes, ajiandae Mheshimiwa Esther Matiko, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. DKT. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Jimbo la Arumeru Magharibi lina wakulima wazuri sana wa mbogamboga, lakini hili jimbo lina miundombinu ambayo hairidhishi hasa ya umwagiliaji, hususan uboreshaji wa mifereji ya asili. Je, ni lini Serikali itajenga Skimu Majimoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali ni moja tu. Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo moja la Mheshimiwa Dkt. Johannes.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mbunge wa Arumeru Magharibi kwamba, mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunajenga miradi ya umwagiliaji maeneo yote nchini ili kuhakikisha kwamba tunaongeza tija kwa mkulima, na mkulima analima katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika eneo lako la Arumeru, na moja ya maelekezo ambayo tulipewa sasa hivi ni kuhakikisha moja, tunakwenda kwenye ile tunasema miradi ya

asili. Kuna ile umwagiliaji ama *Schemes* za asili, tuhakikishe tunaziboresha kwa gharama nafuu ili zianze kuleta matokeo makubwa haraka, wakati huo huo tukiendelea na hii miradi mikubwa ambayo inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wanaarumeru Magharibi wako sehemu ya mpango wa Serikali kutekeleza hilo. Kwa hiyo, ninamthibitishia tu kwamba tuko kwenye kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Kimataifa la Mazao la Lemagwe ni muhimu sana kwa uchumi wa Tarime, Mara, na Taifa, na ujenzi ule wa Soko la Kimataifa unaenda sambamba na ujenzi wa ghala. Ninataka kujua, ni lini sasa unaenda kukamilika baada ya kuwa umesimama kwa muda na mmesainisha mwaka 2025 mkataba? Lini wananchi wa Tarime wanategemea Soko la Kimataifa linaenda kukamilika sambamba na ghala? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwathibitishie tu wananchi wa Tarime kwamba, Soko la Lemagwe tulishasaini mkataba, ambacho kilikuwa kimechelewa ilikuwa ni fedha na tayari tulishaomba fedha Wizara ya Fedha na wametuthibitishia kutupatia kwa ajili ya kumkabidhi mkandarasi na kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunatarajia kwamba mradi ule utakamilika kwa wakati, na kama utachelewa, basi kutakuwa na *extension* ya muda usiozidi miezi sita kabla ya ule mradi kukamilika.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, aulize swali lake.

Na. 168

**Mradi wa Maji Mji wa Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya shilingi bilioni 4.5 kwa wananchi wa Mji wa Karatu ili waweze kupata huduma ya uhakika ya majisafi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Awack, Mbunge wa Jimbo la Karatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji inayolenga kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa Karatu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025 hadi sasa, jumla ya shilingi bilioni 1.742 zimetolewa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu *(KARUWASA)* ikiwa ni sehemu ya ahadi ya Serikali ya kuboresha huduma ya maji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zimewezesha kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maji Ayalabe, Bwawani Namba tatu sambamba na uchimbaji wa visima vitatu vya Endoro, Maliasili pamoja na Tom III ambapo kwa pamoja vina uwezo wa kuzalisha maji lita 200,000 kwa saa. Vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji Karatu Mjini wenye thamani ya shilingi 864,822,827.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi ya maji

katika Jimbo la Karatu kadiri fedha zinavyopatikana ili kuhakikisha miradi inayoendelea inakamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Tlemai.

Waheshimiwa Wabunge, zimeni visemeo vyenu ili tuweze kuwasiliana.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo ya nyongeza. Kwa kuwa upatikanaji wa maji katika Mji wa Karatu ni 52%, na tunaishukuru Serikali imechimba visima vinne katika Mji wa Karatu na visima hivyo vinne ili vikamilike vinahitaji shilingi bilioni 2.7. Lini Serikali itatoa shilingi bilioni 2.7 ili wananchi wa Mji wa Karatu waweze kupata maji katika Mji wa Karatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza, kwa kuwa kuna Mto Endoro katikati ya Mji wa Karatu ambao unatiririsha maji kutoka Mlima Ngorongoro. Je, ni lini Serikali itaweka mpango wa kujenga bwawa ili kuongeza uhitaji wa maji katika Mji wa Karatu na ule mto ukawa sehemu ya chanzo cha kuongeza maji katika Mji wa Karatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake muhimu ya nyongeza yanayogusa mahitaji ya moja kwa moja ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la kwanza, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.7 katika bajeti ya 2026/2027 ili kuhakikisha tunaenda kujenga miundombinu inayotokana na visima vile vitatu ambavyo vimeshachimbwa tayari na vina uwezo wa kutoa lita 200,000 kwa saa. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tayari Serikali imeshaanza kuchukua hatua katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, katika Mji wa Karatu tunalo bwawa ambalo linatoa huduma ya majisafi kwa wananchi wa Karatu Mjini pale, lakini pia kulingana na jiografia ya Karatu, kuna kipindi cha masika maji huwa yanaporomoka kutoka kwenye Milima ya Ngorongoro kule na Hifadhi ya Ngorongoro na hatimaye kuchafua miundombinu na kuharibu bwawa lile ambalo linatoa huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 600 kwenda kujenga mitaro ambayo itazuia maji yanayoshuka ili yasiende kwenye bwawa linalotumika kwa matumizi ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunao mpango mkakati wa miaka mitano ambapo tutaenda kujenga bwawa katika mto. Kuna mto unaitwa Mto Endoro ambapo tutakapojenga lile bwawa, litasaidia kuyachukua yale maji (kuyateka) ili kuzuia mafuriko; pia, tutayatumia kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa Mji wa Karatu kwa sababu ni maji mazuri kabisa, lakini pia kwa jiografia yake itatusaidia kuyatumia bila ya kuwa na gharama ya kuweka *pump* kwa sababu yatakuwa yanashuka kwa *gravity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, jiandae Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Amina Mkumba, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mcharo kwenye Kijiji cha Kisangwa, Bunge lililopita tulienda kuzindua mradi wa maji. Hivi ninavyozungumza, mradi umesimama kwa sababu bado hamjapeleka fedha zaidi ya shilingi milioni 700, na ule mradi ukikamilika, maji yale yataenda mpaka kwenye Chuo cha Kisangwa, ambapo wanafunzi wanapata adha sana ya shida ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itapeleka fedha ili mradi huo ukamilike, wanachuo wanufaike na maji, na wananchi wangu wa Jimbo la Bunda Mjini kwenye Kata ya Mcharo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza, swali muhimu sana kwa wananchi wa Bunda Mjini, kwa sababu sauti yao imesikika na Serikali inatambua kwamba ni kweli kumekuwepo na changamoto ya ucheleweshwaji wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali baada ya kufanya uhakiki wa madai ya hati ambazo zimewasilishwa, sasa tumeanza kulipa awamu kwa awamu ili kuhakikisha kwamba madeni ambayo wakandarasi wanadai, basi yaweze kuanza kulipwa na kumalizika na wao waweze kumalizia miradi yote nchini, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

Waheshimiwa, zimeni visemeo vyenu jamani Mheshimiwa Rweikiza aweze kupata kuongea.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri, nina Mradi wa Maji wa Kemondo Maruku, leo ni mwaka wa sita tangu umeanza kujengwa, lakini hatujapata maji na kuna shida kubwa sana ya maji Vijiji vya Maruku na Kanyangereko, hasa baadhi ya Vijiji vya Kemondo havina maji mwaka wa sita. Ni nini mpango wa Serikali kuhusu mradi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tunayo changamoto ya maji katika eneo la Kemondo, ambapo mradi huu mkubwa ulikuwa ni ahadi ya viongozi wa Kitaifa, lakini pamoja na ahadi hiyo, mradi huo tayari ulikuwa umeshaanza na fedha tayari zimeshapelekwa na utekelezaji ukaanza. Tunatambua kwamba mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtoa hofu Mheshimiwa Wakili Msomi Rweikiza kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunakamilisha miradi yote, na huu Mradi wa Maruku tutaupatia kipaumbele kuhakikisha kwamba katika mwaka huu wa fedha unaenda kukamilika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mkumba.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kuna Mradi wa maji Mchungu katika Jimbo la Kibiti, Kata ya Mwambao na Mradi huu unatoa maji yenye chumvi nyingi sana, Serikali ina mpango gani wa kufunga mtambo *desalination plant* ili watu waweze kupata majisafi na salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia na kubaini changamoto ambayo wananchi wanapitia katika kutumia maji ambayo yana chumvi. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba kwa mujibu wa Sera yetu ya Maji ya Mwaka 2002 Toleo la Mwaka 2025, tunatakiwa kuhakikisha watu wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, ninatumia fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Maji, kuelekeza wataalamu wetu waende wakafanye tathmini, kwanza, kama inawezekana kuyatibu yale maji na ili yanyweke bila ya kuwa na changamoto ya chumvi, ama kama maji hayo chumvi yake ina *concentration* kubwa ambapo haiwezekani, basi tutafute chanzo kingine tukachimbe kisima ili kuhakikisha kwamba tunawafikishia wananchi huduma ya maji yaliyo safi na salama, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba.

**MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la

nyongeza katika eneo hili la maji. Kwanza niishukuru Serikali, inafanya kazi kubwa katika sekta hii hasa katika Jimbo la Peramiho, lakini tuna vijiji sita mpaka sasa hakuna huduma ya maji. Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hii ya maji katika vijiji hivi sita ambavyo vimebaki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba tunavyo vijiji takribani 1,575 ambavyo havijapata miundombinu rasmi ya utoaji wa huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, tunao mpango mkakati ndani ya kipindi cha miaka mitano tutahakikisha kwamba na Serikali imejipanga, awamu kwa awamu tutaenda kuhakikisha kwamba vijiji vyote 1,575 vinapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia bajeti hii katika vijiji hivyo sita, baadhi ya vijiji, ninaomba tukitoka hapa Mheshimiwa Mbunge tukutane ili angalau baadhi ya vijiji tuviingize kwenye bajeti tuanze hatua moja wapo ya kutatua changamoto ya maji katika vijiji hivyo sita vya Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze sana kwa kuchaguliwa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali fupi la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Dayosisi ya Kusini Kati kwa sababu imekuwa iki-*support* sana miradi ya maji Wilaya ya Makete. Tuna Mradi wa Maji wa Mang'oto, Lupalilo, na Tandala; ni mradi wa maji ambao tuliandika andiko tukaleta Wizarani, hatujapata majibu hadi leo. Ni lini Serikali itawajibu wananchi kuhusu mradi huu mkubwa utakaosaidia Kata ya Mang'oto, Tandala na Lupalilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua na tunampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa

kusimamia na kuandika andiko lenye kutoa uelekeo wa nini kifanyike ndani ya Makete. Nimtoe hofu, kuanzia leo nitafuatilia kuhusu andiko hilo, nijue limefikia hatua gani na tutampa mrejesho Mheshimiwa Mbunge ili kujua wananchi wake wanaweza kutatuliwa changamoto yao kwa uharaka zaidi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Kawawa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bwawa la Mto Rufiji ni lini Serikali itaanza ujenzi wake kwa kuwa tumesubiri kwa muda mrefu ahadi hiyo mpaka sasa hatujaona utekelezaji wake? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vyanzo vya uhakika ambavyo tunavitegemea ni Bonde la Mto Rufiji, kwani litatatua changamoto kwa ukubwa wake katika utoaji wa huduma katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Vilevile tunatamani baada ya kuchukua haya maji kuyapeleka Dar es Salaam, tuyachukue pia tuyapeleke mikoa ya Lindi. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali tayari imeshaanza mchakato wa kumpata mshauri ili aanze kufanya upembuzi yakinifu na baada ya hapo, tuweze kufanya usanifu wa kina, ili kupata gharama ya utekelezaji wa mradi huo. Tukishapata gharama, ndipo sasa Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kuutekeleza mradi huo. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, Mbunge wa Busokelo, aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Timida Fyandomo.

Na. 169

**Vivutio vya Kikodi kwa Vijana Wanaoanza Biashara**

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO K.n.y. MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka vivutio maalumu vya kikodi kwa vijana wanaoanza biashara ili kuchochea ajira na kukuza uchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MUSHAMU A. MUNDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni swali No. 1,425. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Lutengano kwa kuwapambania sana wananchi wake wa Jimbo la Busekelo, na kwa namna anavyowasimamia. Pia ninafahamu Mheshimiwa Lutengano amekuwa akiwatetea sana vijana hata wakati akiwa anahudumu kwenye nafasi ya ukurugenzi kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo tulikuwa wote huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inatekeleza mikakati mbalimbali ya kikodi inayolenga kukuza biashara ndogo ndogo, hususan za vijana, na kuhamasisha uingiaji wao katika uchumi rasmi. Miongoni mwa mikakati hiyo, ni utekelezaji wa Mfumo wa Kodi ya Makadirio *(Presumptive Tax Scheme)* unaolenga walipakodi wadogo wasiokuwa na kumbukumbu sahihi za mapato au vitabu vya hesabu, ambapo masharti yake ni mepesi na yanatabirika ili kuwahamasisha wafanyabiashara kusajili biashara zao na kuanza kulipa kodi kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha utaratibu wa kipindi cha neema *(grace period)* kinachowaruhusu wafanyabiashara wapya kufanya biashara bila kulipa kodi kwa muda wa miezi sita tangu kuanza biashara. Hatua hizi zinalenga kuwapa wajasiriamali nafasi ya kukuza biashara zao bila mzigo wa kodi katika hatua za awali. Hii itaongeza ubunifu, kuvutia wafanyabiashara wa sekta isiyo rasmi kuingia kwenye mfumo rasmi, na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali kwa njia endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kutoa vivutio maalumu vya kikodi kwa vijana ili kuchochea uanzishaji wa biashara na ajira, ikiwemo msamaha wa kodi na viwango pungufu, huku ikiendelea kufanya tathmini ya athari zake ili kuhakikisha usawa, ufanisi wa sera, na uendelevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 na maboresho yake ya mwaka 2024, Serikali pia inatoa ahirisho la kodi ya mapato *(Corporate Income Tax)* kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo kwa biashara mpya *(start-ups)*, hatua inayolenga kusaidia biashara changa kukua na hatimaye kuwa walipakodi wakubwa na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timida Fyandomo.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imepitisha vivutio mbalimbali vya kikodi kama *Import Duty Exemption*, *VAT Exemption*, *Capital Allowance,* lakini pia na kuwapa wafanyabiashara na wawekezaji ndani na nje ya nchi *the grace period*, je, ni kwa nini Serikali inachelewesha kuwaruhusu au kuwapa muda mwafaka wa kutumia zile *incentives* ambazo wale wafanyabiashara wanakuwa wanataka kuzitumia na wanaruhusiwa kisheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Je, Serikali ina takwimu ya watu wanaonufaika na vivutio hivi vya kikodi? Kama haina, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba vivutio

hivi haviwanufaishi wachache, bali vinawanufaisha watu wengi wakiwemo vijana? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MUSHAMU A. MUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa vivutio vya kodi katika kuvutia uwekezaji wa ndani na nje. Ni kweli pia kuwa hapo awali kulikuwepo na changamoto zilizosababisha ucheleweshwaji wa utoaji wa vivutio hivyo. Changamoto hizo zilihusisha urasimu wa kiutendaji, ucheleweshwaji wa maamuzi, ukosefu wa utaratibu wa kutosha kati ya taasisi mbalimbali pamoja na mkanganyiko wa tafsiri za baadhi ya sheria na hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kubaini hali hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali madhubuti kupitia taasisi mbalimbali ikiwemo *TISEZA*. Sasa hivi angalau kuna *one stop centre* ambapo wawekezaji wanaweza wakaenda kuwasilisha maombi yao kuhusiana na vivutio stahiki kwenye sekta ambayo wanaenda kuifanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna ushirikishwaji mkubwa wa taasisi kama *TCCIA* ambayo pia tunaitumia kwa ajili ya kuwaelekeza wafanyabiashara vivutio stahiki katika maeneo ambayo wanaenda kuwekeza. Jambo hili inaelekea baada ya hatua hizo linaenda kupungua, na hivyo vivutio vitatoka kwa wakati, hasa kwa *startups* kama vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusiana na takwimu, Serikali kweli inatoa vivutio hivyo, hususan kwa vijana. Hata hivyo, kwa sasa hatuna takwimu zinazoonesha asilimia ambayo inatupa picha ya wale ambao wamefaidika na vivutio hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivutio hivyo vimekuwa vikitolewa, lakini mtazamo siyo vivutio, tathmini imekuwa ikitolewa kwa kuangalia mtazamo mpana kuliko kuangalia asilimia ya watu ambao wanafaidika. Kwa mfano, kwa kuangalia ajira na shughuli za kiuchumi katika jamii. Kwa sasa tunafikiri Wizara ya Fedha

inaweza ikapata takwimu nzuri zaidi pale ambapo sasa tumeanza kutumia mfumo wa *IDRAS* ambao unachukua takwimu za walipa kodi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuko na utaratibu wa kuwaelekeza, na hapa nielekeze kwa dhati kabisa wenzetu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, waweze kuanzisha utaratibu. Ninajua upo utaratibu wa mafunzo kwa wafanyabiashara, hasa vijana ambao wanaanza biashara kwa sasa, hasa kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwawezesha vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa na takwimu na vijana hawa wasipopata mafunzo stahiki kwa ajili ya kutumia zile fedha, zile fedha zitakuwa kama zile ambazo Wabunge tulikuwa tukilalamikia hapa, kwamba, fedha za 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri zimekuwa zikienda na maji bila habari kutokana na vijana kuchukua fedha bila kuwa na maarifa stahiki ya kutumia fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 200 lazima zilete tija kwa vijana. Kwa hiyo, nawaambia na kuwahimiza Mamlaka ya Mapato Tanzania, pamoja na jitihada wanazofanya za kuwapa mafunzo na kutoa vivutio hivyo ambavyo nimeviongelea, watoe mafunzo stahiki kwa vijana, ili mwisho wa siku shilingi bilioni 200 zilete tija kwao. Pia, kama tunavyosisitiza, wawe ni wajasirimali ambao wanakuja ku-*graduate* kuwa wafanyabiashara wakubwa watakaoleta tija na kuinufaisha nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala, swali fupi la nyongeza.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato *(TRA)* wamekuwa wakikusanya kodi kwa wafanyabiashara wetu kwa kupitia mtaji, kitu ambacho kinawakatisha tamaa wafanyabiashara walio wengi wakiwemo vijana, lakini pia, Serikali kukosa mapato halisi. Je, Serikali iko tayari sasa kukusanya kodi kwenye faida, ili mfanyabiashara aweze

kupata moyo na kulichangia Taifa lake kwenye shughuli za maendeleo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MUSHAMU A. MUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijapata swali sehemu ya mwanzo, *TRA* inafanya utaratibu wa kukusanya kodi kupitia nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linasema, *TRA* mfanyabiashara anapoenda kuchukua leseni, pamoja na *TIN*, kodi anayokadiriwa ni pamoja na mtaji wake bila kuangalia kwamba, mtaji ule ameupata wapi? Mitaji mingi ya wafanyabiashara wetu wamekopa. Kwa hiyo, *TRA* inachukua kodi kulingana na mtaji wa mteja alionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan Kunti ninaenda kuanzisha biashara ya shilingi 4,000,000, kwa hiyo, *TRA* inapokuja kuni-*charge* mimi ina-*charge* kupitia ile shilingi 4,000,000 na siyo faida iliyotokana na shilingi 4,000,000. Kwa hiyo, swali langu, ninataka kujua Serikali mko tayari kuchukua kodi kwenye faida badala ya mtaji wa mteja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninafikiri umemwelewa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ENG. MUSHAMU A. MUNDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huo haupo, na ndio maana hata tunavyoongelea *Corporate Tax* tunaongelea kodi kutoka kwenye faida. Hoja hii ninaichukua kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, kama kweli kuna matukio ya wafanyabiashara kulipishwa kodi kutoka kwenye mtaji, kwa sababu, kodi haitakiwi kufilisi biashara hiyo, ndiyo hasa mustakabali wa kodi halisi. Kodi inatakiwa ichukuliwe kutoka kwenye faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongelea wajasiriamali wadogo, wao wamekuwa *exempted* kabisa kutolipa kodi, hasa wale ambao wanazalisha fedha chini ya shilingi 4,000,000. Kwa

hiyo, hata wale ambao ni zaidi ya shilingi 4,000,000 kitakachotokea ni kwamba, watalipa kodi kwenye faida wanayozalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema wazi pia, tumezungumzia kwamba, wajasiriamali wadogo wana msamaha wa kulipa kodi, lakini pia, uki-*graduate* kutoka kwenye msamaha, utapata maelekezo wewe kama mfanyabiashara, ni kwa namna gani unakokotoa faida yako ili ihusishwe kwenye kulipia kodi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunamalizia na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, Mbunge wa Ngorongoro, aulize swali lake.

Na. 170

**Ujenzi wa Barabara Kigongoni hadi Wasso kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. YANNICK I. NDOINYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara kutoka Kigongoni hadi Wasso – Ngorongoro kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Kigongoni ama Mto wa Mbu – Wasso – Loliondo yenye urefu wa kilometa

211 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Sehemu ya Wasso – Sale kilometa 49 umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkataba wa ujenzi kwa sehemu ya Wasso – Loliondo urefu wa kilometa 10 umesainiwa, ambapo taratibu za malipo ya awali kwa mkandarasi zinaendelea. Vilevile, taratibu za manunuzi ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi sehemu za Mto wa Mbu – Selela kilometa 23 na Selela – Engaruka kilometa 27 zinaendelea. Kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa majibu ya Wizara. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa ile barabara inaenda kuifungua wilaya yetu kwa sehemu kubwa sana. Ni kwa nini Serikali inashindwa kuendeleza kile kipande cha kilometa 49 kinachoanzia Sale kuja Engaresero na imekaa kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza, linahusiana na madaraja makubwa ya mito ambayo inatusumbua. Ni kwa nini, Serikali isitumie mpango wa dharura kujenga madaraja mawili ya Mto Moinik na Mto Athumani, ili yaache kusumbua na kuchukua maisha ya wananchi wetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa swali la pili kuhusu madaraja, lakini swali la kwanza sikumsikia vizuri Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndoinyo.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nifafanue. Hii barabara ilikuwa inaitwa Loliondo – Kigongoni na ikaanza kwa kilometa 49 kutoka Waso hadi Sale na

ikasimama kwa muda mrefu. Kwa nini, hicho kipande hakijaendelezwa badala yake inaanza mpya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umemwelewa?

Mheshimiwa Ndoinyo, ninaomba uzungumze kwa utaratibu. Lugha yako kidogo ni ngumu kwetu. *(Makofi)*

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kiswahili hicho cha Kimaasai ni kigumu, ngoja niweke Kiswahili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ilitengenezwa awali kilometa 49 ikasimama kwa muda mrefu, Waziri ametujulisha kwamba, wanaanza Kigongoni kwenda Selela na Selela kwenda Engaruka. Ninauliza, ni kwa nini kipande kipya kinaanza badala ya kuendeleza kile walichoanza mwanzoni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Umemwelewa sasa Mheshimiwa Ndoinyo? Ninafikiri sijui ni sauti kidogo au Mheshimiwa Naibu Waziri umemwelewa sasa? Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa kwamba, tulianza kule Waso – Sale. Sijamwelewa anataka kwamba, tungeanzia Sale kuja huku, ama! Yaani ndiyo kitu ambacho sijakielewa vizuri, ili tujibu vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndoinyo, ongeza sauti kidogo.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Barabara hii ilikuwa inaitwa Loliondo – Mto wa Mbu, ikajengwa kweli kwa kuanzia Loliondo, maana ya Waso kuja Sale, ikasimama. Nilitegemea fedha zikipatikana ianzie Sale ije Engaresero na kwenda mpaka Kigongoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametuambia utaratibu uliopo ni kuanzia Kigongoni. Sasa kipande kingine tofauti kabisa kuelekea Selela na Engaruka, ndiyo swali langu. Kwa nini, waanze kipya badala ya kuendeleza kile walichoanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na swali la pili, ambalo nimelielewa vizuri, kuhusu madaraja yake mawili. Madaraja aliyoyasema, mawili, ni kweli yamekuwa ni moja ya madaraja ambayo yanasumbua sana unapotoka Mto wa Mbu kwenda Loliondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Daraja alilolitaja la Moinik tumepanga kulijenga katika bajeti hii ya 2026/2027 na Daraja la Athumani ambalo lina urefu wa kama mita 80, tunavyoongea sasa, wapo wataalamu wanalifanyia usanifu, ili litangazwe kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha na lianze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili. Ni kweli, tulijenga mwishoni, Waso – Sale kilometa 49 na tutajenga kutoka pale Sale kwenda Loliondo kilometa 10, ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya. Katika hii barabara tumeanzia Mto wa Mbu kwenda Selela na Selela kwenda Engaruka kwa sababu, barabara ni hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pia kwamba, pale Engaruka tunakwenda kujenga kiwanda kikubwa cha magadi. Kwa hiyo, ilikuwa ni muhimu sana katika hiyo barabara kwanza tujenge na ndio maana tumechukua mpango wa dharura kujenga hilo Daraja la Athumani, ambalo linakwenda kujenga kiwanda hicho cha Magadi *(soda ash)*, ili kuweza kurahisisha usafari. Ni barabara hiyo hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge akitoka huku Makao Makuu ya Arusha atapita akiwa anaelekea Loliondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ni kujenga barabara yote baada ya Engaruka - Engaresero hadi Loliondo. Kwa hiyo, tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mpango wa Serikali ni kuijenga yote, lakini tuliona kwanza hili eneo ni muhimu sana, la kimkakati na kiuchumi, tuweze kuimarisha usafiri, ili tuweze kuanza kuzalisha magadi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Chilombe, swali fupi la nyongeza.

Waheshimiwa wengine ninaomba mzime *mic* zenu.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Barabara inayoanzia Tunduru Mjini – Mhesa – Nalasi mpaka Mchoteka imekuwa ikitolewa ahadi na Viongozi wetu wa Kitaifa kwa nyakati tofauti. Viongozi waliowahi kutoa ahadi pale ni pamoja na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyekuwa Rais wa nchi hii, Hayati Mheshimiwa Dkt. Magufuli pamoja na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, juu ya barabara hiyo kujengwa kwa kiwango cha lami. Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila ahadi za Viongozi wa Kitaifa ni kipaumbele cha Serikali kutekeleza hizo ahadi. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaenda kutafuta fedha na pia, katika hiyo barabara hata kabla hatujaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, tunachokwenda kukifanya ni pamoja na kuainisha maeneo korofi ili tuweze kuyaimarisha yawe yanapitika kipindi chote cha mwaka wakati tunatafuta fedha za kuijenga yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umemalizika na sasa ni wakati wa matangazo. Tuna matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii: -

Tunao wageni waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, ambaye ni Waziri wetu wa Nishati; hawa ni Viongozi na Wenyeviti wa Bodi kutoka Wizarani.

Kuna Mheshimiwa Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu, Umeme na Nishati Jadidifu; Dkt. James Mataragio, Katibu Mkuu, Mafuta na Gesi Asilia; Ndg. Janeth Mayanja, Mkuu wa Wilaya ya Chamwino; Prof. Mark Mwandosya, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*; Ndugu Paul Makanza, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Balozi Meja Jenerali (Mstaafu) Jacob Kingu *Ndc,* Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Nishati Vijijini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Halfani Halfani, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Uthibiti wa Mkondo wa Juu wa *Petrol* (*PURA*), Dkt. Lutengano Mwakahesya, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja *(PBPA);* Ndugu Raymond Mbilinyi Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Kukarabati Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme (*ETDCO*), na Wakili. Hassan Minga, Mwenyekiti wa Bodi ya Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati *(EWURA – CCC)*. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu George Nchwali, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mafuta Tanzania *(TANOIL);* Dkt. Hanifa Massawe, Mwenyekiti wa Bodi Kampuni ya Usimamizi wa Miundombinu ya Gesi Asilia *(GASCO);* Ndugu Mhandisi Nkisi Mwihava, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *EWURA;* na Ndugu Lazaro Twange, Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Mussa Makame, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC);* Mhandisi Hassan Said, Mkurugenzi Mkuu Wakala wa Nishati Vijijini *(REA);* Ndugu Gerald Maganga, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*; Mhandisi Charles Sangweni, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA);* na Ndugu Erasto Simon, Mtendaji Mkuu Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja *(PBPA)*. *(Makofi)*

Wengine ni Mhandisi Mathew Mwangomba, Meneja Mkuu Kampuni ya Uendeshaji Jotoardhi Tanzania *(TGDC)*; Mhandisi Richard Mwanja, Meneja Mkuu Kampuni ya Kukarabati Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme *(ETDCO);* na

Mhandisi Khadija Abdallah, Kaimu Meneja Mkuu Kampuni ya Nguzo za Zege Tanzania *(TCPM)*. *(Makofi)*

Wengine ni Mhandisi Baltazar Mrosso, Meneja Mkuu Kampuni ya Usimamizi wa Miundombinu ya Gesi Asilia *(GASCO);* Ndugu James Sanawa, Kaimu Meneja Mkuu Kampuni ya Mafuta Tanzania *(TANOIL);* Ndugu Stella Lupimo, Katibu Mtendaji Watumiaji wa Huduma za Maji na Nishati *(EWURA – CCC);* Mhandisi Innocent Luoga, Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu; Ndugu Godluck A. Shirima, Kamishna wa Petroli; Ndugu Ziana Mlawa, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu; na Ndugu Petro Lyatuu, Mkurugenzi wa Sera na Mipango. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ndejembi ni familia yake kutoka Jijini Dodoma ambao ni Ndugu Subira Rajabu, Mke wa Waziri; Ndugu Elias Ndejembi, Baba Mdogo wa Waziri; Ndugu Malema Ndejembi, Baba Mdogo wa Waziri; Ndugu Jemima Ndejembi, Shangazi wa Waziri; Ndugu Abu Sharifu, Ndugu wa Waziri; na Ndugu Ahmed Abdalla, Ndugu wa Waziri. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni Wakurugenzi Wasaidizi na Wakuu wa Vitengo (Menejimenti ya Wizara ya Nishati), Waagizaji na Wasambazaji wa Mafuta Tanzania *(OMCs)*, Wadau wa Maendeleo *(Development Partners)*, Wakuu wa Makampuni mbalimbali wanaoshughulika na Sekta ya Nishati, Kampuni zinazosimamia Mradi wa *EACOP*, na Wawakilishi wa wazalishaji wa Vifaa vya Ujenzi wa Miradi ya Umeme. *(Makofi)*

Wengine ni Wawakilishi wa Waendelezaji wa Miradi ya kuzalisha na kusambaza umeme kupitia gridi ndogo *(Off grid)*, Wawakilishi wa wakandarasi wa Miradi ya umeme vijijini, Mabenki, Wadau wengine wa sekta ndogo ya umeme, Kamati ya Ulinzi na Usalama na Viongozi wa Dini, Kamati ya Siasa ya Wilaya na Madiwani wa Jimbo la Chamwino. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine ambao tunao leo hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni mgeni wa Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri Wizara ya

Madini, ambaye ni Ndugu Noel Severe, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Arumeru Mkoani Arusha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Yahya Esmail Nawanda, Ndugu Sarah Kimaro, ambaye ni mjasiriamali kutoka Kigamboni, Jijini Dar es Salaam.

Mgeni wa Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, Ndugu Rahel Maghamba Mbunge wa Bunge la Vijana la Afrika Mashariki kutoka Jijini Arusha.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine waliotembelea Bunge leo, ni wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo ambao ni Wajumbe 11 wa Baraza la Vijana kutoka Wilaya ya Mjini Zanzibar. *(Makofi)*

Pia tunao wanafunzi 95 na Walimu Nane kutoka Shule ya Sekondari ya Lombeta Mkoani Moshi. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka huko Moshi, wageni wetu wote tunawakaribisha katika Bunge letu, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Sasa ninamwita Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waziri wa Nishati, kwa ajili ya kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, iliyochambua na kujadili bajeti ya Wizara ya

Nishati, Fungu Na. 58, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na taasisi zake kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu ili kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu ya Nishati kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba hii kama Waziri wa Nishati, ninaomba kwa namna ya kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme kuwa uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kusimamia na kuendeleza sekta ya nishati, ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi na kijamii, maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaahidi kuwa kwa rehema za Mwenyezi Mungu na kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu na wadau wengine wa sekta ya nishati ili kuhakikisha maono ya Mheshimiwa Rais katika maendeleo ya sekta hii na Taifa kwa ujumla yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindi huo unadhihirisha kukubalika kwake kwa Watanzania kutokana na umahiri katika uchapakazi wake, ufuatiliaji katika utendaji wa Serikali ili kuhakikisha sote tunawajibika ipasavyo katika kufikia matarajio ya Watanzania ya kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa safari ya kuelekea kwenye maendeleo ya nchi yetu, inahitaji ushiriki na uwajibikaji wa kila mmoja kwa kuzingatia nafasi, kipaji, uwezo na karama tulizobarikiwa na Mungu, nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuendelea kumuunga mkono Rais katika kuliongoza Taifa letu na kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru kwa maelekezo na miongozo wanayonipa, ambayo imekuwa chachu katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo ya kusimamia na kuendeleza sekta ya nishati. Ninawapongeza pia Mawaziri wote kwa kuteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali katika awamu hii, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioaminiwa na kuchaguliwa na wananchi ili kuwa wawakilishi katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, ikiwemo wewe Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu

aendelee kuwapa hekima na afya njema katika kutekeleza majukumu yenu ya kuwatumikia wananchi kupitia Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Subira Hamisi Mgalu, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mbunge wa Jimbo la Busega, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Kamati kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2026/2027, tarehe 24 Machi, 2026. Nitumie fursa hii kuahidi kuwa Wizara itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwa maendeleo ya sekta hii muhimu katika ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru pia Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka I. Leonard, Makatibu wa Kamati na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu, Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Naibu Waziri wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya umeme na nishati jadidifu; na Dkt. James Mataragio, Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya mafuta na gesi asilia, kwa umahiri na umakini wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, pamoja na ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma na kwa tija na ufanisi katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa upendo, imani, uelewa na ushirikiano mkubwa wanaonipatia ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia Jimboni na Kitaifa kwa mafanikio kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaahidi wananchi wa Jimbo la Chamwino utumishi uliotukuka katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu na kwamba tutaendelea kushirikiana bega kwa bega katika kuhakikisha changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi na Jimbo linapiga hatua kubwa za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru mke wangu mpendwa, Bi. Subira Rajabu, pamoja na wanangu wote wapendwa kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, ninapenda kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu likiongozwa na Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Ilala na Spika wa Bunge hili. Nitoe pole kwa familia, Ndugu, jamaa na wananchi kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Mheshimiwa Jenista Joachim Mgama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho, Mheshimiwa Halima Iddi Nasoro aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Ismani. Wakati wote tutaendelea kuwakumbuka na kuenzi mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahala pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki, na wengine waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Ninamwomba Mwenyezi Mungu awape subira waliopoteza ndugu zao, majeruhi wapone haraka, na Marehemu wote wapumzike kwa amani. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2025/2026 na mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya Taifa lolote yanahitaji uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa gharama nafuu. Ni kwa muktadha huo, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 imetambua nishati kama moja ya vichocheo vitakavyowezesha kufikiwa kwa malengo na shabaha za dira hiyo, ikiwemo kuwa na maisha bora na ustawi kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mwelekeo wa Dira 2050 katika sekta ya nishati ni pamoja na kuwezesha kuwepo kwa mfumo bora wa nishati safi, uliostahimilivu, wenye ufanisi na kuaminika na wa gharama nafuu; na kuwa na miundombinu thabiti ya nishati inayochochea maendeleo ya viwanda na ustawi wa kiuchumi na kijamii na kuliwezesha Taifa letu kuwa mzalishaji wa nishati inayokidhi mahitaji ya ndani na mmoja ya wazalishaji wakuu wa nishati katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme, ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji, jua, upepo, gesi asilia, tungamotaka, jotoardhi na urani, vinavyotuwezesha kuwa na uhakika na salama wa upatikanaji wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeendelea kuchukua hatua kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme uliongezeka na kufikia megawati 4,522.54 ikilinganishwa na megawati 4,031.71 zilizokuwepo mwezi Machi, 2025, sawa na ongezeko la 12.17%, kama inavyofafanuliwa katika jedwali namba moja na kiambatisho namba moja cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili umeme unaozalishwa uweze kutumika na mlaji wa mwisho, hakuna budi kuwekeza katika miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini, ambapo hadi kufikia Machi, 2026 urefu wa miundombinu ya kusafirishia umeme nchini ulikuwa umefikia jumla ya kilomita 8,500.38 ikilinganishwa na kilometa 7,809.67 zilizokuwa zimefikiwa Machi, 2025, sawa na ongezeko la asilimia tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miundombinu ya kusambaza umeme, urefu wa miundombinu hiyo umefikia kilomita 240,229.56 ikilinganishwa na kilomita 200,266.50 zilizofikiwa mwezi Machi, 2025, sawa na 20%, kwa mchanganuo uliopo katika jedwali namba mbili la hotuba yangu ukurasa wa 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali za ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme, kiwango cha upatikanaji wa umeme nchini *(accessibility)* kimeendelea kuongezeka kutoka wastani wa 78.4% mwaka 2020 na kufikia wastani wa 85.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kiwango cha wananchi waliounganishiwa umeme nchini *(connectivity)* kimeongezeka kutoka 37.7% mwaka 2020 hadi 52.1% na mwelekeo wa Serikali ni kuunganisha jumla ya wateja wapya 8,300 ili kufikia 75% ya wananchi waliounganishwa na umeme ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii mijini, vijijini na vitongojini, zimechochea kasi ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini, ambapo yameongezeka na kufikia megawati 2,199.06 yaliyofikiwa tarehe 4 Februari, 2026, sawa na ongezeko la 15.24% ikilinganishwa na megawati 1,908.15 zilizofikiwa tarehe 20 Februari, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jedwali namba tatu katika hotuba yangu, ukurasa wa 17 linafafanua kwa kina kuhusu mwenendo

wa ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini katika mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuimarika kwa upatikanaji wa umeme nchini, nchi yetu pia imeendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa ya mafuta ya petroli (yaani petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege), pamoja na kuwepo na changamoto za upatikanaji wa bidhaa hizi na kuongezeka kwa gharama za upatikanaji wake kilichosababishwa na vita baina ya Marekani, Israel na Iran. Vita hiyo imesababisha kufungwa kwa mlango bahari wa Hormuz *(Strait of Hormuz)* unaopitisha zaidi ya 20% ya mafuta yote duniani, kuathiri visima vya mafuta, mitambo ya kuchakata mafuta ghafi *(refineries)* na maghala ya kuhifadhi mafuta, na hivyo kuathiri mnyororo mzima wa upatikanaji wa mafuta duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita hii imeathiri sana nchi za Mashariki ya Kati yaani (Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Bahrain, Oman na Kuwait) ambapo nchi yetu inaagiza kiasi cha 59% ya mafuta yake, ambapo nchi yetu pia inaagiza kiasi cha 41% ya mafuta kilichosalia kinatokea nchini India, ambapo pia na wao hutegemea kupata mafuta ghafi kutoka Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta ni pamoja na kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* ambalo ni Shirika la Taifa la Mafuta kuagiza kiwango cha mafuta kinachotosheleza kipindi cha miezi mitatu ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upatikanaji wa mafuta duniani na itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati, ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta na hivyo, kutoathiri utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa gesi asilia nchini katika kipindi hiki ulikuwa futi za ujazo milioni 41,530.94 kutoka katika vitalu vya Songo Songo na Mnazibay; ambapo Songo Songo

hutoa futi za ujazo milioni 17,945.19 na Mnazi Bay futi za ujazo milioni 23,585. Gesi asilia hiyo ilitumika katika uzalishaji wa umeme, viwandani, katika vyombo vya moto, taasisi na katika nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliendelea na utekelezaji wa programu, miradi na kazi mbalimbali zilizohusu uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme vijijini, mijini, na vitongojini; utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; pamoja na kuendelea na matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini. Mafanikio mbalimbali yalipatikana kama inavyoelezwa kwa kina katika sehemu B ya hotuba yangu, ukurasa wa 21 hadi 142.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/2026 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 1,965,745,445,000 ambapo shilingi 1,886,513,219,000, sawa na 95.97% ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi 79,232,226,000, sawa na asilimia nne nukta sifuri tatu ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwishoni mwa Machi, 2026 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 1,282,833,545,238, ambapo shilingi 17,281,222,461 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,265,552,322,777 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ambapo utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo: -

(a) Uzalishaji wa umeme kupitia Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere wa Megawati 2,115 uliendelea kupitia mitambo yote tisa ya uzalishaji, kwa kuzingatia mahitaji ya umeme uliopo.

(b) Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua Mkoani Shinyanga, megawati 150, iliyohusisha uzalishaji wa megawati 50 ilikamilika na umeme huo umeingizwa kwenye gridi ya Taifa. Aidha, mradi huu ni wa

kihistoria, kwani ni wa kwanza kutekelezwa na Serikali kati ya miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia chanzo cha nishati ya jua. Hivyo, umewezesha kuongeza wigo wa vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme hapa nchini.

(c) Utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi, megawati 49.5 uliendelea ambapo upande wa ujenzi wa kituo cha uzalishaji umeme, umefikia 23.73%. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 54 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe, pamoja na kusambaza umeme katika vitongoji 18 vilivyomo ndani ya vijiji saba vilivyopitiwa na mradi, ambapo jumla ya wateja 750 zikiwemo shule, vituo vya afya na kaya wamenufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji wa umeme, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yanye urefu wa kilometa 345 umefikia 74.13% ambapo utekelezaji wa miradi mingine ni kama ifuatavyo: -

Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma, yenye urefu wa kilomita 616.5 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya Iringa, Kisada, Iganjo, Tunduma na Sumbawanga, umefikia 77.06%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kilovoti 220 kutoka Songea, Tunduru, Masasi, Maumbika yenye urefu wa kilomita 519.5 na vituo vya kupooza umeme vya Masasi na Maumbika ikiwa ni hatua ya kuunganisha Mikoa ya Lindi na Mtwara kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga yenye urefu wa yenye urefu wa kilomita 135.5 umefikia 60.61%. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga umefikia 48.8%, na kwa upande wa Gridi Imara, utekelezaji wake umefikia 54% ambapo miradi

mbalimbali imekamilika na utekelezaji wa miradi mingine ya Gridi Imara unaendelea kama inavyoonekana katika kiambatisho namba tatu cha hotuba yangu, ukurasa wa 216 hadi 217.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa na hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa huo, pamoja na kuipunguzia *TANESCO* gharama za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta katika mkoa huo, ambapo jumla ya shilingi bilioni 68.4 zimeweza kuokolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi mingine ya kusafirishia umeme uliendelea, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka; ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kwa ajili ya *SGR* (*SGR Lot 3, SGR Lot 4 na SGR 5);* na ujenzi ujenzi wa njia za kusafirisha umeme *(submarine cables)* msongo wa kilovoti 220 kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Serikali ni kuhakikisha kuwa vitongozi vyote 64,259 vya Tanzania Bara vinafikiwa na umeme ifikapo 2030. Ili kuifikia azma hiyo, Serikali ilianza utekelezaji mkubwa wa kupekeka umeme katika vitongoji 9,009 ambapo utakamilika kupeleka umeme katika vitongoji hivyo 9,009 katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ni pamoja na miradi inayoendelea kutekelezwa ya kupeleka umeme vitongojini itakayowezesha vitongoji 50,453 sawa na 78.4% ya vitongoji vyote vya Tanzania Bara kufikiwa na huduma ya umeme ifikapo mwaka 2028. Hatua ambayo itachochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii vitongojini, pamoja na utoaji wa huduma bora katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali kuhusu kupeleka nishati vijijini ni pamoja na kuanza utekelezaji wa mradi kwa kuongeza uunganishaji wa wateja katika vitongoji yaani *(universal hamlet eletrification and last mile customers connectivity)* katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na

Dodoma, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahususi wa Nishati wa Taifa *(National Energy Compact)* ulioridhiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika *(Mission 300)* mwezi Januari, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 3,060 sawa na vitongoji 15 katika kila jimbo uliendelea na kufikia 80% za utekelezaji. Aidha, Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongozi vya Mkoa wa Songwe, Kigoma na Lindi pamoja na maeneo ya migodi midogo midogo, ikiwemo iliyopo Chunya Mkoani Mbeya na Kwa Msisi, Handeni Mkoani Tanga na kilimo katika Mkoa wa Ruvuma, Njombe, Mbeya na Rukwa ili kuchochea shughuli za kiuchumi katika mikoa hiyo, ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa yanafikiwa na huduma za umeme, Serikali kupitia *REA* iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza mifumo ya jua inayojitegemea yaani *(solar home system – SH)* katika makazi 20,000 katika visiwa vidogo 143 vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, na Ziwa Tanganyika; ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya makazi 1,302 yalikuwa yamefungiwa mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa mwaka 2024/2034 uliozinduliwa mwezi Mei, 2024 wenye lengo la kuhakikisha angalau 80% ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma, kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kiafya na kimazingira na kuwezesha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa wananchi na katika taasisi husuan zinazohudumia watu zaidi ya 100.

Mheshsimiwa Mwenyekiti, kutokana na hatua zilizochukuliwa na Serikali, matumizi ya nishati safi ya kupikia yameendelea

kuimarika kutoka asilimia sita nukta tisa mwaka 2021 hadi kufikia 28.6% ya Watanzania wenye nishati safi ya kupikia mwaka 2025, hatua ambayo imechangia katika kupunguza uharibifu wa mazingira dhidi ya matumizi ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia na pia kulinda kulinda afya za wananchi dhidi ya matumizi ya nishati zisizo safi za kupikia. *(Makofi)*

Mheshsimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na uongozi wake uliotuwezesha kuwa na mwelekeo huu wa Kitaifa wa kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanatumia nishati safi ya kupikia, ajenda ambayo imempa heshima ya kuwa kinara wa nishati safi ya kupikia Barani Afrika na Kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali iliendela kutekeleza miradi ya utafutaji, uendelezaji, na uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu mbalimbali, ikiwemo Mnazi Bay, Songo Songo, Mnazi Bay Kaskazini, Eyasi – Wembere, Lindi – Mtwara na Songo Songo Magharibi, ambapo utekelezaji upo katika hatua mbalimbali kama inavyoonekana katika sehemu B (2) ya hotuba yangu, ukurasa wa 84 hadi 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya uzalishaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma eneo la Ntorya Mkoani Mtwara yanaendelea kwa kuanza ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia, lenye urefu wa kilomita 34.20 kutoka Ntorya hadi kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba na kufanya maamdalizi ya uchorongaji wa kisima cha uzalishaji cha Chikumbi -1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026 na kuwezesha uzalishaji wa gesi asilia kiasi cha futi za ujazo milioni 40 hadi 60 kwa siku, kwa kuanzia na uzalishaji kuongezeka hadi kufikia ujazo milioni 140 kwa siku kadri utekelezaji utakavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kwa kimiminika yaani *(Liquefied Natural Gas -*

*LNG)* iliyogunduliwa katika vitalu namba 1, 2, na 4 vilivyopo katika kina kirefu cha bahari, yanaendelea katika mwaka 2025/2026, ambapo hadi Machi, 2026 Serikali na wawekezaji wa mradi walifikia makubaliano katika maeneo mbalimbali ya mradi huo, ikiwemo katika maeneo ya kibiashara na kikodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa majadiliano hayo yapo katika hatua za ukamilishwaji wa masuala ya kisheria kwa pande zote mbili za majadiliano; ambapo kwa upande wa Serikali suala hilo linaratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Serikali imekwishatwaa eneo la mradi baada ya kukamilika kwa taratibu za ulipaji wa fidia kwa wananchi na pia imeendelea kutekeleza miradi ya uwajibikaji kwa jamii *(CSR)* kwa kwa kushirikiana na wabia wa mradi, ikiwemo ujenzi wa Shule ya Msingi ya Likong'o mkoani Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha matumizi ya gesi asilia katika vyombo vya moto, katika viwanda, taasisi na nyumbani, ikiwa ni hatua ya kuhakikisha nishati hii ya asili ambayo nchi yetu imebarikiwa, inatumiwa ipasavyo katika maendeleo ya Taifa letu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi tayari imewezesha ujenzi wa vituo 18 vya gesi iliyoshindiliwa yaani *(Compressed Natural Gas – CNG)* kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya moto, ikilinganishwa na vituo tisa vilivyokuwepo mwezi Aprili, 2025 hatua ambayo imepunguza mahitaji ya matumizi ya mafuta kutoka nje ya nchi na gharama za uendeshaji vya vyombo vya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia uhamasishaji mkubwa wa matumizi ya gesi asilia unaofanywa na Serikali, sekta binafsi imeendelea kuwekeza katika karakana za kufunga mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri, ambapo hadi sasa kuna jumla ya karakana 13, hatua ambayo imepunguza gharama za uwekaji wa mifumo ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali kupitia *TPDC* imejenga karakana na kuikabidhi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo pamoja na kazi ya kuweka mifumo ya matumizi ya gesi kwenye vyombo vya usafiri, karakana hiyo imekuwa sehemu ya mafunzo ya kuandaa vijana watakaoongoza kuwa wataalamu wa eneo hili, watakaoweza kujiajiri na kuongeza karakana binafsi nyingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa usambazaji wa *CNG* unafika maeneo mengi ya nchi. Serikali kupitia *TPDC* ipo katika hatua za ununuzi wa vituo vitano vya *CNG* vinavyohamishika *(Mobile CNG Stations)* ambapo utengenezaji wa vituo hivyo unaendelea. Vituo hivyo vinatarajiwa kuwekwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma kwa awamu ya kwanza na mikoa ya Arusha, Tanga na Kilimanjaro kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuhakikisha kuwa gesi asilia inafika maeneo mbalimbali ya nchi yaliyo mbali na miundombinu ya gesi kwa sasa, Serikali kupitia *TPDC* imeingia makubaliano ya awali na kampuni binafsi sita, kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya *Min-LNG* nchini ili kuhakikisha matumizi ya gesi asilia yanafika katika maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni hatua ya kuimarisha usambazaji wa gesi asilia katika maeneo ya kongani ya viwanda Zegereni, Kibaha katika viwanda vilivyopo Mlandizi na Bandari Kavu ya Kwala, Serikali kupitia *TPDC* imeanza maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi asilia, kutoka Kinyerezi Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani ambapo kwa sasa mshauri mwelekezi anaendelea na kazi ya upembuzi wa kina kwa njia ya kupitisha bomba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa bomba la kusafirishia mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanga uliendelea katika mwaka 2025/2026 ambapo kwa ujumla umefikia 82.6%. Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mafuta nchini, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maghala mapya ya kupokea mafuta kwa pamoja *(Single Receiving Terminal - SRT)* na hifadhi ya kimkakati ya mafuta *(Strategic*

*Petroleum Reserve – SPR)* katika eneo la Kigamboni, kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiwe la msingi la ujenzi wa maghala hayo liliwekwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi Machi, 2026. Serikali iliendelea kutekeleza jukumu la udhibiti wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA)* pamoja na udhibiti wa mkondo wa kati na chini, usafirishaji, uhifadhi na usambazaji kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati ya Maji *(EWURA),* ili kuhakikisha shughuli za sekta ya nishati zinaendelea kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Hatua zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana ni kama inavyoonekana katika sehemu ya B (3) ya hotuba yangu, ukurasa wa 106 hadi 127.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya mwaka 2025/2026, na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho katika Sekta ya Nishati, ninaomba sasa kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati pamoja na mambo mengine, unaongozwa na Sera, Mikakati, Mipango na Malengo mbalimbali ya kisekta na kibajeti ya Wizara ya Mwaka 2026/2027. Wizara pamoja na mambo mengine imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa Kufungua Rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 14 Novemba 2025; na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Nishati kwa kutekeleza

vipaumbele mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vitakavyotekelezwa ni pamoja na kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, ikiwemo kuunganisha mikoa ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa; kuongeza kasi ya kuunganisha umeme kwa wananchi ili kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii; na kuendelea kutekeleza mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project* - Gridi Imara) ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vingine vitakavyotekelezwa ni kufanya matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; na kuendelea na usambazaji wa umeme katika vitongoji, ikiwemo kwenye shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo (migodi, kilimo, viwanda, shule, pampu za maji na vituo vya afya); pamoja na kuwezesha ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuimarisha upatikanaji wa nishati safi na salama kwa vyombo vya moto katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia itaendelea kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2030) na Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa mwaka 2025 - 2030 *(National Energy Compact)*; na kuimarisha uzalishaji wa gesi asilia kwa kutekeleza miradi ya utafutaji na uendelezaji wa nishati hiyo ikiwemo mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG Project)*, mradi wa uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa eneo la Ntorya katika Kitalu cha Ruvuma na miradi ya kielelezo na kimkakati ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi – Wembere, Lindi - Mtwara na Mnazi Bay.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia kwa ajili ya vyombo vya moto *(CNG)*, viwandani, katika taasisi na majumbani pamoja na kuendelea na majadiliano ya kibiashara ya nishati hiyo na nchi nyingine ikiwemo Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyofafanua awali, pamoja na changamoto zitokanazo na vita, ambazo zinaathiri upatikanaji wa bidhaa za mafuta duniani, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa mafuta duniani na kuchukua hatua stahiki, ili kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hizo ambazo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi, usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, jitihada zitaelekezwa katika ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa za mafuta ya petroli ndani na nje ya nchi na kutekeleza shughuli za kiudhibiti katika Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia; kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara, Mashirika na Taasisi ya *TANESCO*, *REA*, *TPDC*, *PBPA*, *EWURA* na *PURA* pamoja na Kampuni Tanzu kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma, tija na ufanisi katika uendelezaji wa mapato; na kuimarisha na kusimamia nguvu kazi ya Wizara, mifumo ya utendaji kazi, upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na kushughulikia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora, Magonjwa Sugu na Yasiyoambukizwa na UKIMWI katika eneo la kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Serikali itaendelea kusimamia mradi wa uzalishaji umeme wa Julius Nyerere wa Megawati 2,115 pamoja na kutekeleza miradi mingine ya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na mradi wa kuzalisha umeme wa jua mkoani Shinyanga wa Megawati 150; Mradi wa kuzalisha umeme kutumia maji wa Malagarasi wa Megawati 49.5; Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Kakono wa Megawati 87.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa usafirishaji wa umeme, Serikali itaendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma. Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma na ujenzi

wa njia ya kusafirishia umeme ya msongo wa kilovolti 220 kutoka Songea – Tunduru – Masasi hadi Mahumbika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea pia na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovolti 400 kutoka Chalinze – Kinyerezi – Mkuranga, Ujenzi wa kituo cha kupooza umeme cha Ibadakuli pamoja na utekelezaji wa Mradi wa Gridi Imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *REA* itaendelea kutekeleza mradi wa kipaumbele wa umeme katika vitongoji awamu ya pili *(B)* inayohusisha kupeleka umeme katika vitongoji 9,009, mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji awamu ya pili *(A)* inayohusisha kupeleka umeme katika vitongoji 3,060 vya majimbo yote ya uchaguzi ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kuunganisha wateja vitongojini *(Universal Hamlet Electrification and Last Mile Customer Connection)* pamoja na mradi wa mifumo ya umeme jua visiwani *((Island Densification Project – IDP)*. Aidha, Serikali kupitia *REA* itaendelea kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutumia nishati ya umeme vijijini katika shughuli za kiuchumi ikiwemo uchakataji wa mazao ya kilimo, umwagiliaji, uvuvi, viwanda vidogo vidogo, migodi, biashara na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya kina kuhusu miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na nishati vijijini iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2026/2027 ni kama inavyoonekana katika sehemu ya C (1) ya hotuba yangu ukurasa wa 148 hadi 176.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034 ambapo mkazo utaelekezwa katika kuziwezesha kaya na taasisi zinazohudumia chakula kwa zaidi ya watu 100 kwa siku kutumia nishati safi ya kupikia kwa kutatua vikwazo na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka 2026/2027 itaendelea na kazi ya utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu mbalimbali, kukamilisha majadiliano baina ya Serikali na Wawekezaji na kuandaa mikataba ya utekelezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG),* pamoja na kujenga miundombinu ya uchakataji, usafirishaji na uhifadhi wa mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaendelea na usambazaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga vituo vya *CNG* katika mikoa mbalimbali nchini na kusambaza gesi asilia majumbani, katika viwanda na taasisi ili kuchochea kasi ya matumizi ya nishati hiyo inayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na mwelekeo wa Serikali ni kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa ya petroli ili kutoathiri shughuli za kiuchumi na hivyo kupitia usafiri na usafirishaji wa bidhaa na huduma. Hivyo, ninaomba niendelee kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali itakayotuhakikishia upatikanaji wa bidhaa ya petroli nchini pamoja na changamoto zilizopo duniani ikiwemo vita na migogoro mbalimbali inayoathiri mnyororo wa upatikanaji wa bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu C (2) ya hotuba yangu ukurasa wa 182 hadi 199 inafafanua kwa kina kuhusu kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2026/2027 kwa miradi mbalimbali itakayotekelezwa katika sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/2026 yalichangiwa pia na ushirikiano ambao Wizara iliupata kutoka kwa wadau mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali ninapenda kuwashukuru washirika wa maendeleo, Jumuiya na Nchi Wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutambua mchango wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)*; Benki ya Dunia *(World Bank)*; *Abu - Dhabi Development Corporation Fund*, *EDCF* ya Korea, *Exim Bank* (China), *KfW* (Germany), *OPEC Fund for International Development*, *SWISS Fund*, *Swedfund*, SIDA (Sweden), *Saudi Fund for Development (SFD)*, Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)*, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* na Umoja wa Ulaya *(EU)*.

Mashirika mengine ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan *(JICA)*, Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNCDF)*, *Geothermal Risk Mitigation Facility (GRMF)*, *Arab Bank for Economic Development in Afrika (BADEA)*, Shirika la Fedha Duniani *(IMF)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO)*, Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA)* pamoja na Shirika la Maendeleo la Uingereza *(UK-Aid)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuzishukuru kwa dhati Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Burundi, Canada, China, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Japan, India, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Korea Kusini, Malawi, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Oman, Rwanda, Saudi Arabia, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Zambia na nchi nyingine kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazishukuru pia Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* na Umoja wa Afrika *(AU)* kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu uendelezaji wa Sekta ya Nishati. Nizishukuru pia kampuni za *Equinor Tanzania As*, *Shell Exploration and Production (T) Limited, Exxon Mobil* na *Ophir Energy*, kwa ushirikiano zinazotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia Kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara ya Nishati katika mwaka 2026/2027, itaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na umeme wa kutosha unaokidhi

mahitaji ya ndani na ziada itakayoweza kuuzwa nje ya nchi na kutupatia fedha za kigeni; kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika vijijini, mijini na vitongojini na kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkazo utaelekezwa katika shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia, kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta; pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Bajeti ya jumla ya shilingi 2,525,401,129,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2026/2027. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) Shilingi 2,462,364,836,000 sawa na 97.5% ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,602,449,735,000 ni fedha za ndani, na shilingi 859,915,101,000 ni fedha za nje; na

(ii) Shilingi 63,036,293,000 sawa na asilimia 2.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 52,939,075,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 10,097,218,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi ya *PURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Spika Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu; Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo; Wenyeviti wa Bunge, ikiwemo wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii, vimeambatishwa vielelezo mbalimbali ambavyo vinafafanua masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**22 APRILI, 2026**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHESHIMIWA DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2026/27 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati (Fungu 58); Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Mkutano huu wa tatu wa Bunge la 13 ili kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa Mwaka 2026/27.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Hotuba hii kama Waziri wa Nishati, naomba kwa namna ya kipekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Wizara hii. Naomba niseme kuwa, uteuzi huu ni dhamana na heshima kubwa kwangu katika kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nishati, ambayo ni kichocheo cha ukuaji wa Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii, maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla. Naahidi kuwa kwa rehema za Mwenyezi Mungu, na kwa kuzingatia miongozo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu, kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu na wadau wengine wa Sekta ya Nishati, ili kuhakikisha maono ya Mheshimiwa Rais katika maendeleo ya Sekta hii na Taifa kwa ujumla yanafikiwa.

**SALAMU ZA PONGEZI**

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), kufuatia Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Ushindi huo unadhihirisha kukubalika kwake kwa Watanzania, kutokana na umahiri katika uchapakazi na ufuatiliaji katika utendaji wa Serikali ili kuhakikisha sote tunawajibika ipasavyo katika kufikia matarajio ya Watanzania ya kuwaletea maendeleo. Kwa kuwa safari ya kuelekea kwenye maendeleo ya nchi yetu inahitaji ushiriki na uwajibikaji wa kila mmoja kwa kuzingatia nafasi, kipaji, uwezo na karama tuliyobarikiwa na Mwenyezi Mungu, nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu na kujiletea maendeleo.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Dkt. Hussen Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi) kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru kwa maelekezo na miongozo wanayonipa, ambayo imekuwa chachu katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ipasavyo ya kusimamia na kuendeleza Sekta ya Nishati. Nawapongeza pia Mawaziri wote kwa kuteuliwa kuziongoza Wizara mbalimbali katika Awamu hii, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote walioaminiwa na kuchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, nakupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Jimbo la Ilala) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao kuliwezesha Bunge hili kutekeleza majukumu yake.

8. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu (Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo) kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile (Mbunge wa Jimbo la Busega) kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Aidha, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri na maoni yao katika kuendeleza na kusimamia Sekta ya Nishati. Naishukuru Kamati kwa kupokea, kujadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2026/27 tarehe 24 Machi, 2026, na nitumie nafasi hii kuahidi kuwa Wizara itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, kwa maendeleo ya Sekta hii muhimu katika ukuaji wa Sekta nyingine za kiuchumi na kijamii nchini.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nimshukuru pia Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard, Makatibu wa Kamati na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushikirikiano mkubwa wanaotupatia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** sina budi kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba (Mb.), Naibu Waziri; Mha. Felchesmi Jossen Mramba, Katibu Mkuu (Umeme na Nishati Jadidifu); na Dkt. James Peter Mataragio, Katibu Mkuu (Mafuta na Gesi Asilia) kwa umahiri na umakini wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Taifa letu. Niwashukuru pia Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake, kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na kutekeleza kikamilifu majukumu yao kwa kujituma, tija na ufanisi.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Chamwino kwa upendo, imani, uelewa na ushirikiano mkubwa wanaonipatia, ambao umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia jimboni na kitaifa kwa mafanikio. Kupitia Bunge lako Tukufu, niwaahidi wananchi wa Jimbo la Chamwino utumishi uliotukuka katika kipindi chote nitakachokuwa nikiwawakilisha katika Bunge hili Tukufu, na kwamba tutaendelea kushirikiana bega kwa bega katika kuhakikisha changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi na Jimbo linapiga hatua kubwa za maendeleo. Aidha, namshukuru mke wangu mpedwa Bi. Subira Adadi Rajabu pamoja na wanangu wote wapendwa kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kijimbo na kitaifa.

**SALAMU ZA POLE**

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa na wananchi kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Jenista Joackim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Isimani. Wakati wote tutaendelea kukumbuka na kuenzi michango yao katika maendeleo ya Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awape subira waliopoteza ndugu, majeruhi wapone kwa haraka na marehemu wote wapumzike kwa amani. Amina.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii imeandaliwa kwa kuzingatia maudhui ya Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2026/27.

## A.1 MAJUKUMU YA WIZARA

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) Na. 386/2025 la tarehe 19 Desemba, 2025, Wizara imekasimiwa usimamizi na uratibu wa majukumu yafuatayo:

a) Kutunga na kutekeleza Sera kuhusu nishati, mafuta na gesi asilia;
b) Kusimamia rasilimali za nishati na petroli;
c) Kuongeza thamani katika rasilimali za petroli;
d) Kuendeleza miundombinu ya mafuta na gesi;
e) Ununuzi wa mafuta kwa pamoja;
f) Huduma za umeme mijini na vijijini;
g) Kuwezesha ushiriki wa watanzania katika shughuli za nishati na petroli;
h) Kuendeleza vyanzo jadidifu na visivyo jadidifu vya nishati;
i) Uratibu wa masuala ya nishati safi ya kupikia;
j) Udhibiti wa nishati na maji;
k) Kuimarisha utendaji na Rasilimali watu ya Wizara; na
l) Kusimamia Idara, Mashirika ya Umma, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.

Aidha, Wizara pia inatekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zilizo chini yake zikiwemo Kampuni Tanzu ambazo ni:

i. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lenye Kampuni tanzu ambazo ni Kampuniya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania *(Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited - TCPM)*; Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme *(Electrical Transmission Distribution Construction and Maintenance Company - ETDCO)* na Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (*Tanzania Geothermal Development Company-TGDC*);

ii. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(Tanzania Petroleum Development Corporation - TPDC)* lenye kampuni zake tanzu ambazo ni TANOIL na GASCO;

iii. Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency - REA)*;
iv. Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (*Petroleum Upstream Regulatory Authority - PURA)*;

v. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(Energy and Water Utilities Regulatory Authority - EWURA)*; na

vi. Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja *(Petroleum Bulk Procurement Agency - PBPA)*.

## A.2 MWELEKEO WA SEKTA YA NISHATI NCHINI

16. ***Mheshimiwa Spika***, maendeleo ya Taifa lolote yanahitaji uhakika wa upatikanaji wa nishati kwa gharama nafuu. Ni kwa muktadha huo, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) imeitambua nishati kama moja ya vichocheo vitakavyowezesha kufikiwa kwa Malengo na Shabaha za Dira hiyo, ikiwemo kuwa na maisha bora na ustawi kwa wote. Hivyo, mwelekeo wa Dira 2050 katika Sekta ya Nishati ni pamoja na kuwezesha kuwepo kwa mfumo bora wa nishati safi ulio stahimilivu, wenye ufanisi, wa kuaminika na wa gharama nafuu; kuwa na miundombinu thabiti ya nishati inayochochea maendeleo ya viwanda na ustawi wa kiuchumi na kijamii; na kuliwezesha Taifa letu kuwa mzalishaji wa nishati inayokidhi mahitaji ya ndani na moja ya wazalishaji wakuu wa nishati katika Ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

### Uzalishaji wa Umeme

17. ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji, jua, upepo, gesi asilia, tungamotaka, jotoardhi na urani vinavyotuwezesha kuwa na uhakika na usalama wa upatikanaji wa nishati ya umeme kwa maendeleo ya Taifa letu. Katika mwaka 2025/26 Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha uzalishaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia

Machi, 2026 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme uliongezeka na kufikia Megawati 4,522.54 ikilinganishwa na Megawati 4,031.71 zilizokuwepo mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 12.17**.

Ongezeko hili la uzalishaji wa umeme limetokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya kuzalisha umeme katika kipindi hiki, ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme jua Kishapu - Shinyanga (Awamu ya Kwanza) wenye uwezo wa Megawati 50. Jedwali Na. 1 ni mchanganuo wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali hadi Machi, 2026. Aidha, *Kiambatisho Na. 1* ni uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa hadi Machi, 2026.

**Jedwali Na. 1: Uwezo wa Mitambo ya Kuzalisha Umeme hadi Machi, 2026 kwa Kutumia Vyanzo Mbalimbali**

| Chanzo | Uwezo wa Mitambo | | Hali ya Uzalishaji Kwa Sasa (MW) | |
|---|---|---|---|---|
| | MW | Asilimia | MW | Asimilia |
| Maji | 2,727.31 | 60.30 | 1,387.50 | 60.20 |
| Gesi Asilia | 1,284.58 | 28.40 | 721.00 | 31.28 |
| Mafuta | 262.36 | 5.80 | 29.40 | 1.28 |
| Jua | 65.00 | 1.44 | 39.00 | 1.70 |
| Tungamotaka | 135.49 | 3.00 | 81.00 | 3.51 |
| Upepo | 2.40 | 0.05 | 1.90 | 0.08 |
| Makaa ya mawe | 45.40 | 1.00 | 45.00 | 1.95 |
| **Jumla** | **4,522.54** | **100** | **2,304.80** | **100** |

Chanzo: **EWURA**

18. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na kiwango cha umeme kilichopo kwenye gridi ya Taifa kupitia vyanzo mbalimbali, hadi kufikia mwezi Machi, 2026, mitambo ya kuzalisha umeme ambayo haijaungwa katika Gridi ya Taifa ilikuwa na uwezo wa jumla ya Megawati 492.94 ambayo inajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 98.16 na Megawati 394.78 zinazalishwa na kampuni binafsi kwa ajili ya matumizi ya kampuni hizo kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na. 2A* na *2B*. Aidha, katika kuhakikisha kuwa mikoa

ya Kagera na Rukwa inapata umeme wa uhakika, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kununua umeme wa jumla ya Megawati 67 kutoka nje ya nchi ambapo Megawati 47 zinanunuliwa kutoka nchini Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera na Megawati 20 kutoka nchini Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa.

**Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

19. ***Mheshimiwa Spika***, ili umeme unaozalishwa uweze kutumiwa na mlaji wa mwisho/mteja, Serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini. Hadi kufikia Machi, 2026 urefu wa miundombinu ya kusafirisha umeme nchini ulikuwa umefikia jumla ya kilomita 8,500.38, ikilinganishwa na kilomita 7,809.67 zilizokuwa zimefikiwa Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 9**. Kwa upande wa miundombinu ya kusambaza umeme, urefu wa miundombinu hiyo umefikia kilomita 240,229.56 ikilinganishwa na kilomita 200,266.25 zilizofikiwa mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 20** kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Urefu wa Miundombinu ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Nchini**

| Na. | Msongo (kilovoti) | Urefu (Kilomita) Hadi Machi, 2025 | Urefu (Kilomita) Hadi Machi, 2026 |
|---|---|---|---|
| **Urefu wa Njia za Kusafirisha Umeme** | | | |
| 1. | 400 | 1,524.75 | 1,524.75 |
| 2. | 220 | 3,860.95 | 4,095.62 |
| 3. | 132 | 1,843.97 | 2,300.01 |
| 4. | 66 | 580.00 | 580.00 |
| **Jumla** | | **7,809.67** | **8,500.38** |
| **Urefu wa Miundombinu ya Kusambaza Umeme** | | | |
| 1. | 33 | 67,241.73 | 83,391.32 |
| 2. | 11 | 12,815.54 | 15,082.35 |
| 3. | 0.4 | 120,208.98 | 141,755.89 |
| **Jumla** | | **200,266.25** | **240,229.56** |

Chanzo: **TANESCO**

20. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na hatua zinazochukuliwa za ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme, kiwango cha upatikanaji wa umeme nchini (*accesibility*) kimeendelea kuongezeka kutoka wastani wa **asilimia 78.4** mwaka 2020 na kufikia wastani wa **asilimia 85.5.** Aidha, kiwango cha wananchi waliounganishiwa umeme nchini (*connectivity)* kimeongezeka kutoka **asilimia 37.7** mwaka 2020 hadi **asilimia 52.1**, na mwelekeo wa Serikali ni kuunganisha jumla ya wateja wapya 8,300,000 ili kufikia asilimia 75 ya wananchi waliounganishiwa umeme ifikapo mwaka 2030.

**Mahitaji ya Umeme Nchini**

21. ***Mheshimiwa Spika***, hatua zinazochukuliwa na Serikali za kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii mijini, vijijini na vitongojini zimechochea kasi ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini, ambapo yameongezeka na kufikia Megawati 2,199.06 yaliyofikiwa tarehe 04 Februari, 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 15.24** ikilinganishwa na Megawati 1,908.15 zilizofikiwa tarehe 20 Februari, 2025. Jedwali Na.3 linaonesha mwenendo wa mahitaji ya juu ya umeme nchini kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26.

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Mahitaji ya Juu ya Umeme (MW) Nchini kwa Mwaka 2024/25 na 2025/26**

| Mwezi | Julai | Agosti | Septemba | Oktoba | Novemba | Desemba | Januari | Februari | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2024/25** | 1,683.57 | 1,670.57 | 1,728.24 | 1,792.53 | 1,888.72 | 1,823.52 | 1,888.72 | 1,908.15 | 1,817.12 |
| **2025/26** | 2,016.65 | 2,050.85 | 2,083.46 | 2,120.21 | 2,151.96 | 2180.5 | 2,186.48 | 2199.064 | 2,123.65 |
| **Ongezeko** | **333.08** | **380.28** | **355.22** | **327.68** | **263.24** | **356.98** | **297.76** | **290.91** | **306.53** |

Chanzo: **EWURA**

**Huduma kwa Wateja**

22. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali, ambapo ilizindua matumizi ya mita janja (*smart meters*) zinazowezesha umeme unaonunuliwa na mteja kuingia moja kwa moja kwenye mita. Hadi Machi, 2026 jumla ya wateja 105,739 walikuwa wameunganishwa na mita janja na zoezi hilo linaendelea kwa

awamu kwenye maeneo yote nchi nzima. Aidha, wateja waliendelea kupewa taarifa mbalimbali kuhusu makatizo ya umeme yanayotokana na kazi za maboresho ya miundombinu ya umeme au dharura, kupitia ujumbe mfupi wa simu (*Bulk SMS*). Hadi Machi, 2026 jumla ya wateja 5,770,559 wamefikiwa kupitia njia hii.

23. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TANESCO pia ilifanya mikutano na wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa Serikali za Mitaa, Wakuu wa Wilaya na Mikoa kote nchini, ili kuwafahamisha mikakati mbalimbali inayotekelezwa ya kuboresha upatikanaji wa umeme katika maeneo yao, kuelimisha wananchi kuhusu ulinzi wa miundombinu ya umeme ili kupunguza vitendo vya uhujumu wa miundombinu hiyo, pamoja na kutoa elimu ya usalama na matumizi ya vifaa vya umeme katika kupikia. Jitihada hizi zimeendelea kuleta matokeo chanya katika kuboresha huduma kwa wateja na kuongeza imani ya wananchi kwa huduma zinazotolewa na TANESCO.

**Mafuta na Gesi Asilia**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** uagizaji wa mafuta nchini umeendelea kufanyika kupitia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (BPS). Kati ya Julai, 2025 na Machi, 2026 nchi ilipokea jumla ya lita bilioni 5.84 za mafuta zikijumuisha lita bilioni 1.63 za petroli, lita bilioni 3.94 za dizeli na lita milioni 260 za mafuta ya taa na ndege. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa, lita bilioni 2.56 (sawa na asilimia 43.84) ziliagizwa kwa ajili ya soko la ndani, ambapo lita bilioni 3.28 (sawa na asilimia 56.16) yalikuwa ni mafuta kwenda nchi jirani.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli (petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege), pamoja na kuwepo kwa changamoto za upatikanaji wa bidhaa hizo na kuongezeka kwa gharama za upatikanaji wake kulikosababishwa na vita baina ya Marekani, Israel na Iran. Vita hiyo imesababisha kufungwa kwa Mlango Bahari wa Hormuz (*Strait of Hormuz*) unaopitisha zaidi ya asilimia 20 ya mafuta yote duniani, kuathiri visima vya mafuta, mitambo ya kuchakata mafuta ghafi

(*refineries*) na maghala ya kuhifadhi mafuta na hivyo kuathiri mnyororo mzima wa upatikanaji wa bidhaa hizo duniani.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** vita hii imeziathiri sana nchi za Mashariki ya Kati (Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Bahrain, Oman na Kuwait) ambapo nchi yetu inaagiza kiasi cha asilimia 59 ya mafuta yake. Aidha, kiasi cha asilimia 41 ya mafuta kilichosalia huagizwa nchini India ambayo pia hutegemea kupata mafuta ghafi katoka Mashariki ya Kati. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta ni pamoja na kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya petroli Tanzania (TPDC), ambalo ni Shirika la Taifa la Mafuta *(National Oil Company)* kuagiza kiwango cha mafuta ya kutosheleza kipindi cha miezi mitatu ijayo (Mei, Juni na Julai, 2026). Aidha, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa upatikanaji wa mafuta duniani na itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kimkakati ili kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta, ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa gesi asilia nchini katika kipindi hiki ulikuwa futi za ujazo milioni 41,530.94 kutoka katika vitalu vya Songo Songo (Futi za ujazo milioni 17,945.19) na Mnazi bay (Futi za Ujazo milioni 23,585.75). Gesi asilia hiyo ilitumika katika uzalishaji wa umeme, viwandani, katika vyombo vya moto, taasisi na majumbani.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi na ufafanuzi kuhusu Mwelekeo wa Sekta ya Nishati nchini, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/26 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2026/27.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliendelea na utekelezaji wa mikakati, programu, miradi na kazi mbalimbali zilizohusu uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini, vijijini na vitongojini; utafutaji na

uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; pamoja na kuendeleza matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini kulingana na bajeti iliyoidhinishwa, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 utekelezaji ulikuwa katika hatua mbalimbali. **Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha kwa Mwaka 2025/26**

30. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Nishati kwa mwaka 2025/26 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Tisa Sitini na Tano, Milioni Mia Saba Arobaini na Tano, Mia Nne Arobaini na Tano Elfu (Shilingi 1,965,745,445,000)** ambapo **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Themanini na Sita, Milioni Mia Tano Kumi na Tatu, Mia Mbili Kumi na Tisa Elfu (Shilingi 1,886,513,219,000)** sawa na **asilimia 95.97** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi Bilioni Sabini na Tisa, Milioni Mia Mbili Thelathini na Mbili, Mia Mbili Ishirini na Sita Elfu (Shilingi 79,232,226,000)** sawa na **asilimia 4.03** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwishoni mwa Machi, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Mbili Themanini na Mbili, Milioni Mia Nane Thelathini na Tatu, Mia Tano Arobaini na Tano Elfu, Mia Mbili Thelathini na Nane (Shilingi 1,282,833,545,238)**, ambapo **Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Mbili Themanini na Moja, Mia Mbili Shirini na Mbili Elfu, Mia Nne Sitini na Moja (Shilingi 17,281,222,461)** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Mbili Sitini na Tano, Milioni Mia Tano Hamsini na Mbili, Mia Tatu Ishirini na Mbili Elfu, Mia Saba Sabini na Saba (Shilingi 1,265,552,322,777)** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**B 1: SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU**

32. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta hii inahusika na kuhakikisha kunakuwepo na uhakika na usalama wa upatikanaji wa nishati ya umeme nchini kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme mijini, vijijini na vitongojini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi.

## B1.1: MIRADI YA UZALISHAJI WA UMEME

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ambayo hutumia kipindi kirefu hadi kukamilika. Aidha, Serikali iliendelea kufanya maandalizi ya awali ya kutekeleza miradi mingine ya kuzalisha umeme, ikiwa ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha utekelezaji wa miradi, usanifu, kulipa fidia na kutafuta fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi hiyo. Hadi kufikia Machi, 2026 utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme ulikuwa kama ifuatavyo:

### (i) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP – MW 2,115)

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati na TANESCO imeendelea kusimamia mradi huu wa kimkakati ambao tayari umekamilika na umeme unaendelea kuzalishwa kupitia mitambo yote tisa (9) ya uzalishaji, kwa kuzingatia mahitaji ya umeme. Aidha, mbali na usimamizi wa mradi, kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kufanya marekebisho madogo madogo (*snags rectification*) na kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa katika kituo cha kupoza umeme cha Chalinze. Sambamba na kazi hizo, TANESCO na Bodi ya Bonde la Mto Rufiji imeingia makubaliano ya ushirikiano katika kutunza vyanzo vya maji na ushirikishwaji wa wadau katika utunzaji wa vyanzo vya maji yanayoelekea katika mradi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika katika mradi huu ni kukamilisha zoezi la udabuaji wa mto Mswiswi wenye urefu wa kilomita 29; na kufanya tathmini ya maeneo ya kupanda miti kwenye madakio (*catchment*) ya bonde la mto Rufiji, ambapo jumla ya miti 5,000 imepandwa katika maeneo ya Wanging'ombe, Kidatu, Kihansi na Mtera. Vilevile, Serikali imefanya zoezi la kufunga mifereji isiyo rasmi katika maeneo ya Wanging'ombe, Kilombero, Mbarali, Ifakara, Iringa, Mahenge na Kilosa na kukamilisha ujenzi wa tuta lenye urefu wa kilomita 11 la kuzuia mafuriko na upotevu wa maji kwenye mto Lumemo katika eneo la Ifakara.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Jua Mkoani Shinyanga – MW 150**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika eneo la Kishapu mkoani Shinyanga, chenye uwezo wa kuzalisha jumla ya Megawati 150. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa mradi huu inayohusisha uzalishaji wa Megawati 50 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 118.68** imekamilika na umeme huo umeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa. Aidha, mradi huu ni wa kihistoria kwa kuwa ni wa kwanza kutekelezwa na Serikali kati ya miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia chanzo cha nishati ya jua. Mradi huu umewezesha kuongeza wigo wa vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme nchini na ni kielelezo cha utashi wa namna Tanzania inavyochukua hatua mahsusi za kuelekea kwenye uzalishaji wa nishati kwa kutumia vyanzo safi na rafiki wa mazingira.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia yenye uwezo wa kuzalisha Megawati 185 pamoja na uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovoti 132 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi – Gongolamboto – Mbagala. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 187.99** sawa na takriban **Shilingi bilioni 517.04.**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na kusimika na kuwasha transfoma Na.3 katika kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi I; ubadilishaji wa nyaya za umeme kutoka kituo cha kupoza umeme cha Gongolamboto hadi kituo cha Mbagala kwa kuweka nyaya zenye uwezo wa kusafirisha MW 170 badala ya MW 80; na kumalizia kazi ya kusimika na kuwasha transfoma mbili (2) katika kituo cha Gongolamboto na Mbagala. Vilevile, kazi ya usimikaji wa tenki la kukusanya maji kutoka vipoza hewa (*chillers*) vya mashine (*gas turbine*) inaendelea na utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 99** kwa upande wa kituo cha kuzalisha umeme

na **asilimia 90.4** kwa upande wa uboreshaji wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Kinyerezi kupitia Gongolamboto hadi Mbagala.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi - MW 49.5**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi huu ambapo hadi kufikia Machi, 2026 utekelezaji kwa upande wa ujenzi wa kituo cha uzalishaji umeme ulikuwa umefikia **asilimia 23.73** ambapo kazi zilizokamilika ni pamoja na uchepushaji wa mto; uchimbaji wa njia za maji (*water ways*) na tenki la kupumulia (*surge tank*); uchimbaji wa nyumba ya mitambo *(power house*); ujenzi wa kambi za muda za mkandarasi; na usimikaji wa mtambo wa kusaga kokoto na kuchanganyia zege (*batching plant*). Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 54 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe, pamoja na kusambaza umeme katika vitongoji 18 vilivyomo ndani ya vijiji saba (7) vilivyopitiwa na mradi ambapo jumla ya wateja 750 zikiwemo shule, vituo vya afya na kaya wamenufaika na mradi huu.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zinazoendelea katika ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme ni pamoja na uchimbaji wa eneo la ujenzi wa tuta (*main dam*) na eneo la kituo cha kupokelea umeme (*switch yard*), ujenzi wa nyumba ya mitambo (*power house*), njia za maji (*water ways*), madaraja (*culverts*) kwenye barabara na kambi za kudumu na ofisi (*permanent camps*). Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 144.14** sawa na takriban **Shilingi bilioni 396.44**.

**(v) Ukarabati wa Mitambo katika Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya kuzalisha umeme katika Kituo cha Hale chenye uwezo wa kuzalisha Megawati 21 ambapo utekelezaji kwa upande wa *Lot 1* iliyohusisha uchimbaji wa handaki na ujenzi wa barabara imekamilika.

Aidha, *Lot 2* inayohusisha ujenzi wa jengo la kupokea umeme (*switchyard)*, njia ya kuchepusha umeme (*by pass line*), matengenezo ya jumba la mitambo (*power house civil works*), eneo la '*intake*', kituo cha kupoza umeme na nyumba ya mitambo umefikia **asilimia 75.95.** Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 21.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 58.31**.

**(vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87.8**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme chenye uwezo wa Megawati 87.8 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 38.7 kutoka Kakono hadi Kyaka, mkoani Kagera. Hadi kufikia Machi, 2026 Serikali kupitia TANESCO ilikuwa imekamilisha maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na kituo cha kupoza umeme pamoja na tathmini ya usanifu (*conceptual design*) ya ujenzi wa bwawa.

Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 308.38** sawa na takriban **Shilingi bilioni 848.16**.

**(vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuzalisha umeme wa Megawati 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhudji mkoani Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa. Ili kuimarisha kasi ya utekelezaji wa mradi huu, Serikali inakusudia kuutekeleza kwa ushirikiano na Sekta Binafsi kupitia utaratibu wa Ubia Baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP*).

**(viii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unalenga kuzalisha umeme wa Megawati 222 kwa kutumia maji ya mto Rumakali mkoani Njombe pamoja na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 65 kutoka kwenye mitambo ya uzalishaji wa umeme hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo mkoani Mbeya. Serikali kupitia TANESCO inaendelea kufanya maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya majadiliano na wadau mbalimbali walioonesha nia ya kutekeleza mradi kwa kushirikiana na TANESCO kupitia utaratibu wa PPP ili kuongeza kasi ya utekeleza wake.

**(ix) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Gesi Asilia wa Mtwara – MW 300**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kiasi cha Megawati 300 kwa kutumia gesi asilia mkoani Mtwara, ambapo hatua za awali za ulipaji wa fidia kiasi cha Shilingi milioni 500 zimetekelezwa, na taratibu za kuwezesha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliosalia katika vijiji vya Kisiwa na Namgogoli vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara zinaendelea. Aidha, Serikali kupitia TANESCO iliendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, ambapo katika kipindi hiki ilipeleka mtambo mwingine wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 20 na hivyo kuongeza uwezo wa uzalishaji wa umeme katika mikoa hiyo kufikia Megawati 77.90 kutoka Megawati 57.5 zilizokuwepo awali, ambapo mahitaji ya umeme katika mikoa hiyo ni Megawati 38.5.

**(x) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Upepo - MW 100 Kititimo Mkoani Singida**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ni moja ya miradi ya nishati jadidifu inayotarajiwa kuchangia katika kuongeza vyanzo mchanganyiko (*energy mix*) vya uzalishaji wa nishati nchini na hivyo kupunguza utegemezi katika vyanzo vya sasa vya mafuta.

Hadi Machi, 2026 taratibu zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kufanya Upembuzi Yakinifu na kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya TANESCO na Mwekezaji kwa ajili ya kutekeleza mradi.

**(xi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia Jua - MW 130 wa Zuzu Dodoma**

47. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu umeendelea katika kipindi hiki ambapo hadi Machi, 2026 Serikali kupitia TANESCO ilikuwa imekamilisha Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme jua wa Megawati 130 katika eneo la Zuzu mkoani Dodoma. Aidha, Serikali kupitia TANESCO imesaini Hati ya Makubaliano (MoU) na mwekezaji, Kampuni ya Mirambo Power Limited kwa ajili ya kuanza kuzalisha Megawati 15 za awali, ambapo hatua inayofuata ni kufanya upekuzi wa kina *(Due Diligence*) ili kujiridhisha na uwezo wa kampuni hiyo, kabla ya kuendelea na hatua za utekelezaji wa mradi.

**(xii) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua - MW 100 Same**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Sweden (*Swedfund*) inakusudia kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi wa kuzalisha umeme jua Megawati 100 katika eneo la Same mkoani Kilimanjaro, ikiwa ni hatua ya maandalizi ya kuzalisha umeme kupitia chanzo hicho. Aidha, hadi Machi, 2026 Serikali kupitia TANESCO ilikuwa katika hatua za mwisho za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu katika eneo hilo.

**B 1.2: MIRADI YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA UMEME**

**(i) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Bwawa la Julius Nyerere hadi Chalinze – kV 400 na Kituo cha Kupoza Umeme cha Chalinze**

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 160 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Chalinze mkoani Pwani pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambao kwa sasa upo katika hatua za uangalizi. Aidha, njia hiyo na kituo cha

kupoza umeme cha Chalinze vinatumika kusafirisha na kuingiza umeme unaozalishwa JNHPP katika Gridi ya Taifa na kuendelea kutumika nchini. Utekelezaji wa mradi huu umegharimu **Shilingi bilioni 158.1** fedha zilizotolewa na Serikali kwa **asilimia 100**.

**(ii) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma**

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze hadi Dodoma yenye urefu wa kilomita 345 na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 74.13**. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa misingi kwa ajili ya nguzo za kusafirishia umeme; ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Zuzu; na ukaguzi na usafirishaji wa vifaa vikiwemo nguzo, transfoma na *reactors.* Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha usafirishaji na usambazaji wa umeme unaozalishwa JNHPP na kuwezesha kuwafikia watumiaji wengi katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Kanda za Kati, Ziwa, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini. Utekelezaji wa mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 507.99.**

**(iii) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 616.5 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya Iringa, Kisada, Iganjo, Tunduma na Sumbawanga. Hadi Machi, 2026, utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 77.06**, na kazi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa vituo zinaendelea. Aidha, taratibu za kusafirisha vifaa vya mradi kutoka Bandari ya Dar es Salaam zikiwemo transfoma na *reactors* kwenda kwenye eneo la mradi zinaendelea. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 593.19** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.63.**

**(iv) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi – Mkuranga**

52. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 135.5 kutoka Chalinze kupitia Kinyerezi hadi Mkuranga. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Kinyerezi na Mkuranga pamoja na upanuzi wa kituo cha Chalinze. Hadi Machi, 2026 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 60.61**. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha mfumo wa usafirishaji wa umeme katika Gridi ya Taifa na pia kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa ajili ya uzalishaji katika maeneo ya viwanda wilayani Mkuranga. Utekelezaji wa mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 560.36.**

**(v) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Rufiji – Mkuranga**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO inatarajia kutekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka katika Bwawa la Julius Nyerere (Rufiji) hadi Mkuranga. Kazi zilizofanyika hadi Machi, 2026 ni pamoja na kukamilisha Hadidu za Rejea kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Athari kwa Mazingira *(Environmental Impact Assesment)*. Kutekelezwa kwa mradi huu kutawezesha kuwepo kwa njia mbadala ya kusafirisha umeme unaozalishwa JNHPP.

**(vi) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa – Singida - Shinyanga na kituo cha kupoza umeme cha Ibadakuli, Shinyanga. Hadi Machi, 2026 utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 48.8** na ujenzi unaendelea. Utekelezaji wa mradi huu unagharimu **Dola za Marekani milioni 80.62** sawa na takriban **Shilingi bilioni 221.73**.

**(vii) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa *(National Grid Stabilization Project)* – Gridi Imara**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Gridi Imara unatekelezwa na Serikali kupitia TANESCO kwa kutumia fedha za ndani ambao unalenga kuimarisha miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, mradi unahusisha pia ufungaji wa mitambo na vifaa vya kisasa, ubadilishaji wa nguzo za miti kwa kusimika nguzo za zege, ufungaji wa nyaya zenye uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa pamoja na transfoma. Utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 54** ambapo miradi saba (7) kati ya 27 imekamilika na utekelezaji kwa miradi mingine unaendelea. Miradi iliyokamilika ni:

a) Ujenzi wa njia ya kusambaza umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 60 kutoka Nyakanazi hadi Kakonko na kutoka Nyakanazi hadi Lusahunga;
b) Ujenzi wa njia ya kusambaza umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 16 inayounganisha kituo cha Nyakanazi, Bulyanhulu na Geita;
c) Mradi wa kuboresha njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Ubungo kupitia Chalinze hadi Hale kwa kubadilisha nyaya za umeme kutoka Megawati 80 hadi Megawati 150;
d) Mradi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme *(Automatic Voltage Regulator)* Songwe Mkwajuni na Mbangala;
e) Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita saba (7) kutoka Ilala hadi Kurasini kwa kutumia waya wa ardhini *(underground cable)*;
f) Ujenzi wa kituo cha kusambaza umeme *(switching station)* msongo wa kilovoti 33 katika eneo la Msigani lililopo Mbezi; na
g) Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia vituo vya Ipole na Inyonga.

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi 20 ya mradi huu iliyosalia ni kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.3.*

### (viii) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kupoza Umeme katika Kila Wilaya Nchini

56. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unaendelea kutekelezwa kupitia utekelezaji wa mradi wa Gridi Imara Awamu ya Kwanza ukilenga kuimarisha usambazaji na kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika kila eneo nchini kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na jamii. Utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya mradi wa Gridi Imara unahusisha Wilaya 15 ambapo utekelezaji umekamilika katika Wilaya za Mlele, Mpanda, Urambo na Sikonge. Aidha, utekelezaji unaendelea katika Wilaya za Uvinza, Rombo, Masasi, Ukerewe, Kibaha, Mkuranga, Tunduru, Bariadi, Handeni, Lushoto na Kilindi. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Shilingi bilioni 639.17.**

### (ix) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(Grid Rehabilitation and Upgrading Project - TTGRUP)*

57. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kukarabati na kuboresha vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini na unagharamiwa na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo (AFD) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika mafungu matatu kwa gharama ya **Euro milioni 70.37** sawa na takriban **Shilingi bilioni 222.59** kama ifuatavyo:

- Fungu la kwanza linahusisha ukarabati na maboresho ya vituo nane (8) vya kupoza umeme kwenye Gridi ya Taifa ambapo ukarabati na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Mlandizi, Same na Bukoba umefikia **asilimia 87**; ukarabati na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Mbeya, Tabora na Mufindi umefikia **asilimia 86**; na ukarabati na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Musoma na Mwanza umefikia **asilimia 73**. Aidha, kwa sasa kazi zinazoendelea ni kukamilisha ukarabati wa vituo pamoja na kufunga mfumo wa '*Automatic Generation*

*Control (AGC)*' kwenye vituo vya kuzalishia umeme wa gesi Kinyerezi I, Ubungo I, Ubungo II, na Tegeta na utekelezaji wake umefikia **asilimia 98.1**.

- Fungu la pili lilihusisha ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya mawasiliano katika njia za kusafirisha umeme za Kondoa – Babati – Mbulu – Karatu; Shinyanga – Mabuki – Mwanza – Bunda – Musoma; na Iringa – Mufindi – Makambako – Mbeya zilizopo katika Gridi ya Taifa ambapo utekelezaji wake ulikamilika mwezi Desemba, 2024.

- Fungu la tatu linahusisha ufungaji wa vifaa vinavyotumika kuendeshea na kuongozea mfumo wa Gridi ya Taifa (SCADA) ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 98.3.**

**(x) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

58. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 166.17 kutoka Benaco hadi Kyaka mkoani Kagera. Hadi Machi, 2026 Mkandarasi ameendelea na uwasilishaji wa vifaa vya ujenzi katika eneo la mradi pamoja na usanifu wa michoro ya mradi huo. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za ulipaji wa fidia ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya **Shilingi bilioni 1.6** zimelipwa kwa wananachi wanaopisha eneo la mradi wa njia ya kusafirisha umeme na **Shilingi milioni 351** zimelipwa kwa wananchi wanaopisha eneo la kituo cha kupoza umeme cha Benaco na taratibu za kukamilisha malipo ya fidia zinaendelea. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 57.62** sawa na takriban **Shilingi bilioni 61.58**.

**(xi) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Makutopora Hadi Tabora (SGR Lot 3) na kutoka Tabora hadi Isaka (SGR Lot 4) kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa

kilovoti 220 kutoka Makutopora hadi Tabora *(SGR Lot 3)* na kutoka Tabora hadi Isaka *(SGR Lot 4)* kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika katika *Lot 3* ni pamoja na Upembuzi Yakinifu na usanifu wa muundo dhana *(conceptual design);* na kuendelea na uandaaji wa Hadidu za Rejea kwa ajili ya taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi. Kwa upande wa *Lot 4* kazi iliyofanyika ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Reconnaissance Survey*). Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi katika maeneo hayo ili waweze kulipwa fidia.

**(xii) Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Mwanza Hadi Isaka kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR Lot 5)**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Mwanza hadi Isaka kwa ajili ya uendeshaji wa treni ya umeme. Hadi Machi, 2026 uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi ulikuwa umekamilika na Serikali inaendelea na malipo ya fidia ambapo **Shilingi bilioni 8** zimelipwa kwa wananchi wanaopisha mradi.

**(xiii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Sumbawanga Hadi Kigoma Kupitia Mpanda (Km 480) na Kituo cha Kupoza Umeme Mpanda**

61. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 480 kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Mpanda. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 372.5** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.02**. Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Maendeleo Afrika kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi huu.

**(xiv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 Kutoka Segera – Same – Lemugur (Kisongo) Arusha**

62. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Segera kupitia Same hadi Lemugur (Kisongo) Arusha. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA); na uthamini wa mali za wananchi wanaopisha eneo la mradi na taratibu za upatikanaji wa fedha za fidia zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Wadau wa Maendeleo ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 182** sawa na takriban **Shilingi bilioni 500.57**.

**(xv) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme *(Submarine Cables)* Msongo wa Kilovoti 220 Kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 49.95 kutoka Ununio – Dar es Salaam kwenda Unguja na msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa kilomita 87 kutoka Tanga kwenda Pemba kupitia chini ya Bahari (*submarine cables*). Aidha, mradi unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 109.2 kutoka Mkuranga hadi Mafia. Kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, usanifu wa awali wa mradi na tathmini ya mali za wananchi ambapo taratibu za malipo ya fidia zinaendelea kufanyika. Kwa sasa Serikali kupitia TANESCO ipo katika hatua za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa mradi. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 282.57** sawa na takriban **Shilingi bilioni 777.17**.

**(xvi) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Ibadakuli - Masaka)**

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha diplomasia ya uchumi nchi za Tanzania na Uganda zinakusudia kujenga njia ya

kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Ibadakuli (Tanzania) kwenda Masaka (Uganda). Ujenzi wa njia hiyo utatekelezwa sambamba na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Ibadakuli, Nyakanazi na Kyaka. Hadi Machi, 2026 zoezi la uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha eneo la mradi lilikuwa limekamilika. Aidha, kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na kutafuta fedha za kutekeleza mradi huu.

**(xvii) Mradi wa Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na Msongo wa Kilovoti 220 Segera – Tanga**

65. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera na msongo wa kilovoti 220 ya Segera – Tanga. Mradi unahusisha pia ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Segera na Tanga. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu, Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) pamoja na usanifu wa mradi. Aidha, taratibu za utafutaji fedha kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi zinaendelea. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 237** sawa na takriban **Shilingi bilioni 651.84**.

**(xviii) Mpango Kabambe wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Msongo wa Kilovoti 220 katika Majiji ya Mbeya, Arusha na Mwanza**

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inakusudia kuimarisha mfumo wa usambazaji wa umeme msongo wa kilovoti 220 katika majiji ya Mbeya, Arusha na Mwanza ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika utakaochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo. Aidha, Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya usambazaji umeme msongo wa kilovoti 220 katika majiji hayo umekamilika na taratibu za utafutaji wa fedha za utekelezaji wa mradi zinaendelea.

### (xix) Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma

67. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kuboresha na kuimarisha miundombinu ya usambazaji umeme katika Jiji la Dodoma, ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya umeme linalochochewa na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii na kuongezeka kwa idadi ya watu katika Jiji hili. Utekelezaji wa mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 150.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 412.83**. Hadi Machi, 2026 kazi zilizokamilika ni pamoja na Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika Jiji la Dodoma (*Dodoma ring circuit)*. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 kutoka Zuzu – Msalato – Ihumwa – Kikombo – Zuzu pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Msalato, Ihumwa na Kikombo.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inaendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme mkoani Dodoma kwa kubadilisha nguzo za miti na kuweka nguzo za zege kwenye njia mbalimbali za kusambaza umeme. Hadi Machi, 2026 jumla ya nguzo 3,105 zimebadilishwa sawa na **asilimia 98** ya lengo ambapo zoezi hilo linaendelea. Aidha, Serikali imekamilisha maboresho ya njia ya usambazaji umeme msongo wa kilovoti 11 kutoka mjini kati hadi Bungeni kwa kubadilisha nyaya zisizofunikwa kwa kuweka nyaya zilizofunikwa(*insulated conductors*).

### (xx) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma

69. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na usambazaji umeme katika vijiji 18 vilivyopo katika eneo la mradi. Aidha, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme umekamilika na ipo katika hatua ya uangalizi na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme umefikia **asilimia 45.15.**

Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 186.93** sawa na takriban **Shilingi bilioni 514.13**.

### (xxi) Utekelezaji wa Miradi Mingine na Matengenezo ya Mitambo

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANESCO iliendelea kufanya ukaguzi na matengenezo ya mitambo mbalimbali ya kuzalisha umeme ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini. Matengenezo ya mitambo iliyokamilika ni pamoja na Mtwara I (mitambo yote 13); Mtwara II (mtamboNa.16); Tegeta (mitambo yote mitano (5)); Ubungo I (mtambo Na. 2 na Na.12); Ubungo II (mtambo Na. 3) na Ubungo III (mitambo yote mitatu (3)). Aidha, matengenezo mengine yameendelea kufanyika katika kituo cha Kinyerezi I (mitambo yote nane (8)); Kinyerezi II (mitambo yote nane(8)); Somanga (mitambo yote mitatu (3)); Kidatu (mitambo Na.1 na Na.4); Mtera (Mitambo yote miwili (2)); New Pangani (mitambo yote miwili (2)) na Kihansi (mitambo yote mitatu (3)). Vilevile, matengenezo yamehusisha miundombinu ya kusafirisha umeme, ikiwa ni pamoja na kubadilisha nyaya za zamani na kuweka za kisasa zenye uwezo wa kubeba umeme mwingi katika njia za kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 za Same - Kiyungi na Hale – Same.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho ya miundombinu ya umeme yamefanyika pia katika vituo vya kupoza umeme kwa kuongeza transfoma katika maeneo mbalimbali vikiwemo vituo vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam (Chang'ombe na Mbagala), Dodoma (Dodoma Mjini), Kagera (Kasiga na Muleba), Mwanza (Mwanza South), Arusha (Njiro), Shinyanga (Ibadakuli), Lindi (Lindi Mjini na Mahumbika), Iringa (Mafinga), Tanga (Kange) na Pwani (Mlandizi). Aidha, Serikali inaendelea na maboresho ya vituo vingine katika maeneo mbalimbali nchini kama inavyoonekana katika *Kiambatisho Na.4*.

## B 1.3: UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MIKAKATI YA UENDELEZAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na utekelezaji wa mikakati na mipango mbalimbali ya uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu kama ifuatavyo:

### a) Mpango Mahususi wa Nishati wa Taifa

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati inaratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati *(National Energy Compact)* wa Miaka Mitano (2025 - 2030) ambao unajulikana kama *Mission 300*. Mpango huo unalenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa umeme kutoka asilimia 78.4 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2030; kuongeza kasi ya kuunganisha umeme nchini kutoka asilimia 46 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 75 mwaka 2030; kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika uzalishaji wa umeme kutoka asilimia 61.8 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 75 ifikapo mwaka 2030; kuongeza kiwango cha matumizi ya nishati safi ya kupikia kutoka asilimia 6.9 ya mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 75 mwaka 2030; na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika Sekta ya Nishati kwa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 4.39 sawa na takriban Shilingi trilioni 11.218 ifikapo mwaka 2030. Hadi Machi, 2026 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake zinazotekeleza Mpango huo imeandaa miradi inayolenga kutekeleza malengo ya Mpango huo, ambapo utekelezaji unaendelea. Aidha, mpango wa kusimamia utekelezaji umeandaliwa ili kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa.

### b) Mpango Kabambe wa Uendelezaji Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2024 (*Power System Master Plan Update 2024 - PSMP 2024*)

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imekamilisha mapitio ya Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Umeme wa Mwaka 2024 kwa kuhuisha Mpango wa Mwaka 2020 ili uendane na hali ya sasa na ya miaka 25 ijayo kuhusu sekta ndogo ya umeme. Hatua hii inatokana na kuendelea kuongezeka kwa kasi ya mahitaji ya umeme nchini,

ukuaji wa soko la umeme, maendeleo ya teknolojia na vipaumbele vya Serikali ili kuweza kufikia matarajio ya kitaifa yaliyobainishwa katika Dira 2050, ikiwemo kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa gharama nafuu kwa wananchi wote ifikapo 2050, ili kujenga uchumi wa viwanda na huduma za kijamii zilizo bora. Vilevile, Mpango umezingatia umuhimu wa kuongeza uwiano wa nishati safi (maji, jua, upepo, jotoardhi na nyuklia) sambamba na kupunguza utegemezi wa vyanzo visivyo endelevu na ambavyo siyo rafiki kwa mazingira ili kulinda mazingira na kuendana na malengo ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huo pia umebainisha umuhimu wa kuimarisha mahusiano ya kikanda katika uendelezaji wa Sekta ya Nishati kwa kubainisha miradi ya kipaumbele ili kuimarisha miundombinu ya Gridi ya Taifa na nchi za jirani hususan zilizopo katika Jumuiya za Kikanda za EAC na SADC. Vilevile, Mpango umebainisha mikakati ya kuimarisha ushirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi ya ndani na nje ya nchi katika ugharamiaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme.

**c) Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati *(Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap)***

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati imekamilisha uandaaji na kuanza kutekeleza Mkakati wa Nishati Jadidifu na Mpango wake wa Utekelezaji wa Mwaka 2024 - 2034. Mkakati huo pamoja na mambo mengine, unalenga kuimarisha uwezo wa kitaifa wa uzalishaji wa nishati jadidifu utakaoliwezesha Taifa kuwa na vyanzo mchanganyiko vya umeme unaoendana na mahitaji ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira.

**d) Mpango wa Utekelezaji wa Matumizi Bora ya Nishati *(Comprehensive Energy Efficiency Action Plan 2025- 2034)***

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati inakamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Matumizi Bora ya Nishati (2025 - 2034). Mpango huo utatumika kama nyenzo muhimu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati (2024 – 2034). Aidha, Mpango huo pamoja na mambo mengine umebainisha vipaumbele mbalimbali vitakavyotekelezwa ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya nishati, kuongeza ufanisi wa mitambo na vifaa, na kuimarisha usalama wa nishati kwa muda mrefu. Vilevile, Mpango kazi huo pia utajikita katika kuhamasisha Watanzania kutumia nishati kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia bora ili kupunguza gharama za matumizi, upotevu wa umeme na kutunza mazingira bila kupunguza uzalishaji au ubora wa huduma.

**e) Ushiriki katika Mkutano wa 30 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP30)**

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilishiriki katika Mkutano wa 30 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Conference of the Parties - COP 30)* uliofanyika tarehe 10 - 21 Novemba, 2025 Belem nchini Brazil. Ushiriki katika Mkutano huo ulilenga kuimarisha nafasi ya Tanzania katika maamuzi ya kimataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo kuhusu ufadhili wa miradi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuonesha mafanikio mbalimbali ambayo Nchi imeyapata katika uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi. Kwa ujumla, Wizara ilitumia Mkutano huo kama jukwaa la kimkakati katika jitihada za kuimarisha ushawishi katika mikakati ya kuendeleza miradi ya Sekta ya Nishati hususan inayolenga kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

**f) Ushiriki katika Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(International Atomic Energy Agency – IAEA)***

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki Mkutano Mkuu wa 69 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria kuanzia tarehe 15 hadi 19 Septemba, 2025. Mkutano huo ulihusisha Nchi Wanachama 180 kujadili hatua zilizofikiwa katika matumizi salama ya nishati ya nyuklia katika afya, kilimo na chakula. Tanzania imekuwa mwanachama wa IAEA tangu mwaka wa 1976, na tayari imesaini Mpango wa Nchi (CPF) wa mwaka 2023 hadi 2027 na Shirika hilo, unaotumika kama mwongozo wa ushirikiano wa kimkakati na kiufundi na IAEA, hususan katika kuendeleza na kukuza matumizi ya nishati ya nyuklia nchini. Kupitia Mkutano huo, Serikali ya Tanzania ilitumia nafasi yake ya uanachama kuelezea utayari wake wa kuanza kutumia nishati ya nyuklia kuzalisha umeme kwa kuzingatia miongozo, kanuni na sheria zilizowekwa na IAEA.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mkutano huo pia, Wizara ilifanya mikutano ya pembeni na Wadau mbalimbali wa nyuklia na kueleza lengo lake la kuzalisha umeme wa nyukilia. Maandalizi ya Mpango wa Tanzania kuanza kuzalisha umeme wa nyuklia yanaendelea, ambapo tayari uchambuzi umefanyika kuhusu masuala ya msingi ya kuzingatiwa ili kutekeleza azma hiyo, kuunda Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu utekelezaji wa Mpango huo pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam wa ndani katika ngazi mbalimbali.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika hilo la Kimataifa linakusudia kutuma Wataalam wake wa kiufundi ***(Mission for Integrated Nuclear Infrastructure Review)*** kwa ajili ya kufanya ukaguzi na mapitio ya miundombinu na matayarisho ya awali ili kutusaidia kufanya tathmini ya miundombinu iliyopo na kuona utayari wake katika uzalishaji wa umeme wa nyuklia kwa kutekeleza programu itakayohakikisha uzalishaji wa nishati hiyo unakuwa salama kwa binadamu na mazingira; wa uhakika na endelevu kwa kushirikisha wadau wote muhimu ikiwemo wanaohusika na udhibiti, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; na uwepo wa miundombinu wezeshi kama vile barabara na maji pamoja na

Sera na Mipango madhubuti itakayosaidia uandaaji na utekelezaji wa programu madhubuti ya kuzalisha umeme wa nyuklia. Ujumbe huo unatarajiwa kuwasili nchini katika kipindi cha mwaka 2026/27.

## B 1.4: UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO

### a) Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania *(TGDC)*

82. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TANESCO ya TGDC imeendelea kutekeleza miradi ya kuendeleza rasilimaliza joto ardhi nchiniu kiwemo mradi wa Ngozi uliopo mkoani Mbeya ambao unatarajiwa kuzalisha Megawati 70. Hadi Machi, 2026, TGDC ilikuwa imeanza uchorongaji wa kisima cha kwanza cha jotoardhi (NZB3) ili kuhakiki kiwango na ubora wa rasilimali ya jotoardhi, kukamilisha tafiti na uhakiki unaoendelea pamoja na ununuzi na usimikaji wa mitambo (*turbines*). Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 336** sawa na takriban **Shilingi bilioni 924.12**. Vilevile, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mshauri Mwelekezi atakayesimamia kuanza kwa uchorongaji wa visima katika mradi wa Kiejo-Mbaka uliopo mkoani Mbeya, kwa lengo la kuhakiki rasilimali ya jotoardhi katika eneo hilo.

### b) Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania *(TCPM)*

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TANESCO ya TCPM imekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza nguzo za zege kilichopo mkoani Tabora na kuanza uzalishaji wa nguzo hizo tarehe 18 Februari, 2026. Kukamilika kwa kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha nguzo 80 - 120 kwa siku ni mojawapo ya utatuzi wa kimkakati wa changamoto ya upatikanaji, usafirishaji na bei ya nguzo za zege hususan kwa mikoa ya Kanda za Magharibi, Ziwa na Kati. Vilevile, Serikali inakusudia kuanza ujenzi wa kiwanda cha pili mkoani Mbeya ambapo kwa sasa usanifu wa awali unaendelea. Pia, Serikali kupitia TCPM inaendelea kushirikiana na wazalishaji binafsi wa nguzo za zege kwa lengo la kuimarisha uzalishaji na usambazaji

wa nguzo hizo na hivyo kukabiliana na ongezeko la uhitaji wake katika maeneo mbalimbali nchini.

### c) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TANESCO ya ETDCO imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa umeme nchini. Hadi Machi, 2026 miradi iliyokuwa inaendelea kutekelezwa ni pamoja na:

i. Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji mkoani Mbeya ambao umefikia asilimia 83 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2027;

ii. Mradi wa usambazaji wa umeme katika maeneo ya Kilindi na Simanjiro ambao unahusisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji umeme katika maeneo ya makazi ya wananchi; na

iii. Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 220 ya Masasi – Mahumbika pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme, ambapo Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) pamoja na kuweka mipaka (*demarcation)* ya njia ya kusafirisha umeme vimekamilika na kazi ya usanifu (*design)* inaendelea. Gharama za mradi huu ni **Shilingi bilioni 210.02.**

### B 1.5: MIRADI YA NISHATI VIJIJINI

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza nishati vijijini, ikiwa ni pamoja na miradi ya kusambaza umeme vitongojini, mradi wa kufunga na kusambaza mifumo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua katika makazi yaliyo vijijini na maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa ikiwemo visiwa vya Tanzania Bara pamoja na ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatavyo:

**a) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili B *(Hamlet Eletrification Project – HEP IIB)***

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuhakikisha kuwa vitongoji vyote Tanzania Bara vinafikishiwa umeme ifikapo mwaka 2030/31. Ikiwa ni utekelezaji wa azma hiyo, tarehe 17 Januari, 2026 Serikali kupitia REA ilisaini Mikataba 30 na Kampuni 17 (za ndani 11 na za nje 6) kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi mahsusi wa kupeleka umeme katika Vitongoji 9,009 kwenye mikoa 25 (ukiondoa Dar es Salaam). Kwa sasa Wakandarasi wanaendelea na usanifu wa kina na kuandaa michoro katika maeneo ya mradi, ikiwa ni hatua za awali kabla ya kuagiza vifaa vya mradi na kuanza utekelezaji. Mradi huu unagharimu jumla ya **Shilingi trilioni 1.416** na unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa kati (kilovoti 33) zenye urefu wa kilomita 13,181; njia za msongo mdogo (kilovoti 0.4/0.23) zenye urefu wa kilomita 14,016; ufungaji wa transfoma 9,009 zenye uwezo wa kVA100 na kVA200; na kuunganisha wateja wa awali 290,300.

***a)* Mradi wa Kuunganisha Wateja Vitongojini – *Universal Hamlet Electrification and Last Mile Customers Connection***

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imeanza utekelezaji wa mradi wa kuongeza uunganishaji wa wateja katika vitongoji *(Universal Hamlet Electrification and Last Mile Customers Connection)* ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa Nishati wa Taifa *(National Energy Compact)* ulioridhiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika (*Mission 300*) mwezi Januari, 2025. Serikali kupitia REA imeanza utekelezaji wa mradi huu katika mikoa mitatu ya Pwani, Morogoro na Dodoma ambao unalenga kusambaza umeme katika jumla ya mitaa 279. Hadi Machi, 2026 taratibu za kuwapata Wakandarasi wa kutekeleza mradi huu zilikuwa zimekamilika na mikataba kusainiwa.

a) **Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili A – *(Hamlet Electrification Project – HEP IIA*)**

88. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kilomita 528 za njia za umeme msongo wa kati na kilomita 6,158 za njia za umeme msongo mdogo pamoja na kufunga transfoma 3,056 ili kufikisha umeme kwenye vitongoji 3,060 sawa na vitongoji 15 kwa kila Jimbo pamoja na kuunga wateja wa awali 101,106. Hadi Machi, 2026 njia za umeme za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 371, na njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 5,408 zilikuwa zimejengwa. Aidha, maeneo 2,089 na wateja wa awali 29,326 walikuwa wamefikishiwa huduma za umeme. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 80**.

a) **Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji vya Mikoa ya Songwe na Kigoma**

89. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kupeleka umeme katika vitongoji 667 katika mikoa ya Songwe (vitongoji 307) na Kigoma (vitongoji 360). Mradi unahusisha pia ujenzi wa njia za umeme msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 698; ujenzi wa njia za umeme msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,336; ufungaji wa transfoma 694 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 20,622. Hadi Machi, 2026 njia za umeme za msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 683, na njia za umeme msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,317 zilikuwa zimejengwa. Aidha, jumla ya vitongoji 661, Songwe (vitongoji 301) na Kigoma (vitongoji 360) vimeunganishwa na jumla ya wateja wa awali 10,523 wameunganishiwa umeme. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 97**.

a) **Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vijiji-Miji (*Peri Urban III*)**

90. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza umeme katika vijiji-miji, mitaa na vitongoji 516 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji katika mikoa nane (8) ambayo ni Geita, Kigoma, Kagera, Mbeya, Mtwara, Singida, Tabora na Tanga. Mradi pia unahusisha ujenzi wa njia za umeme wa msongo wa

kati zenye urefu wa kilomita 467; ujenzi wa njia za umeme wa msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 1,178; ufungwaji wa transfoma 484 pamoja na kuunganisha wateja wa awali 24,463. Hadi Machi, 2026 maeneo 511 yalikuwa yamefikiwa na umeme na wateja 16,620 kati ya 24,463 wameunganishiwa umeme. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia wastani wa **asilimia 97**.

**a) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Maeneo ya Migodi Midogo, Viwanda na Maeneo ya Kilimo katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya na Rukwa**

91. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa kilomita 1,396 za msongo wa kati na kilomita 1,010 za msongo mdogo pamoja na kufunga transfoma 621 ili kufikisha umeme katika migodi midogo, viwanda na maeneo ya kilimo 619 pamoja na wateja wa kawaida 13,011. Hadi Machi, 2026 ujenzi wa njia za kusambaza umeme wa msongo wa kati zenye urefu wa kilomita 1,396.42 na njia za msongo mdogo zenye urefu wa kilomita 987.15 zilikuwa zimejengwa. Aidha, maeneo 594 na wateja 6,869 walikuwa wamefikishiwa umeme ambapo kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 94**.

**a) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji vya Mkoa wa Lindi**

92. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ni mahsusi kwa ajili ya kusambaza umeme katika vitongoji vya Mkoa wa Lindi. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 352.45 za njia za umeme msongo wa kati na kilomita 430 za njia za umeme msongo mdogo pamoja na kufunga transfoma 230 ili kufikisha umeme katika vitongoji 230 na kuunga wateja wa awali 7,590.

Hadi Machi, 2026 mkandarasi alikuwa amesimika nguzo za msongo wa kati kilomita 304 kati ya kilomita 352.5 na kilomita 411 kati ya kilomita 429.9 za msongo mdogo, na kazi za uvutaji wa nyaya na ufungaji wa transfoma pamoja na uwashaji wa vitongoji zimeanza. Utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 46**.

**a) Mradi wa Kuwezesha Waendelezaji Binafsi wa Miradi ya Nishati katika Maeneo Yaliyo Mbali na Ambayo Hayajafikiwa na Gridi ya Taifa**

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa yanafikiwa na huduma za umeme, Serikali kupitia REA imewezesha waendelezaji binafsi kutekeleza miradi mbalimbali ya nishati jadidifu inayotokana na nguvu za jua, upepo, maji na tungamotaka katika maeneo ambayo yapo nje ya Gridi ya Taifa ikiwemo visiwani, kwa kuwapatia ruzuku na mikopo ya masharti nafuu. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa gridi ndogo na uunganishaji wateja na mifumo inayojitegemea ya umeme jua. Ruzuku zinazotolewa kwa waendelezaji binafsi zinahusu maandalizi ya miradi; ujenzi wa miradi; na ufadhili wa mradi wa nishati jadidifu kwa utaratibu wa malipo kwa matokeo. Aidha, Serikali kupitia REA inatoa mikopo ya riba nafuu kwa ajili ya uendelezaji wa miradi.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia programu hii miradi inayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

**(i) Mradi wa Kusambaza Mifumo ya Jua Inayojitegemea *(Solar Home System - SHS)* katika Makazi 20,000**

95. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha usambazaji na ufungaji wa mifumo ya jua inayojitegemea *(Solar Home System - SHS)* katika makazi 20,000 katika visiwa vidogo 143 vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 11** kupitia Mpango wa *Tanzania Rural Electrification Expansion Program - TREEP*. Aidha, Serikali kupitia REA ilisaini mikataba na watoa huduma sita (6) (Greenleaf Technology Solution Company Ltd, Trinity Solar Energy Ltd, L'S Solution Ltd, Rafiki Energy Ltd, JV: Star Media (T) Ltd & Kangala Engineering Co. Ltd pamoja na Volt Africa Limited) kwa ajili ya kutekeleza mafungu 17 ya mradi huo ambao watasambaza mifumo 20,000 ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya makazi 1,302 yamefungiwa mifumo na wananchi wanaendelea kupata huduma.

**(ii) Mradi wa Kuwezesha Upatikanaji Umeme kwa Matokeo Awamu ya Pili Kupitia Gridi Ndogo**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Malipo kwa Matokeo Awamu ya Pili (*Result Based Financing - RBF II)* ili kusambaza nishati katika maeneo ya vijijini. Mpango huu unafadhiliwa na Serikali za Sweden na Uingereza. Aidha, baada ya kukamilika kwa RBF I, Serikali kupitia REA ilitoa fursa kwa waendelezaji wa miradi ya umeme kupitia vyanzo vya nishati jadidifu kuomba ufadhili ambapo waendelezaji wanne (4) ambao ni Mwenga Hydro Limited (Mufindi), Luponde Hydro (Njombe), Volt Africa (Ukerewe) na Matembwe Village (Njombe) wamejitokeza kuwekeza katika miradi ya kuanzisha gridi ndogo au kuunga wateja wapya kwenye gridi ndogo zinazofanya kazi. Jumla ya gharama za miradi yote ni **Dola za Marekani milioni 8.5** sawa na takriban **Shilingi bilioni 23.39** na Serikali itachangia **Dola za Marekani milioni 3.56** sawa na takriban **Shilingi bilioni 9.79** ambapo wateja wa awali 6,063 katika vijiji 44 wataunganishiwa huduma za umeme.

**(iii) Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kusambaza Bidhaa za Mafuta ya Petroli Vijijini**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA inalenga kusogeza huduma ya bidhaa za mafuta ya petroli kwa wananchi katika maeneo ya vijijini kwa kutoa mikopo kwa waendelezaji wa vituo hivyo ili waweze kujenga vituo husika katika maeneo ya vijijini. Maeneo yanayolengwa ni yale yaliyopo umbali usiopungua kilomita saba (7) kutoka barabara za TANROADS na kusiwe na kituo kingine cha mafuta. Kiasi cha juu cha mkopo kinachotolewa ni **Shilingi 133,000,000.00** ambazo zitarejeshwa kwa kipindi kisichozidi miaka saba (7) kwa riba ya **asilimia 5**.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea kupokea maombi kutoka kwa waombaji, kuyachambua na kuyawasilisha Benki maombi yanayokidhi vigezo kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya kifedha. Jumla ya maombi 32 yamepokelewa katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ambapo maombi 11 yaliwasilishwa Benki kwa kuwa yalikidhi vigezo vilivyotolewa na REA. Aidha, Benki ya Azania

baada ya kupitia maombi hayo inaendelea na zoezi la utoaji wa mikopo kwa waendelezaji watatu (3) wa miradi waliokidhi vigezo vya kibenki vya kupata mikopo ya kuendeleza miradi hiyo. Serikali kupitia REA inaendelea kupokea maombi ya mikopo kutoka kwa waendelezaji.

### B 1.6: UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034) uliozinduliwa Mei, 2024. Lengo la Mkakati huo ni kuhakikisha kuwa angalau asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Ili kufikia lengo hilo, Mkakati umejikita katika kupunguza gharama za nishati, vifaa na majiko sanifu ya kupikia; kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia; na kuandaa, kuhuisha na kuoanisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo wezeshi ya kufanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Mkakati umejikita pia katika kuhamasisha uwekezaji katika nishati safi ya kupikia; kuongeza wigo wa tafiti na bunifu za teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia; na kuimarisha uelewa wa jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia. Kutokana na jitihada zinazotekelezwa, kiwango cha watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia kimeongezeka kutoka **asilimia 6.9** mwaka 2021 hadi kufikia **asilimia 28.6** ya watanzania wenye nishati safi ya kupikia mwaka 2025. Kazi zilizofanyika katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ni pamoja na:

#### a) Utoaji wa Elimu Kuhusu Umuhimu wa Nishati Safi ya Kupikia

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha wananchi katika maeneo ya mijini na vijijini kutumia nishati safi ya kupikia. Uhamasishaji huo umefanyika kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio na televisheni, mitandao ya kijamii, makongamano, maonesho,

warsha na mikutano ya hadhara. Aidha, ili kuimarisha utoaji wa elimu kwa wananchi, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo pamoja na Sekta Binafsi inaendelea na shughuli za uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi *(community outreach)* katika mikoa yote nchini.

**b) Ujenzi wa Miundombinu ya Kusambaza Gesi Asilia kwa Ajili ya Kupikia katika Mikoa ya Pwani na Lindi**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa na TPDC kwa kushirikiana na REA na unahusisha ujenzi wa mabomba ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa kilomita 44.4 pamoja na kuunganisha gesi asilia kwenye nyumba 1,000 katika maeneo yanayopitiwa na bomba hilo hususan kwa mikoa ya Lindi na Pwani. Hadi Machi, 2026 ujenzi wa kilomita 28 umekamilika na nyumba 471 pamoja na shule moja (1) zimeunganishiwa mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwa ajili ya kupikia katika eneo la Mnazi Mmoja – Lindi na nyumba 530 katika Mkoa wa Pwani eneo la Kisemvule – Mkuranga zimeunganishwa na miundombinu ya gesi asilia kwa ajili ya kupikia.

**c) Usambazaji wa Mitungi ya Gesi ya LPG (*LPG Starter Packs*)**

103. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huu unahusisha usambazaji wa mitungi 452,455 ya LPG ya kilo 6 pamoja na vichomeo *(burners*) na figa (*trivet*) kwa bei ya ruzuku ya **asilimia 50**. Hadi Machi, 2026 jumla ya mitungi 346,251 sawa na **asilimia 76.5** ya mitungi yote iliyo katika mpango huu imesambazwa kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

**d) Usambazaji wa Majiko Banifu kwa Bei ya Ruzuku**

104. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huu unahusisha usambazaji wa majiko banifu 200,000 katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa bei ya ruzuku kati ya asilimia 80 hadi asilimia 85. Gharama ya mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 6** sawa na takriban **Shilingi bilioni 16.50** kupitia mpango wa *Tanzania Rural Electrification Expansion Program – TREEP*. Hadi Machi, 2026 Serikali kupitia REA ilikuwa

imesambaza jumla ya majiko banifu 49,136 pamoja na majiko janja ya umeme (*induction cookers*) 7,292.

**e) Ufungaji wa Mifumo ya Nishati Safi ya Kupikia katika Taasisi Zinazohudumia Watu Zaidi ya 100**

105. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza mpango wa usambazaji wa nishati safi ya kupikia kwa taasisi kubwa zinazolisha zaidi ya watu 100 kwa siku nchini. Kipaumbele cha utekelezaji wa programu hii kimeanza kwa kuhakikisha taasisi za elimu, afya na huduma za kijamii zinapata suluhisho kwa kufungiwa miundombinu ya nishati safi ya kupikia. Kwa kuanzia, Serikali ilitekeleza programu hii katika taasisi za magereza, kambi za Jeshi la Kujenga Taifa, Shule za Sekondari na Chuo cha VETA Mtwara. Hadi Machi, 2026 jumla ya taasisi 1,350 zinazohudumia zaidi ya watu 100 kwa siku zimehamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

## B.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta hii inajumuisha mnyororo mzima wa thamani wa mafuta na gesi asilia; ikihusisha mkondo wa juu (utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia) na mkondo wa kati na chini (uchakataji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia). Aidha, sekta hii inahusisha pia ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ya usafirishaji, uhifadhi na biashara ya mafuta na gesi asilia. Katika mwaka 2025/26 Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuendeleza Sekta hii ambapo mafanikio mbalimbali yaliweza kupatikana.

### B.2.1 MIRADI YA UENDELEZAJI NA UZALISHAJI WA GESI ASILIA

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki uzalishaji wa gesi asilia uliendelea kwenye vitalu viwili (2) vya Mnazi Bay na Songo Songo ambavyo ndivyo vinavyozalisha nishati hiyo kwa sasa. Aidha, hatua zilichukuliwa katika uendelezaji wa vitalu vya gesi asilia ambavyo tayari kuna ugunduzi vya Ruvuma (Ntorya) pamoja na vilivyopo baharini (Kitalu Na. 1, 2 na 4) kwa ajili ya mradi wa LNG. Hatua ya utekelezaji ni kama ifuatavyo:

### a) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Mnazi Bay

108. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa gesi asilia katika kitalu hiki kilichopo katika Mkoa wa Mtwara uliendelea ambapo wastani wa futi za ujazo bilioni (bcf) 23.60, sawa na wastani wa futi za ujazo milioni 110 kwa siku (mmscfd) zilizalishwa. Utekelezaji wa mpango wa kuchoronga visima vitatu (viwili vya uzalishaji [MB-5 na MS-2] na kimoja cha utafutaji [KASA-1]) umeendelea. Hadi Machi 2026, uchorongaji wa kisima kimoja (MB-5) cha uzalishaji ulikamilika na sasa uzalishaji wa majaribio unaendelea katika kisima hicho. Aidha, uchorongaji wa kisima cha pili (MS-2) umefikia asilimia 40 na utakamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2026. Ukamilishaji wa shughuli za uchorongaji wa visima vyote vitatu unatarajiwa kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kwa kiasi cha futi za ujazo milioni 45 hadi 55 kwa siku.

### b) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Songo Songo

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha uzalishaji wa gesi asilia cha Songo Songo kimeendelea na uzalishaji wa wastani wa futi za ujazo bilioni (bcf) 17.9 sawa na futi za ujazo milioni 84.7 kwa siku (mmscfd) kulingana na mahitaji. Aidha, kufuatia leseni ya kitalu hiki kufikia ukomo mwezi Oktoba, 2026 Serikali inaendelea kufanya majadiliano na Mwekezaji kwa lengo la kuhuisha muda wa leseni kwa kipindi cha pili cha uendelezaji wa gesi asilia katika kitalu hiki.

### c) Kitalu cha Ruvuma (Eneo la Ntorya)

110. ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya uzalishaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma kilichopo eneo la Ntorya mkoani Mtwara yanaendelea. Kazi zilizofanyika hadi Machi, 2026 ni pamoja na kuanza ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia lenye urefu wa kilomita 34.20 kutoka Ntorya hadi Kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba. Gharama za ujenzi wa bomba hiloni **Shilingi bilioni 106** ambapo kwa sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 37**. Aidha, maandalizi ya uchorongaji wa kisima cha uzalishaji cha Chikumbi-1 yanaendelea. Vilevile, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya majaribio ya uzalishaji wa kisima cha Ntorya-2 pamoja na marekebisho ya kisima cha Ntorya-1 zinaendelea.

111. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026 ambapo kukamilika kwake kutawezesha uzalishaji wa gesi asilia kwa kuanzia na kiasi cha futi za ujazo milioni 40 hadi 60 kwa siku (mmscfd) na kuongezeka hadi kufikia futi za ujazo milioni 140 kwa siku pindi uendelezaji zaidi utakapokamilika.

**d) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)***

112. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu namba 1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu cha bahari ili kuwa kimiminika kwa ajili ya kuuzwa katika masoko ya kimataifa na matumizi ya ndani ya nchi. Hadi Machi, 2026 Serikali na wawekezaji wa mradi wameendelea na majadiliano katika maeneo mbalimbali ya mradi huo ambapo makubaliano yamefikiwa katika maeneo ya kibiashara na kikodi. Kwa sasa majadiliano hayo yapo katika hatua za ukamilishwaji wa masuala ya kisheria kwa pande zote mbili za majadiliano ambapo kwa upande wa Serikali suala hilo linaratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, Serikali imekwishatwaa eneo la mradi baada ya kukamilika kwa taratibu za ulipaji wa fidia kwa wananchi na pia imeendelea kutekeleza miradi ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) kwa kushirikiana na wabia wa mradi, ikiwemo ujenzi wa Shule ya Msingi Likong'o mkoani Lindi.

**B.2.2 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC iliendelea na utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vinne (4) vya kimkakati kama ifuatavyo:

**a) Kitalu cha Eyasi – Wembere**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu hiki kipo kwenye Bonde la Ufa la Afrika Mashariki, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania katika mikoa ya Arusha, Manyara, Shinyanga, Simiyu, Singida na Tabora. Hadi Machi, 2026 kazi za mradi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D za

urefu wa kilomita 484.70. Aidha, kazi za uchukuaji wa taarifa za mitetemo aina ya 2D zenye urefu wa kilomita 914 zinaendelea na hadi sasa zimefikia **asilimia 67.72** ya utekelezaji. Pia, uchakataji wa taarifa za mitetemo kilomita 1,174.70 umeshaanza na unaendelea (zaidi ya kilomita 690 zimeshaanza kufanyiwa kazi). Matokeo ya tathmini ya taarifa hizi zinazokusanywa yatawezesha kufahamu eneo lenye mashapo yanayohifadhi mafuta, hivyo kuwezesha uchorongaji wa kisima cha utafiti katika eneo hilo. Vilevile, Serikali kupitia TPDC inaendelea kumtafuta Mbia mwenye uzoefu, utaalamu na fedha wa kushirikiana naye katika kuendeleza kazi za kitalu hiki.

**b) Kitalu cha Lindi – Mtwara**

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Lindi–Mtwara ni eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia lililopo katika Halmashauri za Wilaya ya Mtwara na Mtama. Hadi Machi, 2026 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na zoezi la uchukuaji wa taarifa za mitetemo katika mfumo wa 3D kwa eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 736 ambao umefikia **asilimia 31.6**. Aidha, kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii inaendelea na imefikia **asilimia 90**; na kazi za utambuzi na uthamini wa mali zitakazoathiriwa na ujenzi wa njia na mkuza wa pembezoni zimefikia **asilimia 52**. Vilevile, maandalizi ya uchakataji na tafsiri ya taarifa ili kubaini maeneo yenye mashapo yanayofaa kwa ajili ya kuchoronga visima vya utafutaji yanaendelea. Kazi hizi za awali hadi kukamilika kwake, zitagharimu takriban **Shilingi bilioni 86.56**.

**c) Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini**

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini kipo baharini, Kusini Mashariki mwa Tanzania. Hadi Machi, 2026 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kufanyika kwa stadi na tafiti za awali katika kitalu, mapitio ya taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D (*3D seismic data*) zenye urefu wa kilomita za mraba 131 zilizofanyika hapo awali na kubaini viashiria vya uwepo wa mafuta au gesi asilia katika kitalu hicho. Aidha, mpango wa uchorongaji kisima (*drilling plan*) umekamilika. Serikali kupitia TPDC inaendelea na taratibu za kumtafuta mbia wa kimkakati mwenye uzoefu,

utaalamu na fedha za uchorongaji wa kisima cha utafutaji ili kushirikiana naye katika uendelezaji wa kitalu hiki.

**d) Kitalu cha Songo Songo Magharibi**

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Kitalu cha Songo Songo Magharibi kipo katika kina kifupi cha bahari, Magharibi mwa Kitalu cha Uzalishaji cha Songo Songo. Hadi Machi, 2026 kazi zilizoendelea kufanyika ni pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) kwa ajili ya ukusanyaji wa taarifa za mitetemo. Aidha, taratibu za kumpata mkandarasi wa kukusanya taarifa za mitetemo zenye urefu wa kilomita 240 zimekamilika na pia Serikali kupitia TPDC inaendelea na utafutaji wa mbia wa kimkakati mwenye uzoefu na utaalamu wa kiteknolojia na fedha atakayeshirikiana na TPDC katika hatua ya kuchoronga kisima cha utafutaji.

**MIRADI YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA**

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi ya usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia ndani na nje ya nchi, ambapo hatua za utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

**a) Usambazajiwa Gesi Asiliakatika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani umekuwa ukifanyika kwa njia mbili ambazo ni kwa njia ya mabomba na katika mfumo wa gesi iliyoshindiliwa (CNG) na kusafirishwa kwa kutumia malori *(CNG tube trailer trucks)*. Hadi Machi, 2026 Serikali kupitia TPDC ilikamilisha uunganishaji wa mfumo wa mawasiliano (SCADA) kati ya kituo kikuu cha CNG kilichopo eneo la Mlimani City (*mother station*) na vituo vya kusambazia gesi asilia (*daughter stations*) vilivyopo Muhimbili na Kibaha. Aidha, Serikali kupitia TPDC imeendelea na uendeshaji wa kituo kikuu cha CNG cha Mlimani City pamoja na kuuza gesi asilia kupitia kituo hicho chenye uwezo wa kuhudumia hadi **bajaji 2,000**, **magari madogo 1,200**, **mabasi**

**makubwa 60** pamoja na magari ya kusafirishia gesi iliyoshindiliwa ***(CNG tube trailers)*** **10** kwa siku.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na bei za mafuta zisizotabirika kwenye Soko la Dunia, Serikali ya Awamu ya Sita pamoja na mambo mengine, imeendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa matumizi ya CNG katika vyombo vya moto yanaendelea kuimarika nchini. Ikiwa ni utekelezaji wa azma hiyo, Serikali kupitia TPDC kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imewezesha ujenzi wa vituo 18 vya CNG ambavyo vinaendelea kutoa huduma, na vituo vingine nane (8) vipo katika hatua za ujenzi.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** uwepo wa miundombinu hiyo umeendelea kuhamasisha wamiliki wa vyombo vya usafiri kuongeza mifumo ya matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo hivyo. Hadi sasa kuna jumla ya vyombo vya usafiri na usafirishaji zaidi ya 20,000 vinavyotumia gesi asilia vikihusisha magari madogo, magari makubwa, malori, mabasi ya abiria (yakiwemo ya mwendokasi) na bajaji. Vilevile, hadi Machi, 2026 zaidi ya kampuni binafsi 86 za ndani na nje ya nchi zilikuwa zimepewa idhini ya kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia nchini.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuchochea matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri, Serikali ilishaondoa kodi ya ushuru wa forodha kwa magari yanayoagizwa yakiwa yameshafungwa mfumo wa matumizi ya gesi asilia na inaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya punguzo la kodi kwenye vifaa vinavyotumika kwenye uongezaji wa mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye magari. Aidha, kupitia uhamasishaji mkubwa wa matumizi ya gesi asilia uliofanywa na Serikali, Sekta Binafsi imeendelea kuwekeza katika Karakana za kufunga mfumo wa matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri ambapo hadi sasa kuna jumla ya karakana 13.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Ongezeko la karakana hizi limesaidia kupungua kwa gharama za uwekaji wa mifumo ya matumizi ya gesi asilia kwenye magari ambapo kwa sasa, kwa magari madogo gharama ni kati ya Shilingi **1,500,000** hadi **1,800,000** ikilinganishwa na awali ilipokuwa Shilingi **2,000,000** hadi

**2,500,000.** Katika hatua nyingine, Serikali kupitia TPDC imejenga Karakana na kuikabidhi kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo pamoja na kazi ya kuweka mifumo ya matumizi ya gesi kwenye vyombo vya usafiri, Karakana hiyo imekuwa sehemu ya mafunzo ya kuandaa vijana watakaoongeza wataalam wa eneo hili watakaoweza kujiajiri na kuongeza Karakana binafsi nyingi zaidi.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa usambazaji wa CNG unafikia maeneo mengi ya nchi, Serikali kupitia TPDC ipo katika hatua za ununuzi wa vituo vitano (5) vya CNG vinavyohamishika (*Mobile CNG stations*) ambapo utengenezaji wa vituo hivyo unaendelea. Vituo hivyo vinatarajiwa kuwekwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma kwa awamu ya kwanza na mikoa ya Arusha, Tanga na Kilimanjaro kwa awamu ya pili. Aidha, katika kuhakikisha kuwa gesi asilia inafika maeneo mbalimbali ya nchi yaliyo mbali na miundombinu ya gesi kwa sasa, Serikali kupitia TPDC imeingia makubaliano ya awali na kampuni binafsi sita (6) kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya Min – LNG nchini ili kuhakikisha matumizi ya gesi asilia yanafika maeneo mengi ya nchi.

**b) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia Kuanzia Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani**

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imeanza maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani, ili kuimarisha usambazaji wa gesi asilia katika maeneo ya kongani ya viwanda Zegereni – Kibaha, viwanda vya Mlandizi, Bandari kavu ya Kwala na Chalinze. Hadi Machi, 2026 Mshauri Mwelekezi alikuwa anaendelea na kazi ya upembuzi wa kina wa njia ya kupitisha bomba hilo. Gharama za utekelezaji wa mradi huu zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 300.**

**c) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania hadi Uganda**

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda ziliendelea na

maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania hadi Uganda. Hadi Machi, 2026, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba baina ya Tanzania na Uganda *(Bilateral Agreement)* wa namna ya utekelezaji wa mradi katika hatua ya Upembuzi Yakinifu; na kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu huo.

**d) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia Kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Mombasa (Kenya)**

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Kenya ziliendelea na maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu, ambapo kazi zilizotekelezwa ni pamoja na Wataalamu kuendelea kuboresha nyaraka za maridhiano kwa ajili ya kuidhinisha nyaraka muhimu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayefanya Upembuzi Yakinifu wa mradi.

**B.2.4 MIRADI YA KUHIFADHI, KUSAFIRISHA NA BIASHARA YA MAFUTA**

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuhifadhi na kusafirisha mafuta nchini kama ifuatavyo:

**a) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani (Tanga) Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*)**

129. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu umeendelea katika mwaka 2025/26 ambapo kwa ujumla umefikia **asilimia 82.6**. Aidha, kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kambi 14 zinazotumika kwa ajili ya wafanyakazi na hifadhi ya mabomba. Vilevile, ujenzi wa vituo vinne (4) vya kuongeza msukumo wa mafuta *(pump stations)* na vituo viwili (2) vya kupunguza msukumo wa mafuta *(pressure reduction stations)* umekamilika kwa **asilimia 74.60.** Pia, ujenzi wa miundombinu ya matenki ya kupokelea na kuhifadhi mafuta katika eneo la Chongoleani, Tanga umekamilika kwa **asilimia 89.20** na ujenzi wa miundombinu ya kituo cha kupokea

mafuta (*terminal*) umekamilika kwa **asilimia 60.90**. Aidha, ujenzi wa Ghati pamoja na miundombinu ya kupakilia mafuta ghafi kwenye meli (*Load off Facility - LoF*) umefikia **asilimia 88.10;** na kiwanda cha kuweka mifumo ya upashaji na utunzaji joto (*Thermal Insulation System - (TIS) plant*) katika Kijiji cha Sojo, Wilaya ya Nzega kimekamilisha kazi kwa mabomba yote ya mradi yenye urefu wa kilomita 1,462. Gharama za utekelezaji wa mradi huu ni **Dola za Marekani bilioni 5.65** sawa na takriban **Shilingi trilioni 15.54.**

**b) Mradi wa Uanzishwaji wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*)**

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika miaka ya karibuni Dunia imeshuhudia migogoro ya kisiasa, vita na changamoto za kiusalama, hususan katika kanda za nchi zinazozalisha mafuta ya petroli kwa wingi duniani. Hali hiyo imekuwa ikiathiri mnyororo wa upatikanaji wa bidhaa hizo kwa nchi mbalimbali, ikiwemo Tanzania na kusababisha bei za bidhaa hizo kuongezeka na hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii katika nchi husika. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inakusudia kujenga kituo kikubwa cha kupokea na kuhifadhi mafuta jijini Dar es Salaam ili kuendelea kuhakikisha usalama na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za petroli nchini pamoja na nchi jirani *(petroleum hub)*. Aidha, Serikali imekamilisha andiko la mradi wa uanzishaji wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta (SPR) na inaendelea na uboreshaji wa nyaraka mbalimbali za kisheria zitakazowezesha uanzishwaji na uendeshaji wa hifadhi ya mafuta ya kimkakati.

**c) Mradi wa Ukarabati wa Tenki Namba 8 Kigamboni**

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imekamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ukarabati wa Tenki Na. 8 ambapo majadiliano na mkandarasi huyo yamekamilika. Aidha, Mshauri Mwelekezi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira zitokanazo na ukarabati wa Tenki hilo amekamilisha kazi hiyo na TPDC imepata cheti cha Mazingira toka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Vilevile, zabuni ya kumpata

mkandarasi atakayefanya kazi ya kuondoa mabaki ya mafuta ghafi (*sludge disposal*) imekamilika.

**d) Ushiriki wa TPDC katika Biashara ya Mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*)**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 TPDC imeendelea kushiriki katika zabuni za kila mwezi za uagizaji wa mafuta kupitia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS)*. Aidha, TPDC ilishinda zabuni sita (6) na kuingiza nchini tani za ujazo 609,668.39 za mafuta ya dizeli kupitia mfumo huo.

**e) Mradi wa Bomba Jipya la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Tanzania hadi Zambia (New TAZAMA)**

133. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es Salaam - Tanzania hadi Ndola – Zambia lenye urefu wa kilomita 1,710. Kulingana na makadirio ya mwanzo, bomba hili litakuwa na uwezo wa kusafirisha angalau tani milioni tano (5) kwa mwaka. Bomba hili pia litakuwa na matoleo matatu (3) kwa upande wa Tanzania katika maeneo ya Morogoro, Makambako na Songwe. Aidha, kutakuwepo na matoleo mawili (2) kwa upande wa nchi ya Zambia katika maeneo ya Mpika na Serenje. Lengo la kujenga bomba hili ni kukidhi mahitaji ya sasa na baadaye ya usafirishaji wa bidhaa za mafuta kwa nchi za Tanzania, Zambia na nchi za jirani zikiwemo DRC na Malawi. Hadi Machi, 2026 Upembuzi Yakinifu ulikuwa umekamilika na maandalizi ya utekelezaji wa mradi yanaendelea.

**B.2.5 MRADI WA USIMAMIZI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA RASILIMALI ZA ASILI NCHINI**

134. ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Desemba, 2025 Serikali ilikamilisha utekelezaji wa mradi huu uliolenga kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali kusimamia rasilimali za asili zilizopo nchini kwa njia ya mafunzo na ununuzi wa vifaa. Mradi huu ulianza kutekelezwa Juni, 2017 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB).

Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 29.54** sawa na **Shilingi bilioni 64.8** ambapo AfDB imechangia **Dola za Marekani milioni 26.59** sawa na **Shilingi bilioni 61.85** na Serikali ya Tanzania itachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na **Shilingi bilioni 6.86**. Taasisi zilizonufaika na mradi huu ni pamoja na Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, TPDC, TPA, PURA, ZURA, EWURA, NEEC, TRA na ZRB.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizotekelezwa hadi kukamilika kwa mradi ni pamoja na: kukamilisha uundaji wa mfumo wa uondoshaji shehena mipakani kwa Tanzania Bara na Zanzibar; ununuzi na usimikaji wa midaki (*X Ray Portal Scanner*) miwili katika Bandari ya Dar es Salaam ikiwemo vifaa vya kuhodhi mfumo wa dirisha la pamoja la kieletroniki; uhuishaji wa Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Model Production Sharing Agreement - MPSA*) kupitia PURA; uanzishaji wa vituo vya kujengea wananchi uwezo chini ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC); na kuwajengea uwezo wataalamu wa Serikali kupitia mafunzo ya muda mfupi na mrefu kuhusu masuala ya mafuta na gesi.

**B.2.6 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMPUNI TANZU ZA TPDC**

**a) TANOIL Investments Limited (TANOIL)**

136. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TPDC ya TANOIL Investments Limited imeendelea kusimamia biashara ya uuzaji wa mafuta kama kampuni ya kununua na kuuza mafuta (*Oil Marketing Company - OMC*) ambapo hadi Machi, 2026 imefanikiwa kuuza lita za ujazo 12,033,500 kwa bidhaa za petroli na dizeli. Aidha, ili kutanua wigo wa biashara, TANOIL inakamilisha taratibu za kuanzisha biashara ya vilainishi na uuzaji wa gesi ya LPG ambapo Upembuzi Yakinifu na Mpango wa Biashara hiyo vimekamilika.

**b) GAS Company (T) Limited (GASCO)**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni tanzu ya TPDC ya GASCO imeendelea kusimamia kwa ufanisi uendeshaji, matengenezo na ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia nchini

ambapo hadi Machi, 2026 Kampuni hiyo imeendelea kuendesha kwa ufanisi kituo kikubwa cha CNG kilichopo Mlimani City – Dar es Salaam; kushiriki na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya vituo vinne (4) vya CNG vinavyomilikiwa na kampuni binafsi; na kuendelea kusimamia uendeshaji wa mitambo ya kuchakata na kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

### B.3 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SEKTA YA NISHATI KUPITIA PURA NA EWURA

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliendelea kutekeleza jukumu la udhibiti wa shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli kupitia Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) pamoja na udhibiti wa mkondo wa kati na chini (usafirishaji, uhifadhi na usambazaji) kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ili kuhakikisha shughuli za Sekta ya Nishati zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo pamoja na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

#### B.3.1 MAMLAKA YA UDHIBITI MKONDO WA JUU WA PETROLI (PURA)

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA imeendelea kutekeleza jukumu la usimamizi na udhibiti wa shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Katika kipindi cha hadi Machi, 2026, PURA imesimamia uzalishaji wa gesi asilia katika vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo ambapo uzalishaji umeendelea kuwa wa uhakika kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini. Aidha, katika kipindi hicho, usimamizi wa shughuli za uchorongaji wa visima vitatu (3), viwili (2) vya uzalishaji na kimoja (1) cha utafutaji katika Kitalu cha Mnazi Bay uliendelea. Kwa sasa uchorongaji wa kisima kimoja cha uzalishaji umekamilika na uzalishaji wa majaribio unaendelea. PURA inaendelea kusimamia ukamilishaji wa uchorongaji wa visima viwili (2) vilivyosalia. Sambamba na hilo, PURA inaendelea kusimamia shughuli za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika Vitalu vya Eyasi – Wembere na Lindi – Mtwara ambapo kazi za uchukuaji wa data za mitetemo zinaendelea.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** PURA imeendelea pia kufanya uhakiki, udhibiti na ukaguzi wa gharama na mapato katika mikataba hai ya Ugawanaji Mapato (PSA) kati ya Serikali na Wawekezaji 11 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2026 ukaguzi wa gharama za mwaka 2023 na 2024 ulikamilika. Tangu Mamlaka imeanza kuhakiki mikataba hiyo mwaka 2017, Serikali imeweza kuokoa jumla ya **Shilingi bilioni 322** kutoka katika madai ya wawekezaji na kurudishwa kwenye Mfuko wa Ugawanaji Mapato kati ya Serikali na Wawekezaji hao.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na shughuli hizo, Serikali kupitia PURA imeendelea kutangaza fursa za uwekezaji katika shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli nchini kupitia makongamano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ya mafuta na gesi asilia. Hadi kufikia Machi, 2026, PURA imeshiriki katika makongamano ya Kimataifa ya mafuta na gesi asilia mawili (2) yaliyofanyika Afrika Kusini na Ghana. Lengo la kuhamasisha uwekezaji huo ni kutoa fursa kwa wawekezaji katika maandalizi ya duru ya tano ya kunadi vitalu.

### B.3.2 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

142. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kupitia EWURA ilitekeleza majukumu mbalimbali ya kiudhibiti kama ifuatavyo:

#### a) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Kati na Chini wa Gesi Asilia

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia shughuli za udhibiti katika Mkondo wa Kati na Chini wa gesi asilia kwa kufanya kaguzi katika miundombinu iliyopo katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Dar es Salaam. Miundombinu hiyo ni ya uchakataji minne (4), usafirishaji miwili (2), mtandao wa usambazaji wenye urefu wa kilomita 243 na vituo 18 vya kujazia gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) kwenye magari. Hadi Machi, 2026, jumla ya kaguzi 68 zilifanyika katika miundombinu hiyo zikijumuisha kaguzi 50 katika miundombinu ya usambazaji na vituo vya CNG na kaguzi 18 katika miundombinu ya uchakataji na usafirishaji wa

gesi asilia. Miundombinu iliyokaguliwa ilikidhi viwango vya ubora unaotakiwa.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026 EWURA ilitoa vibali 9 vya ujenzi wa vituo vya CNG katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Ruvuma. Katika Mkoa wa Dar es Salaam vibali vya ujenzi saba (7) vilitolewa katika maeneo ya Mbezi Beach, Mbagala, Kigamboni, Buguruni, Mwenge, Kinyerezi na Gongolamboto. Aidha, katika Mkoa wa Morogoro kibali kimoja (1) kimetolewa katika eneo la Msamvu na Mkoa wa Ruvuma kibali kimoja (1) kimetolewa katika Wilaya ya Tunduru. Vilevile, EWURA imetoa vibali viwili (2) vya ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia iliyoshindiliwa *(CNG receiving facility)* kwa viwanda vilivyopo Kibaha mkoani Pwani.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** EWURA ilitoa jumla ya vibali saba (7) vya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha na kusafirisha gesi asilia kwa kampuni binafsi na TPDC, kati ya hivyo vibali vinne (4) ni vya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha gesi asilia kwenye viwanda, taasisi, migahawa ya chakula na majumbani, viwili (2) kwa ajili ya ujenzi wa mabomba ya kuunganisha gesi asilia kwenye vituo vya CNG na kimoja (1) ni cha ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Ntorya mpaka Madimba. Sambamba na vibali hivyo, EWURA ilitoa jumla ya leseni 17 ambapo tisa (9) ni za uendeshaji wa vituo vya CNG, saba (7) za usafirishaji wa CNG na moja (1) ni leseni ya usambazaji wa gesi asilia kwa mkoa wa Pwani. Mchanganuo wa leseni na vibali vilivyotolewa hadi Machi, 2026 ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5.

***Jedwali Na. 5:* Mchanganuo wa Leseni na Vibali vya Ujenzi Vilivyotolewa kwa ajili ya Ujenzi na Uendeshaji wa Miundombinu ya Gesi Asilia**

| Na. | Aina ya leseni/kibali | Idadi | Maeneo |
|---|---|---|---|
| 1. | Vibali vya ujenzi wa vituo vya CNG | 9 | Dar es Salaam, Morogoro na Ruvuma |
| 2. | Vibali vya ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi asilia iliyoshindiliwa | 2 | Pwani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Vibali vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenye vituo vya CNG | 2 | Dar es Salaam |
| 4. | Vibali vya ujenzi wa mabomba ya kupeleka gesi asilia kwenda kwenye viwanda, taasisi, migahawa ya chakula na majumbani | 4 | Dar es Salaam na Pwani |
| 5. | Kibalicha ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutokaNtorya mpaka Madimba | 1 | Mtwara |
| 6. | Leseni za uendeshaji wa vituo vya CNG | 9 | Dar es Salaam |
| 7. | Leseni za usafirishaji wa CNG (CNG Supply licence) | 7 | Pwani na Dar es Salaam |
| 8. | Leseni ya usambazaji wa gesi asilia mkoa wa Pwani (Distriubution License) – TPDC | 1 | Pwani |
| **Jumla** | | **35** | |

Chanzo: **EWURA**

146. ***Mheshimiwa Spika***, utoaji wa vibali na leseni umeendelea kuongezeka kila mwaka ambapo hadi Machi, 2026 EWURA ilitoa jumla ya leseni 18 za uendeshaji wa vituo vya CNG. Hatua hii inaonesha mwitikio mkubwa wa ushiriki wa sekta binafsi katika mnyororo wa usambazaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo usafirishaji, viwandani na katika taasisi. Kufuatia mwamko huo, Serikali itaendelea kuimarisha na kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuchochea kasi ya ushiriki wa

sekta binafsi katika usambazaji wa gesi asilia hususan katika mikoa ya kimkakati kama vile Morogoro, Dodoma, Mbeya na Tanga. Nitumie fursa hii kuendelea kutoa wito kwa sekta binafsi kuchangamkia fursa za uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia nchini, kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi katika kutumia nishati hiyo kwa matumizi mbalimbali, ikiwemo katika vyombo vya moto.

**b) Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Bidhaa za Mafuta ya Petroli**

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia Mkondo wa Kati na Chini unaohusisha shughuli za mafuta na gesi, ili kuhakikisha upatikanaji wa uhakika na usalama wa bidhaa za mafuta nchini pamoja na ubora wa miundombinu yake. Usimamizi huo umefanyika kwa kutoa vibali vya ujenzi wa mindombinu, leseni za biashara pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali. Aidha, hadi Machi, 2026, EWURA ilitoa jumla ya **leseni 636** kwa ajili ya biashara mbalimbali katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi kama inavyofafanuliwa katika Jedwali Na.6.

***Jedwali Na.6:*** **Leseni za Biashara ya Mafuta Zilizotolewa Kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026**

| Aina ya Leseni | Mpya | Zilizohuishwa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kituo cha Mafuta Mijini | 177 | 267 | **444** |
| Kituo cha Mafuta Vijijini | 49 | 30 | **79** |
| Ghala la kuhifadhia Mafuta | 1 | 4 | **5** |
| Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi | 16 | 13 | **29** |
| Usambazaji wa gesi ya LPG | 21 | 4 | **25** |
| Uuzaji Jumla wa gesi ya LPG | 1 | 2 | **3** |
| Uuzaji Jumla wa Mafuta | 36 | 3 | **39** |
| Uuzaji Jumla wa Vilainishi | 8 | 4 | **12** |
| **Jumla Kuu** | **309** | **327** | **636** |

Chanzo: **EWURA**

148. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026 EWURA ilitoa vibali 288 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta ambapo vibali 137 vilikuwa kwa ajili ya mjini na vibali 143 kwa vituo vya vijijini. Aidha, vibali vitano (5) vilitolewa kwa ajili ya miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa watumiaji wakubwa kama vile viwanda na migodi, kibali kimoja (1) kwa ajili ya maghala ya kuhifadhi na kujaza LPG, kibali kimoja (1) kwa ajili ya maghala ya kuhifadhi mafuta na kibali kimoja (1) kwa ajili ya kiwanda cha kutengeneza vilainishi.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na EWURA ni kusimamia taratibu za uagizaji na usambazaji wa mafuta nchini; kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ambapo jumla ya sampuli 648 kutoka katika vituo na maghala ya mafuta zilipimwa ubora na sampuli 608 sawa na **asilimia 93.83** zilikidhi viwango stahiki vya ubora. Vituo 22 ambavyo vilikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango vilichukuliwa hatua za kisheria ikiwemo kufungiwa na kutozwa faini. Aidha, EWURA ilikagua ubora wa miundombinu 544 ya mafuta ambapo miundombinu 473 sawa na **asilimia 86.95** ilikidhi viwango vya ubora ikiwemo vigezo vya masuala ya afya, usalama na mazingira. Wamiliki wa vituo 95 ambavyo havikukidhi viwango walielekezwa kufanya marekebisho.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA ilifanya marekebisho ya Kanuni mbili (2) ili kuimarisha usambazaji wa mafuta na gesi ya LPG nchini. Kanuni zilizofanyiwa marekebisho ni *The Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages), (Amendments) Rules, 2025* ili kujumuisha matumizi ya vituo vya mafuta vya mfumo wa kontena *(containarised petrol station)* kwa lengo la kuchochea uwekezaji wa vituo vya gharama nafuu vijijini na kuongeza upatikanaji wa mafuta. Aidha, *The Petroleum (Liquefied Petroleum Gas Operations) (Amendment) Rules, 2025* zilifanyiwa marekebisho ili kuboresha masharti ya utoaji leseni na kujumuisha matumizi ya gesi ya LPG kwenye magari *(Autogas)* ili kuongeza chaguo la nishati mbalimbali kwa watumiaji na kupunguza athari kwa mazingira.

**c) Utekelezaji wa Programu ya Uwekaji Vinasaba katika Mafuta**

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA imeendelea kutekeleza programu ya uwekaji vinasaba katika mafuta ili kudhibiti ubora na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki ya kodi. Hadi Machi, 2026 kiasi cha lita bilioni 1.51 za mafuta ya petroli, lita bilioni 2.02 za mafuta ya dizeli na lita milioni 2.80 za mafuta ya taa ziliwekewa vinasaba. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 14** na **asilimia 10** kwa mafuta ya petroli na dizeli mtawalia na pungufu ya **asilimia 40** kwa mafuta ya taa yaliyowekewa vinasaba kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25.


152. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile EWURA ilifanya ukaguzi na kupima vinasaba katika vituo 672, ambapo vituo 50 sawa na asilimia 7.44 vilikutwa na mafuta yasiyokidhi viwango na kuchukuliwa hatua za kisheria, ikiwemo kufungiwa, kutozwa faini na kupelekwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kulipa kodi walizokwepa. Pia, EWURA ilifanya ufuatiliaji wa usambazaji wa mafuta na kubaini vituo vitatu (3) vilikuwa vimeficha mafuta kwa jili ya kusubiri bei mpya. Hatua za kisheria zilichukuliwa kwa vituo hivyo ikiwemo kufungiwa na kutozwa faini.

**d) Matumizi ya Mafuta Nchini**

153. ***Mheshimiwa Spika,*** wastani wa matumizi ya mafuta kwa siku nchini umeendelea kuongezeka na kufikia lita milioni 6.28 kwa petroli na lita milioni 8.42 kwa dizeli ikilinganishwa na lita milioni 5.45 kwa petroli na lita milioni 7.61 kwa dizeli zilizotumika kila siku kwa mwaka 2024/25. Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 15.23** kwa petroli na **asilimia 10.64** kwa dizeli ambalo linaashiria kuendelea kuongezeka kwa mahitaji ya mafuta kutokana na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii nchini zikiwemo kilimo, ujenzi, usafirishaji, migodi na maendeleo ya viwanda.


154. ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa wastani wa matumizi ya mafuta ya petroli na dizeli kwa mwezi hadi kufikia Machi, 2026 ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na.1 na Kielelezo Na. 2.

***Kielelezo Na.1*: Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Petroli (Lita) kwa Mwezi, Mwaka 2024/25 na 2025/26**





Chanzo: **EWURA**

***Kielelezo Na.2:* Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Dizeli (Lita) kwa Mwezi, Mwaka 2024/25 na 2025/26**




155. ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutokana na juhudi za Serikali zinazoendelea katika kuunganisha umeme vijijini na kwenye vitongoji pamoja na matumizi ya taa zinazotumia nishati ya jua. Matumizi ya mafuta ya taa yameendelea kupungua kutoka wastani wa lita 19,185 kwa siku mwaka 2024/25 hadi lita 11,628 kwa siku mwaka 2025/26. Kielelezo Na.3 kinaonesha mwenendo wa matumizi ya mafuta ya taa kwa mwaka 2024/25 na 2025/26.

***Kielelezo Na.3:* Mwenendo wa Wastani wa Matumizi ya Mafuta ya Taa (Lita) kwa Siku, Mwaka**




**2024/25 na 2025/26**

Chanzo : **EWURA**

### B.3.3 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA

156. ***Mheshimiwa Spika,*** bei za mafuta katika soko la dunia ziliendelea kushuka ambapo kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026 bei ya mafuta ghafi ilishuka kwa **asilimia 14** na kufika wastani wa **Dola za Marekani 66** kwa pipa ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 76** kwa pipa kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Hata hivyo, bei hizo zimeanza kuongezeka kutokana na vita inayoendelea Mashariki ya Kati. Jedwali Na.7 linaonesha mwenendo wa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia.

***Jedwali Na.7*: Mwenendo wa Bei ya Mafuta Ghafi katika Mwaka 2024/25 na 2025/26 (Dola za Marekani kwa Pipa)**

| Mwezi | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|
| Julai | 84 | 71 |
| Agosti | 79 | 68 |
| Septemba | 73 | 67 |
| Oktoba | 75 | 65 |
| Novemba | 73 | 63 |
| Desemba | 73 | 61 |


| | | |
|---|---|---|
| Januari | 78 | 63 |
| Februari | 75 | 67 |
| Machi | 71 | 102 |
| **Wastani** | **76** | **70** |
| Badiliko | | **- 8%** |

Chanzo**: EWURA**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** mwenendo wa bei za mafuta ghafi katika Soko la Dunia ulisababisha kushuka kwa bei za mafuta yaliyosafishwa kuanzia mwezi Julai, 2025 hadi Februari, 2026. Hata hivyo, kuanzia mwezi Machi, 2026 bei hizo zimeanza kuongezeka kwa kasi kufuatia uwepo wa vita katika nchi za Mashariki ya Kati. Athari za vita zimesababisha kufungwa kwa mlango wa bahari wa Hormuz ambapo meli nyingi za mafuta zinatumia mlango huo na hivyo kusitisha usafirishaji wa mafuta kwenda nchi mbalimbali.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia zilikuwa na wastani wa **Dola za Marekani 679.60** kwa tani ya petroli, **Dola za Marekani 715.27** kwa tani ya dizeli na **Dola za Marekani 757.11** kwa tani ya mafuta ya taa na ndege ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 687.64** kwa tani ya mafuta ya petroli, **Dola za Marekani 660.90** kwa tani ya dizeli na **Dola za Marekani 694.48** kwa tani ya mafuta ya taa na ndege katika kipindi kama hicho mwaka 2024/25. Mabadiliko haya ni sawa na punguzo la **asilimia moja** kwa mafuta ya petroli, ongezeko la **asilimia 8** kwenye mafuta ya dizeli na ongezeko la **asilimia 9** kwenye mafuta ya taa na ndege. Kielelezo Na. 4 kinaonesha mwenendo wa bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia kati ya Julai, 2025 na Machi, 2026.

***Kielelezo Na.4:* Mwenendo wa Bei za Mafuta Yaliyosafishwa katika Soko la Dunia katika Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 (USD kwa Tani)**




Chanzo: **EWURA**


159. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia vita inayoendelea katika nchi za Mashariki ya Kati bei za mafuta zimeendelea kupanda katika Soko la Dunia kwa **asilimia 69.12** kwa mafuta ya petroli, **asilimia 104.30** kwa mafuta ya dizeli na **asilimia 115.83** kwa mafuta ya taa na ndege kati ya mwezi Februari na Machi, 2026.

## B.3.4 MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

160. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA iliendelea kutoa bei kikomo za bidhaa za mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya taa kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazosimamia ukokotoaji wa bei za mafuta. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026, EWURA imetangaza bei za mafuta ya petroli, dizeli na taa ambazo ni stahimilivu. Bei hizo zilishuka mfululizo *(continous decreasing trend)* kuanzia Septemba hadi Desemba, 2025 ambapo ilichangiwa na kupungua kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia (*FOB price*) na kushuka kwa wastani wa gharama za kubadilisha fedha za kigeni (*applicable exchange rate*). Hata hivyo, bei zilianza kupanda kuanzia mwezi Januari, 2026 hadi Machi, 2026, hii ni kutokana na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia na kupanda kwa gharama za kubadilisha fedha za kigeni.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** wastani wa bei za mafuta nchini hadi Machi, 2026 zimeendelea kushuka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Mathalani, kwa Mkoa wa Dar es Salaam bei za mafuta kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 zilishuka kwa wastani wa **asilimia 4.0** kwa mafuta ya petroli, **asilimia 2** kwa mafuta ya dizeli na **asilimia 1** kwa mafuta ya taa na ndege, ambapo wastani wa bei ya petroli kwa lita ilikuwa **Shilingi 2,838**, dizeli **Shilingi 2,791** na mafuta ya taa **Shilingi 2,827** ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta hayo kwa kipindi cha mwaka 2024/25 ambapo zilikuwa petroli **Shilingi 2,957**, dizeli **Shilingi 2,845** na mafuta ya taa **Shilingi 2,842** kwa lita. Kielelezo Na. 5. kinaonesha ulinganifu wa wastani wa bei za mafuta nchini mwaka 2024/25 na 2025/26.

***Kielelezo Na. 5*: Wastani wa Bei za Rejareja Nchini (TZS/Lita) Mwaka 2024/25 na 2025/26**




Chanzo: **EWURA**

## B.3.5 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SHUGHULI ZA UMEME

162. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi, 2026 Serikali kupitia EWURA ilikuwa imetoa leseni tatu (3) kwa kampuni za kuzalisha umeme kiasi cha **Megawati 48.72** kwa ajili ya matumizi binafsi na leseni sita (6) za muda mfupi kwa kampuni zinazotarajia kuzalisha umeme kiasi cha **Megawati 29.55**. Aidha, EWURA iliidhinisha mikataba minne (4) ya kuuziana umeme kati ya TANESCO na wazalishaji binafsi ya jumla ya **Megawati 19.9** na hivyo kufanya umeme unaotarajiwa kuongezeka kupitia mikataba na leseni hizo kufikia jumla ya **Megawati 98.17** kama inavyoonekana katika


*Kiambatisho Na.5A na 5B*. Vilevile, hadi Machi, 2026 jumla ya **leseni 1,002** za mafundi umeme zilitolewa. Utoaji wa leseni hizo umewezesha kuwapata mafundi wenye elimu na ujuzi wa ufungaji wa mifumo bora na salama ya umeme kwenye majengo ya wananchi ikiwemo maeneo ya vijijini.

## B.4 HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA NCHINI

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutumia Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) katika uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli nchini tangu ulipoanza kutumika rasmi mwezi Januari, 2012. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya zabuni 83 zilitangazwa kwa njia ya ushindani wa kimataifa kwa kigezo cha gharama ndogo za uletaji wa mafuta nchini (*premium*). Aidha, kati ya zabuni 10 hadi 12 zilishindanishwa kila mwezi ambapo wazabuni tisa (9) hadi 10 ikiwemo TPDC walishiriki katika zabuni hizo.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya lita bilioni 5.84 za bidhaa za mafuta ya petroli ziliagizwa ambapo petroli ilikuwa lita bilioni 1.63, dizeli lita bilioni 3.94 na mafuta ya taa/ndege lita milioni 260 katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026. Kati ya mafuta hayo yaliyoagizwa katika kipindi husika, lita bilioni 2.56 sawa na **asilimia 43.83** yalikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 3.28 sawa na **asilimia 56.16** yalikuwa kwa ajili ya nchi jirani. Aidha, bidhaa hizo ziliagizwa na kupokelewa kupitia Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Kielelezo Na. 6 kinaonesha jumla ya kiasi cha bidhaa za mafuta kilichoagizwa kwa mgawanyo wa kila aina ya mafuta kwa kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026.


***Kielelezo Na. 6:* Mchanganuo wa Bidhaa za Mafuta zilizoagizwa kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026**




Chanzo: **PBPA**

165. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ufanisi wa mfumo wa BPS hali ya upatikanaji wa mafuta imeendelea kuwa imara na kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa mafuta katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, ufanisi wa mfumo huo umewezesha nchi jirani kuendelea kuutumia katika uagizaji wa mafuta kupitia bandari zilizopo nchini. Kielelezo Na.7 kinaonesha jumla ya kiasi cha mafuta kilichoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani na nchi jirani.

***Kielelezo Na.7* : Kiasi cha Mafuta Kilichoagizwa kwa ajili ya Matumizi ya Ndani na Nchi Jirani kuanzia Julai, 2025 hadi Machi, 2026**




Chanzo: **PBPA**

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutumia miundombinu ya Kampuni ya TIPER kama kituo cha kupokea mafuta kwa pamoja (*Single Receiving Terminal - SRT*). Kituo hicho kina uwezo wa kupokea meli mbili (2) hadi tatu (3) za mafuta ya dizeli kwa mwezi ambapo kila meli ina ujazo wa hadi lita milioni 120. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) inaendelea na ujenzi wa maghala mapya ya kupokelea mafuta kwa pamoja (SRT) katika eneo la Kigamboni ambapo mwezi Machi, 2026 Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi. Ujenzi wa miundombinu hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2027 na utasaidia kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli (*demurrage*) kwa kuongeza ufanisi wa upakuaji mafuta kuendana na muda unaotakiwa kimataifa (chini ya saa 72 kwa meli kubwa na saa 36 kwa meli za kati).

167. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia PBPA imeendelea kuongeza ufanisi wa usimamizi wa upakuaji mafuta kutoka kwenye meli kwenda kwenye hifadhi za kampuni za mafuta kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (SCADA). Hatua hii imeimarisha udhibiti wa upotevu wa mafuta wakati wa upakuaji wa mafuta hayo kutoka kwenye meli. Mfumo huu unasoma kiasi cha mafuta yanayopita katika mita (*flowmeter*) za Serikali zilizopo Kurasini (KOJ), Kigamboni (SBM), Tanga na Mtwara na kulinganisha kiasi hicho na mafuta yanayopita mita za kampuni za mafuta na kupokelewa kwenye maghala ya kuhifadhi mafuta. Uwepo wa mfumo huu umepunguza upotevu wa mafuta kutoka **asilimia 0.5** kabla ya mfumo hadi **asilimia 0.1** baada ya mfumo huo.

## B.5 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI NA USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

168. ***Mheshimiwa Spika,*** Watanzania wameendelea kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii zilizopo katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia kupitia shughuli zinazotekelezwa. Jitihada mbalimbali zinafanyika ikiwa ni pamoja na kuboresha na kusimamia miongozo na kanuni zinazosimamia ushirikishwaji *(local content)* na urejeshaji kwa jamii (CSR) katika miradi ya mafuta na gesi asilia nchini. Jitihada hizo ni pamoja na Serikali kuendelea kuhakikisha kuwa Kampuni zilizowekeza katika

shughuli za mafuta na gesi asilia zinatoa kipaumbele cha ajira kwa wazawa na zinawajibika kuishirikisha jamii husika ipasavyo katika kuibua na kutekeleza miradi kwenye jamii husika.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa wazawa na urejeshaji kwa wananchi kwenye miradi mbalimbali ya mafuta na gesi asilia unaendelea kuongezeka, ambapo hadi Machi, 2026 kampuni za kitanzania 186 zilisajiliwa na kufikia jumla ya kampuni 2,535 zenye sifa ya utoaji wa huduma mbalimbali ikiwa ni pamoja na afya, fedha, chakula, ulinzi, mafuta ya kuendesha mitambo na ukarabati wa miundombinu ya gesi asilia. Aidha, urejeshaji kwa jamii unaendelea kuimarika hususan katika utekelezaji wa miradi ya elimu, afya, maji, usafirishaji na upatikanaji wa nishati. Kampuni hizo pamoja na kampuni zinazotoa huduma zimefaidika kwa kupata kandarasi na kutoa huduma zenye thamani ya zaidi ya **Shilingi trilioni 1.325** ambapo fedha hizo zimeingia kwenye mzunguko wa uchumi wa nchi.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya watanzania 110 wamepata ajira katika shughuli mbalimbali katika sekta ikiwemo shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi-Wembere na Lindi-Mtwara, uendelezaji na uzalishaji katika vitalu vya Mnazi Bay, Songo Songo na Ruvuma (eneo la Ntorya). Shughuli hizi zimewezesha idadi ya ajira kuongezeka na kufikia 335 kutoka 225 Machi, 2025, ambapo ongezeko limechagizwa na kuongezeka kwa ujuzi na uwezo wa wataalamu wa ndani.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mkondo wa kati na chini ikiwemo utekelezaji wa mradi wa EACOP, hadi Machi, 2026 jumla ya watanzania 2,431 wenye ujuzi wa chini na kati wameajiriwa katika fani mbalimbali za uhandisi (ujenzi, mitambo, umeme), usimamizi wa mazingira na usalama, maendeleo ya jamii na nyinginezo. Vilevile, mafunzo mbalimbali ya kuimarisha uwezo katika teknolojia ya ujenzi na usimamizi wa mitambo ya mafuta na gesi yameendelea kutolewa kupitia mradi wa EACOP na kuwezesha idadi ya ajira kufikia 9,194 katika mradi huo hadi sasa. Aidha, EACOP inashirikiana na Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) Moshi kuhaulisha teknolojia kwa makundi mbalimbali kwa vijana ili kuwaimarisha katika kazi

mbalimbali. Kupitia programu hiyo jumla ya vijana 120 wamepatiwa mafunzo ya kuendesha shughuli za mradi mara utakapokamilika.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu pia umezalisha jumla ya ajira 11,155 ambapo ajira 8,756 zimetolewa kwa watanzania na 2,399 zimetolewa kwa raia wa kigeni. Vilevile, jumla ya bidhaa na huduma zenye thamani ya **Dola za Marekani milioni141.68** sawa na takriban **Shilingi bilioni 389.63** zilinunuliwa kutoka soko la ndani.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji inaendelea kuwajibika kwa jamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma na uhusiano kati ya wawekezaji na jamii husika katika eneo la mradi. Hadi Machi, 2026 miradi mbalimbali ilikuwa inaendelea kutekelezwa, ikiwa ni pamoja na:

(i) Ujenzi wa Shule ya Msingi Likong'o katika Manispaa ya Lindi ambapo utekelezaji wake umefikia **asilimia 81**; na

(ii) Ujenzi wa kivuko kitakachounganisha Songo Songo na Kilwa kinachojengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 5.2** na kinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026.

## B.6 UIMARISHAJI UTENDAJI KAZI NA UTOAJI WA HUDUMA

174. ***Mheshimiwa Spika***, kuwepo kwa tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kunahitaji pamoja na mambo mengine, nguvu kazi inayokidhi mahitaji na yenye utaalamu, sifa na uzoefu stahiki. Wizara na Taasisi zake ina jumla ya watumishi 8,078 wa kada mbalimbali ambao wanatekeleza majukumu kwa mujibu wa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa Umma. Serikali katika mwaka 2025/26 iliwapeleka mafunzo watumishi 2,120, kuwapandisha vyeo watumishi 1,614 pamoja na kuajiri watumishi 38. Vilevile, Taasisi ya TANESCO inatarajia kuajiri watumishi 1,940 kabla ya kumalizika kwa mwaka 2025/26. Aidha, ili kuhakikisha kunakuwepo na mazingira bora ya utekelezaji wa majukumu,

Wizara ilikamilisha ujenzi wa jengo la ofisi Mtumba na imehamia katika jengo hilo.

175. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia iliendelea kusimamia masuala mbalimbali ya Kiutumishi na Utawala ili kuimarisha tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake na utoaji wa huduma, ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi, kusimamia mfumo wa upimaji utendaji kazi Serikalini, kusimamia mifumo ya kielekroniki inayotumika katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na kushughulikia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora, magonjwa sugu na yasiyoambukizwa na UKIMWI katika eneo la kazi.

## B.7 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2025/26

176. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 Wizara imepata mafanikio mbalimbali katika utekelezaji wa Bajeti ikiwa ni pamoja na:

a. Kuimarika kwa uzalishaji wa umeme ambapo uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme umeongezeka na kufikia Megawati 4,522.54 ikilinganishwa na Megawati 4,031.71 zilizokuwepo mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 12.17**;

b. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua uliopo Kishapu, mkoani Shinyanga, inayohusisha uzalishaji wa Megawati 50 na hivyo kuiwezesha nchi yetu kuweka historia ya kuanza uzalishaji wa kiwango kikubwa cha umeme utokanao na jua. Aidha, hatua hii imeongeza wigo wa vyanzo vya kuzalisha umeme nchini ambavyo ni safi na rafiki wa mazingira;

c. Kiwanda cha kutengeneza nguzo za zege kilichojengwa na TCPM mkoani Tabora chenye uwezo wa kuzalisha wastani wa nguzo 120 kwa siku kimekamilika, na hivyo kuongeza wigo na uhakika wa upatikanaji wa nguzo za

zege kwa ajili ya usafirishaji na usambazaji wa umeme hususan katika mkoa wa Tabora na mikoa ya jirani;

d. Miundombinu ya kusafirisha umeme nchini imeongezeka na kufikia jumla ya kilomita 8,500.38, ikilinganishwa na kilomita 7,809.67 zilizokuwa zimefikiwa Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 9**. Aidha, miundombinu ya kusambaza umeme, imeongezeka na kufikia kilomita 240,229.56 ikilinganishwa na kilomita 200,266.25 zilizofikiwa mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 20**;

e. Serikali imekamilisha kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa na hivyo kuimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa huo pamoja na kuipunguzia TANESCO gharama za uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta katika mkoa huo, ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 68.4** zimeweza kuokolewa. Aidha, utekelezaji wa mradi wa njia ya kusafirisha umeme ya Ibadakuli - Simiyu pamoja na kituo cha kupoza umeme cha Simiyu unaendelea, ambapo kukamilika kwake kutaimarisha upatikanaji wa umeme katika mkoa wa Simiyu;

f. Serikali imeanza kutekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme katika Vitongoji 9,009 ambao utakamilika katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Hatua hii pamoja na miradi inayoendelea kutekelezwa ya kupeleka umeme vitongojini, itawezesha vitongoji 50,453 sawa na **asilimia 78.4** ya vitongoji vyote 64,359 vya Tanzania Bara kufikishiwa huduma ya umeme ifikapo mwaka 2028, hatua ambayo itachochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii vitongojini pamoja na utoaji wa huduma bora katika maeneo hayo;

g. Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa umeme nchini (*accesibility*) kutoka wastani wa **asilimia 78.4** mwaka 2020 na kufikia wastani wa **asilimia 85.5**. Aidha, kiwango cha wananchi waliounganishiwa umeme nchini (*connectivity*) kimeongezeka kutoka **asilimia 37.7** mwaka 2020hadi **asilimia 52.1**;

h. Matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini yameendelea kuimarika kutoka **asilimia 6.9** mwaka 2021 hadi kufikia **asilimia 28.6** ya watanzania wenye nishati safi ya kupikia mwaka 2025. Kwa namna ya kipekee, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongea Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono na uongozi wake uliotuwezesha kuwa na mwelekeo huu wa kitaifa wa kuhakikisha wananchi wetu wanatumia nishati safi ya kupikia, agenda ambayo imempa heshima ya kuwa kinara wa nishati safi ya kupikia Barani Afrika na kimataifa;

i. Vituo vya kujazia gesi asilia katika vyombo vya moto *(CNG filling stations)* vimeongezeka na kufikia vituo 18 mwezi Machi, 2026 ikilinganishwa na vituo tisa (9) mwezi Aprili, 2025. Aidha, kampuni binafsi zaidi ya 86 za ndani na nje ya nchi zimepewa idhini ya kuwekeza katika miradi ya gesi asilia kama mbadala wa mafuta ya petroli na dizeli kwenye vyombo vya moto;

j. Utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani (Tanga) Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP)* umefikia **asilimia 82.60**, ikilinganishwa na **asilimia 55**, mwezi Aprili, 2025; na

k. Nchi imeendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli (petroli, dizeli na taa) na bei za bidhaa hizo zimeendelea kuwa himilivu na hivyo kutoathiri shughuli za uzalishaji, usafirishaji na utoaji wa huduma kwa jamii.

## B.8 CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

177. ***Mheshimiwa Spika***, miradi ya nishati inahitaji uwekezaji mkubwa *(capital intensive)* ili kupata matokeo yanayotarajiwa, hatua ambayo pamoja na jitihada kubwa za uwekezaji zinazofanywa na Serikali, bado ni muhimu kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi katika kufanikisha utekelezaji wake. Hivyo, mwelekeo wa

Wizara ni kuendelea kushirikiana na wadau hawa ili mchango wao uweze kutumika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya nishati ambayo ipo katika hatua za maandalizi.

## C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2026/27

178. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/26, na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho katika Sekta ya Nishati, napenda sasa kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/27.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** usimamizi na uendelezaji wa Sekta ya Nishati pamoja na mambo mengine, unaongozwa na Sera, Mikakati, Mipango na Malengo mbalimbali ya kisekta, kitaifa na kimataifa. Hivyo, katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2026/27, Wizara imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050); Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV), 2026/27–2030/31; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa Kufungua Rasmi Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dodoma, tarehe 14 Novemba 2025; na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/27;

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imezingatia pia maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati nyingine za Bunge uliotolewa kwa nyakati tofauti; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Nne 2023-2030 (*National Anti - Corruption Strategy and Action Plan Phase Four (NACSAP IV) 2023-2030*); Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 - 2034); Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 (*National Energy Compact 2025 - 2030*) ulioidhinishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika kuhusu Nishati; Sera, Sheria, Mikakati na Programu mbalimbali za Kisekta na Taifa pamoja na maoni ya wadau wa kisekta; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) ya Mwaka 2030 na Mikataba na

Itifaki mbalimbali za Kimataifa zinazohusu Sekta ya Nishati ambazo Tanzania ni Mwanachama.

181. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha na kuendeleza Sekta ya Nishati kwa kutekeleza vipaumbele mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Sekta Binafsi. Vipaumbele vitakavyotekelezwa ni pamoja na kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, ikiwemo kuunganisha mikoa ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa; kuongeza kasi ya kuunganisha umeme kwa wananchi ili kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii; kuendelea kutekeleza mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Project-Gridi Imara)* ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini; kufanya matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; na kuendelea na usambazaji wa umeme katika vitongoji, ikiwemo kwenye shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo (migodi, kilimo, viwanda, shule, pampu za maji na vituo vya afya) pamoja na kuwezesha ujenzi wa vituo vya mafuta vijijini ili kuimarisha upatikanaji wa nishati safi na salama kwa vyombo vya moto katika maeneo hayo.

182. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia itaendelea kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034) na Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati wa Mwaka 2025 - 2030 *(National Energy Compact 2025 - 2030);* na kuimarisha uzalishaji wa gesi asilia kwa kutekeleza miradi ya utafutaji na uendelezaji wa nishati hiyo ikiwemo mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG Project)*, mradi wa uendelezaji wa gesi asilia iliyogunduliwa eneo la Ntorya katika Kitalu cha Ruvuma na miradi ya kielelezo na kimkakati ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya Eyasi – Wembere, Lindi - Mtwara na Mnazi Bay. Maeneo mengine ya kipaumbele ni kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia kwa ajili ya vyombo vya moto (CNG), viwandani, katika taasisi na majumbani pamoja na kuendelea na majadiliano ya kibiashara ya nishati hiyo na nchi nyingine ikiwemo Kenya na Uganda.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto zitokanazo na vita, ambazo zinaathiri upatikanaji wa bidhaa za mafuta duniani, Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji wa mafuta duniani na kuchukua hatua stahiki, ili kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hizo ambazo ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi, usafiri na usafirishaji. Vilevile, jitihada zitaelekezwa katika ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa za mafuta ya petroli ndani na nje ya nchi na kutekeleza shughuli za kiudhibiti katika Sekta ya Nishati. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi asilia; kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi/Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya TANESCO, REA, TPDC, PBPA, EWURA na PURA pamoja na Kampuni Tanzu kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma, tija na ufanisi katika uendeshaji na mapato; na kuimarisha na kusimamia nguvu kazi ya Wizara, mifumo ya utendaji kazi, upatikanaji wa vitendea kazi pamoja na kushughulikia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora, Magonjwa Sugu na Yasiyoambukizwa na UKIMWI katika eneo la kazi.

## C.1 SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

### C.1.1 MIRADI YA KUZALISHA UMEME

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itatekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ili kuendelea kuhakikisha nchi inakuwa na umeme wa kutosha, uhakika na endelevu, kutokana na umuhimu wa nishati hii katika ukuaji wa Taifa letu, maendeleo ya kijamii na utoaji wa huduma bora. Miradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

#### a) Miradi Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji

#### (i) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua Mkoani Shinyanga – MW 150

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kukamilisha utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi utakaohusisha

ukamilishaji wa majengo *(buildings finishing and furniture),* ujenzi wa barabara za ndani pamoja na kazi ndogo ndogo zilizosalia *(snags)*. Vilevile, Serikali itakamilisha usanifu wa awamu ya pili ya mradi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha umeme wa jua wa Megawati 100. Jumla ya **Shilingi bilioni 83.49** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 49.5**

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na ujenzi wa tuta kuu (*main dam)*, njia ya kusafirisha maji kuelekea kwenye jengo la mitambo (*headrace culvert*), tenki la kupumulia (*surge tank*) na jengo la mitambo *(power house)*. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa kituo cha kupoza na kusafirisha umeme *(switch yard*) na ujenzi wa nyumba za kudumu. Jumla ya **Shilingi bilioni 74.82** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP – MW2,115)**

187. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na usimamizi na uratibu wa mradi huu, kulipa fedha za zuio (*retention money*) kulingana na masharti ya mkataba, kulipa stahiki za Mshauri Mwelekezi (TECU) kwa huduma za usimamizi wa mradi, pamoja na kugharamia shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa mradi katika kipindi cha matazamio (*Defects Notification Period – DNP*) ili kuhakikisha mradi unakamilika na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango vya kimkataba na kitaalamu. Jumla ya **Shilingi bilioni 350** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**(iv) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono MW - 87.8**

188. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizopangwa kutelekezwa ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi, kukamilisha taratibu za kuwapata wakandarasi wa ujenzi, Mshauri Mwelekezi wa kusimamia mradi na kuanza ujenzi wa bwawa na njia ya kusafirisha umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 2** fedha za

ndani na **Shilingi billioni 93.19** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

### (v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185

189. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika mradi huu ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mitambo na vituo vya kupoza umeme wa msongo wa kilovolti 132/33 katika maeneo ya Mbagala na Gongolamboto na kukamilisha kazi ndogo ndogo (*snags*) zilizosalia katika kipindi cha matazamio ya mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 3.85** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi tajwa.

## b) Miradi ya Uzalishaji wa Umeme Iliyopo katika Hatua za Maandalizi

### (i) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358

190. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi, kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya usimamizi wa mradi na kukamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi *(EPC contractor)* wa bwawa la kuzalisha umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 115** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

### (ii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali – MW 222

191. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi, kukamilisha taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi (*Transaction Adviser*) kwa ajili ya maandalizi ya zabuni, na kuendelea na taratibu za kumpata mwekezaji wa mradi kwa utaratibu wa *Build, Operate and Transfer* (BOT). Aidha, Serikali kupitia TANESCO inaendelea kufanya majadiliano na wawekezaji mbalimbali walioonesha nia ya kushiriki utekelezaji wa mradi huu kupitia

utaratibu wa Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) hatua inayolenga kuongeza kasi ya utekelezaji wake. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme Jua - MW 100 Same na MW 100 Singida**

192. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka ujao wa fedha 2026/27 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Impact Assessment – ESIA).* Jumla ya **Shilingi bilioni 1.15** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iv) Maandalizi ya Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Nishati ya Nyuklia Pamoja na Vyanzo Vingine**

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa mchanganyiko wa vyanzo vya nishati ya umeme nchini, Serikali katika mwaka 2026/27 itaanza maandalizi ya miradi mikubwa ya kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo vipya ikiwa ni mwelekeo wa kuwa na Megawati 70,000 za umeme ifikapo mwaka 2050 kwa mujibu wa Dira 2050. Kazi zitakazotekelezwa ni kuratibu utekelezaji wa hatua za awali za maandalizi ya kiufundi ili kuanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya nyuklia pamoja na vyanzo vingine nchini ili kufikia MW 8,000 ifikapo mwaka 2030. Jumla ya **Shilingi bilioni 7** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mpango huu.

**(v) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kikonge – MW 321**

194. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa Megawati 321 kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Ruhuhu mkoani Ruvuma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 96 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya awali ya mradi ili kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya maandalizi ya zabuni za utekelezaji wa mradi kwa utaratibu

wa PPP. Jumla ya **Shilingi milioni 100** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya kazi hiyo.

**(vi) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia Mtwara - MW 300**

195. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha wananchi waliopisha mradi huu mkoani Mtwara wanalipwa viwango stahiki vya fidia, Serikali itahuisha daftari la uthamini wa mali za wananchi hao na kuendelea na ulipaji wa fidia. Hatua hiyo itawezesha utekelezaji wa mradi huu ambao kukamilika kwake kutaongeza kiwango cha umeme katika Gridi ya Taifa. Jumla ya **Shilingi milioni 500** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

**(vii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia Kinyerezi III - MW 1,000**

196. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha Megawati 1,000 za umeme kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Kinyerezi – Dar es Salaam. Kazi zitakazotekelezwa ni kuhuisha Upembuzi Yakinifu, kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA) na tathmini ya mali kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 200** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

## C.1.2 MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUSAMBAZA UMEME

### a) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo katika Hatua za Utekelezaji

**(i) Mradi wa Kusafirisha Umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze – Kilovoti 400 na Kituo cha Kupoza Umeme, Chalinze**

197. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kufanyika katika mradi huu ni kukamilisha malipo ya mkandarasi wa mradi kwa mujibu wa mkataba ili kuwezesha kukamilisha majukumu ya kimkataba na kufunga rasmi utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 10** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Sumbawanga kupitia Mbeya na Tunduma (TAZA)**

198. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi, kukamilisha ujenzi wa njia na vituo vya kupoza umeme pamoja na shughuli ndogo ndogo (*snags*). Jumla ya **Shilingi bilioni 4** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 167.78** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Dodoma (*NEG Phase 2*)**

199. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha eneo la mradi, kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na kufanya majaribio ya kiufundi, uhakiki na kuwasha rasmi njia ya umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 200** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(iv) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze - Kinyerezi - Mkuranga (*NEG Phase 1*)**

200. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya njia ya kusafirisha umeme, usimikaji wa nguzo za umeme, uvutaji wa nyaya pamoja na kufanya majaribio na kuwasha rasmi njia ya umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.05** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(v) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma**

201. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha kazi ndogo ndogo zilizosalia *(snags),* kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe mkoani Kigoma na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha

Nyakanazi. Jumla ya **Shilingi bilioni 28.43** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vi) Mradi wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (*National Grid Stabilization Projects)* – Gridi Imara**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa zitahusisha kukamilisha malipo ya hati za madai ya wakandarasi kwa mujibu wa masharti ya mikataba, kutekeleza miradi 20 iliyosalia kati ya 27 ya umeme inayojumuisha njia za kusafirisha umeme, vituo vya kupoza umeme na njia za kusambaza umeme kwa kuzingatia mikataba husika. Jumla ya **Shilingi bilioni 265** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vii) Mradi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Gridi ya Taifa *(TANESCO Transmission Grid Rehabilitation and Upgrading - TTGRUP)***

203. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya wakandarasi na Mshauri Mwelekezi sambamba na kukamilisha kazi zilizosalia wakati wa kipindi cha uangalizi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 26.89** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(viii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Benaco hadi Kyaka**

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi na kuanza ujenzi na usimikaji wa misingi ya minara ya kusafirishia umeme. Aidha, kazi nyingine zitakazofanyika ni uvutaji wa nyaya pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Benaco. Jumla ya **Shilingi bilioni 3** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 63.47** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ix) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli, Shinyanga**

205. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha ulipaji wa fidia, ujenzi wa kituo cha kupoza

umeme na ununuzi na ufungaji wa kifaa cha kudhibiti umeme (STATCOM). Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**b) Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Umeme Iliyopo Katika Hatua ya Utayarishaji**

**(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera, Msongo wa Kilovoti 220 kutoka Segera – Tanga na Msongo wa kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo**

206. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Chalinze – Segera, kilovoti 220 Segera – Tanga na kilovoti 220 kutoka Chalinze – Bagamoyo, kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 15** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 151.38** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Segera – Same - Arusha (*Lemugur*)**

207. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuanza taratibu za awali za ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi pamoja na kuendelea na majadiliano na Wadau wa Maendeleo ili kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Jumla ya **Shilingi milioni 200** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

**(iii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 220 kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Umeme (SGR *Lot* 3, *Lot* 4, *Lot* 5 na *Lot* 6)**

208. ***Mheshimiwa Spika***, kazi zilizopangwa kufanyika katika kipande cha *Lot 3* ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi; kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi; na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Vilevile, katika *Lot 4* kazi

zitakazotekelezwa ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; na kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi. Aidha, kazi zitakazotekelezwa katika *Lot 5* ni kukamilisha malipo ya fidia; na kuendelea na ujenzi wa mradi. Vilevile, katika *Lot 6* (Tabora hadi Kigoma), Serikali itafanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii na kuanza uthamini wa mali za wananchi wanaopisha eneo la mradi. Jumla ya **Dola za Marekani milioni 125** sawa na takriban **Shilingi bilioni 343.80** zimetengwa kupitia Fungu la SGR kwa ajili ya kutekeleza miradi hii.

**(iv) Ujenzi wa Njia za Kusafirisha Umeme *(Submarine Cables)* Msongo wa Kilovoti 220 Kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar na Mafia**

209. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi, kumpata Mshauri Mwelekezi wa kusimamia ujenzi wa mradi na kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.5** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 31.28** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(v) Mradi wa Kusafirisha Umeme Msongo wa Kilovoti 400 kutoka Tanzania hadi Uganda (Ibadakuli - Masaka)**

210. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni kumpata Mshauri Mwelekezi, kuendelea na taratibu za ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi pamoja na kuwapata wakandarasi. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.9** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(vi) Mradi wa Njia ya Mzunguko wa Kusafirisha Umeme (*Dodoma Ring Circuit*) Msongo wa Kilovoti 220**

211. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali italipa fidia wananchi wanaopisha eneo la mradi wa njia ya mzunguko wa kusafirisha umeme katika Jiji la Dodoma, kuwapata wakandarasi na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.06** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

**(vii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Misigiri, Singida**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa katika mradi huu ni kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi, kuweka mipaka ya eneo la mradi pamoja na kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 150** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

**(viii) Ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mbinga, Ruvuma**

213. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huu ni kufanya uthamini wa mali za wananchi wanaopisha mradi, kuweka mipaka ya eneo la mradi pamoja na kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 100** zimetengwa na TANESCO kwa ajili ya mradi huu.

**c) Ukarabati wa Vituo vya Kuzalisha Umeme vya Mtera (MW 80), Kihansi (MW 180), Pangani (MW 68) na Nyumba ya Mungu (MW 8)**

214. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itaendelea na ukarabati wa vituo hivi vya kuzalisha umeme ili kuhakikisha vituo hivyo vinafanya kazi kwa ufanisi. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu, kuanza taratibu za kuwapata Washauri Elekezi na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii. Jumla ya **Shilingi bilioni 1.03** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

## C.1.3 UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TANESCO (ETDCO, TCPM NA TGDC)

**a) Kampuni ya Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usafirishaji na Usambazaji Umeme (ETDCO)**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya ETDCO, itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 132 kutoka Urambo hadi Kidahwe kupitia kituo cha kupoza umeme cha Nguruka.

Aidha, Serikali itakamilisha utekelezaji wa miradi ya umeme katika vitongoji 105 mkoani Mbeya inayosimamiwa na REA; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuunganisha vitongoji 262 katika Wilaya ya Nyasa na Mbinga mkoani Ruvuma; vitongoji 358 wilayani Mpanda, Mlele na Tanganyika mkoani Katavi; kuendelea na usambazaji wa umeme katika maeneo ya Kilindi na Simanjiro; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilometa 128 kutoka Masasi hadi Mahumbika pamoja na kituo cha kupoza umeme.

**b) Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)**

216. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya TCPM itaendelea na uzalishaji na usambazaji wa nguzo za zege kupitia kiwanda chake cha Tabora. Aidha, Serikali itaanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa kiwanda cha pili kitakachokuwa kinamilikiwa na TCPM mkoani Mbeya pamoja na kuendelea na utaratibu wa kushirikiana na Wawekezaji Binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha nguzo za zege katika mikoa mbalimbali isiyokuwa na viwanda hivyo.

**c) Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC)**

217. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia kampuni tanzu ya TANESCO ya TGDC itaendelea na utekelezaji wa miradi ya jotoardhi ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha uhakiki wa rasilimali ya jotoradhi na kufanya tathmini ya visima vya uhakiki katika eneo la mradi wa Ngozi. Vilevile, Serikali itaajiri Mshauri Mwelekezi (*Drilling Consultant*) wa kusimamia programu ya uchorongaji wa visima vya uhakiki katika mradi wa Kiejo-Mbaka. Pia, kazi nyingine itakayofanyika ni kukamilisha utafiti wa kina wa kisayansi katika eneo la Natron mkoani Arusha. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.00** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.33** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

**C.1.4 MIRADI YA NISHATI VIJIJINI**

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya nishati vijijini na vitongojini ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo

ya jamii katika maeneo hayo. Programu na miradi itakayotekelezwa ni kama ifuatavyo:

a) **Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili B (*Hamlet Eletrification Project – HEP IIB*)**

219. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa uunganishaji wa umeme katika vitongoji 9,009 kwa kujenga miundombinu ya kilomita 13,181 za njia za msongo wa kati, kilomita 14,016 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 8,003 za kVA 100 na 1,006 za kVA 200 na uunganishaji wa wateja wa awali 290,300. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2025/26 kwenye mikoa 25 (isipokuwa Dar es Salaam). Kwa mwaka 2026/27, jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

b) **Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Awamu ya Pili A (*Hamlet Eletrification Project – HEP IIA*)**

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa uunganishaji wa umeme katika vitongoji 3,060 vya Majimbo 204 ya Uchaguzi nchini sawa na wastani wa vitongoji 15 kwa kila Jimbo. Wigo wa mradi unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kilomita 528 za njia ya msongo wa kati, kilomita 6,040 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 3,056 na uunganishaji wa wateja wa awali 100,704. Jumla ya **Shilingi bilioni 75** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

c) **Mradi wa Kuunganisha Wateja Vitongojini – *Universal Hamlet Eletrification and Last Mile Customer Connection***

221. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutekeleza mradi wa kuongeza uunganishaji wa wateja vitongojini *(Universal Hamlet Eletrification and Last Mile Customers Connectivity)* ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mahsusi wa Nishati wa Taifa *(National Energy Compact)* ulioridhiwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika *(Mission 300)* mwezi Januari, 2025. Katika mwaka 2026/27, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi huu katika mikoa mitatu ya Pwani, Morogoro na Dodoma ambao unalenga kusambaza umeme katika jumla

ya mitaa 279. Aidha, Serikali itatekeleza mradi huu kwa kujumuisha vitongoji vya mikoa mingine iliyosalia. Jumla ya **Shilingi bilioni 188.8** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 127.98** fedha za nje zitatumika kutekeleza mradi huu.

**d) Mradi wa Kupeleka Umeme katika Vitongoji Mkoa wa Lindi (*Hamlet Electrification Project - Lindi*)**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Norway itaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika Mkoa wa Lindi ambapo kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme msongo wa kati yenye urefu wa kilomita 352.45, msongo mdogo wa kilomita 430 na kufunga transfoma 230. Lengo la mradi huu ni kufikisha umeme katika vitongoji 230 ambapo wateja wa awali 7,590 wataunganishiwa umeme. Aidha, Serikali kupitia REA itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi ya umeme katika shughuli za uzalishaji na matumizi ya nishati safi ya kupikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.00** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

**e) Mradi wa Ufungaji wa Mifumo ya Umeme Jua Visiwani (*Island Densification Project – IDP*)**

223. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha usambazaji na ufungaji wa mifumo ya jua inayojitegemea kwa wakazi 20,000 katika visiwa vidogo 143 vilivyopo katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Sambamba na kuendelea na utekelezaji wa mradi huu, Serikali kupitia REA itawaunganishia umeme jumla ya wateja 7,257, kati ya hao wateja 4,400 wataunganishwa na mifumo ya umeme jua inayojitegemea na wateja 2,857 wataunganishwa na gridi ndogo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa *National Energy Compact*. Jumla ya **Shilingi bilioni 18** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huu.

**f) Mradi wa Kusambaza Umeme katika Vitongoji Pembezoni mwa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki (EACOP)**

224. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA kwa kushirikiana na Kampuni ya EACOP itaanza kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vitongoji vilivyopo pembezoni mwa vituo vya kusukuma mafuta katika bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania katika mikoa nane (8) inayopitiwa na bomba hilo. Kazi zitakazofanyika ni kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme wa msongo wa kati ya urefu wa kilomita 18.42 na msongo mdogo ya urefu wa kilomita 40 katika vitongoji 17 vya mikoa ya Kagera (13) na Geita (4) ili kuunganisha wateja 759. Aidha, Serikali itaainisha wigo wa kazi katika mikoa ya Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga ikiwa ni hatua ya awali kabla ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme katika mikoa hiyo. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.20** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 2.60** fedha kutoka Kampuni ya EACOP zitatumika kutekeleza kazi hizo.

**g) Mpango wa Matumizi ya Nishati kwa ajili ya Kuzalisha Mali – (*Productive Use of Energy*)**

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA imekusudia kuendelea kuwezesha mpango wa kuhamasisha wananchi kutumia nishati kwa ajili ya kuzalisha mali ili kuongeza thamani ya mazao na huduma mbalimbali zikiwemo za umwagiliaji katika mashamba ya kilimo; mashine za kukoboa na kusaga nafaka mchangayiko; kuongeza thamani ya mazao ya bahari na maziwa ikiwemo mwani, dagaa na samaki; kuwezesha kuunganisha nishati katika viwanda vidogo vijijini; kuwezesha kuunganisha umeme katika migodi midogo ikiwemo Chunya (Mbeya) na kwa Msisi-Handeni (Tanga); na kuwezesha maeneo ya biashara kufikiwa na huduma za nishati ili kuboresha utolewaji wa huduma mbalimbali na kuongeza kipato kwa wananchi na Taifa.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazofanyika ni kuwapata watoa huduma kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa vifaa; na kutoa ruzuku kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum pamoja na taasisi binafsi kwa ajili ya kuwapatia

vifaa vya matumizi bora ya nishati. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.00** fedha za ndani zitatumika kutekeleza Mpango huu.

### h) Mpango wa Kuwezesha Waendelezaji wa Nishati Jadidifu

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kuwawezesha waendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuendelea kutoa ruzuku za ujenzi wa miradi hiyo na kutoa msaada wa kiufundi kwa waendelezaji hao ili kuwajengea uwezo wa kuendeleza miradi hiyo. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.0** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

## C.1.5 UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA

228. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034 ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kushirikiana na wadau kusambaza nishati safi ya kupikia na teknolojia zake kwa gharama nafuu; kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, ushiriki katika maonesho na mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa na makongamano; na kuhamasisha Sekta Binafsi na Umma kushiriki katika kuimarisha upatikanaji wa malighafi na miundombinu ya uhakika ya nishati safi ya kupikia katika maeneo mbalimbali nchini. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na kuandaa, kuhuisha na kuoanisha Sera, Sheria, Kanuni na miongozo wezeshi itakayofanikisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kushirikiana na Taasisi za umma na binafsi ili kuongeza wigo wa tafiti na ubunifu wa teknolojia zinazohusu nishati safi ya kupikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 10** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Hatua nyingine zitakazochukuliwa ni:

**a) Uwezeshaji wa Nishati Safi ya Kupika katika Kaya**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea na usambazaji wa mifumo mbalimbali ya nishati safi ya kupikia ikiwemo mitungi ya LPG, majiko banifu, na majiko ya umeme kwenye kaya 200,000 katika maeneo ya vijijini na vijiji-miji. Kazi zitakazofanyika ni kuwapata watoa huduma wa nishati safi ya kupikia na kusambaza mifumo ya nishati hizo katika mikoa 25 Tanzania Bara. Jumla ya **Shilingi bilioni 15.00** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya kazi hizo.

**b) Uwezeshaji wa Nishati Safi katika Taasisi Zinazohudumia Chakula Zaidi ya Watu 100 kwa Siku**

230. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kuwezesha usambazaji wa mifumo mbalimbali ya nishati safi ya kupikia ikiwemo mifumo ya LPG, majiko banifu, mkaa mbadala pamoja na majiko ya umeme katika taasisi 300 zinazotoa huduma ya chakula kwa watu zaidi ya 100 kwa siku. Kazi zitakazofanyika ni kupata taasisi zitakazofungiwa mifumo hiyo kupitia fursa zitakazotangazwa na Serikali kupitia REA; kuwapata watoa huduma wa nishati safi ya kupikia; na kusimika mifumo hiyo kwa taasisi zitakazokidhi vigezo. Jumla ya **Shilingi bilioni 15.00** fedha za ndani zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**c) Kuwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Kusambaza Gesi Asilia katika Mkoa wa Pwani Awamu ya Pili**

231. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA na TPDC zitaendelea kushirikiana kutekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya kupikia katika kaya 500 za Kijiji cha Kisemvule kilichopo Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.00** fedha za ndani zitatumika kutekeleza mradi huo.

d) **Uwezeshaji wa Mitambo ya Kutengeneza Mkaa Mbadala**

232. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia REA itaendelea kutoa ruzuku kwa wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye mahitaji maalum ili kutengeneza mkaa mbadala na majiko banifu. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na kupata vikundi vitakavyonufaika na kuwapata watoa huduma watakaosambaza mashine za kutengeneza mkaa na majiko hayo ili kusambaza huduma hizo kwa makundi hayo. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.0** fedha za ndani zitatumika kugharamia mpango huu.

### C.1.6 KURATIBU, KUSIMAMIA NA KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA MIKAKATI MBALIMBALI KATIKA SEKTA NDOGO YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

233. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuandaa, kuhuisha na kutekeleza Mipango na Mikakati mbalimbali katika Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu ili kuendeleza Sekta hiyo. Mipango na Mikakati hiyo ni pamoja na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (*Power System Master Plan 2024 Update*); Mkakati wa Taifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*National Energy Efficiency Strategy*) wa Mwaka 2024 – 2034; Mkakati wa Maboresho ya Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Roadmap – ESI-RSR, 2025 - 2035*); Mpango Kabambe wa Kupeleka Nishati Vijijini (*Rural Energy Master Plan - REMP*) wa Mwaka 2022; Mkakati wa Taifa wa Nishati Jadidifu (*National Renewable Energy Strategy and its Implementation Roadmap*) wa Mwaka 2024 - 2034; na Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (*National Clean Cooking Strategy 2024 - 2034*).

234. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia itaendelea na utekelezaji wa Mpango Mahususi wa Taifa wa Nishati *(National Energy Compact 2025 - 2030)* ikiwa ni pamoja na kuunganishia umeme kaya 1,700,000 kwa mwaka, kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika Sekta Ndogo ya Umeme na Nishati Jadidifu pamoja na uratibu wa utekelezaji wa Mpango huu ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 5.4** zimetengwa.

## C.2 SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

235. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mwaka 2026/27 itaendelea kusimamia na kuendeleza Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia ili kuhakikisha uhakika wa upatikanaji na usalama wa bidhaa za petroli na gesi asilia nchini. Miradi na kazi zitakazotekelezwa zinahusisha utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia kama ifuatavyo:

### C.2.1 MIRADI YA UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI

**a) Kitalu cha Eyasi – Wembere**

236. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na shughuli za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Eyasi–Wembere ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha awamu ya pili ya uchukuaji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilomita 321; kukamilisha, kuchakata na kutafsiri taarifa za mtetemo za mfumo wa 2D za urefu wa kilomita 1,360; na kuendelea na stadi za kijiolojia na kijiofizikia. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

**b) Kitalu cha Lindi – Mtwara**

237. ***Mheshimiwa* Spika,** Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi za utafiti wa awali wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Lindi-Mtwara ikiwa ni pamoja na kuchukua taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D kwa awamu ya pili katika eneo la kilomita za mraba 386.3; kukamilisha uchakataji na kutafsiri taarifa za mitetemo zilizochukuliwa katika eneo la kilomita za mraba 739.3 na kuendelea na stadi za kijiolojia na kijiofizikia. Aidha, Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi ya kumtafuta mbia wa kimkakati mwenye uzoefu, utaalamu na fedha kwa ajili ya kushirikiana nae katika kuendeleza kazi za kitalu hicho. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

### c) Kitalu cha Songo Songo Magharibi

238. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na kazi za utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Kitalu cha Songo Songo Magharibi kwa kukamilisha uchukuaji na uchakataji wa taarifa za mitetemo za mfumo wa 3D katika eneo la kilomita za mraba 421 zilizo katika kina kifupi cha bahari. Jumla ya **Shilingi bilioni 83.21** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

## C.2.2: MIRADI YA UENDELEZAJI NA UZALISHAJI WA GESI ASILIA

### a) Kitalu cha Uzalishaji wa Gesi Asilia cha Mnazi Bay

239. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika kitalu hiki ni pamoja na kuendelea na uzalishaji wa gesi asilia kulingana na mahitaji na kukamilisha kazi ya uchorongaji wa kisima cha utafiti (Kasa - 1). Jumla ya **Shilingi bilioni 81.04** zimetengwa na TPDC kwa ajili kutekeleza kazi hizo.

### b) Kitalu cha Ruvuma (Eneo la Ntorya)

240. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji itaendelea na shughuli za uendelezaji wa gesi asilia katika Kitalu cha Ruvuma eneo la Ntorya kwa kuchoronga kisima kimoja (1) cha utafutaji cha Chikumbi-1 na ukarabati wa visima viwili (2) vya Ntorya-1 & 2 vitakavyotumika katika uzalishaji wa gesi asilia. Kukamilika kwa kazi hizo kutawezesha kuanza uzalishaji ambapo kiasi cha futi za ujazo milioni 40 hadi 60 kinatarajiwa kuzalishwa kwa siku. Jumla ya **Shilingi bilioni 20.35** zimetengwa na TPDC kwa ajili utekelezaji wa mradi huu.

### c) Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika *(Liquefied Natural Gas – LNG)*

241. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inashirikiana na makampuni ya kimataifa ya nishati katika utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha majadiliano na kuandaa mikataba ya utekelezaji wa mradi kati ya Serikali na wawekezaji; kuandaa na kutekeleza mpango wa matumizi ya

ardhi ya eneo la mradi; kushiriki katika utayarishaji wa Mpango wa Uendelezaji wa Mradi *(Project Development Plan);* na kuendelea na utoaji wa elimu na kuhamasisha wananchi kuhusu fursa na manufaa ya mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 20** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizo.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mradi huu Tanzania itatambulika kimataifa katika biashara ya LNG, mapato ya Serikali yatokanayo na mauzo ya gesi asilia yataimarika, uwekezaji katika utafutaji na uendelezaji wa gesi asilia nchini utaongezeka, ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii utaimarika, matumizi ya gesi asilia nchini yataongezeka, na kuongezeka kwa fedha za kigeni nchini. Aidha, mradi utaongeza fursa za ushiriki wa Watanzania na kampuni za ndani katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia.

### C.2.3 : MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI WA GESI ASILIA

#### a) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Ntorya (Kitalu cha Ruvuma) hadi Kiwanda cha Kuchakata Gesi Asilia cha Madimba

243. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita 34.2 la kusafirisha gesi asilia itakayozalishwa katika Kitalu cha Ruvuma eneo la Ntorya hadi kiwanda cha kuchakata gesi asilia cha Madimba. Bomba hilo linatarajiwa kuwa na uwezo wa kusafirisha gesi asilia takriban futi za ujazo milioni 140 kwa siku kwa ajili ya kuchakatwa katika kiwanda hicho na kuingizwa katika miundombinu ya Taifa ya usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi mbalimbali nchini. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi ghafi yenye mgandamizo mkubwa na miundombinu yake. Jumla ya **Shilingi bilioni 21.82** zimetengwa na TPDC kwa ajili utekelezaji wa mradi huu.

**b) Upanuzi wa Kiwanda cha Kuchakata Gesi cha Madimba – (*Madimba Gas Processing Plant Expansion*)**

244. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC imepanga kuongeza mtambo mmoja (1) mpya wenye uwezo wa kuchakata futi za ujazo milioni 70 kwa siku katika kiwanda cha Madimba ili kukidhi ongezeko la kiasi cha gesi kinachotarajiwa kuchakatwa kwa siku kutokana na ongezeko la uzalishaji kutoka visima vya Ntorya na Mnazi Bay. Kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kuchakata futi za ujazo milioni 210 kwa siku ambapo baada ya upanuzi huo uwezo wa kiwanda utafikia futi za ujazo milioni 280 kwa siku. Jumla ya **Shilingi bilioni 143.2** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**c) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Gesi Asilia kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze – Pwani**

245. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba lenye urefu wa kilomita 93 la kusafirisha gesi asilia yenye mgandamizo mkubwa kutoka kituo cha kupokelea gesi asilia kilichopo Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Chalinze. Bomba hilo litawezesha upatikanaji wa gesi asilia katika maeneo ya kongani ya viwanda Zegereni - Kibaha, viwanda vya Mlandizi, Bandari Kavu ya Kwala na Chalinze na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya kiuchumi na viwanda katika ukanda husika. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha usanifu wa mradi na kuanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa bomba. Jumla ya **Shilingi bilioni 121.70** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**C.2.4: MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAMBAZAJI WA GESI ASILIA**

246. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kuongeza mtandao wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza kasi ya matumizi ya gesi asilia kwa shughuli mbalimbali ikiwemo uzalishaji wa umeme, viwandani, vyombo vya moto, katika taasisi na majumbani. Ili kuongeza mtandao wa usambazaji wa gesi asilia nchini, Serikali kupitia TPDC imejipanga kutekeleza miradi ifuatayo:

**a) Miradi ya Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani**

**i) Ujenzi wa Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi Asilia Katika Mkoa wa Dar es Salaam**

247. ***Mheshimiwa Spika*** mradi huu unalenga kujenga mtandao wa usambazaji wa gesi asilia katika maeneo mbalimbali yaliyo karibu na miundombinu ya gesi asilia jijini Dar es Salaam. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia na kuunganisha wateja wapya 1,000 kwa ajili ya matumizi ya taasisi na majumbani katika maeneo ya Ubungo, Sinza, Mikocheni na Lugalo Barracks. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika maeneo ya Upanga, Muhimbili, Masaki, Kawe na Mbweni kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia. Jumla ya **Shilingi bilioni 6.00** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**ii) Ujenzi wa Bomba la Kusambaza Gesi Asilia kutoka Kisemvule hadi Mbagala**

248. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kutoka eneo la Kisemvule mkoani Pwani hadi kituo cha CNG kilichopo Mbagala pamoja na kufikisha huduma ya gesi kwa wateja wa viwandani waliopo katika eneo la viwanda Zakhiem. Pia, mradi unahusisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia kwa ajili ya kuwaunganishia wateja wa viwandani. Shughuli za ujenzi zitaanza kutekelezwa katika mwaka 2026/27 ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 8.23** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**b) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia katika Mikoa ya Lindi na Mtwara**

249. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kusambaza miundombinu ya gesi asilia katika maeneo ya Mtwara Mjini, hususan Soko la Samaki la Mtwara, maeneo ya Kata ya Shangani, maeneo ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, nyumba za makazi ya watumishi wa Benki Kuu - Mtwara, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,

pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali, majengo ya biashara, hoteli, migahawa na makazi yaliyopo katika eneo hilo. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha taratibu za kuanza kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji na kuunganisha taasisi na wateja wa majumbani kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.20** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**c) Ujenzi wa Vituo vya Kugandamiza na Kusambaza Gesi Asilia *(Compressed Natural Gas – CNG)***

250. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na ujenzi wa vituo vinavyohamishika vya kusambaza gesi asilia iliyoshindiliwa *(Mobile CNG stations)* kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa gesi asilia katika Mikoa iliyo mbali na miundombinu ya gesi hiyo. Usambazaji huo utafanyika kwa kutumia magari maalum ya kusafirisha gesi *(CNG trucks)* kutoka vituo mama vilivyopo Dar es Salaam na kufikisha katika maeneo husika. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na usimikaji wa vituo vitano (5) katika mikoa ya Dar es Salaam (2), Morogoro (1) na Dodoma (2). Vilevile, Serikali kupitia TPDC itaendelea na utafutaji wa maeneo na kuanza kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha kwa ajili ya ujenzi wa vituo viwili (2) kwa kila Mkoa. Jumla ya **Shilingi bilioni 22.06** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**d) Mradi wa Usambazaji wa Gesi Asilia – Mtumba, Dodoma**

251. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma. Utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa kituo cha kupokelea gesi (*Gas Receiving Terminal*) itakayosafirishwa na magari maalum kutoka kituo mama cha CNG kilichopo Mlimani City - Dar es Salaam; na ujenzi wa kituo cha kupunguza mgandamizo, mtandao wa usambazaji pamoja na kituo cha kujazia gesi asilia kwenye magari. Mtandao huo utaunganisha majengo ya Wizara, ofisi za Balozi, taasisi mbalimbali za Serikali, majengo ya biashara, hoteli, migahawa pamoja na makazi yaliyopo katika eneo hilo. Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira

na Jamii na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji wa gesi hiyo. Jumla ya **Shilingi bilioni 14.40** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### C.2.5 : MIRADI YA KUSAFIRISHA GESI ASILIA KWENDA NCHI JIRANI ZA UGANDA NA KENYA

252. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya gesi asilia Afrika, Serikali itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Dar es Salaam (Tanzania) kwenda nchi za Uganda na Kenya ambapo kwa upande wa bomba la kwenda Uganda kazi zitakazofanyika ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii. Aidha, kwa upande wa bomba la kwenda nchini Kenya Serikali inatarajia kuanza taratibu za kumpata Mshauri Mwelekezi atakayesimamia mradi huu. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.18** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

### C.2.6 : MIRADI YA KUSAFIRISHA NA KUHIFADHI MAFUTA

a) **Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania *(East African Crude Oil Pipeline - EACOP)***

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC kwa kushirikiana na Kampuni ya EACOP itaendelea na utekelezaji wa mradi wa EACOP ambapo Serikali kwa kushirikiana na Kampuni hiyo itaendelea na ujenzi wa bomba, matenki ya kupokelea mafuta na gati inayoendelea kujengwa Chongoleani – Tanga kwa ajili ya upakiaji wa mafuta katika meli. Aidha, Serikali itafanya tathmini ya matumizi ya baadhi ya maeneo ya makambi ya ujenzi pamoja na karakana iliyopo Sojo – Tabora ili maeneo hayo yaweze kunufaisha wananchi baada ya mradi kukamilika. Vilevile, wananchi wataendelea kuelimishwa kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo hususan katika maeneo yanayopitiwa na mradi sambamba na kutekeleza miradi ya uwajibikaji kwa jamii katika sekta za elimu, afya, maji, mazingira na miundombinu. Jumla ya

**Shilingi bilioni 100** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuchangia utekelezaji wa mradi huu.

**b) Mradi wa Bomba Jipya la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Tanzania hadi Zambia (*New TAZAMA Pipeline*)**

254. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha majadiliano na kuandaa mikataba ya uendeshaji wa mradi kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia, kufanya usanifu wa kihandisi *(Front End Engineering Design – FEED)* pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (ESIA). Jumla ya **Shilingi bilioni 5.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**c) Mradi wa Ukarabati wa Tenki Namba 8 – Kigamboni, Dar es Salaam**

255. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPDC itaendelea na ukarabati wa Tenki Namba 8 lililopo katika eneo la TIPER – Kigamboni, Dar es Salaam lenye uwezo wa kuhifadhi mafuta lita milioni 45. Kukamilika kwa Tenki hili kutaongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 9.72** zimetengwa na TPDC kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**C.2.7 : UTENDAJI WA KAMPUNI TANZU ZA TPDC**

**a) TANOIL Investments Limited (TANOIL)**

256. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TANOIL itaendelea kushiriki katika biashara ya kununua na kuuza mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na kuanza biashara ya LPG na vilainishi vya vyombo vya moto na mitambo. Jumla ya **Shilingi bilioni 78.21** zimetengwa na TPDC kupitia TANOIL kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

**b) GAS Company (T) Limited (GASCO)**

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia GASCO itaendelea kutekeleza majukumu yake ya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya gesi asilia nchini pamoja na vituo vya CNG

vinavyomilikiwa na Serikali. Vilevile, Serikali kupitia kampuni hiyo itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia majumbani, kwenye taasisi, viwandani na katika vituo vya CNG. Jumla ya **Shilingi bilioni 124.18** zimetengwa na TPDC kupitia GASCO kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### C.2.8 : UDHIBITI WA MASUALA YA MKONDO WA JUU WA PETROLI KUPITIA PURA

258. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PURA itaendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Usimamizi huo utajumuisha kuandaa Mpango wa Tafiti za Awali *(Reconnaissance Survey)* kwa maeneo yenye viashiria vya mafuta na gesi asilia; kugawanya maeneo katika vitalu vya utafutaji *(block demarcation)*; kuandaa taarifa za kina za kijiolojia na kijiofizikia katika vitalu vitakavyoingizwa kwenye mnada; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika maeneo ya utafutaji pamoja na kushiriki katika maonesho na makongamano mbalimbali ya mafuta na gesi asilia kwa lengo la kufanikisha Duru ya Tano ya Kunadi Vitalu vya Utafutaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli hizo.

### C.2.9 : UDHIBITI WA MASUALA YA NISHATI KUPITIA EWURA

259. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia EWURA itaendelea kusimamia na kudhibiti Sekta ya Nishati nchini kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zilizo bora na uhakika na maendeleo ya Sekta. Usimamizi na udhibiti huo utafanyika kwa kutoa vibali vya ujenzi wa miundombinu, leseni za biashara pamoja na kufanya kaguzi mbalimbali kwa ajili ya kuhakiki ubora wa miundombinu, bidhaa za petroli na gesi asilia. Aidha, ili kuboresha usimamizi wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia, EWURA itaendelea kuboresha mfumo wa kidijitali wa usimamizi wa biashara ya mafuta na gesi asilia kuanzia uagizaji, usambazaji na uuzaji kwenye vituo vya mafuta na gesi asilia.

### C.2.10 : URATIBU WA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia PBPA itaendelea kuratibu shughuli za uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa kutumia mfumo wa BPS. Aidha, PBPA itaendelea kuboresha mfumo wa usimamizi wa BPS (*BPS Management Information System*) ambao unalenga kuwezesha shughuli zote za BPS kufanyika kidijitali ikiwemo usajili wa kampuni za mafuta; uthibitishaji wa awali wa kampuni zinazoshiriki kwenye zabuni za uletaji mafuta nchini; maoteo ya mahitaji ya mafuta; usimamizi wa zabuni; usafirishaji wa mafuta; na masuala ya fedha. Vilevile, mfumo huo utasomana na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali zinazoshirikiana na PBPA katika uagizaji wa mafuta. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.00** zimetengwa na PBPA kwa ajili ya kazi hiyo.

### C.2.11 KUIMARISHA UTENDAJI KAZI NA UTOAJI HUDUMA

261. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio katika utekelezaji wa mipango ya Wizara yanahitaji rasilimaliwatu toshelevu na yenye sifa, maarifa, ujuzi na ubunifu. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itaendelea kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi wa umma kwa kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuongeza motisha kwa watumishi. Katika mwaka 2026/27 Wizara na Taasisi zake zitaendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuzingatia Mpango wa Mafunzo ambapo jumla ya watumishi 5,207 watapatiwa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi katika nyanja mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi na kuimarisha huduma bora kwa wananchi.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza fursa ya ajira pamoja na kuendana na Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Wizara na Taasisi zake zitaajiri watumishi 1,439 na kuwapandisha vyeo watumishi 933. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza programu mbalimbali zinazolenga kulinda na kuimarisha nguvukazi ya Wizara, ikiwemo udhibiti wa Magonjwa Sugu na Yasiyoambukizwa, Afya ya Akili, maambukizi ya VVU/UKIMWI, pamoja na kuendelea na kudhibiti masuala ya rushwa kwa kutoa elimu pamoja na kuanzisha mifumo mbalimbali ya TEHAMA.

## D. USHIRIKISHWAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA YA NISHATI

263. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuvutia Sekta Binafsi ili iweze kushiriki katika utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya Sekta ya Nishati nchini ikiwemo uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme pamoja na mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi asilia. Aidha, Serikali itaendelea kuandaa na kuhuisha miongozo mbalimbali ya umeme kwa lengo la kuendelea kuvutia wawekezaji binafsi kuwekeza katika sekta hiyo.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika miradi ya nishati vijijini ambapo kupitia REA, itaendelea kuziwezesha na kuzisimamia kampuni binafsi zinazotekeleza programu na miradi mbalimbali ya nishati vijijini na vitongojini. Pia, Serikali kupitia REA itaendelea kutoa fursa za mikopo nafuu kwa waendelezaji wa vituo vya mafuta vijijini kupitia utaratibu ulioainishwa kwenye Mwongozo wa Kutekeleza Mradi wa Kuwezesha Ujenzi wa Vituo Vidogo vya Kuuza Mafuta Vijijini.

265. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia Serikali itaendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia nchini. Aidha, ili kuhakikisha gesi asilia iliyopo nchini inaendelea kuwanufaisha watanzania, Serikali kupitia TPDC itaendelea kutoa idhini kwa wawekezaji binafsi kujenga vituo vya CNG katika maeneo mbalimbali nchini. Vilevile, Serikali kupitia EWURA itaendelea kutoa vibali na leseni za ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza mafuta na gesi asilia kwa Sekta Binafsi ili kuendelea kuongeza ushiriki wa sekta hiyo katika shughuli za mkondo wa kati na wa chini wa mafuta na gesi asilia.

## E. SHUKRANI

266. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kuendelea kuwashukuru Viongozi wenzangu katika Wizara ya Nishati, Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati; Mhandisi Felchesmi Jossen Mramba, Katibu Mkuu (Umeme na Nishati Jadidifu); na Dkt. James Peter Mataragio, Katibu Mkuu

(Mafuta na Gesi Asilia) kwa namna wanavyonisaidia kuhakikisha majukumu tuliyokasimiwa yanatekelezwa ipasavyo kwa tija na ufanisi. Niendelee kuwashukuru pia Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa ujumla, kwa jitihada wanazoweka katika kuhakikisha malengo ya Wizara yanafikiwa. Aidha, naishukuru Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla kwa michango yao katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati. Vilevile, napenda kuvishukuru vyombo vya habari kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutoa elimu na hamasa kwa umma kuhusu masuala ya nishati. Ni matumaini yangu kuwa, ushirikiano huu utazidi kuimarika katika mwaka 2026/27 kwa manufaa ya Taifa letu na Wananchi wake kwa ujumla.

## E.1: USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA SEKTA YA NISHATI

267. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26 yalichangiwa pia na ushirikiano ambao Wizara iliupata kutoka kwa Wadau mbalimbali. Kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo, Jumuiya na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Abu - Dhabi Fund for Development (ADFD), Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea), Exim Bank (China), KfW (Germany), OPEC Fund for International Development, SWISS, Swedfund, Sida (Sweden), Saudi Fund for Developmnet (SFD), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Umoja wa Ulaya (EU). Mashirika mengine ni Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Shirika la Mitaji ya Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNCDF), Geothermal Risk Mitigation Facility (GRMF), Arab Bank for Economic Development in Afrika (BADEA), Shirika la Fedha Duniani (IMF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) pamoja na Shirika la Maendeleo la Uingereza (UKAid).

***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kuzishukuru kwa dhati Serikali za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Burundi, Canada, China, Ethiopia, Falme za Kiarabu, Japan, India, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Korea Kusini, Malawi, Misri, Morocco, Msumbiji, Namibia, Norway, Oman, Rwanda, Saudi Arabia, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Zambia na nchi nyingine kwa kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Nazishukuru pia Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Afrika (AU) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu uendelezaji wa Sekta ya Nishati. Nizishukuru pia kampuni za Equinor Tanzania As, Shell Exploration and Production (T) Limited, Exxon Mobil na Ophir Energy, kwa ushirikiano zinazotupa katika kufanikisha utekelezaji wa mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia Kuwa Kimiminika (*Liquefied Natural Gas – LNG*).

**F. HITIMISHO**

268. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara ya Nishati katika mwaka 2026/27, itaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na umeme wa kutosha unaokidhi mahitaji ya ndani na ziada itakayoweza kuuzwa nje ya nchi na kutupatia fedha za kigeni; kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika mijini, vijijini na vitongojini na kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini. Aidha, mkazo utaelekezwa katika shughuli za utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia, kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta; pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi na kusambaza bidhaa hizo.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Bajeti ya jumla ya **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Tano Ishirini na Tano, Milioni Mia Nne na Moja, Mia Moja Ishirini na Tisa Elfu (Shilingi 2,525,401,129,000)** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2026/27. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi Trilioni Mbili, Bilioni Mia Nne Sitini na Mbili, Milioni Mia Tatu Sitini na Nne, Mia Nane Thelathini na Sita Elfu (Shilingi 2,462,364,836,000)** sawa na **asilimia 97.5** ya Bajeti yote ya Wizara ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Sita na Mbili, Milioni Mia Nne Arobaini na Tisa, Mia Saba Thelathini na Tano Elfu (Shilingi 1,602,449,735,000)** ni fedha za ndani, na **Shilingi Bilioni Mia Nane Hamsini na Tisa, Milioni Mia Tisa Kumi na Tano, Mia Moja na Moja Elfu (Shilingi 859,915,101,000)** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi Bilioni Sitini na Tatu, Milioni Thelathini na Sita, Mia Mbili Tisini na Tatu Elfu (Shilingi 63,036,293,000)** sawa na **asilimia 2.5** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni Hamsini na Mbili, Milioni Mia Tisa Thelathini na Tisa, Sabini na Tano Elfu (Shilingi 52,939,075,000)** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Tisini na Saba, Mia Mbili Kumi na Nane Elfu (Shilingi 10,097,218,000)** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi wa Wizara na Taasisi ya PURA.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii, vimeambatishwa vielelezo mbalimbali ambavyo vinafafanua masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.nishati.go.tz*

271. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, ahsante sana kwa hotuba hiyo na imeungwa mkono, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Subira Mgalu aje kuwasilisha taarifa ya Kamati.

**MHE. SUBIRA K. MGALU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Fungu 58 – Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza ni utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

(ii) Sehemu ya Pili inaeleza kuhusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iii) Sehemu ya Tatu ni Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

(iv) Sehemu ya Nne ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na

(v) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026

pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, kupitia ziara ya terehe 12 hadi 18 Machi, 2026 na vikao vya terehe 23 na 24 Machi, 2026 Kamati ilifanya yafuatayo: -

(i) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 118 (1));

(ii) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 (Kanuni ya 120 (1));

(iii) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iv) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uweke *microphone* vizuri, weka *mic* vizuri sauti iweze kutoka vizuri.

**MHE. SUBIRA K. MGALU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Fungu 58 – Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Fungu 58 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo: -

(i) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli;

(ii) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida; na

(iii) Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa upatikanaji wa fedha; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Fungu 58 – Wizara ya Nishati ilitengewa bajeti ya jumla ya shilingi 1,965,745,445,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 79,232,226,000 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,886,513,219,000 zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea shilingi 1,165,387,590,900.58 sawa na wastani wa 59.28% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi 15,041,546,556.22 sawa na wastani wa asilimia 1.3 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 1,150,346,044,344.14 sawa na wastani wa 98.7% ni fedha za bajeti ya maendeleo kama zinavyoonekana kwenye kielelezo cha kwanza cha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha katika bajeti ya fungu 58 hususan katika miradi ya maendeleo. Kamati ilihoji juu mapokezi kidogo ya fedha za matumizi ya kawaida ikiwa kama hayakuathiri utekelezaji wa shughuli za Wizara ukizingatia na umuhimu wa Sekta hii ya Nishati nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea ufafanuzi kwamba fedha hiyo iliyopokelewa licha ya kuwa chini ya wastani uliotakiwa kufika hadi kufikia Februari, 2026, bado haikuathiri utendaji kazi wa Wizara. Tunaipongeza Wizara kwa kuweza kuridhika na kiasi walichopokea na hii ni uthibitisho kwamba bado kuna uwezekano Serikali na Taasisi zake kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kupunguza gharama za uendeshaji Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya ziada yanapatikana aya ya 2.4 ya taarifa yetu kuhusu utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida pamoja na bajeti ya matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Nishati ilitengewa jumla ya shilingi1,886,513,219,000 ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,466,020,274,000 zilikuwa ni fedha za ndani, na shilingi 420,492,945,000 zilikuwa ni fedha za nje. Mwenendo wa mapokezi ya fedha za maendeleo unafafanuliwa katika kielelezo cha nne cha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya fedha za maendeleo za nje imeongezeka ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa. Kamati ilielezwa kwamba bajeti hiyo imeongezeka kutokana na washirika wa maendeleo kutimiza ahadi zao walizitoa kipindi cha nyuma. Vilevile Kamati iliambiwa kwamba fedha hizo zilizotoka kwa washirika wa maendeleo zilizingatia mikataba ya utekelezaji wa miradi inayoendelea ya kusambaza nishati vijijini na ujenzi wa njia za kusafirishia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya jumla ya fedha za maendeleo na inaipongeza sana Serikali kwa kuendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi kwa sekta ya nishati, isipokuwa kwenye mapokezi ya fedha za maendeleo inayotokana na vyanzo vya ndani ya nchi. Maana hadi kufikia Februari, 2026, Wizara ilikuwa imepokea shilingi 420,492,945,000 sawa na 27.97% ya bajeti ya fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba, inapeleka fedha za maendeleo zilizosalia kama ilivyoidhinishwa na Bunge hadi kufika Juni 30, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 120(1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa maendeleo kati ya tarehe 12 – 18 Machi, 2026 katika mikoa ya, Tabora, Shinyanga, na Geita. Katika ziara hiyo, Kamati ilifanya tathmini ya baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Tathmini iliyofanyika ilijumuisha uchambuzi wa mapokezi ya fedha, hali ya utekelezaji wa miradi husika pamoja na changamoto za utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ufafanuzi kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha kutengeneza Nguzo za Zege, Mradi namba 3177, Tabora. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya kutengeneza Nguzo za zege Tanzania, ambayo ni kampuni tanzu ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kiwanda hicho una thamani ya shilingi 7,911,457,500, hadi Kamati inatembelea mradi mkandarasi alikuwa ameshalipwa jumla ya shilingi 6,350,916,303.75 sawa na 80% ya thamani ya mkataba. Kamati ilielezwa kwamba kiwanda hiki kimeshakamilika na kimeshaanza uzalishaji wa nguzo za zege na kina uwezo wa kuzalisha nguzo 80 hadi 120 kwa siku. Vilevile Kamati ilielezwa kwamba kiwanda hiki kinatoa fursa za ajira za moja kwa moja 62 na ajira za muda 52 kwa wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 3102 Ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia jua Kishapu. Mradi huu unahusisha ujenzi wa mtambo wa megawati 150 za umeme wa jua kwa awamu mbili, awamu ya kwanza ujenzi wa mtambo wa megawati 50 na awamu ya pili ujenzi wa megawati 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa awamu zote mbili utagharimu jumla ya shilingi 323,096,440,545 ambazo ni fedha za mkopo kutoka Shirika la Maendeleo la Ufaransa. Aidha, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 2.84 kulipa fidia kwa wananchi waliopisha mradi. Hadi Kamati inatembelea mradi huo awamu ya kwanza ilikuwa imefika 94.8% na maandalizi ya ujenzi wa mtambo wa awamu ya pili yameanza na kwa mujibu wa mkataba awamu ya pili ya mradi huo inatarajiwa kukamilika Disemba, 2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao utaenda kuongezea

kiwango cha uzalishaji umeme kwa kiasi cha megawati 150 ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka historia ya kutekeleza mradi mkubwa wa kwanza wa kuzalisha umeme wa jua megawati 150 ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa. Aidha, hadi Kamati inatembelea, megawati 50 za awamu ya kwanza ya mradi zilikuwa zimeshaingizwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 3111, mradi wa ujenzi wa kituo cha kupooza na kusafirisha umeme cha Ibadakul Shinyanga. Mradi huu ni sehemu ya miradi ya uboreshaji wa gridi ya Taifa (Gridi Imara) ambao utakuwa na uwezo wa kupokea na kupoza umeme wa kilovoti 400 kususha 220 mpaka 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani ambazo ni shilingi 207,992,924,950. Kamati ilielezwa kwamba mradi huu ni muda wa miezi 22 na utakapokamilika unatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa Taifa ikiwemo kuunganisha njia ya msongo wa kilovoti 220 kwa ajili ya kuendesha treni ya Mwendokasi. Vilevile utasaidia shughuli za uchimbaji wa madini katika maeneo ya migodi iliyopo kanda ya ziwa na hivyo kuwezesha sekta ya madini kukusanya mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza juhudi za Serikali kupitia *TANESCO* kwa kuboresha miundombinu ya Sekta ya nishati kupitia mradi wa gridi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji kumi na tano katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama pamoja na Halmashauri ya Msalala pamoja vitongoji 15 katika Manispaa ya Geita, kwa maelezo zaidi yanapatikana katika Ibara 2(6)(4) na Ibara 2(6)(5), lakini Kamati imejiridhisha kwamba umeme umeunganishwa katika vitongoji vyote hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya ukaguzi Kamati ilijionea maendeleo mbalimbali yanayaotokana na mradi huu

ikiwemo shughuli za kiuchumi na kwa wananchi ambazo zinatumia nishati ya umeme. Kwa ujumla, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya maendeleo ya miradi ya kupeleka umeme vitongojini awamu ya pili A, katika Mikoa ya Shinyanga na Geita na mikoa mingine iliyopo Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya kiongozi wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzindua mpango wa kupeleka umeme vitongojini awamu ya pili B, ambapo jumla ya vitongoji 9009 vitapelekewa miundombinu wa umeme kwa gharama ya trilioni 1.2. Hakika huu ni mpango mkubwa wa kwanza na wa aina yake katika historia ya usambazaji wa nishati ya umeme vitongojini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 58, Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Vipaumbele vya Wizara, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu 58 Wizara ya Nishati inalenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali kama zinavyoonekana katika aya ya 3.1 ya taarifa yetu na kama ambavyo vilielezwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ikiwemo kuunganisha Mkoa wa Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa bajeti katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Nishati Fungu 58, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,525,401,129,000 ambapo kati ya fedha inayoombwa, shilingi 63,036,293,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 2,462,364,836,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongezeka kwa wastani wa asilimia saba nukta sita ukilinganisha na Bajeti ya shilingi 1,965,745,445,000 iliyotengwa kwa mwaka wa fedha unaoisha Juni, 2026, kama inavyoonekana katika kielelezo Na. 5 cha taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la Bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 ni kutokana na Serikali kuongeza shilingi

575,851,617,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hata hivyo, kama ambavyo kielelezo namba tano kinavyoonesha, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepungua kwa 20.44 % ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Nishati inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi 4,000,000 ambayo sawa na lengo la ukusanyaji wa maduhuli katika mwaka wa fedha unaoisha wa 2025/2026 kama ambavyo maelezo ya ufafanuzi yameonekana katika aya ya 3.3 ya taarifa yetu, pamoja na aya ya 3.4 na aya 3.5 imeeleza kwa kina bajeti ya matumizi ya kawaida na bajeti ya miradi ya maendeleo na kama ilivyowasilishwa mapema kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa kamati; maoni ya jumla: Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha hasa ndani katika kutekeleza majukumu ya Fungu 58 ya Wizara ya Nishati, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nishati kufanya yafuatayo: -

(a) Kuongeza ufanisi zaidi na ubunifu zaidi katika utendaji kazi wa Wizara na taasisi zake ambao utakaochochea kuboresha huduma zinazohusiana na Sekta ya Nishati nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni miongoni mwa vichocheo muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

(b) Kubuni vyanzo vipya vya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara ya Nishati, ambavyo vitaiwezesha Wizara na Serikali kujiongezea mapato na hivyo kuendelea kutenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(c) Wizara ihakikishe kwamba, huduma zinazotolewa na taasisi zake, zinakuwa bora zaidi ili kukidhi matarajio ya wadau wa sekta ya nishati; na

(d) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu na kuwepo kwa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, usimamizi madhubuti utasaidia taasisi hizo kuweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na wakati huo huo zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma na upatikanaji wa nishati nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mahususi; kipaumbele cha upatikanaji wa nishati vijijini. Kamati inaipongeza Wizara na Serikali kupitia *REA* kwa kuwezesha upatikanaji wa Nishati ya umeme hadi vitongojini. Hali hii itasaidia kuongeza kasi ya uzalishaji na ukuaji wa maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba umeme unaopelekwa maeneo ya vijijini, ambavyo leo vijiji vyote vya Tanzania vina umeme, unafika hadi kwenye shughuli kuu za uzalishaji za maeneo ya vijijini kama Kilimo na ufugaji, miradi ya maji na kuunganisha kwenye taasisi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kushauri kwamba upatikanaji wa nishati vijijini uendane na juhudi za makusudi za kuboresha miundombinu ikiwemo kutenga bajeti ya matengenezo ya mara kwa mara, na ya haraka pale miundombinu ikiwemo transfoma zinapoathiriwa na majanga ya asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama za upatikanaji wa nishati safi kwa wananchi, licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kusambaza na kuchochea matumizi ya nishati safi

kwa wananchi, bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa nishati hiyo na gharama pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba vituo vya mawakala wa kusambaza nishati safi nchini havijaenea maeneo ya vijijini, hivyo hali hiyo huongeza gharama za usafiri kwa wananchi ambao wengi vipato vyao ni vya chini. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inasambaza mawakala hadi maeneo ya vijijini ili kuwezesha upatikanaji rahisi wa nishati safi na kuondoa gharama za usafirishaji. Utekelezaji huo utachangia kwa kiasi kikubwa kuenea na matumizi ya nishati safi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania. Kamati inatambua jitihada za Serikali kupitia *TPDC* katika ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Kinyerezi hadi Chalinze pamoja na miradi mbalimbali. Ni ushauri wa Kamati kuhakikisha kwamba Serikali iharakishe ujenzi wa bomba hilo ili kurahisisha upatikanaji wa gesi asilia nchini ili kuendana na mkakati wa Kitaifa wa matumizi ya nishati safi ikiwemo gesi asilia. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kwenye mambo yafuatayo: -

(a) Serikali ihakikishe kwamba inaharakisha ujenzi wa vituo vya gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye mikoa mbalimbali kwa kuanzia na mikoa iliyopewa kipaumbele ambayo ni Morogoro, Dodoma, Arusha na Mwanza.

(b) Serikali kupitia *TPDC* na *PURA* isimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi gesi asilia kwa ufanisi ili kuimarisha upatikanaji wa nishati ya uhakika ambayo itaweza kuchangia na kukuza uchumi wa viwanda, wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

(c) Serikali kupitia *TPDC* iongeze kipaumbele pia kwenye miradi ya usambazaji wa gesi asilia nchini.

(d) Serikali ihakikishe kwamba mazungumzo baina ya wawekezaji wa mradi wa *LNG* Lindi yanakamilika mapema iwezekanavyo ili kuwezesha mradi huo kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo yote, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika miradi ya usambazaji wa gesi asilia, kwa kuwa miradi hiyo ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati itakayoongeza matumizi ya gesi katika uzalishaji wa umeme, matumizi majumbani na viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Gridi Imara. Pamoja na juhudi za Serikali kuboresha gridi ya Taifa kupitia mradi Gridi Imara bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inakamilisha kwa wakati mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme ikiwemo njia ya Chalinze - Dodoma, Chalinze - Kinyerezi-Mkuranga na Chalinze - Segera ili kuwezesha umeme wote unaozalishwa na Bwawa la Mwalimu Nyerere uweze kutumika ipasavyo katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa mafuta na kupanda bei ya gharama za mafuta nchini. Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali kwa hatua ambazo inazichukua kutafuta suluhu ya upatikanaji wa mafuta nchini na kwa bei ambayo ni himilivu kwa wananchi. Katika kipindi hiki cha kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kulikosababishwa na vita kati ya Marekani na mshirika wake Israel dhidi ya Iran.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia vikao tulivyokaa tarehe 2 na tarehe 8 Aprili, 2026 kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na taarifa kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa mafuta nchini na bei ya bidhaa za mafuta. Taarifa pia ilifafanua uamuzi wa Serikali kuhusu *TPDC* kupewa jukumu la kuagiza mafuta, kwa kipindi cha dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifafanuliwa kwamba *TPDC* imeingia makubaliano ya kuleta mafuta kwa muda wa miezi mitatu kwa *premium* ile ile ambayo wamekubaliana. Hivyo *TPDC* haitaathirika na kupanda kwa *premium* katika kipindi chote cha mkataba. Aidha, kwa mujibu ya mkataba huo, *TPDC* ina nafasi ya kujadiliana na msambazaji endapo *premium* itashuka ili kuleta unafuu kwa mraji wa bidhaa za petroli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilieleza Kamati kwamba uamuzi huo ni kwa mujibu wa Sheria. Sheria imeruhusu utaratibu mbadala wa kununua mafuta katika kipindi cha dharura kupitia kifungu cha 5(1) na 181 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 4A.(2) ya Kanuni za uagizaji wa mafuta kwa pamoja za mwaka 2017 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu hivi vinampa mamlaka Waziri anayesimamia masuala ya nishati kuweka utaratibu mbadala wa kununua mafuta nje ya mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja ili kuhakikisha nchi inakuwa na mafuta ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliihakikishia Kamati kwamba kiwango cha mafuta kinachotarajiwa kuingia nchini kitaendana na mahitaji halisi yatakayowasilishwa na wauzaji wa jumla kupitia uratibu wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja na kwamba mafuta yatapatikana kwa muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati iliridhishwa na utaratibu uliotumika wa kuipa *TPDC* na hatimaye kupatikana mzabuni wa bei nafuu ambaye atakuwa na jukumu hilo, na kwamba kulikuwa utaratibu shindani ndani ya miezi mitatu. Licha ya jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutatua changamoto hii, Kamati ina ushauri ambao uliwasilishwa kupitia taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa hatua za muda mrefu ambazo zinalenga kutatua upatikanji wa mafuta nchini na siku za baadaye kupitia utafiti wa mafuta unaoendelea katika kitalu cha Eyasi Wembele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iangalie uwezekano wa kufanya uhamisho wa fedha kati ya mafungu *Reallocation between votes,* za matumizi ya kawaida zinazoonekana kuwa na fedha, na kuzielekeza fedha hizo katika ruzuku ya mafuta kwa lengo la kudhibiti kupanda kwa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku kwenye mafuta, ambayo itasaidia kutoa ahueni kwenye gharama za bei za mafuta nchini kwa kipindi hiki cha miezi mitatu, huku ikiendelea kufanya tathmini juu ya athari za vita inayoendelea, juu ya mwenendo wa upatikanaji na bei za mafuta na hatua hii Kamati inaamini Serikali yetu inayoongzwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ina upendo na Watanzania, na kama ilivyofanya mwaka 2022 ilivyotoa ruzuku ya jumla ya shilingi bilioni 494 kwa ajili ya bei za mafuta Mei – Julai, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa matenki ya kuhifadhi mafuta. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa juhudi na ushauri ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Hali hii imesaidia Kamati katika kutekeleza jukumu ulilotupa la kufanya tathmini na kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali juu ya namna gani au hatua zipi zinaweza kuchukuliwa ili kunusuru wananchi wa Tanzania na changamoto hii ya kupanda kwa bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inamshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na Waziri wa Nishati Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa ushirikiano aliotoa wakati wa kujadili jambo ambalo tulikabidhiwa na Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii, namshukuru Mheshimiwa Spika Mussa Azzan Zungu kwa kuliongoza Bunge vyema na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Barran Sillo kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Spika kutekeleza majukumu yake, pamoja na Wenyeviti wa Bunge ukiwemo Mheshimiwa Najma Giga kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika kuendesha Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa, ninawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa imani yao kwangu na kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Ninapenda kuwaahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya kuongoza Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Wajumbe wa Kamati yangu ya Nishati na Madini, wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Nishati pamoja na taasisi zilizoko chini yake. Maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Wizara ya Nishati. Ninaomba majina yao yaingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa ushirikiano walionipa. Ninaahidi kuwatumikia ili kuijenga Bagamoyo yetu. Ninaishukuru pia familia yangu kwa ushirikiano walionipa wakati wa kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge wa Chamwino kwa kazi nzuri tangu ameteuliwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati akisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri mahiri wa Nishati Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati pamoja na wakuu wa taasisi zake *REA, TPDC, EWURA, PPBA, TANESCO, PURA* na kampuni tanzu zote chini ya uongozi wa Makatibu Wakuu wa Wizara ya Nishati ambao ni: Mhandisi Felchesmi Jossen Mramba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia umeme na nishati jadidifu; na Katibu Mkuu Dkt. James Mataragio ambaye anashughulikia mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya sekta ya nishati na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii. Ninawashukuru Wenyeviti wa Bodi zote za Taasisi chini ya Wizara ya Nishati pamoja na Wajumbe wa Bodi kwa kazi nzuri ya kusimamia taasisi na ushirikiano kwa Kamati pamoja na wadau wote wa sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru sana Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Wakili Baraka Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, ninaomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 50 - Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

***[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 121(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, mwaka , 2025]***

---

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na

Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya **Fungu 58 – Wizara ya Nishati** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya **Kanuni ya 121 (4)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge za mwaka 2025 na imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo: -

a) **Sehemu ya Kwanza** ni Utangulizi na inaeleza kuhusu Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) **Sehemu ya Pili** inaeleza kuhusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

c) **Sehemu ya Tatu** ni Uchambuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027;

d) **Sehemu ya Nne** ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na

e) **Sehemu ya Tano** ni Hitimisho.

### 1.2. Namna Kamati ilivyotekeleza Majukumu yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Kupitia ziara ya terehe 12 hadi 18 Machi, 2026 na vikao vya terehe 23 na 24 Machi 2026 Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 118 (1));

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 (Kanuni ya 120 (1));

c) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Msingi na Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Fungu 58 kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (2).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

a) Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli.

b) Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida.

c) Utekelezaji wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 2.2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Fungu 58 – Wizara ya Nishati** ilitengewa bajeti ya jumla ya **Sh. 1,965,745,445,000**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 79,232,226,000** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 1,886,513,219,000** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea **Sh. 1,165,387,590,900.58** sawa na wastani wa **asilimia 59.28** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, **Sh. 15,041,546,556.22** sawa na wastani wa **asilimia 1.3** zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Sh. 1,150,346,044,344.14** sawa na wastani wa **asilimia 98.7** ni fedha za bajeti ya maendeleo kama ambavyo **Kielelezo Na. 1** kinafafanua.

*Kielelezo 1:* ***Mwenendo wa upatikanaji wa Fedha wa Fungu 58 kwa mwaka wa Fedha 2025/2026***

| MAPOKEZI | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 79,232,226,000 | 15,041,546,556.22 | 18.98% |
| **MIRADI YA MAENDELEO** | 1,886,513,219,000 | 1,150,346,044,344.14 | 60.7% |
| **JUMLA** | **1,965,745,445,000** | **1,165,387,590,900.58** | **59.28%** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha katika Bajeti ya Fungu 58 hususan katika Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika** Kamati ilihoji juu mapokezi kidogo ya fedha za matumizi ya Kawaida ikiwa kama hayakuathiri utekelezaji wa

shughuli za Wizara ukizingatia na umuhimu wa Sekta hii ya nIshati nchini

Kamati ilipokea ufafanuzi kwamba fedha hiyo iliyopokelewa licha ya kuwa chini ya wastani uliotakiwa kufika hadi kufikia Februari 2026 ,bado haikuathiri utendaji kazi wa Wizara.Tunaipongeza Wizara kwa kuweza kuridhika na kiasi walichopokea na hii ni uthibitisho kwamba bado kuna uwezekano Serikali na Taasisi zake kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kupunguza gharama za uendeshaji Serikalini.

### 2.3 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Nishati liidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Sh. 4,000,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni stakabadhi nyinginezo na marejesho ya fedha za umma . Hadi kufikia Februari, 2026, makusanyo yalikuwa ni **Sh. 6,140,000** sawa na **asilimia 153.5** ya malengo waliyojiwekea. Mchanganuo wa mwenendo wa makusanyo unafafanuliwa katika **Kielelezo Na. 2**.

*Kielelezo 2:* ***Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli katika Mwaka wa Fedha 2025/2026***

| Chanzo cha Mapato | Kiasi kilichopangwa | Kiasi kilichokusanywa | Asilimia ya lengo |
|---|---|---|---|
| Stakabadhi nyinginezo | 1,000 | 0 | 0 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 3,999,000 | 6,140,000 | 153.5% |
| **JUMLA** | **4,000,000** | **6,140,000** | **153.5%** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, mwenendo wa makusanyo ya **Fungu 58– Wizara ya Nishati** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni wa kuridhisha. Kwakuwa hadi kufikia Februari 2026 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa umevuka lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba kuvuka huko kwa lengo la ukusanyaji wa maduhuli kunatokana na urejeshwaji wa

masurufu ya safari ambazo watumishi hawakusafiri kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa uzalendo huo waliounesha, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa kuwa chanzo hicho kilichowezesha kuvuka lengo sio cha kukitegemea kwa wakati wote.

### 2.4 Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Nishatii ilitengewa jumla ya **Sh. 79,232,226,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha **Sh. 9,299,920,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (PE) wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake na **Sh. 69,932,306,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari 2026, jumla ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizokuwa zimetolewa ni **Sh. 15,041,546,556.22** sawa na **asilimia 18.8** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo**, Sh. 5.763.351,902.88** zilkuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (P.E.) na **Sh. 9,278,194,653.34** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.) kama ambavyo Kielelezo Na. 3 kinafafanua.

***Kielelezo 3: Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kufikia Februaei, 2026***

| Na. | Matumizi | Bajeti ya Mwaka 2025/26 | Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2026 | Asilimia ya Fedha Zilipokelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Matumizi Mengineyo (OC) | 69,932,306,000 | 9,278,194,653.34 | 13% |
| 2. | Mishahara (PE) | 9,299,920,000 | 5,763,351,902.88 | 61.9% |
| **Jumla Ndogo** | | **79,232,226,000** | **15,041,546,556.22** | **18.98** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/26 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa fedha za matumizi mengineyo kwa wakati ili kuwezesha Wizara kutekeleza malengo yaliyokusudiwa kabla ya kuisha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Nishati ilitengewa jumla ya **Sh. 1,886,513,219,000** ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,466,020,274,000** zilikuwa ni fedha za ndani, na **Sh. 420,492,945,000** zilikuwa ni fedha za nje. Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Maendeleo unafafanuliwa katika Kielelezo Na. 4 kwa muhtasari.

*Kielelezo 4:* ***Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Maendeleo Bajeri ya 2025/2026***

| CHANZO | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 (TZS) | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2026 (TZS) | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 1,466,020,274,000 | 420,492,945,000 | 27.97% |
| **FEDHA ZA NJE** | 420,492.945,000 | 740,303,022,546.10 | 176.06% |
| **JUMLA** | **1,886,513,219,000** | **1,150,346,044,344.14** | **61%** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2025/26 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya fedha za maendeleo za nje imeongezeka ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa.Kamati ilielezwa kwamba bajeti hiyo imeongezeka kutokana na washirika wa maendeleo kutimiza ahadi zao walizitoa kipindi cha nyuma.Vilevile Kamati iliambiwa kwamba fedha hizo zilizotoka kwa washirika wa maendeleo zilizingatia mikataba ya utekelezaji wa miradi inayoendelea ya kusambaza nishati vijijini na ujenzi wa njia za kusafirishia umeme.

**Mheshimiwa Spika** Kamati imeridhishwa na mwenendo wa mapokezi ya jumla ya Fedha za Maendeleo na inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya sekta ya nishati nchini isipokuwa kwenye mapokezi ya fedha za maendeleo inayotokana na vyanzo vya ndani ya nchi. Hadi kufikia Februari 2026 Wizara ilikuwa imepokea 420,492,945,000 sawa na asilimia 27.97 ya Bajeti ya fedha za ndani iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**,Ni ushauri wa Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba Serikali inapeleka fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge hadi kufika tarehe 30 Juni 2026.Kutokupatikana kwa ukamilifu kwa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kunaweza kuathiri mpango kazi na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara ukizingatia umuhimu wa sekta ya Nishati kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

### 2.6 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kati ya tarehe 12 – 18 Machi, 2026 katika mikoa ya, Tabora, Shinyanga, na Geita . Katika ziara hiyo, Kamati ilifanya tathmini ya baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Tathmini iliyofanyika ilijumuisha uchambuzi wa mapokezi ya fedha, hali ya utekelezaji wa miradi husika pamoja na changamoto za utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

#### 2.6.1 Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kutengeneza Nguzo za Zege (Mradi Na. 3177), Tabora.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za zege Tanzania (TCPM) ambayo ni kampuni tanzu ya Tanesco. Kampuni hii ndiyo yenye dhamana ya kusimamia uzalishaji wa nguzo kwa kujenga viwanda vya

kuzalisha nguzo za zege na kuthibitisha ubora wa nguzo zinazozalishwa na Kampuni binafsi.

**Mheshimwa Spika,**ujenzi wa kiwanda hicho una thamani ya **shilingi 7,911,457,500.00** (ikijumuisha na kodi). Hadi kamati inatembelea mradi Mkandarasi alikuwa ameshalipwa jumla ya **shilingi 6,350,916,303.75** sawa na **asilimia 80** ya thamani ya mkataba. Aidha Kamati iliomba ufafanuzi juu ya uwezo wa kiwanda kwenye uzalishaji, maendeleo yake toka kuanzishwa na namna wananchi na Serikali itakavyonufaika na Mradi huu.

**Mheshimiwa spika,** Kamati ilielezwa kwamba kiwanda hiki kimeshakamilika na kimeshaanza uzalishaji wa nguzo za zege na kina uwezo wa kuzalisha nguzo 80 hadi 120 kwa siku.Vilevile kamati ilielezwa kwamba kiwanda hiki kinatoa fursa za ajira za moja kwa moja 62 na ajira za muda 52 kwa wazawa.

**Mheshimiwa Spika**,kutokana na ukaguzi huo wa mradi,Kamati imejiridhisha kuwa mradi huo ukiendelea kutekelezwa kwa kadri ilivyokusudiwa utakuwa na manufaa kwa Serikali ikiwemo upatikanji wa mapato kupitia kodi na kurahisisha upatikanaji wa nguzo za zege na mawasiliano kwa maeneo ya kanda ya Magharibi,kanda ya kati na kanda ya Ziwa.

### 2.6.2 Mradi Na. 3102 Ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia jua Kishapu (Shinyanga)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa huu unahusisha ujenzi wa mtambo wa megawati 150 za umeme wa jua kwa awamu mbili,awamu ya kwanza ujenzi wa mtambo wa megawati 50 na awamu ya pili ujenzi wa mtambo wa megawati 100.

**Mheshimiwa Spika,**Mradi huu kwa awamu zote mbili utagharimu jumla ya shilingi 323,096,440,545.00 ambazo ni fedha za mkopo kutoka Shirika la maendeleo la Ufaransa.Aidha Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 2.84 kulipa fidia kwa wananchi waliopisha mradi.

**Mheshimiwa Spika,**hadi Kamati inatembelea mradi huo awamu ya kwanza ilikuwa imefika asilimia 94.8 na maandalizi ya ujenzi wa

mtambo wa awamu ya pili yameanza na Kwa mujibu wa mkataba awamu ya pili ya mradi huo inatarajiwa kukamilika Disemba 2027**.**

**Mheshimiwa Spika**,kwa ujumla Kamati imeridhishwa na utekelezaji wa mradi huu ambao utaenda kuongeza kiwango cha uzalishaji umeme kwa kiasi cha megawati 150 ambazo zitaingia kwenye Gridi ya Taifa.Ni rai ya Kamati kwa Serikali kuhakikisha kwamba inapeleka fedha za kutosha na kumsimamia mkandarasi aliyepewa tenda hiyo ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati na hivyo kuboresha upatikanaji wa umeme kwa Kanda ya ziwa na maeneo ya jirani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan** kwa kuweka historia ya kutekeleza mradi mkubwa wa kwanza wa kuzalisha umeme wa jua Megawati 150 ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya Taifa,Aidha hadi Kamati inatembelea megawati 50 za awamu ya kwanza ya mradi zilikuwa zimeshaingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

### 2.6.3 Mradi Na. 3111 – Mradi wa ujenzi wa kituo cha kupooza na kusafirisha umeme cha Ibadakul((Shinyanga)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ni sehemu ya miradi ya uboreshaji wa Gridi ya Taifa (Gridi Imara) ambao utakuwa na uwezo wa kupokea na kupoza umeme wa kilovoti 400/220/33. Mradi huu pia utahusu ujenzi na ufungaji wa transfoma (mashine umba) nne zenye uwezo tofauti, ujenzi wa reactors 4 zenye ukubwa wa 50MVAr na ufungaji wa mtambo wa kuimarisha upatikanaji umeme(STATCOM) ambao utakuwa na uwezo wa 250 MVAr**.**

**Mheshimiwa Spika** Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani ambazo ni **Shilingi 207,992,924,950**. Kamati ilielezwa kwamba mradi huu ni muda wa miezi 22 na umeanza kutekelezwa rasmi tarehe 2 Januari 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba 2026.

Mradi utakapokamilika unatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa Taifa ikiwemo kuunganisha njia ya msongo wa kilovoti 220

kwa ajili ya kuendesha treni ya Mwendokasi. Vilevile kupitia msongo wa juu wa kilovoti 400 utasaidia shughuli za uchimbaji wa madini kwa maeneo ya migodi iliyopo kanda ya ziwa na hivyo kuwezesha sekta ya madini kukusanya mapato ya kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi za Serikali kupitia TANESCO katika kuboresha miundombinu ya Sekta ya nishati nchini kupitia mradi wa Gridi imara.

### 2.6.4 Mradi Na. 3180 – Mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji kumi na tano katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na Halmashauri ya Msalala

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na wakala wa Nishati Vijijini (REA) ambaye anatekeleza miradi mbalimbali itakayowezesha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji.

**Mheshimiwa Spika**,Mkoa wa Shinyanga una jumla ya vijiji 509 na vitongojji 2704. Hadi Kufikia Machi 2026 vijiji vyote 509 na vitongoji 1,180 vya mkoa wa Shinyanga vilikuwa vimeshapokea huduma ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,**hadi kufikia Machi 2026 Jimbo la Kahama mjini mradi ulikuwa umefika kwenye vitongoji 15 na wateja 369 wameshaunganishiwa umeme.Kwa upande wa jimbo la Msalala tayari mradi umeshatekelezwa kwa vitongji 15 na wateja 174 kati ya 495 walikua tayari wameshaunganishiwa umeme

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Miradi hii ni kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa wananchi waliopo maeneo ya vijijni, na kwa muktadha huo Serikali ihakikishe kwamba inawafikia wananchi wote waliobaki. Vilevile mchakato wa upelekaji wa umeme katika vitongoji uambatane na kutenga fedha za matengenezo na maboresho ya miundombinu inayopeleka umeme ambayo inaweza kuharibiwa na majanga ya asili.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla Kamati inapongeza jitihada za Serikali kwa kuibua Mradi kama huu ambao utasaidia kuboresha upatikanaji wa umeme nchi nzima.

### 2.6.5 Mradi Na. 3113 Mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji kumi na tano katika Manispaa ya Geita

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mkoa wa Geita, Mradi huu unahusisha kupeleka umeme kwenye vitongoji 105 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 21.8**. Hadi kufikia Februari 2026 mradi ulikuwa umefikia silimia 80 na vitongoji 73 vilikuwa vimeshaunganishiwa umeme.

**Mheshimiwa Spika.**Jimbo la Geita mjini jumla ya vitongoji 15 vimeshafikishiwa umeme.Kamati ilipotembelea mwezi Machi 2026 wateja 66 kati ya 311 walikuwa wameshaunganishiwa umeme.Kwa upande wa Geita Vijijini mradi umetekelzwa kwenye vitongoji 15 na unatarajiwa kuwapatia huduma ya umeme wateja wapatao 482.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara ya ukaguzi Kamati ilijionea maendeleo mbalimbali yanayaotokana na mradi huu ikiwemo shughuli za kiuchumi kwa wananchi ambazo zinatumia nishati ya umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya maendeleo ya miradi ya kupeleka umeme Vitongojini awamu ya IIA (HEP IIA) katika mkoa wa Geita na mikoa mingine iliyopo Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati pia inaipongeza Serikali ya awamu ya sita chini ya kiongozi wetu **Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzindua mpango wa kupeleka umeme vitongojini Awamu ya IIB, ambapo jumla ya vitongoji 9009 vitapelekewa miundombinu wa umeme kwa gharama ya trilioni 1.2.

Hakika huu ni mpango mkubwa wa kwanza na wa aina yake katika historia ya usambazaji wa nishati ya umeme vitongojini.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Fungu 58 – Wizara ya Nishati inalenga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya kibajeti vikiwemo vifuatavyo: -

a) **Gridi ya Taifa:** Kuunganisha mikoa ya Rukwa, Kagera, Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa na kuendelea kuimarisha Gridi ya Taifa ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika.

b) **Matumizi ya Nishati safi**: Kukuza matumizi ya Nishati safi ya kupikia kwa kuendelea kutekeleza mpango wa taifa wa Nishati wa mwaka 2025-2030.

c) **Gesi Asilia**: kuimarisha uzalishaji wa gesi asilia, kutafuta na kuenndeleza Nishati hiyo ikiwemo mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika **(Liquefied Natural gas-LNG Project**) na kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia kwa ajili ya vyombo vya moto (CNG).

d) **Upatikanaji wa bidhaa za Mafuta**: Kuhakikisha nchi inakua na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa kusimamia mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System-BPS) na ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi na usafirishaji wa bidhaa hizo ndani na nje ya nchi.

e) **Taasisi zilizo chini ya Wizara**: Kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara pamoja na kampuni Tanzu katika kutoa huduma zenye tija na ufanisi.

### 3.2 Muundo wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 2,525,401,129,000** ambapo kati ya fedha inayoombwa, **Sh. 63,036,293,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 2,462,364,836,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 7.6** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,965,745,445,000** iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha unaoisha Juni 2026. Kielelezo Na.5 kinafafanua kwa muhtsari ulinganisho kati ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Kielelezo 5: Ulinganisho wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| MAELEZO | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 79,232,226,000 | 63,036,293,000 | -16,195,933,000 | -20.44% |
| MIRADI YA MAENDELEO | 1,886,513,219,000 | 2,462,364,836,000 | +575,851,617,000 | +7.6% |
| **JUMLA** | **1,965,745,445,000** | **2,525,401,129,000** | **559,655,684,000** | **+44.66%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 58 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni kutokana na Serikali kuongeza **Sh. 575,851,617,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, kama ambavyo **Kielelezo Na. 5** kinavyoonesha, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepungua kwa **asilimia 20.44 %** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha Juni 2026.Kamati ilielezwa kwamba upungufu huo wa bajeti ya matumizi ya Kawaida umechangiwana ukomo wa bajeti ya Serikali(ceiling)

### 3.3 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Nishati inaomba kuidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Sh. 4,000,000** ambayo sawa na lengo la ukusanyaji wa maduhuli katika Mwaka wa Fedha unaoisha wa 2025/2026 Kielelezo Na. 6.

**Kielelezo 6: Ulinganisho wa makadirio ya Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| CHANZO | 2025/2026 | 2026/2027 | ONGEZEKO/ UPUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Marejesho ya Fedha za Umma (Recovery of Public Money) | **3,999,000** | **3,999,000** | **4,000,000** | **0** |
| Stakabadhi nyinginezo | **1,000** | **1,000** | **0** | **0** |
| **JUMLA** | **4,000,000** | **4,000,000** | **4,000,000** | **0** |

***Chanzo**: Randama ya Wizara ya Nishati Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na Usanifu wa Kamati.*

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imefanya tathmini kuhusu kutobadilika kwa makadirio kwenye vyanzo vya ukusanyaji wa maduhuli. Kamati imebaini kuwa vyanzo vya maduhuli kwa mwaka 2026/2027 vinafanana na vyanzo katika mwaka 2025/2026. Hii ni kutokana na kwamba vyanzo vya ukusanyaji wa maduhuli havijaongezeka.

**Mheshimiwa Spika**, Ni matarajio ya Kamati kuwa hadi kumalizika kwa robo ya nne ya mwaka wa fedha 2025/2026 kuna uwezekano kiwango cha makusanyo kikaongezeka. Hivyo ni ushauri wa Kamati kwa Wizara kuongeza kiwango cha makadirio ya maduhuli kwa miaka ijayo.

**Mheshimiwa Spika** kutokana na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli,Kamati inashauri Wizara ifanye jitihada zitakazoibua vyanzo zaidi vya mapato na hivyo kuongeza wigo wa mapato yatokanayo na ukusanyaji wa maduhuli.

### 3.4 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, **Fungu 58 – Wizara ya Nishati** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 63,036,293,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 10,097,218,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 52,939,075,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepungua kwa **Sh. 16,195,933,000**sawa **asilimia 20.44** ukilinganisha na **Sh. 79,232,226,000** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama ambavyo Kielelezo Na. 7 kinaonesha.

**Kielelezo 7: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya kawaida kati ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mwaka wa Fedha 2026/2027**

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 9,299,920,000 | 10,097,218,000 | +797,298.000 | 8% |
| MATUMIZI MENGINEYO (O.C.) | 69,932,306,000 | 52,939,075,000 | 16,993,231,000 | 24% |
| **JUMLA** | **79,232,226,000** | **63,036,293,000** | **16,195,933,000** | **0.44%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 58 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa sababu ya kupungua kwa ukomo wa bajeti *(ceiling)* ambao umeathiri sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali.

### 3.5 Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Fungu 58– Wizara ya Nishati inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 2,462,364,836,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, **Sh. 1,602,449,735,000** ni Fedha za Ndani, sawa na **asilimia 65.07** na **Sh. 859,915,101,000** ni Fedha za Nje, sawa na **asilimia 34.9** ya bajeti iliyotengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imeongezeka kwa Shilingi **575,851,615,000** sawa na wastani wa **asilimia 30.5** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 1,886,513,219,000** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Ongezeko hilo linajionyesha katika Kielelezo Na. 8.

**Kielelezo 8: Ulinganisho wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kati ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 na mwaka wa Fedha 2026/2027**

| MIRADI YA MAENDELEO | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | BAJETI YA MWAKA 2026/2027 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| **FEDHA ZA NDANI** | 1,466,020,274,000 | 1,602,449,733,000 | 136,429,459,000 | +35.44% |
| **FEDHA ZA NJE** | 420,492,945,000 | 859,915,101,000 | 439,422,156,000 | +51.1% |
| **JUMLA** | **1,886.513,219,000** | **2,462,364,836,000** | **575,851,615,000** | **30.5%** |

***Chanzo:*** *Randama ya Fungu 58 na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleomeongezeka kwa fedha za ndani na fedha za nje. Hivyo ni ushauri wa Kamati kwa Wizara na Serikali kuhakiisha kwamba miradi inayoenda kutekelezwa inaenda kuleta Tija na maendeleo ya wananchi wa Tanzania,kwakuwa fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo zinatokana na kodi za wananchi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kutoa fedha hasa ndani katika kutekeleza majukumu ya **Fungu 58 – Wizara ya Nishati**, hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi wa wizara na taasisi zake ambao utakaochochea kuboresha huduma zinazohusiana na Sekta ya Nishati nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni miongoni mwa vichocheo muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa Wananchi na Taifa letu.

b) Kubuni vyanzo vipya vya ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara ya Nishati,ambavyo vitaiwezesha Wizara na Serikali kujiongezea mapato na hivyo kuendelea kutenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

c) Serikali ihakikishe kwamba, huduma zinazotolewa na taasisi zake, zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau wa sekta ya nishati; na

d) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu *(sustainability)* na kuwepo kwa thamani ya fedha *(value for money)*.

**Mheshimiwa Spika**, aidha Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, usimamizi madhubuti utasaidia taasisi hizo kuweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na wakati huo huo zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma na upatikanaji wa Nishati nchini.

## 4.2 Maoni Mahsusi

### 4.2.1 Kipaumbele kwa upatikanaji wa Nishati Vijijini

**Mheshimiwa Spika** Kamati inaipongeza Wizara na Serikali kupitia REA kwa kuwezesha upatikanaji wa Nishati ya umeme hadi vijijini.

Hali hii itasaidia kuongeza kasi ya uzalishaji na ukuaji wa maendeleo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na pongezi hizo bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba umeme unaopelekwa maeneo ya vijijini unafika hadi kwenye shughuli kuu za uzalishaji za maeneo ya vijijini kama Kilimo na ufugaji

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kushauri kwamba upatikanaji wa Nishati Vijijini uendane na juhudi za makusudi za kuboresha miundombinu ikiwemo kutenga bajeti ya matengenezo ya mara kwa mara, na ya haraka pale miundombinu ikiwemo transforma zinapoathiriwa na majanga ya asili.

### 4.2.2 Gharama na Upatikanaji wa Nishati kwa Wananchi

**Mheshimiwa Spika**, Licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika kusambaza na kuchochea matumizi ya nishati safi kwa wananchi bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa Nishati hiyo na gharama pia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba vituo au mawakala wa kusambaza nishati safi nchini hawajenea maeneo ya vijijini hivyo hali hiyo huongeza gharama za usafiri kwa wananchi ambao wengi vipato vyao ni vya chini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inasambaza mawakala hadi maeneo ya vijijini ili kuwezesha upatikanaji rahisi wa nishati na kuondoa gharama za usafirishaji. Utekelezaji huo utachangia kwa kiasi kikubwa kuenea na matumizi ya nishati safi nchini.

### 4.2.3 Shirika la maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua jitihada za Serikali kupitia TPDC Katika ujenzi wa bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka kinyerezi hadi Chalinze.Ni ushauri wa Kamati kuhakikisha kwamba Serikali iharakishe ujenzi wa bomba hilo ili kurahisisha upatikanaji wa gesi asilia nchini ili kuendana na mkakati wa Kitaifa wa

matumizi ya nishati safi ikiwemo gesi asilia.Hivyo Kamati inaishauri Serikali kwenye mambo yafuatayo:-

a) Serikali ihakikishe kwamba inaharakisha ujenzi wa vituo vya gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) kwenye mikoa mbalimbali kwa kuanzia na mikoa iliyopewa kipaumbele ambayo ni Morogoro,Dodoma,Arusha na Mwanza.

b) Serikali kupitia TPDC isimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi gesi asilia kwa ufanisi ili kuimarisha upatikanaji wa nishati ya uhakika ambayo itaweza kuchangia na kukuza uchumi wa wananchi,viwanda na Taifa kwa ujumla.

c) Serikali kupitia TPDC kuongeza kipaumbele pia kwenye miradi ya usambazaji wa gesi asilia nchini.

d) Serikali ihakikishe kwamba mazungumzo baina ya Wawekezaji wa mradi wa LNG Lindi yanakamilika mapema iwezekanavyo ili kuwezesha mradi huo kuanza kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na hayo yote Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika miradi ya usambazaji wa gesi asilia, kwa kuwa miradi hiyo ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati itakayoongeza matumizi ya gesi katika uzalishaji wa umeme, matumizi majumbani na viwandani.

### 4.2.4 Mradi wa Gridi Imara

**Mheshimiwa spika,** pamoja na juhudi za serikali za kuboresha gridi ya Taifa kupitia mradi gridi Imara bado Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu ya kusafirisha umeme ikiwemo njia ya Chalinze- Dodoma,Chalinze-Kinyerezi-Mkuranga na Chalinze-Segera Tanga ili kuwezesha umeme wote unaozalishwa na bwawa la Mwalimu Nyerere uweze kutumika ipasavyo katika maeneo yote nchini.

### 4.2.5 Hali ya Upatikanaji wa mafuta na kupanda bei ya gharama za mafuta nchini mwezi Aprili 2026

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi zinazofanywa na Serikali kwa hatua ambazo inazichukua kutafuta suluhu ya upatikanaji wa mafuta nchini na kwa bei ambayo ni himilivu kwa wananchi Katika kipindi hiki cha kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia kulikosababishwa na vita kati ya Marekani na mshirika wake Israel dhidi ya Iran.

**Mheshimiwa Spika,**kupitia vikao tulivyokaa tarehe 2 na tarehe 8 Aprili mwaka 2026 kwa maelekezo yako, Kamati pamoja na taarifa kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa mafuta nchini na bei ya bidhaa za mafuta.Taarifa hiyo ilifafanua uamuzi wa Serikali kuhusu TPDC kupewa jukumu la kuagiza mafuta,kwa Kipindi hiki cha dharula**.**

**Mheshimiwa Spika**,Kamati ilifafanuliwa kwamba TPDC imeingia makubaliano na supplier ya kuuziwa mafuta kwa muda wa miezi mitatu (Mei hadi Julai 2026) kwa premium ile ile waliyokubaliana, hivyo TPDC haitaathirika na kupanda kwa premiums katika kipindi chote cha mkataba. Aidha, kwa mujibu ya Mkataba huo, TPDC ina nafasi ya kujadiliana na Msambazaji (Supplier) huyo endapo premium itashuka ili kuleta unafuu kwa mlaji wa bidhaa za petroli.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilieleza Kamati kwamba uamuzi huo ni kwa mujibu wa Sheria. Sheria imeruhusu utaratibu mbadala wa kununua mafuta katika kipindi cha dharura kupitia kifungu cha 5(1) na 181 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 4A. (2) ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja za mwaka 2017 pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2024. Vifungu hivi vinampa Mamlaka Waziri anayesimamia masuala ya nishati kuweka utaratibu mbadala wa kununua mafuta nje ya mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja ili kuhakikisha nchi inakuwa na mafuta ya kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Serikali iliihakikishia Kamati kwamba Kiwango cha mafuta kinachotarajiwa kuingia nchini kitaendana na mahitaji halisi yatakayowasilishwa na Wauzaji wa Jumla (OMC)

kupitia Uratibu wa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoj na kwamba mafuta yatapatikana kwa muda wote.
Aidha Kamati iliridhishwa na utaratibu wa kushindanisha makampuni 11ambayo yalishindanishwa na PBPA (4) na TPDC (7) na hatimaye kumpata mzabauni ambaye bei zake ni nafuu na atakuwa na jukumu hilo kwa miezi mitatu(3). Licha ya jitihada hizo zinazofanywa na Serikali katika kutatua changamoto hii Kamati ina Ushauri ufuatao;

a) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa hatua za muda mrefu ambazo zinalenga kutatua upatikanji wa mafuta nchini kwa wakati huu na kwa siku za baadae kupitia utafiti wa mafuta unaoendelea katika kituo cha *Eyasi Wembele*.

b) Serikali iangalie uwezekano wa kufanya uhamisho wa fedha kati ya mafungu (Reallocation between votes) za matumizi ya kawaida zinazoonekana kuwa na fedha, na kuzielekeza fedha hizo katika ruzuku ya mafuta kwa lengo la kudhibiti kupanda kwa bei.

c) Serikali iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku kwenye mafuta,ambayo itasaidia kutoa afueni kwenye gharama za bidhaa za mafuta nchini kwa kipindi hiki cha miezi mitatu(3) huku ikiendelea kufanya tathmini juu ya athari za vita inayoendelea, juu ya mwenendo wa upatikanaji na bei za mafuta.

d) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi iharakishe utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa matenki ya kuhifadhi mafuta (strategic oil reserve).

**Mheshimiwa Spika**, nichukuwe fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi kwa juhudi na Ushauri ambao umekuwa ukiutoa kwa Kamati.Hali hiyo imesaidia Kamati katika kutekeleza jukumu ulilotupa la kufanya tahmini na kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali juu ya namna gani au hatua zipi zinaweza kuchukuliwa ili kunusuru wananchi wa Tanzania na changamoto hii ya kupanda kwa bei ya mafuta nchini.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Aidha, namshukuru Naibu Spika, Mhe. Daniel Barran Sirro (Mb.) kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Nishati pamoja na taasisi zilizo chini yake. Maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb. - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Agustino Philipo Mulugo, Mb.
4. Mhe. Joseph Kasheku Msukuma, Mb.
5. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb.
6. Mhe. Aisha Msantu Mduyah, Mb.
7. Mhe. Mariam Anzuruni Mungula, Mb.
8. Mhe. Abuu Jumaa Hamoud, Mb.
9. Mhe. Nassor Said Nassor, Mb.
10. Mhe. Lulu Guyo Mwacha, Mb.
11. Mhe. Kija Limbu Ntemi, Mb.
12. Mhe. Esther Lukago Midimu, Mb.
13. Mhe. Sandali Chilombe Fadhili, Mb.
14. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb.
15. Mhe. Paul Kapalata Neto, Mb.
16. Mhe. Ali Khalil Mirza, Mb.
17. Mhe. Jacqueline Chrisant Mzindakaya, Mb.
18. Mhe. Eng. Amos William Maganga, Mb.

19. Mhe. Eng. Chacha Mwita Wambura, Mb.
20. Mhe. Dotto Jasson Bahemu, Mb.
21. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb.
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb.
23. Mhe.Godwin Oloyce Mollel,Mb.
24. Mhe. Samira Khalfan Amour, Mb

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius John Ndejembi, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb). Aidha niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Nishati pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Makatibu wakuu wa Wizara ya Nishati ambao ni Mhandisi Felchemi Jossom Mramba,Katibu Mkuu Wizara ya Nishati anayeshughulikia Umeme na Nishati jadidifu na Katibu Mkuu Dkt. James Peter Mataragio ambaye anashughulikia mafuta na gesi asilia. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya nishati, na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Wakili Baraka Leornard Idelphonce kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

### 5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 58 – Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Subira Khamis Mgalu, Mb.
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
22 Aprili, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Khamis, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa taarifa hiyo ya Kamati.

Tunaanza sasa Waheshimiwa Wabunge na mchangiaji wetu tutaanza na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo. Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuanza mchango huu. Waheshimiwa Wabunge yote tuliongea kwenye mambo ya mipango sasa hii Wizara ndiyo Wizara husika kweli kweli. Mataifa yote duniani mambo ya uchumi na ustawi wa kila Taifa, unategemea nishati. Kwa kuwa mambo yake ni mazito na ni mazuri, leo mchango wangu utakuwa kuhusu uzalishaji wa umeme; mambo ya usafirishaji, usambazaji na mambo ya gesi asilia hayo tutatafuta siku nyingine kwa sababu muda hautoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaeleze vilevile ndugu zangu historia ya *TANESCO* ambayo ndiyo inatoa umeme na kusambaza. Enzi za ukoloni ilikuwepo *DARESCO* ilikuwa inatoa umeme kwa ajili ya Dar es Salaam, halafu ilikuwepo *TANESCO* Tanganyika ya mwaka 1961, lakini ilikuwa inahudumia wale viongozi wetu wa Kikoloni. *TANESCO* mpya imeanzishwa mwaka 1964 na inafanya vizuri. Ina mizigo mizito lakini inafanya vizuri na vizuri zaidi ni *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli *REA* lazima tuipongeze sasa. Tunaipongeza Serikali yetu na bajeti inavyozidi kuendelea. Tulikuwa kwenye mabilioni tukaja kwenye shilingi trilioni moja leo hii naona wamefika shilingi trilioni 2.6. Hongera kwa Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuongeza bajeti ya hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kujadili uzalishaji wa umeme ninaweza tu nikawaeleza tutazalisha kutoka hapa, hapa, hapa, hapa itakuwa haina maana, ni lazima niende na mifano iliyofanikiwa na iliyokuwa inafanana na sisi. Wabunge wasisahau kwamba mapinduzi ya kiuchumi ya viwanda, *first industrial*

*revolution* ya mwaka 1760 mpaka 1860, hiyo miaka 100 ya kwanza. Mapinduzi haya makubwa yalitegemea nishati na teknolojia kubwa ilitegemea makaa ya mawe kuchemsha maji ili kupata *engine* zinazotumia mvuke *(steam engine)*. Kwa hiyo, unaona hapa *first industrial revolution* bado ilikuwa ni nishati. *Second industrial revolution* 1870 mpaka mwaka 1960 ndiyo tumeanza *mass production*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilicholeta mafanikio hayo nayo ni ugunduzi wa umeme (nishati). Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nimechukua nchi ambayo tulikuwa tunafanana nayo imefanikiwa na ndivyo nitakavyotoa vyanzo vyao vya uzalishaji wa umeme na kupendekeza vyanzo vya uzalishaji wa umeme wa Tanzania. Kwanza Mheshimiwa Waziri amefanya vizuri nimemsikia anataja vyanzo, yuko sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongezea hapo, nimetoa mifano ya nchi mbili ambazo kila mara na tunazifuatilia duniani. Wanasayansi wanazifuatilia kweli kweli India na China, lakini kwa ajili ya muda leo hebu niende na moja, nikienda na mbili muda hautatosha, halafu kama nilivyowaeleza inabidi wapige makofi taratibu huku wanachukua na takwimu. Kwa hiyo mapinduzi makubwa ya China yalifanywa baada ya Mao kufariki, aliyekuja yule Ding mwaka 1978 ndiyo mapinduzi makubwa kweli kweli ya uchumi wa China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kabla ya mwaka 1978 Uchumi wa China ukuaji wake ulikuwa kama uchumi wa Tanzania wa asilimia sita (*growth)*. Ilikuwa asilimia sita inakwenda, inashuka, inakwenda, inashuka kama wa Tanzania ulivyo sasa hivi. Hiyo China ilikuwa kabla ya 1978, baada ya 1978 uchumi wao ukakua kwa kasi kubwa sana kwa zaidi ya 10%, wakati mwingine ulifika 15%, ndiyo maana mlisikia ninapendekeza kwamba Dira yetu ya Maendeleo kufanikiwa lazima uchumi ukue kwa zaidi ya 10% kufikia hiyo trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mwaka 1978 *GDP per capita* ya China ilikuwa dola 156, lakini umeme waliokuwa wanatumia mtu mmoja mmoja, *consumption of electricity per person per annum* ilikuwa *kilowatt* 255, karibu tunalingana hapo.

Hata hivyo, miaka 48 toka 78 mpaka leo *GDP* yao imeenda zaidi ya dola 14,000 na matumizi ya umeme ya mtu mmoja mmoja yameenda zaidi ya *kilowatt* yaani *unit* zaidi ya 7,000, tunafanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tanzania kabla sijapendekeza vyanzo hali yetu ilivyo tulikuwa na ile *Vision 2025* tulisema kufika mwaka jana tulivyokuwa tumejipangia *GDP per capita* iwe dola 3,000 na *capacity* yetu ya kuzalisha umeme nchi nzima iwe zaidi ya *megawatt* 10,000. Hivyo tulijipangia hivo kufikia mwaka jana. Tulikuwa tunatoka *megawatt* 1,500 mpaka *megawatt* 10,000. Sasa kilichopo mbele yetu 2,050, tunasema tunataka kupata *GDP per capita* dola 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja bado sijafikia hata mapendekezo yale, twende polepole. Sasa hapo wanakula muda wangu wapunguze na kweli yeye ndiye amesema, safi kabisa Mheshimiwa Musukuma. Sasa *GDP* 7,000 ndiko tunakokwenda, trilioni moja na umeme wetu sasa hivi ni *megawatt* takriban 4,400 na matumizi ya umeme ya mtu mmoja mmoja ni *unit* 243. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowaeleza China walikuwa kama sisi wamefanikiwa na sisi nao tunaweza kufanikiwa, hiyo ni *point* ya muhimu kwamba kufanikiwa tunaweza. Sasa kutokana na hiyo, ninatoa mapendekezo ya vyanzo vya uzalishaji wa umeme. Tunahitaji umeme mwingi, tunahitaji umeme wa bei nafuu, tunahitaji umeme unaotabirika kwamba upo. Tutakavyokaribia 2,050 tutaingia kwenye uchumi wa kutumia *data center*, hatuna *data center* hata moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *data center* moja inatumia karibu *megawatt* 100, hatuna hata moja. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge umeme haujatosha, tumejitahidi lakini haujatosha. Kwa hiyo, ninaongelea umeme wa kuelekea 2,050 vyanzo: kikundi cha kwanza ni *none fossil* yaani jadidifu *green economy,* ninapendekeza tuwekeze sana kwenye umeme jua *(solar)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa China 20% ya umeme wao sasa hivi ni wa *solar* wana asilimia, ndiyo maana sisi tutatumia

asilimia tusilinganishe na wingi sisi ni wadogo lakini *shares percentage* inabaki pale pale. Umeme wao sasa hivi China wa jua ni 26% wanazalisha *gigawatt* 1,232 kwa hiyo muwe mnazidisha na 1,000 kupata *megawatt,* nibaki kwenye *gigawatt* huku. Tanzania kwa *solar* nimemsikia vizuri Mheshimiwa Waziri, ninashukuru ule wa Shinyanga umeanza kazi tulikuwa na *megawatt* 15 tumeongeza *megawatt* 50. Kwa hiyo, tuzidi kuzalisha umeme kutoka kwenye jua kwa sababu jua likiwaka sana unapata *watts* 1,000 kwa kila *square meter* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili umeme wa upepo. China sasa hivi nchi nzima umeme wao uwezo wake ni 13% wana *gigawatt* 498 zidisha mara 1,000 upate *megawatt.* Tanzania upepo hatujapata lakini spidi ya upepo inayoweza kuzalisha umeme inatakiwa iwe meta 11 kwa sekunde kama ile ya pale Same na ile ya kule Makambako. Kwa hiyo twende kwenye upepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha tatu *hydro* (maji) hii tunayo tayari. Kwa sasa hivi China 13% ya umeme wao ni *hydro,* wana *gigawatt* 498. Sisi ndio chanzo kikubwa cha umeme wetu kwa zaidi ya 68% tuna *gigawatt* 2.7 yaani *megawatt* 2,800 hivi, tuongeze kwenye maji. Ukitaka kujua kwamba kweli maji yanazalisha umeme mwingi duniani ulikuwa unatoka *Three Gorges* kwa wale ambao wameenda China. Huo mtambo mmoja ulikuwa unazalisha *gigawatt* 22, yaani *megawatt* 2,500; linganisha na bwawa la kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wanajenga jipya kabisa kule Tibet, litazalisha *gigawatt* 60 yaani wanazalisha wanajenga mitambo ya kuzalisha *megawatt* 60,000 kutoka kwenye bwawa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kingine cha nne, ninakaribia kumaliza nilipewa muda …

**MWENYEKITI:** Nimekuongezea dakika tatu.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika tatu, haya ninamalizia. Chanzo cha nne ni

*nuclear,* kwa sasa hivi China wanazalisha *gigawatt* 125 kwa *nuclear* ambayo ni *1.5%* ya umeme wao, sisi hatujaanza na ndiyo tunaanza pale Mkuju, tuna *uranium* nyingi katika maeneo mengi nchini likiwemo lile la kule Namtumbo ambapo tuna kama tani 60,000. Kwa hiyo, twende kwenye *nuclear*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba tano *biomass;* kwa China ni asilimia 1.3 ya umeme wao wote unatoka *biomass* ambayo ni *gigawatt* 50 yaani *megawatt* 50,000, sisi ya kwetu tuna *megawatt* 20.5 karibu ni 0.52. Kwa hiyo, tuongeze kwenye *bio energies.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba sita ni *geothermal* na Tanzania tumeanzisha kampuni ya *geothermal,* lakini China asilimia 1.2 ya umeme wao unatoka kwenye *geothermal* ambayo ni *gigawatt* 46 na umeme wa dunia ya sasa unaitwa ni ule *battery storages,* wanatunza umeme kwenye *battery h*alafu baadaye wanautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha pili, kikubwa sasa ndiyo *fossil fuels,* namba nane ni *natural* gas. Sisi Tanzania tunazalisha zaidi ya 28% ya umeme wetu ni *natural gas* ambayo karibu ni 1.1 *gigawatt* zaidi ya *megawatt* 1,000. China ni *2.8% of the total installed capacity,* inatoka kwenye *natural gas* ambayo ni *gigawatt* 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha tisa ni makaa ya mawe (*coal);* China ni zaidi ya *gigawatt* 1,100 ambayo ni 31% ya umeme wa China wote. Sisi tulikuwa na *megawatt* 10 kule Mbeya umeenda unapotea, lakini *reserve* yetu ya makaa ya mawe ni zaidi ya tani bilioni tano ya makaa ya mawe tuliyonayo Tanzania, lakini hatuna hata *megawatt*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni *petroleum* ambayo China wanaachana nayo, sisi tuna *megawatt* 103 ambayo ni karibu 2.6% ya umeme wetu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi ndivyo vyanzo 10 ambavyo tunapaswa kuongeza kuzalisha umeme tupate umeme mwingi wa bei nafuu na unaotabirika. Bei ya sasa ya senti tisa za Marekani kwa *unit* tukiwa na umeme mwingi na tukitaka kufanya

mageuzi ya viwanda lazima tushushe umeme wetu uje kwenye bei ya senti sita mpaka saba za Marekani mengine tutaongea siku nyingine. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga na Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda wajiandae.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia siku hii ya leo katika bajeti hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha sisi sote tuna afya na tumeweza kuwemo ndani ya hili Bunge. Pia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo anatusimamia na kutuongoza kama Kiongozi wetu Mkuu katika nchi yetu hii ya Tanzania. Pamoja na yeye niwapongeze sana na kuwashukuru wasaidizi wake wa karibu Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali hasa Wizara yetu hii ya Nishati. Kiukweli bila kificho na kila mmoja na kila Mtanzania anaona jinsi gani ambavyo Wizara ya Nishati inafanya kazi nzuri hapa Tanzania. Wizara hii imekuwa ni mojawapo ya Wizara ya mfano katika kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata umeme. Siyo kupata umeme tu hata katika *service* pale ambapo kunakuwa kuna changamoto Wizara hii watu wake wamekuwa waki-*respond* kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana watendaji wote wa *TANESCO* Tanzania kwa jinsi ambavyo wana-*respond* kwenye matatizo ya umeme yanavyokuwa yametokea kwa uharaka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee sana ni ushahidi uliotosha kabisa kuona jinsi ambavyo Wizara imeshughulika na suala la mafuta. Nchi zingine jirani tunaona kwamba kuna changamoto kubwa na wengine wamefika sehemu hata vituo havina mafuta lakini kwa Tanzania tunajivunia Wizara yetu, tunajivunia Mheshimiwa Rais wetu kwa jinsi ambavyo amehakikisha masuala ya mafuta kwetu Tanzania hatujapata upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tunavyozungumza, kwa taarifa ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba, mafuta tunayo na siyo tu kwa taarifa, ukienda kwenye vituo Tanzania nzima utakuta vituo vyote vimefunguliwa na mafuta yanapatikana. Kwa jambo hili ninapenda kuwapongeza sana Wizara ya Nishati ambayo inaongozwa na Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na mambo mazuri hayo, ninapenda kusema jambo moja. Katika maisha changamoto inapotokea inatengeneza fursa. Sasa katika suala zima la changamoto ya mafuta ilivyotokea tumeona kwamba, kuna fursa zingine zimejitokeza ambazo, kama Serikali na kama Wizara na kama Taifa, tunahitaji kuharakisha na kuongeza nguvu kuhakikisha tunaendelea kwenye hivyo vipaumbele vingine, ili pale ambapo mafuta yanaleta changamoto tuweze kupata njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hapa tunayo gesi, lakini pia, tunao umeme ambao tunaona kabisa kwamba, tuna mpaka *excess*. Tunajua kwamba, nchi zingine duniani zinabadilika, zinatoka kwenye kutegemea sana mafuta zinaenda kwenye kutegemea gesi pamoja na umeme. Sisi hapa Tanzania, wale ambao tumefanikiwa kwenda kwenye maonesho ya *TANESCO* pale, kwenye Wizara ya Nishati tumeona gari ambalo linatumia umeme. Kama leo tungekuwa tunayo magari mengi Tanzania yanayotumia umeme tusingekuwa tunawaza sana mafuta kwa sababu tungekuwa tume-*switch* na tunatumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kuangalia pia, Tanzania hapa tunayo gesi na kuna magari tayari yameanza kutumia gesi.

Ombi langu na ushauri wangu sasa kwa Serikali ni kwamba, tuongeze kasi kwa Tanzania nzima kuongeza hizi *filling station* za gesi, tuongeze hizi sehemu za kuchaji magari, ili tuhamasishe Watanzania wengi zaidi waweze kuagiza haya magari na inapotokea *crisis* kama hii, basi tuweze kupata *alternative* ambayo watu wanaweza wakatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia magari ya Dangote yanaweza yakatoka kule Mtwara mpaka Dar es Salaam kwa kutumia gesi, lakini hayo hayo magari ya Dangote hayawezi kuondoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza, kuelekea Kanda ya Ziwa kwa kutumia gesi. Wakifika Dar es Salaam inakuwa ni kituo na huku hivi inakuwa hakuna. Kwa hiyo, tukifanikiwa kuongeza *filling stations* za gesi na umeme watu hawatanunua magari na tutapunguza tatizo la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ninaomba pia, niweze kuzungumzia jambo moja lingine ambalo ninatamani niishauri Wizara yetu ya Nishati. Tunajua kabisa miundombinu yote ya umeme inamilikiwa na *TANESCO*, muundombinu wowote unapokuwa mahali popote huo muundombinu unaanza kumilikiwa na *TANESCO*. Sasa Wizara imesema kuna Sheria ipo inaruhusu mwekezaji kujiunganishia umeme halafu akawa anarudishiwa kwa asilimia kidogo kidogo, hela kiasi inaenda kwenye Wizara na kiasi anajirudishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tunalifahamu watu wachache sana. Ninaiomba Wizara iende kutangaza jambo hili, iwafahamishe wawekezaji, ili kila mwekezaji anapotaka kuweka umeme, anapokuwa na mradi wake, asisubiri *TANESCO* mpaka ipate bajeti, asisubiri Wizara mpaka ipate bajeti, aweze kujivutia umeme akiwa na *assurance* kwamba, ile pesa itarudishwa. Maana kama akiwa na *assurance* hiyo atapeleka hakika umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kuna jambo kubwa ambalo ninalichukua kuwapongeza sana *REA*. *REA* wamefanya kazi kubwa hapa Tanzania, wamesambaza umeme, umefika sehemu nyingi sana, lakini kuna jambo moja dogo ambalo wakati mwingine linachafua ule uzuri wa jambo lile ambalo limefanyika; kuna sehemu moja unakuta mwananchi mmoja anafanyiwa

*connection* na *REA* na mwananchi mwingine anafanyiwa *connection* na *TANESCO*. Gharama za ku-*connet* watu hawa ambao wako sehemu moja ni tofauti. Ninaiomba Serikali iende ikafanye tathmini upya kwa jambo hili. Ione jinsi gani inaweza ikasimamia na kuondoa hizi dosari ndogo ambazo mwisho mwisho wa siku zinaweza kuharibu jambo kubwa zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na Mungu awabariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Mwita Wambura, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga. Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Livingstone Lusinde wajiandae.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye sekta hii muhimu sana katika uchumi wa Taifa letu, ambayo ni Sekta ya Nishati. Ninaendelea pia kuipongeza sana Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo kwa ujasiri na uthabiti mkubwa, amejitoa kikweli kweli kabisa kuona kwamba, tunakuwa na mageuzi katika Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nchi yetu inaenda katika uchumi wa kati, uchumi wa viwanda. Ni uchumi ambao unahitaji sana sekta ya nishati kuwa imara, ndiyo hapo kwa hakika tutaweza kufika katika uchumi wa kati wa daraja la juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Wizara ya Nishati kwa kweli, wameleta mageuzi makubwa kweli kweli, kwenye sekta hii ya umeme. Ndugu zangu tukitaka kujua kwamba, hao watu wamefanya kazi kubwa hebu tuangalie tumetoka wapi, tuko wapi na *then* tuweze ku-*project* kuona kwamba, hao watu wanataka kutupeleka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka mpaka mwaka 2007, takribani miaka 43 toka *TANESCO* imeanza, Mheshimiwa Prof.

Muhongo amesema *TANESCO* imeanza mwaka 1964; nchi hii vijiji vyenye umeme vilikuwa 506 tu sawa na 4.1% ya vijiji vyote 12,318. Leo hii tunavyoongea vijiji vyote 12,318 tayari vina umeme na zaidi ya 61% ya vitongoji vyote 64,359 vina umeme. Leo tunaona mabadiliko makubwa ya kiuchumi na vilevile ya kijamii kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakati tukiwa shuleni, nimesoma hapa Dodoma, tulikuwa tunasoma kwa kutumia vibatari, tena vibatari vyenyewe vya *made by mimi,* leo hii mpaka kule vijijini hawa vijana wetu wanasoma kwa kutumia umeme wa *TANESCO*. Kwa kweli, ni jambo ambalo inabidi tuwapongeze sana na huu umeme vijijini tunaona umeleta mabadiliko makubwa. Leo hii vijana wana shughuli za kiuchumi wanaziendesha kulekule vijijini, tunawapongeza sana kwa kazi kubwa hii mliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke inawezekana miaka miwili, mitatu, hapo nyuma nikisema kero ninaona labda, kama hili neno ni dogo, tulikuwa na janga kubwa sana ndugu zangu Watanzania. Tulikuwa na kitu kinachoitwa mgao wa umeme, mgao wa umeme umetusumbua sana. Ulifanya hata uzalishaji wetu ukawa na changamoto nyingi kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyote vilijiendesha kwa shida na kufanya gharama za uendeshaji kuwa kubwa kwa sababu, walikuwa wanatumia umeme wa majenereta yanayoendeshwa kwa dizeli. Changamoto tulizopata zilikuwa ni kero kubwa kweli kweli, lakini leo hii ndugu zangu, binadamu tumeumbwa yale mambo mabaya huwa tunayasahau, habari ya mgao wa umeme tumeanza kuisahau tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tutakumbuka kwamba, uunganishaji wa umeme miaka mitano, mingapi kule nyuma, ilikuwa ni changamoto kubwa kwelikweli. Unakuta mwananchi amejenga nyumba yake vizuri, lakini kuunganisha umeme ilikuwa ni kazi, afadhali hata kujenga nyumba kuliko kuunganisha umeme; unaomba umeme inachukua miezi sita mpaka mwaka mzima bado hujaunganisha umeme. Leo hii ndani ya siku 10 mpaka 30 ukishaomba unaunganishiwa umeme, sisi

wote hapa ni mashahidi. Haya ni mageuzi makubwa na ni mabadiliko makubwa kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, hata kazi za dharura unaenda kuripoti; miaka mitano iliyopita kule nyuma, unaripoti hapa kwangu, kwenye bomba kuna cheche zinatoka. Ilikuwa inachukua saa 24 mpaka 48 na wakati mwingine uzalendo unakutoka, unawatafuta vishoka wanakuja wanagongagonga pale, ili kuondoa tatizo uweze kuendelea na maisha, lakini leo hii ukiripoti ndani ya saa nne, sisi wote hapa ni mashahidi, tayari unaona vijana wamefika wamefanya kazi yako, maisha yanaendelea. Kwa kweli, ni jambo ambalo linahitaji kupongezwa kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo tunajua *TANESCO* ilikotoka, walikuwa wanajiendesha kwa hasara, lakini mpaka hivi sasa *TANESCO* wanaenda kwa faida, tumeona wamerekodi faida ya takribani shilingi bilioni 500, jamani, hayo ni mageuzi makubwa, ndiyo. Waheshimiwa Mawaziri wanastahili pongezi na washikilie palepale kuona kwamba, Watanzania wanazidi kusonga mbele. Kubwa kabisa ndugu zangu Watanzania tusingependa sasa kuona tunarudi kule tulikotoka, tuhakikishe kwamba, haya mafanikio tuliyoyafikia tunayasimamia vizuri, ili kuona kwamba, haturudi tena kwenye mgao wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusudi tusiweze kurudi kwenye mgao wa umeme tuhakikishe kwamba, Serikali inaendelea kufanya uwekezaji wa uhakika na hususani, kwanza kwenye matengenezo ya mitambo tuliyonayo. Lazima tuhakikishe kwamba, matengenezo yetu yanatengenezwa kulingana na *specifications* ambazo wataalam wametuwekea. Tukikosa hapo kuna uwezekano tukarudi kule nyuma, kitu ambacho kwa kweli, kitakuwa hakifai na hatutarajii kabisa kuona tunarudi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Mheshimiwa Profesa Muhongo amesema tuendelee katika uzalishaji wa umeme na sina sababu ya kurudia kwa sababu, Profesa ameeleza vizuri kwelikweli, lakini tuhakikishe kwamba, hizi *megawatt* 4,000, katika Taifa la Watanzania zaidi ya milioni 60

bado hazitoshi. Hata hizo *megawatt* 8000 kufika mwaka 2030 juhudi iendelee, bado haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameelezea mambo ya *energy per capital*. *Energy per capital* wenzetu wako mbali, sisi leo hii bado tuko chini ya kilowatt 300 kwa kila Mtanzania, ni kidogo sana hiyo. Kwa hiyo, tuhakikishe uzalishaji wetu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, ninarudi sasa upande upande wa *REA*. Ninaungana na wenzangu wote kupongeza sana taasisi yetu ya *REA* kwa kweli, wameendelea kufanya kazi nzuri. Leo hii tunaongelea kwamba, vijiji vyote 12,318 vimekwisha, 61% ya vitongoji vyote 64,359 vimekwisha na bado tunaendelea, kufikia mwaka 2030 tutakuwa na 100%, lakini hili linaweza vilevile likatu-*take by surprise* tukasema kwamba, labda yawezekana kazi ya *REA* inakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kama ni kazi ya *REA* sasa ndiyo inaanza kwa sababu, wahenga wetu walituambia, walitufundisha kwamba, kuzaa mtoto siyo kazi, kazi kubwa ni kumlea. *REA* wametuzalia mtoto; sasa je, huyu mtoto apate kwashakoo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia katika kipindi hiki kifupi katika ule mtandao wa umeme wa msongo wa kilovoti 33 ambao *TANESCO* wanaumiliki, takriban kilomita 80,000 *REA* wamechangia zaidi ya kilomita 38,000. Huu mtandao si kitu chepesi ni kitu kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tumeona njia za umeme za *three phases* zimekuwa ni kubwa sana. Mradi wa gridi imara tunaomba kwa kweli, usimamiwe kwa nguvu zote kwa sababu, kweli pamoja na mambo mazuri haya, lakini bado kuna changamoto ya kukatika kwa umeme kwa sababu, mtandao wa *three phases* umekuwa mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuwa na mtandao wa kilomita 80,000 na kwa *REA* pekee yake 38,000 kwa kipindi kifupi hiki maana yake ni nini? Maana yake mtandao wa kilomita 38,000 ni zaidi ya nguzo 400,000 zimeweza kuingia kwenye

*system* kwa muda huu mmoja. Maana yake ni kwamba, hizi nguzo zimetengenezwa kwa teknolojia moja, kwa *spec* moja. Maana yake ni kwamba, zitazeeka pamoja na kuna uwezekano zitakufa pamoja. Sasa ni lazima hilo tulione kwamba, *ok,* sasa tunaenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanaweza yakatokea majanga kwamba, leo umekaa hapo unasikia kwa watani zangu kule Pwani nguzo 800 zimeanguka, hujakaa sawa unaambiwa hapa Dodoma zimeanguka 600, hujakaa sawa unaambiwa kule Kagera zimeanguka 200. Hilo litakuwa ni janga, tuanze kuliangalia na kuona tunaenda namna gani na ndiyo maana nimesema kwamba, kama ni kazi ya *REA,* sasa kazi yake ndiyo inaanza. Hakika tufanye kila linalowezekana, kama kuna uwezekano tuwaongezee hata bajeti, ili waanze kazi ya kumlea huyu mtoto kusudi aweze kuwa na faida katika Taifa la Tanzania.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Amosy William.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Livingstone Lusinde wajiandae.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, ninachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, ninachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, hasa katika kuiendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nishati ninaweza kusema katika Mkoa wetu wa Mtwara tayari vijiji 785 vyote vina umeme. Sasa hivi vitongoji 2,798, kati ya vitongoji 3,421 tayari vimeshapata

umeme na kazi inayoendelea ni kupeleka umeme katika vitongoji 555. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninapenda kujikita katika mambo machache. Mheshimiwa Profesa Muhongo, mwalimu wangu, ameongea kuhusu *data* na nitajitahidi kidogo kuzungumzia mambo mawili, matatu ya Mkoa wa Lindi na Mtwara. Jambo la kwanza ni suala la Gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu leo tuna miaka zaidi ya 65, lakini Mkoa wa Lindi na Mtwara haujaunganishwa na Gridi ya Taifa. Sisi Lindi na Mtwara kwa Miradi ya *SONGAS,* ambayo wakati inafanya kazi ilikuwa inazalisha zaidi ya *megawatt* 180 mpaka 190, lakini pia, gesi asilia inatoka Mtwara na hizo zote zinachangia katika Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai matumizi ya rasilimali za nchi hii ni ya watu wote, lakini mpaka leo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha bajeti yake kesho, ninaomba alete majawabu kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Ni lini wataunganishwa na Gridi ya Taifa, ambayo katika mikoa yote sasa hivi tumebaki sisi Lindi na Mtwara? Yaani wote wameunganishwa, bado sisi Lindi na Mtwara. Halafu sisi ndiyo tunatoa gesi nyingi, ambayo pia, inachangia katika Gridi yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai gesi ni rasilimali ya nchi yote, lakini sisi ambao tuna gesi ni muhimu pia, kupata vipaumbele hivyo. Kwa hiyo, sisi tunajua kuna mkandarasi anayejenga *line* kubwa, ambayo inatoa umeme kutoka Songea mpaka Masasi anaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 53. Ninaomba Mheshimiwa Waziri aje na majawabu ya lini sasa mkandarasi yule alitoka *site*? Je, kama yupo, tayari ameanza kazi? Kama hajaanza kazi, Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu, nitashikilia shilingi yake na shemeji yangu yupo pale ili anipe majawabu ya Lindi na Mtwara, lini sasa mradi mkubwa huu na hii mikoa miwili itaunganishwa katika Gridi ya Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kwenye *REA,* hesabu ni rahisi sana. Kwa hesabu ya kawaida, hapa katika Mkoa wa

Mtwara kuna vijiji 77 katika huu mpango wa pili, yaani *Home let Electrification Project 2B*, Mkoa wa Mtwara una vijiji 77, Mkoa wa Lindi una vijiji 159, jumla kuu ukijumlisha hivi vijiji vyote unapata vitongoji 77 na vitongoji vya Lindi 159. *In total* ukijumlisha unapata vitongoji 555.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua tu kuchukua *sample*. Ukienda Ruvuma wenzetu vitongoji ambavyo vipo katika hii *Hepic Two* ambayo ni *Home let Electrification Project 2B* wana jumla ya vitongoji 634, ni zaidi ya vitongoji vyote vya Mtwara na Lindi. Nikachukua hesabu nyingine, Mkoa wa Mwanza wao wana jumla ya vitongoji 634, lakini jumla kuu ya Mtwara na Lindi ni vitongoji 555.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha bajeti yake aje na mpango kabambe wa kuongeza vitongoji katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, ili atuongezee tufikie vitongoji 700 ambapo sasa tutakuwa na 350 Lindi na 350 Mtwara, tutakuwa tumefanya kazi kubwa na tumepiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza Mradi wa Dharura wa Masasi - Newala. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hakika, mwaka huu tulikuwa na *RCC*, nilizungumza kuhusu shida ya umeme katika Jimbo la Newala na Mkoa mzima wa Mtwara. Mtwara unakatika umeme zaidi ya mara 20, leo Waziri alinipigia aliniambia siyo mara 20 nipunguze kidogo, lakini nikamwambia twende Newala tukakae mimi na yeye, akaniambia ni kweli unakatika sana, lakini hakutaka kukubaliana na mimi zaidi ya mara 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme, baada ya kelele zangu, kumbe Waheshimiwa Wabunge kupiga kelele inasaidia. Mheshimiwa Rais alisikia akaidhinisha *4.6 billion* kujenga Mradi wa Dharura kutoka Masasi mpaka Newala. Nichukue nafasi hii, mimi ni mgumu wa kupongeza, lakini nimkupongeze Waziri, pia ninampongeza *DG* wa *TANESCO*. Hakika nilimwambia Waziri, asingeweza kukamilisha huu mradi leo hii, kama ningeikamata shilingi yake na mradi huu ukikamilika wananchi wa Newala

wanaenda kupata umeme wa uhakika, tena umeme usio na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunatumia umeme wa kilometa zaidi ya 1,850 kufika Newala. Maana yake utoke unakotoka Lindi, ufike Mtwara, ufike Nanyamba, ufike Tandahimba, unakuja Newala tayari. Shida ikitokea Nanyamba tayari wananchi wa Newala wanaenda kupata matatizo. Kwa hiyo, Waziri anapokuja kuhitimisha bajeti yako, aje na majawabu atuambie sasa huu mradi wetu wa dharura ambao alisema unakamilika Machi mwaka huu, je utakamilika lini ili wananchi wa Newala waweze kunufaika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia ningependa kuchangia ni Mradi wa *LNG*. Mradi wa *LNG* kila siku umekuwa kwenye maneno tu. Nilikuwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi, wakati huo ndiyo gesi inatoka, haitoki, tulipambana sana na Rais Mstaafu Jakaya Kikwete, alitoa shilingi 6,000,000,000 mwaka 2015 kulipa wananchi wa eneo la Likong'o.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa *DC* kipindi hicho na wakatuambia mradi huu utakuja kusainiwa ndani ya miezi minne au mitano ijayo. Ameondoka, amekuja Mheshimiwa Magufuli naye tukaambiwa mradi huu sasa unahitajika ufanyiwe marekebisho, *review* kubwa inatakiwa kufanyika, lakini tukae mkao wa kula, lakini wale wananchi wa Likong'o tayari tumeshawalipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amekuja mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan, wanatuambia sasa tuko katika majadiliano ya mwisho. Sisi hatutaki kusikia majadiliano ya mwisho, watuambie wanasaini lini mkataba ule. Maana yake ni nini? Wenzetu wa Msumbiji wana matatizo makubwa sana, tayari wameshakamilisha kusaini, wameshasainiana mikataba ya dola 20,000,000,000 katika Mkoa wa Cabo Delgado, ambayo ni zaidi ya 50,000,000,000,000 katika Mkoa wa Cabo Delgado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu walikuwa na matatizo ya *Al-Shabaab* na nini na *TotalEnergies* tayari wameshaanza kazi wanaendelea na kazi pale. Sisi bado maendeleo, sisi mchakato

unaendelea, sisi mchakato unaendelea, mchakato unaendelea, wenzetu wa Cabo Delgado, Msumbiji na Mtwara ni baba mmoja, mama mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa Waziri anapokuja kuhitimisha atuambie sasa huu Mradi wa *LNG* utaanza lini ili na sasa wenzetu wa Msumbiji wakianza kufanya kazi na sisi huku tuanze kufanya kazi ili tuwe na *win-win situation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie, huu Mradi wa *LNG,* ninafikiri wananchi wa Mtwara na Lindi hawataki tena kusikia haya maneno wanasaini, wanasema basi tumwachie Mwenyezi Mungu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuhitimisha, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atamalizia.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Nishati. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa bajeti nzuri, bajeti ambayo imebeba taswira ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ukurasa Namba 16 kwenye maelezo ya chama inasema CCM inatambua kuwa umeme ni kichocheo muhimu cha ukuaji wa shughuli za maendeleo ya kiuchumi. Kwa kuzingatia haya katika kipindi cha mwaka 2025 - 2030 itatendelea kuisimamia Serikali kuongeza kasi ya uzalishaji wa umeme na kuimarisha usambazaji wake, lengo ni kuona kuwa kila kaya inakuwa na huduma ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, hii ndiyo bajeti ya kwanza tunashuhudia katika asilimia mia moja ya bajeti, asilimia 97.5 zinaenda kwenye maendeleo. Hakuna mpinzani wa nchi hii anaweza kupinga jambo kubwa kama hili ambalo Waziri anaonyesha kwa dhati na kwa dhamira ya moyo kwamba anaenda kuinua Taifa letu kwenye suala la umeme. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na tunaamini kwamba hata walioko nje, vijana wenzetu watatuunga mkono kwenye Bajeti ya Nishati ya mwaka wa fedha 2025/2026. Hongera sana Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia mambo machache. Jambo la kwanza, niwapongeze Katibu Mkuu wa Wizara, lakini na wote ambao wanasimamia *customer care* ya *TANESCO* imebadilika, kumekuwa na *improvement* kubwa sana. Tunawapongeza kwa kuboresha *customer care*, kumekuwa kukitokea dharura tunaona kabisa kuna mabadiliko, watu wanapata taarifa kwa wakati, watu wanahudumiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo ambavyo wanasema vijana hawataki kona kona na wao wameonyesha kwamba hawataki kona kona kwenye kutoa taarifa ya changamoto za umeme zinavyotokea ili kuondokana na kipindi hiki ambacho dunia inakimbizana na taarifa potofu, wao wamekuwa wakiwahi, tunawashukuru sana sana sana kitengo cha *TANESCO* na *emergency* kwa maana ya kitengo kile cha *emergency* na *customer care*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine kwa Mheshimiwa Waziri, kwenye bajeti yake, asilimia kubwa imejikita kwenye uzalishaji, usambazaji wa umeme. Nizungumze jambo moja tu kwamba, ukisoma Dira matarajio yetu baada ya mwaka 2050, tunategemea kutumia umeme *megawatt* 20,000 – 59,000, tafsiri yake lazima tuongeze *speed* ya kuzalisha umeme. Tuzalishe umeme lakini pia tuendelee na hoja yake ya kuimarisha gridi ya Taifa, gridi imara kwa sababu tutazalisha umeme, lakini gridi ya Taifa kama itakuwa au gridi imara itakuwa ni mbovu, umeme hautawafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumkumbusha Waziri kwamba, wananchi wa Makete tunalo Bwawa la Umeme la Rumakali. Bwawa hili ni bwawa linalohitajika sana limeshafanya *demarcation*, limeshafanya *evaluation*, tunachohitaji ni wananchi walipwe, bwawa liweze kuanza kujengwa na umeme uanze kuzalishwa pale. Wakifanya hivi watasaidia nchi yetu kwa sababu tusije tukafika kipindi ambacho tutapata mgao wa umeme wakati sasa hivi tuna nafasi ya kutafuta vyanzo mbalimbali, vyanzo vya upepo, vyanzo vya gesi na vyanzo vingine. Kwa hiyo kwa niaba ya wananchi wa Makete nikukumbushe hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia kwa sababu Makete wakati ninaingia kuwa Mbunge tulikuwa na vijiji 32 tu vyenye umeme, leo ninazungumza, vijiji vyote vina umeme. Watanzania lazima wafahamu, Taifa letu sisi siyo kijiwe fulani kidogo au kama ni nchi ndogo, unavyozungumzia umeme unawaka Mtwara, ndivyo umeme unavyowaka kule Bunda kwa Esther Bulaya, unavyozungumzia umeme unawaka Makete, ndivyo ambavyo umeme unawaka kule Korogwe, nchi nzima Rais Samia amefikisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa, ni jambo la heshima na nchi yetu siyo nchi tambarare, ni nchi yenye milima na mabonde, lakini *TANESCO* wamefanya kazi. Tunawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya usambazaji wa umeme, waendelee kusambaza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waziri wamesambaza umeme, wametufikia, *distribution* yetu imeenda vizuri, *REA* wakimaliza kusambaza umeme, nini kinafuata? Tunajua kuna sheria ya *Rural Energy Act* ya mwaka 2005, tunaamini baadaye watahitaji kuwachukua *REA* na kuwaweka *TANESCO*. Ushauri wangu kama Mbunge na ushauri wa wananchi wengi, kwa sababu *distribution* itakuwa imeenda sehemu kubwa ya nchi, tafsiri yake ni lazima tuongeze *manpower* ya watu kuwahudumia tofauti na hapo tutabaki na *TANESCO* wako Wilayani tu kwenye Kata na pengine kutakuwa na changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vema kama Waziri afikirie ni jinsi gani ya kuifanya *REA* iendelee ku-*exist* ili ihudumie *distribution*. Tunatamani shirika la *TANESCO* libaki kwenye *production* na *transmission*, suala la *distribution* tuiachie *REA* ifanye kazi hiyo isimamie hapo ili wananchi wetu tena wasigeuke kero kwa sababu katika nchi yoyote ile *revolution* inafanyika kwenye mambo mawili ambayo ni barabara na umeme na wamefanya kazi kubwa sana kwenye umeme, tunahitaji wananchi wapate huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu ninatamani angalia namna gani sasa wananchi huko waliko, umeme *KIOSK* zipatikane kwenye kila Kata au kila Tarafa ili wananchi waweze kupata huduma kwa wakati waweze kuhudumiwa kuliko kusubiria wilayani. Kwa sababu kuna sehemu kama Makete ukitoka Matamba kwenda kuitafuta kata nyingine iliko ni zaidi ya kilometa mia moja, huyo mwananchi akisubiria hilo tatizo linalomsumbua. Kwa hiyo, ninatamani waimarishe hilo eneo la kuhakikisha kwamba huduma inawafikia wananchi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, nchi yetu katika nchi 20 Barani Afrika sisi tumo kwenye usambazaji wa umeme, hii ni ripoti ya *World Bank* ya mwaka 2023. Katika nchi 20 ambazo zipo katika Barani Afrika sisi tuko katika usambazaji wa umeme kwa wananchi wetu. Tafsiri yake ni nini Mheshimiwa Waziri? Tafsiri yake ni kwamba wananchi wengi watahitaji kuendelea kuutumia umeme na watahitaji huduma ya umeme hususani kwenye viwanda na maeneo mengine kwa sababu tunayo ilani yetu ambayo inasema tunaenda kujenga viwanda, kongani ya viwanda kwenye kila wilaya. Tafsiri yake ni kwamba matumizi ya umeme yatakuwa ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapa tu mfano mmoja Matumizi ya umeme kwa Mkoa wa Iringa kwa mwaka mmoja ni sawasawa na matumizi ya mwezi mmoja ya Mgodi wa Geita. Mgodi wa Geita unatumia umeme kwa mwezi mmoja ambao ni sawasawa na mwaka mzima wa Mkoa Iringa, tafsiri yake mahitaji ya umeme yataendelea kuwa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza kwamba sasa hivi Geita wameingiza gridi ya Taifa kwa sababu pale nyuma walikuwa wanakata kutokana na kwamba walikuwa na changamoto, tunahitaji kuongeza uzalishaji wa umeme kwenye nchi yetu, ajitahidi sana Mheshimiwa Deo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku moja Rais alitumia lugha hii, unaweza ukawa kiongozi lakini usipate nafasi ya kuongoza, lakini unaweza ukawa kiongozi ukapata matukio mawili tu ya kuongoza katika uongozi wako. Moja kati ya tukio ambalo Waziri ameongoza ni hili la mafuta na tunaamini lingine atakalotuongoza ni jinsi gani ya kuhudumia na kuhakikisha kwamba umeme unazalishwa ndani ya nchi yetu, siyo kila kiongozi anapata nafasi ya kutuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Magufuli alikuwa ni kiongozi, lakini alipata nafasi ya kutuongoza kwenye miradi ya kimkakati ambayo hadi sasa tunaendelea nayo, alipata nafasi ya kutuongoza kwenye suala la *COVID*, nchi ikatoka na ikaenda, sasa tunaamini hata wao kwenye Wizara hii kama vijana, wana maono wanafikiria, watuongoze kwenye uzalishaji wa umeme mwingine zaidi ili aweze kuwasaidia Watanzania wengi kadri ambavyo tunafikiria. Kwa sababu tofauti na hapo Mheshimiwa Waziri tutaenda kwenye *disaster,* umeme utakwisha, umeme utapungua, mahitaji ni makubwa na tumesambaza kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Makete niendelee kusisitiza Mheshimiwa Deo, sina mambo mengi ya kuzungumza, ninaomba wananchi na Wabunge wenzangu wote tuunge mkono hii bajeti ya Nishati. Tuunge mkono bajeti ya Nishati kwa sababu ukizungumzia vijana wa Tanzania umeme ulivyowafikia vijijini, wengi wameanzisha saluni, wengi wameanzisha sehemu ya kuchomelea, wengi wameanzisha vitu vingi. Vijana Tanzania Wizara hii wamewafanya wainuke kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Wabunge bajeti hii 97.5% tuwaunge mkono Mheshimiwa Deo, tumuunge mkono Naibu Waziri Salome, hatumuungi tu mkono Mheshimiwa Deo tunaunga mkono Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Ilani ambayo

imebeba mustakabali wa Taifa letu, Ilani ambayo imebeba *revolution* ya viwanda ya Taifa letu, Ilani ambayo imebeba kwamba tunaenda kufanya mabadiliko ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana na nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Kutokana na muda, mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii adhimu kabisa ili niweze kutoa mchango wangu katika hii Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ni Mbunge sasa ninaweza kusema ni miongoni mwa Wabunge wachache wa vipindi vingi, ni kipindi changu cha nne hapa Bungeni. Kwa hiyo, nina uzoefu siyo haba, nina uzoefu mkubwa na ninataka niwaambie ndugu zangu, bajeti zote zilizopita za Serikali katika Wizara hii asilimia kubwa ilikuwa inakwenda kwenye matumizi ya kawaida, lakini leo tunaona bajeti hii kwa mara ya kwanza 97% inakwenda kwenye maendeleo. 97% inakwenda kwenye maendeleo, asilimia mbili, tatu tu zinabaki kwa ajili ya matumizi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona nia ya Mheshimiwa Rais, unaona nia ya Waziri pamoja na Wizara yake, namna wanavyotaka kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. Ujue unaweza kutenga bajeti kati ya 100%, 70% ikaenda kwenye matumizi binafsi, vitafunwa, mishahara nini, lakini hapa tunaona 97% ya fedha zote zinakwenda kwenye maendeleo kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, tunaona *seriousness* ya Serikali katika fedha zote zilizotengwa shilingi 1,500,000,000,000, zote ni za kwetu, zote ni za ndani. Shilingi 63,000,000,000 tu ndiyo zinatoka nje kwa wafadhili. Kwa hiyo, tunaona namna ambavyo

Serikali imejitoa muhanga kuhakikisha kwamba mambo haya ya maendeleo kuhusu nishati ya umeme yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama hapa nikazungumza sana kuhusu mafuta nikaishauri Serikali kwamba tujenge hifadhi yetu ya mafuta, Serikali yetu ni sikivu ninampongeza sana Rais. Nimeona Wizara hii, Rais walimwalika akaenda kuzindua ujenzi wa matanki ya mafuta ya kwetu, sasa mara nyingi ukijua kulaumu ujue na kusifia, huwezi kujua kitu kimoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anayefanya kazi ya lawama anafanya kazi rahisi siku zote, wewe unajenga nyumba kwa shida kubwa, anakuja mwenzako anakwambia mbovu, nyumba hii mbovu unamuuliza, hata kibanda hana! Kwa hiyo, unaweza kuona namna ambavyo wengine wanafanya kazi ya lawama kwa sababu ni kazi rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpongeze sana Waziri kwa hatua wanazozichukua, tumesambaza umeme kwa kiwango kikubwa, Wabunge wametahadharisha, lakini ninataka niwaombe jambo lingine ambalo humu halijazungumzwa. Umeme mwingi tuliojenga vijijini sasa hivi ugomvi mkubwa watu wanataka umeme mkubwa kwenye kila kijiji, wanataka umeme wa *three phase* ili ukiwasha mashine ya maji umeme usizimike kwenye taasisi zingine, maana yake sasa hivi ukiwasha mashine ya maji mtu wa kuchomelea hawezi, mtu wa mashine ya kusaga hawezi. Sasa tunataka umeme mkubwa kwenye vijijini ili shughuli zote ziweze kufanyika kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiseme sasa wachomeleaji msichomelee, mashine zimeni, kwa sababu sisi tunajaza maji kwenye tenki, hapana! Vijiji navyo vinahitaji umeme mkubwa kwa ajili ya maendeleo. Hatutaki umeme wa kumulika tu sasa tunataka umeme wa kufanyia kazi kwenye viwanda vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona namna ambavyo Mheshimiwa Rais amepewa u-*champion* wa gesi duniani. Wizara yenu hii Mheshimiwa Deo pamoja na mwenzake Salome Makamba na Katibu Mkuu *Engineer* Mramba ni Wizara

watambuka. Hao wakizalisha gesi safi ya kupikia ya kutosha wataondoa adha kwenye Wizara zingine, hata mkaa wataokoa hautakatwa mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkaa unakatwa mwingi kwa sababu watu hawana nishati nyingine ya kupikia, Mheshimiwa Rais kawatwisha zigo hilo wao, wahakikishe kwamba nishati safi ya kupikia inapatikana vijijini na mijini, kwa sababu mijini ndiyo waagizaji wakubwa wa mkaa kutoka vijijini. Kwa hiyo, Wizara hii ni Wizara mtambuka, wakisimamia wakafanya kazi kwa bidii mambo mengi yatakuwa yako safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* inapoteza mapato mengi sana, kwa nini? Tulisema taasisi za Serikali zisomane, kuna *TANESCO* kuna nyingine taasisi haiko kwao, ninafikiri inaitwa *WMA* ambao wao ni Wakala wa Taifa wa Vipimo. Mita nyingi tunazotumia za umeme zinatakiwa kupimwa kabla ya kufungiwa kwa mteja. Sasa tunaangalia kuna mita nyingi zimefungwa kwenye majumba yetu na kwenye taasisi mbalimbali hazijapimwa, matokeo yake nini kinatokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza umeme tunaibiwa, wale watumiaji wajanja kwenye viwanda kama mita haijapimwa umeme unaweza ukapita bure, pili unaweza ukamwadhibu mtu kwamba ametumia umeme mwingi kumbe mita ile haijapimwa inatumia umeme mwingi wakati yeye hana matumizi makubwa ya umeme kiasi hicho. Kwa hiyo, tunashauri mita za umeme zipimwe na zifungwe *seal* ili mwananchi ajue mita yangu ni sahihi. Watu weo wakija kukagua kwa mwananchi wanasema wewe unaiba umeme, kumbe haibi umeme mita ni mbovu, mita haijapimwa! Sasa unamlaumu vipi mlaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafikiri wakizipima mita zote za umeme nchi nzima wakawafungia wananchi, uwezekano wa ninyi kukusanya mapato halali ni mkubwa kuliko sasa ambapo wanachukua tu mita zingine zinafungwa bila kupimwa. Hebu chukulia viwanda vikubwa, vitatu tu vikiwa vinapitisha umeme kwenye mita bila kuhesabiwa ni hasara kiasi gani *TANESCO* inapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukulia mwananchi wa kawaida tu mtaani, unapita unamwambia anaiba umeme, unamfungia kupata huduma za umeme. Hapana, tusifanye ulinzi wa buibui! Buibui anaweka ulinzi wa uzi mwenye ule uzi anaouweka buibui ananasa mbu, ananasa nzi lakini akija ndege anauchukua ule uzi anapita nao moja kwa moja, tuweke sheria zinazoangalia pande zote mbili mlaji na wao wenyewe

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kadri unavyosambaza huduma za umeme ndivyo ambavyo unahitaji vifaa vingi. Ninashauri Serikali iimarishe viwanda vya ndani vya kuzalisha vifaa vya umeme, ili wakati mwingine tusije tukakaa hapa tunasubiri *transformer* itoke China, tunasubiri sijui nini itoke wapi, sisi wenyewe hatuna uwezo wa kutengeneza? Tuimarishe viwanda vyetu ili hivi vifaa viwe vinazunguka katika mzunguko wa ndani ya Taifa, tukitaka vifaa tuvipate hapa na viwe na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna wanasayansi wa kutosha, Mawaziri vijana wamewekwa hapo, hebu wssomane pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Judith waone namna gani wanaweza wakatufanyia kazi nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kwenye vitongoji, hapa nimeona tunazungumzia habari ya Ilani ya Chama ni sawa, lakini tungekuwa kila Wizara ikae pamoja na kitabu cha sensa ya watu na makazi, kitawaongoza kujua wingi wa watu hapa. Unajua kuna sehemu wamepeleka huduma nyingi, watu wachache, kuna sehemu watu wengi, huduma kidogo, kwa sababu hawakai na kitabu cha sensa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri akiwa na sensa ya watu na makazi itamwongoza kusema hivi umeme ninaowapelekea hawa watu utawatosha, lakini waking'ang'ana tu kwamba tunapeleka kila wilaya, kwa mfano hata huduma tu za *emergency* hivi utalinganisha Wilaya ya Chamwino na baadhi ya Wilaya? Wilaya ya Chamwino *square* kilometa zake tu sehemu nyingine ni Mkoa. Sasa nguzo kumi zikianguka Ilangali, nguzo zingine zimeanguka Haneti hilo gari linaanzia wapi? Tunawagombanisha wananchi na Rais wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengine wa *TANESCO* ambao siyo waadilifu wanasema unajua tuko tunashughulikia Ikulu, unashughulikia Ikulu wananchi nao si wanatakiwa wapate umeme? Kwa hiyo, ningeshauri tuangalie ukubwa wa wilaya ikiwezekana tuzikate katika *zones,* wilaya inayostahili magari mawili ipewe magari mawili, hata kama wilaya ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wilaya zingine wataziumiza kwa sababu ni wilaya kubwa na zinahudumia watu wengi, kama Wilaya ya Uyui ninaambiwa hapa nayo anapeleka gari moja haiwezekani! Ninaona ndugu yangu Mheshimiwa Nape anatingisha anasema bwana hata Jimboni kwangu nikipata nafasi nitapiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri kwamba tufike mahali tukiimarishe Kitengo cha *Emergency* kifanye kazi, hawa watu wamepambana mwaka huu kwenye mvua hii tumewaona, tunapita huko mitaani tunakuta vijana wetu wanakesha kubeba nguzo kwenye mapori makubwa, wanastahili pongezi jamani siyo kila kitu ni kulaumu tu! Watu wanajitoa kwa ajili ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wameng'atwa na nyoka wengine huko porini wamepoteza Maisha, sisi tulipata taarifa, ni vitu vya kutisha wanalipambania Taifa hili liweze kwenda, sisi hatuwezi kukaa hapa kama hatuoni, tuongeze juhudi za kuwasogezea vifaa karibu, vifaa vingi na ikiwezekana tuendelee kusomesha vijana wetu ili waendelee kulibeba Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo yamezungumzwa mengi katika Wizara hii, lakini nilisema nizungumze kuipongeza Serikali, kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa msimamo wake hasa wa kuhakikisha kwamba akina mama wanapika kwa kutumia gesi iliyo salama kuhakikisha tunakuwa *champion* wa gesi, haya mambo mengine tutaendelea tutasukumana taratibu, lakini yale ya msingi tuyasimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde kwa kuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, nitataja Waheshimiwa ambao wataanza kuchangia jioni, tutaanza na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, watafuatia Mheshimiwa Samira Khalifani Amour, Mheshimiwa Ali Khalil Mirza, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula. Hao ndiyo watakuwa wachangiaji wetu wa jioni kwa kuanzia.

Waheshimiwa Wabunge, hapa ninalo tangazo kutoka kwa Katibu kwa Wabunge wote wa CCM, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaume wa CCM wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi miaka 45 kuwa, kutakuwa na Kikao Saa 7.00 Mchana baada ya kipindi hiki cha Asubuhi kumalizika, yaani mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Kikao hicho kitafanyika kwenye Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo wahusika wote waliotangaziwa wanaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninasitisha Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**22 APRILI, 2026**

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na mjadala wa hoja iliyoko mbele yetu. Sasa ninamwita Mheshimiwa Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Samira Khalifani Amour na Mheshimiwa Ali Khalil Mirza ajiandae.

Mheshimiwa Samira.

**MHE. SAMIRA K. AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kipekee kabisa ninapenda kukupongeza kwa kunipatia nafasi na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni ya leo kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Waziri wetu wa Nishati na dada yangu Naibu Waziri kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini na maendeleo kwa Watanzania kwa ujumla. Kipekee kabisa ninapenda kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote ni mashahidi, mwaka 2024 alizindua mkakati wa nishati safi ya kupikia. Jambo hili liliinua matumaini mapya na mazuri yanayoonyesha namna wananchi wa kawaida, hasa vijijini, watakavyokwenda kunufaika na mkakati huu ifikapo 2034. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijikite kuchangia nishati safi ya kupikia. Sote ni mashahidi, tumeona Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa ni kinara wa kuhamasisha matumizi safi ya nishati ya kupikia. Hii ni ishara tosha kwamba anatujali wanawake wa Tanzania. Kwa hakika tunapika kwa haraka, familia zetu zimeweza

kula kwa wakati na tunaendelea na majukumu mengine ya kukuza uchumi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuishauri Serikali yangu, tumesikiliza vizuri hotuba na Bajeti ya Nishati kwa mpango mkakati mzuri waliouweka ili kurahisisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia. Ninaomba nishauri; tuweke mikakati bora, tujikite zaidi kushughulikia, kama jinsi tunavyoweza kupata mafuta katika vijiji, kwenye wilaya, ukiwa na shilingi 2,000 unapata mafuta ya taa, basi vivyo hivyo tuboreshe tuweze kupata gesi. Tuingie makubaliano na sekta binafsi, wale ambao wana *filling stations* waweze kuuza na gesi, pale mwananchi wa kijijini atakapokuwa na shilingi 2,000 au 3,000 aweze kupata kilo moja ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kagera ninapotoka, kwa wanawake wa kijijini kabisa, mwanamke wa Nkwenda huko, mwanamke wa Kituntu, kumwambia kwamba kanunue gesi ya shilingi 25,000 inakuwa ni mtihani sana. Akipata unafuu wa kuweza kununua gesi kwa bei ndogo kutokana na fedha yake aliyonayo tutafikia malengo yale Dkt. Samia Suluhu Hassan anayotamani kuyaona kwa kila mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema; Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa ni kinara. Kama tunavyosikia sasa hivi kuna ruzuku ya mitungi ya gesi. Ninaomba nishauri Serikali yangu, pindi wanapohitaji kugawa hiyo mitungi ya gesi basi vyema tukashirikishwa sisi Wabunge wa Viti Maalum, kwa sababu ndiyo tunaojua wanawake wanaohitaji hiyo mitungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Dkt. Samia Suluhu Hassan akiendelea kuhamasisha. Hata jana amekutana na makundi ya mamalishe na babalishe. Hiyo yote ni ishara kwamba amedhamiria na anatamani kuona kila Mtanzania anatumia nishati safi ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kusema; Wizara ya Nishati imejipanga vizuri, ninawapongeza sana. Tunaona sasa hivi kama ni umeme tunaenda kupata umeme kwa kila kitongoji. Ninapenda kuwashukuru sana; lakini niwaombe Wabunge wenzangu tushirikiane na Mheshimiwa Waziri wetu. Anajituma

sana na maendeleo tunayaona. Bajeti ina matumaini kwa kila Mtanzania. Ninaomba tumpitishie bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi ya kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Ali Khalil Mirza, atafuatiwa na Mheshimiwa Marirta Kivunge, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. ALI KHALIL MIRZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu ili kuchangia, ninapenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima nikaweza kufanikisha shughuli hii. Aidha, ninachukua nafasi hii pia kukishukuru Chama changu Cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kukiwakilisha chama chetu katika Jimbo la Kiembe Samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwendelezo huo huo ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni hii. Kwanza ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri yenye maono, yenye maelekeo, inayotia moyo na inayoonekana inaelekea wapi katika kuliendeleza Taifa letu, hasa katika sekta hii ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna maendeleo ya uchumi au ya jamii yanayoweza kuendelea bila nishati iliyokuwa ya uhakika na nishati ambayo itakuwa na bei nafuu. Tumeona mipango yetu ya Dira 2025 – 2030 na 2030 – 2050, imeelekeza kwamba kwanza kuwe na uchumi utakaokuwa kutoka asilimia 5.7 kwenda asilimia saba na pia kuelekea katika uchumi wa shilingi trilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo hayo ambayo yanatarajiwa yote yanategemea nishati ya umeme. Hakuna maendeleo, hakuna uwekezaji na hakuna ukuaji wowote wa biashara na uchumi utakaoweza kufanikiwa bila umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeziona juhudi ambazo zimechukuliwa chini ya uongozi wa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu

Hassan, za kuongeza umeme kutoka uliokuwa megawati 1,400 hadi leo megawati 2,500. Hayo ni maendeleo makubwa ambayo yataweza kubeba matumaini ya sisi kuendelea kama uchumi wetu ulivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uendelezaji wa nishati ya umeme, sera ya nishati ya umeme imeeleza kwamba tunaweza kuwa na umeme mbadala na vyanzo mbalimbali. Hilo ni moja ambalo limezungumzwa tangu asubuhi, kwa hivyo ninapenda kulisisitiza kwamba tuingie katika umeme mbadala katika nyanja mbalimbali; umeme wa jua, umeme wa upepo, umeme wa bahari na kadhalika. Hiyo itatupa uhakika zaidi, umahiri zaidi wa upatikanaji umeme uliokuwa wa uhakika na umeme ambao utakuwa wa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia suala la umeme ninapenda kuzungumzia kidogo suala la gesi. Tuna mazungumzo yanayoendelea ya gesi ya shilingi bilioni 42; na hii ndiyo *game changer* katika nchi yetu. Mazungumzo hayo tunaomba yaendelee vizuri na yatakapokamilika ninategemea kwamba nchi yetu itapiga hatua kubwa ya kimaendeleo, lakini pia mapato ya nchi yatazidi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sisi tunaendelea katika mazungumzo hayo, ningeshauri taasisi inayosimamia masuala ya gesi na petroli ikajitayarisha katika eneo la elimu. Tunahitaji kuwafunza vijana wetu, tunahitaji kuwapeleka katika vyuo mbalimbali ili tujitayarishe kabisa katika hizo *technicalities* za eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu kwa upande wa *technically*, hata kwa upande wa wale watakaoingia katika mazungumzo *(negotiations),* sisi tunahitaji ku-*develop* katika *negotiation skills* zetu ili tuweze kuwa sawasawa na wale ambao sisi tutakuwa tunazungumza nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, ninapenda kuunga mkono moja kwa moja Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Marirta Kivunge, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula ajiandae.

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama na kuchangia katika Bunge lako Tukufu, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kunipa kibali cha kuwa mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kukishukuru chama changu, Chama Cha Mapinduzi, chini ya Mwenyekiti Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniona ninafaa na kuniteua kuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Arusha. Vile vile, ninawashukuru wanawake wa Mkoa wa Arusha kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao, ninawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta maendeleo katika sekta ya nishati. Kwa pamoja ninapenda kuipongeza Wizara ya Nishati, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Deogratius Ndejembi; ninapenda kumpongeza Naibu Waziri, Salome Makamba na ninapenda kuwapongeza watendaji wote kwa juhudi kubwa ya kuboresha upatikanaji wa umeme na nishati safi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Arusha tumeshuhudia maendeleo makubwa. Kati ya vitongoji 1,505, vitongoji 945 vimeshapata nishati ya umeme. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii inafungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa Arusha, hususan wanawake. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwemo Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Mtera. Miradi hii ya kimkakati imepunguza changamoto ya kukatika kwa umeme. Sisi wote ni mashahidi, umeme ulikuwa unakatika mara kwa mara, ukipita unakutana na

majenereta yanawaka, lakini sasa hivi changamoto hiyo imepungua. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, Mkoa wa Arusha bado una changamoto. Takriban vitongoji 400 havijafikiwa na huduma ya umeme na tukizingatia Mkoa wa Arusha ni kitovu cha utalii, mjini na vijijini. Ninaishauri Serikali kuharakisha kupeleka umeme katika vitongoji vilivyobakia kusudi maendeleo ya kiuchumi yaweze kuendelea kwa wananchi wa Arusha hususan wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wako. Ninamwita Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula na Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba iliyowasilishwa na Waziri wa Nishati. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nishati kwa namna ambavyo wameweza kufanya kazi kubwa katika kusambaza umeme kwenye maeneo yetu. Kipekee zaidi ninawapongeza Shirika la *REA* kwa kazi kubwa na ya kihistoria ambayo wameifanya, ya kusambaza umeme katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni wa pili kwa sasa ukiacha Afrika Kusini kwenye *connectivity* ya umeme. Yaani ule umeme ambao sasa unaenda kwa mlaji sisi tupo nafasi ya pili. Jambo hili ni kubwa kwetu kihistoria; na ninataka niseme, kwamba tuendelee kuiunga mkono Wizara hii ya Nishati pamoja na *REA* ili Watanzania wengi waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri wa Nishati. Katika vitongoji ambavyo vimeweza kutoka kwa maeneo mengi kwa Wabunge, nimepata vitongoji 98; na Wilaya yangu ya Bahi ina vitongoji 520 na sasa vitongoji 300 vitakuwa na umeme. Kasi hii tunayoenda nayo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, kwamba bado lipo tatizo la kuunganishiwa umeme. Mwananchi akitaka kuweka umeme kwenye nyumba yake anaambiwa unatakiwa uchangie nguzo hapa nne, nguzo tatu, inafika mpaka shilingi 600,000 mwananchi atoe. Ninadhani hatutendi haki katika jambo hili. Suala la kununua nguzo, suala la kuweka nguzo si suala la yule mlaji wa mwisho, ni suala la *TANESCO* ndiyo wanaotakiwa waniletee nguzo pale. Kwa kufanya hivyo, kwa sababu mimi ni mteja wao wa kudumu ile gharama ya nguzo itakuja kukatwa baadaye. Tukifanya hivi tutasaidia wananchi wengi waweze kuweka umeme katika nyumba zao; lakini kumwambia mwananchi alipie umeme mimi ninaiona siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine; umeme wetu sasa tunazalisha megawati 4,522, lakini umeme wetu kama ilivyo katika maeneo mengine, ni kwamba unatoka kwenye *source* mpaka kule unakokwenda kuwashwa kwenye balbu, hakuna sehemu unasema utautunza halafu baadaye uweze kwenda kwa mlaji wa mwisho, tunafanya hivi. Sasa, bado ninaishauri Serikali ipime *exactly megawatt* tunazozipata kwa walaji ni kiasi gani. Sawa tuna jumla ya tunazozalisha lakini je, *exactly* kwa walaji ni kiasi gani? Maana yangu nini; ni kwamba upo upotevu mkubwa wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nichangie kuhusu upimaji wa mita tunazofungiwa kwa ajili ya LUKU zetu za umeme. Wakala wa vipimo ndiye anayepima zile mita za LUKU kabla mlaji hajaanza kuzitumia. Bahati mbaya *TANESCO,* ukilinganisha na wenzao wa Wizara ya Maji, imekuwa haipimi zile mita. *TANESCO* kwa mwaka inatumia mita kati ya 500,000 mpaka 800,000 lakini hazipimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hazipimwi shida inakuja wapi? Ninaweza nikapewa LUKU au mita ambayo inakuwa haiwezi kusoma umeme. Ninaweza nikanunua umeme, nikakaa nao miezi mitano au ninaweza nikanunua umeme nikatumia siku mbili umeme umekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko kwenye Kamati ya Viwanda. Tulitembelea pale kwa Wakala wa Vipimo na

wakasema na kilio hiki ni kikubwa. Walisema kwamba *TANESCO* hawataki. Sisi tukasema, tusiiseme *TANESCO* pamoja kama *TANESCO,* ninadhani ni ile idara ya manunuzi. Kwa sababu mtu anayeuza zile mita jukumu la kwamba lazima zipimwe ni suala la kisheria katika ile Sheria ya Vipimo, Sura Na. 340. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mtu mwingine anaweza akajiuliza umuhimu wa kupima ni nini? Umuhimu wa kupima zile mita ndiyo kama huu niliosema; ninaweza nikauziwa mita ambayo haisomi au ninaweza nikauziwa mita ambayo nikiweka umeme wangu unaisha haraka, vile vile, hata hitilafu nyingine za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kupima kiwango cha umeme kupitia kwenye ile sheria na kwenye kanuni ile ya 22 unaangalia kiwango cha *watts* zilizokwenda, lakini vile vile hata kiwango cha *temperature*; sasa hiyo ni ya kitaalam. Kwa hiyo, shida nyingine ya nyumba zetu kuungua na ajali za umeme zinatokana na kifaa kile ambacho pale kinasoma umeme unaoingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba Mheshimiwa Waziri anavyokuja ku-*windup* kwenye bajeti hii, ni kwamba *TANESCO* ni lazima wale *supplier* wanaowauzia mita wasiwape kabla hazijapimwa kwa sababu watu wa maji wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mita moja kwa mlaji wa kawaida ni shilingi 10,000 halafu wale wa biashara ni shilingi 20,000. Wale wa migodi nadhani na viwanda nayo iko juu kidogo. Sasa bei ile wanaweza wakaifanya kwamba wakai-*subsidize* kwamba badala ya yule *supplier* alipe pale, wao wanaweza kuweka utaratibu gani namna ambavyo wanaweza kuifidia. Ninaomba jambo hili liweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1976 tuliweza kuzindua *TIPER* (kampuni ya kusafisha mafuta hapa nchini). Bahati mbaya tukaja kuacha zoezi lile la kusafisha mafuta tumekuwa tunaagiza. Ninaomba jambo hili Serikali sasa ilifanyie kazi. Kwanza kwa mwaka jana tumepitisha lita bilioni 11, bilioni sita za mafuta ya hapa nchini, bilioni tano kwa mafuta kwa ajili ya *transit*. Kwa hiyo

tuna mahitaji makubwa sana. Kwa kufanya hivyo sisi tutakuwa tuna-*supply* mafuta kwa Nchi za Congo na nchi zote zinazotutegemea. Sawa mafuta ya Uganda yanapita kwetu hapa na yana mkataba na yale makampuni mawili ya Ufaransa na China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukaongea kwamba na sisi tununue *crude oil* tusafishe hapa tuweze kuuza na nchi yetu itakuwa haina shida ya mafuta. Ninadhani Serikali isiwaze hela, iwaze wazo zuri hili kwamba tuwe na *refinery* hapa ili tuweze kutengeneza mafuta ya kwetu hapa na tuweze kuziuzia nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, imetokea kwamba suala zima la sintofahamu iliyotokea ya kupanda kwa mafuta na hili ninaloliongea tukishakuwa na *refinery* ya kwetu ina maana tutakuwa na uwezo wa kuwa na *stability* kubwa na *security of supply* ya mafuta katika nchi yetu na wananchi wetu tutaweza kuwauzia katika bei ndogo zaidi kwa sababu mafuta tutazalisha hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wako. Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula, atafuatiwa na Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha, Mheshimiwa Asha Salum Motto ajiandae.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili kuweka mchango wangu katika Wizara yetu hii ya Nishati. Kwanza kabisa ninaanza kwa kumshukuru Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia zawadi ya uhai na kuweza kusimama katika Bunge hili Tukufu kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ya moyo ninapenda kutoa pongezi zangu na shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake makubwa juu ya kutuletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara. Nikiwa kama Mjumbe wa Kamati kwa kweli tunaridhishwa na namna ambavyo Wizara inapambana kutatua changamoto za wananchi, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na msemo ambao unasema kwamba 'Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu', lakini ukitafakari upya utaona kabisa nishati ndiyo *engine* ya maendeleo ya sekta zote. Ninasema hivyo kwa sababu hakuna viwanda bila nishati ya umeme, hakuna biashara bila nishati ya umeme, hakuna hata hicho kilimo cha kisasa bila nishati ya umeme, lakini hakuna teknolojia bila nishati ya umeme. Hapo utakubaliana nami kwamba nishati ndiyo *engine* ya maendeleo ya sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Taifa lolote lililowahi kupiga hatua bila kuwekeza kwenye nishati ya umeme. Hapa hata tukiangalia Mataifa ambayo yamefanikiwa, tukiangalia China zamani ilikuwa ni Taifa la kilimo, lakini leo China ni kiwanda cha dunia kwa sababu waliwekeza kwenye nishati ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninaomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mwanamama shupavu, jasiri, mzalendo na mwenye maono makubwa. Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani suala la upatikanaji wa umeme vijijini lilikuwa limefika 66%, lakini leo tunavyoongea, suala la umeme vijijini upatikanaji wa umeme vijijini limebaki kuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo ndiyo Rais ambaye anatambua kwamba nishati ya umeme ndiyo *engine* ya maendeleo ya Taifa letu. Lakini tumeona tumeshatoka kwenye *level* ya vijiji tuko kwenye vitongoji na kwenyewe tunapiga hatua na muda si mrefu tunakwenda kumaliza tatizo la upatikanaji wa umeme katika vitongoji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutuma salamu za Wanarukwa. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani

hajatusahau Wanarukwa. Wakati anafika suala la upatikanaji wa umeme vijijini lilikuwa 58%, leo Rukwa vijiji vyote 339 vina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi Rukwa tuna vitongoji 1,816. Katika vitongoji hivyo, vitongoji 1,507 vyote tayari vina umeme na vitongoji 300 vilivyobaki hivyo, vitongoji 156 tayari mkandarasi yuko *site*. Tunapotoa kura za kishindo kwa Mheshimiwa Dkt. Samia tuna sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hayo ndiyo mafanikio ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya katika sekta hii. Tunaona dhamira yake ya vitendo ya kutuletea maendeleo Taifa letu kupitia nishati. Hapa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais amewaamini sana, wao ni vijana, kasi yao ni nzuri, tunafurahishwa na namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yao. Mungu awabariki sana, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuleta maombi ya Wanarukwa. Pamoja na jitihada nzuri ambazo zimefanywa na Serikali, kwenye upande wa umeme, tuna Kituo cha Kupozea Umeme cha Malangali, kiko Wilaya ya Sumbawanga Mjini. Sisi Sumbawanga tunachukua umeme pia kutoka Zambia, lakini umeme ule unatutosha kwa matumizi ya mwanga na shughuli za kawaida. Leo Mheshimiwa Rais ameshatoa shilingi bilioni 200 kuwawezesha akina mama na vijana wakajikwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama watahitaji kuanzisha viwanda vidogo, vijana watahitaji kuanzisha viwanda vidogo. Sasa tunahitaji kupata umeme wa uhakika utakaoenda kukidhi matamanio na matarajio ya wananchi wetu. Upatikanaji wa kituo hiki cha kupozea pale Sumbawanga, Malangali utatusaidia sisi watu wa Rukwa kuwa na umeme wetu wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulipaswa kuwa umekamilika mwezi Aprili mwaka huu, lakini kwa changamoto ambazo zipo, mradi huo mpaka sasa haujakamilika. Ninamwomba sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri, yeye ni msikivu, lakini wewe ni mchapakazi. Namwomba sana atusaidie

kuhakikisha Mradi huu wa Kituo cha Kupozea Umeme wa Malangali unakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi maalum kutoka kwa wanawake wa Mkoa wa Rukwa. Ukiangalia hali ya nishati safi ya kupikia katika Mkoa wetu wa Rukwa, hii ni ajenda ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan moja ya ajenda zake anatamani kuona akina mama wa Taifa hili wanatumia nishati safi na salama ya kupikia, lakini kwetu sisi Mkoa wa Rukwa, hali ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ni 11.4% tu na 88% ya wananchi wa Rukwa wanatumia mkaa na kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, akina mama wa Rukwa wanahitaji wapewe elimu, akina mama wa Rukwa wanahitaji waambiwe manufaa sahihi ya kutumia nishati safi, lakini akina mama wa Rukwa wanahitaji kuwezeshwa vitendea kazi hasa hiyo mitungi ambayo iko kwenye ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua akina mama ndiyo wako mstari wa mbele kuhakikisha familia zinakwenda vizuri. Kwa hiyo, tutakapotatua changamoto hii ya kuhakikisha akina mama wanapika vizuri, akina mama wanapika kwa haraka lakini akina mama wanapata pia afya njema kutokana na matumizi safi ya kupikia. Kwa hiyo ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Rukwa tuko tayari kupokea mafunzo kutoka Wizarani kwake. Wakati wowote tushirikishe wanawake wapo tutawaandaa waweze kupewa mafunzo, lakini pia waweze kupewa vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hapa kwa dhati ya moyo kulipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninampongeza Mheshimiwa Spika, lakini ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo tulishughulikia changamoto ya mafuta wakati imetokea siku chache zilizopita. Mheshimiwa Spika aliongoza vikao vingi, lakini pia timu ya Wizara, lakini na Waheshimiwa Wabunge maoni yao na ushauri wao. Ndiyo maana mpaka leo Taifa letu lipo kwenye utulivu mkubwa sana, Waheshimiwa Wabunge ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tumeona dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais na ameshaelekeza kwamba ofisi yake ibane matumizi, lakini hatujui vita itakwenda mpaka lini. Sisi kama Serikali lazima tujiandae kuchukua tahadhari, mafuta kama yataendelea kupanda hali za wananchi wetu zitakuwa mbaya zaidi. Kwa hiyo, kama Serikali ninaungana na ushauri wa Kamati, tujiandae kisaikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mwaka 2022 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilipotokea vita ya Ukraine, alitoa shilingi bilioni 100 kila mwezi kwa ajili ya kuweka ruzuku kwenye mafuta. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri aangalie namna nzuri ambayo kama vita itaendelea tuone namna nzuri ya kwenda kuwasaidia wananchi wetu ili wasiende kupata mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa machache haya, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sylvia. Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Salum Motto na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga ajiandae.

**MHE. LULU G. MWACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninachukua fursa hii kukushukuru sana kwa nafasi uliyonipa ya kuchangia Wizara hii muhimu, mahususi ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jemedari wetu kwa kazi kubwa anayoifanya katika kusukuma maendeleo katika sekta nzima ya nishati. Pia ninawapongeza wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kukimbiza gurudumu la maendeleo katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii pia kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi, Waziri wa Nishati pamoja na dada yangu Mheshimiwa Salome Makamba

pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya hasa katika kipindi hiki cha mpito katika Taifa letu. Ninampongeza sana kaka yangu ninaona hata amepungua kidogo baada ya *Strait of Hormuz* kufungwa lakini ninawatia moyo sana, kazi siyo rahisi, lakini nina hakika tutapita salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea suala la nishati tunaongelea uhai wa uchumi wetu, tunaongelea fursa za ajira kwa vijana wetu, tunaongelea matumaini ya kila mwanamke wa Taifa hili kujikwamua kiuchumi kupitia Sekta ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaongelea kila mfanyabiashara mdogo mdogo ambaye ana nia ya kupanua biashara yake na kuongeza kipato chake. Tunapojadili hotuba hii, tunapojadili bajeti hii tuna nia ya dhati ya kuhakikisha wananchi wetu wanaendelea kujikwamua kiuchumi kupitia Wizara yetu ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana kuipongeza Serikali yangu, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio makubwa waliyofanya katika Sekta hii ya Nishati. Kumetekelezwa mradi mkubwa wa umeme wa jua ambao ni *megawatts* 150 ambao mpaka kufikia sasa *megawatts* 50 zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mradi mkubwa wa kupokea na kupoza umeme ambao ni wa *kilowatts* 400 kwenda 220 mpaka 33. Mradi huu umetekelezwa kwa fedha za ndani ambazo ni shilingi bilioni 2.7 ambazo ni fedha zetu wenyewe za ndani. Hii yote ni katika kuimarisha Sekta hii ya Nishati ambayo inaendelea kuwaletea matokeo chanya Watanzania wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kuipongeza Serikali kupitia *TANESCO* kwa kuendelea kuimarisha miundombinu ya nishati ambayo imeweza kufikisha umeme mpaka vijiji vyote. Mpaka saa hizi tumeendelea kwenye vitongoji ambapo miezi kadhaa iliyopita mradi mkubwa wa shilingi trilioni 1.2 umesainiwa

kufikisha umeme kwenye vitongoji 9,009 kwenye nchi yetu yote. Kwa hivyo, ninaipongeza sana Serikali kupitia Wakala wake wa *REA*. Ninaipongeza pia Serikali kwa ajili ya nishati hii safi ya kupikia ambayo katika hili Mheshimiwa Rais amekuwa *champion* wetu Barani Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya Serikali katika Sekta hii ya Nishati, lakini kumekuwa na changamoto kubwa katika *fees* ya *connectivity* ya umeme kwenye vijiji vyetu. Umeme wa *REA* ilisemekana kuunganishwa ni shilingi 27,000, lakini kuna baadhi ya vijiji ambavyo wanaunganishiwa ule umeme kwa shilingi 370,000. Tunakuwa hatuwatendei haki wale wanavijiji ambao wanatakiwa waunganishiwe kwa shilingi 370,000. Hivyo ninaiomba sana Serikali yangu, ninaomba sana sana tuwe na *fair price* kwa watu wote wa vijijini. Tuangalie namna ambavyo kwa hao watu wa vijijini tunaweza tukapunguza *price* ikawa kote *fair* kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo limejitokeza wananchi wengi wa vijijini wanalalamika, kuna suala la ulipaji wa *units*. Mwanakijiji akilipa umeme zaidi ya shilingi 9,000 anatolewa kwenye ule mfumo wa chini kupelekwa mfumo wa kati. *Let's say* kuna mtu mjini kamnunulia umeme wa shilingi 100,000, kesho wanamtoa kutoka kwenye ule mfumo wa chini wanampeleka kwenye mfumo wa kati ambao baada ya hapo anakuwa analipa gharama zaidi. Kwa mwananchi wa kijijini anashindwa anakuwa anakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kila mwananchi wa Kitanzania aweze kuunganishiwa umeme na aweze kutumia kwa gharama nafuu. Kwa hivyo, ninaiomba sana Serikali waangalie pia na suala la bei hiyo kwamba akiwa ni shilingi 9,000 akizidisha anatakiwa awe analipa zaidi. Tunaomba sana Serikali waangalie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye suala la nishati safi ya kupikia, kwenye hili suala ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara nzima ya Nishati. Wananchi wa kijijini wakishanunua gesi wanashindwa kuendelea kununua kwa wakati mwingine kwa sababu ya bei zake zinakuwa kubwa.

Mwananchi wa kijijini anashindwa kununua kwa shilingi 25,000 ama shilingi 56,000. Kwa hivyo, ninaomba Serikali yangu iangalie namna ambavyo hawa wanakijiji waweze kununua gesi kulingana na kipato chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, isiwe lazima iwe kwamba lazima anunue kilo sita ule mtungi mdogo ama ule mtungi mkubwa kilo 15, basi kuwe kuna ujazo hata wa kilo moja kwamba leo ana shilingi 3,000 anaweza kununua gesi ya shilingi 3,000, leo ana shilingi 6,000 ama shilingi 5,000 wanaweza kununua gesi ya shilingi 5,000 ama shilingi 6,000. Kwa sababu mwananchi wa kijijini leo anaona bora akanunue mkaa wa shilingi 5,000 ama shilingi 2,000 aendelee kupikia mkaa au kuni kutokana na gharama kubwa za gesi. Kwa hivyo ninaiomba Serikali yangu sana iendelee kupunguza gharama za gesi ambapo tutakwenda kuwasaidia wananchi hususan vijana na wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali yangu kuhusu suala la mafuta, hapa tunapopitia kipindi cha mpito Serikali imehakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kubaki salama. Lakini niishauri Serikali yangu iendelee kuhakikisha inakuwepo na *reserve* kubwa ya mafuta, ili wakati mwingine jambo kama hili linavyotokea tunakuwa hatuna wasiwasi kwamba wananchi wetu watakosa mafuta. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali yangu iendelee kuwaangalia wananchi wake kwa namna ya jicho la tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lulu, ahsante sana. Nimemwita Mheshimiwa Asha Salum Motto, atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daud Silanga, Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah ajiandae.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Nishati 2026/2027. Dira ya Maendeleo ya Taifa imethibisha kuwa nishati ni kichocheo muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu ambapo inawezesha ukuaji wa viwanda, inaongeza

tija katika uzalishaji, lakini inaboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii sana kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta hii ya nishati, nimpongeze sana kaka yangu Waziri na Naibu Waziri wa Nishati, kazi wanazozifanya zinaonekana kwa vitendo, nishati ni muhimu kwa Taifa letu na tunasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia kuona maboresho ya uzalishaji wa umeme kwa kiasi kikubwa sana, tunaona ukamilishaji wa Bwawa kubwa sana la Mwalimu Nyerere limefikia 98%. Hii ni kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, niipongeze sana *TANESCO* (Shirika la Umeme Tanzania) kwa maboresho ya miundombinu ya umeme katika kupitia Kampuni Tanzu ya *ETDCO*. Kampuni hii inafanya kazi kubwa. Hivyo, ninaomba niishauri Serikali kuongeza kiasi cha fedha kwenye kampuni hii ili iweze kufikia maeneo mengi Nchini Tanzania. Kwa sababu miundombinu mingi iliyopo ni ya zamani, sehemu nyingi tunatumia nguzo zile za zamani, kwa hiyo unakuta wakati mwingine umeme unakatikakatika kutokana na uchakavu wa miundombinu ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia kwa uzalishaji wa nguzo bora na za kisasa za umeme Nchini Tanzania, kwa kweli hii hatua ni kubwa, maana zamani nguzo zilikuwa zinatoka nje kwa gharama kubwa sana. Ninaomba niishauri Serikali kupitia Shirika hili la *TANESCO* ambalo ndiyo wasimamizi, hii Kampuni Tanzu ambayo inatwa *TCPM* inayozalisha hizi nguzo, iangalie namna bora ya kutawanya uzalishaji badala ya kutangaza tenda kwa makampuni yenyewe ikafanye mazungumzo kwenye zile sehemu ambazo zinazalishwa *cement,* makampuni yale yanayozalisha *cement. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hizi nguzo zinatumia *cement* yale makampuni yatakuwa yana uwezo wa kuzalisha zile nguzo bora kwa kutumia viwango vizuri vya *cement*. Kwa kuwa

Tanzania tuna viwanda vingi sana vya *cement* kila kiwanda kikitengeneza *cement,* basi *TANESCO* iweze kuhudumia kwa *zone* ambazo kunatokea vile viwanda. Hivyo, itapunguza gharama ya nguzo zile mpya na hatimaye kila Mtanzania atapata nguzo mpya na bora ambazo zile zimetumia *cement. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishauri Serikali kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati ni kubwa, ninashauri Wizara hii iongezewe bajeti hasa hasa kwenye Shirika la *TPDC*. Shirika hili la *TPDC* linafanya kazi kubwa sana na lina miradi mingi ya kimkakati kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la *TPDC* linafanya Mradi wa Kusambaza Miundombinu ya Gesi Asilia Majumbani, mradi ambao unatumia gharama kubwa sana na mpaka sasa hivi ni kaya elfu moja mia mbili na kitu ndizo zimeweza kufikia, lakini ukichunguza ni kutokana na kukosekana kwa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaishauri Serikali ione haja ya kuiongezea Shirika la *TPDC* bajeti ili waweze kuongeza tija na kuweza kuwafikia wananchi wengi katika usambazaji wa miundombinu ya gesi, ambapo kila Mtanzania aweze na yeye kufanya maamuzi ya kutumia gesi kama vile anavyotumia umeme, kama vile anavyotumia maji. Kwa hiyo, kila nyumba ikipata mtandao huu wa mabomba ya gesi itarahisisha pia kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* pia inashughulika na Mradi wa *EACOP,* lakini inashughulika na Mradi wa Utafiti wa Gesi Asilia pamoja na mafuta ambao uko Eyasi kule Wembere. Mradi huu una gharama kubwa sana na kwa kuwa sasa hivi tunanyanyasika na mafuta haya kutoka kwa wenzetu huko nje, ninaishauri Serikali kuona haja ya kuwekeza kwa kiasi kikubwa sana kwenye Shirika hili ili watafiti waongeze kasi ya kutafuta visima vya gesi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaimani Tanzania tuna rasilimali hii kubwa maeneo mengi sana isiwe tu *TPDC* kuonekana Mtwara,

nina imani hata Mwanza, Manyara na sehemu nyingine za Tanzania pia tunaweza tukapata mafuta kwa wingi na au gesi kwa wingi ili Serikali iweze kuwekeza. Hata hivyo, *TPDC* ina mradi wa *LNG* ambao kimsingi utakuwa mkombozi sana Nchini Tanzania endapo utakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri kwamba kwa kuwa Serikali imekuwa na imani kubwa kwa hili Shirika la *TPDC* kwa kulipa jukumu la kuagiza mafuta nje kwa kipindi hiki cha uhaba wa mafuta. Ninaomba Serikali yetu sikivu iendelee kuliamini Shirika la *TPDC* kuendelea kuwa waagizaji wakubwa wa mafuta yote nchini ili wale wafanyabiashara wengine wabaki kuwa *oil marketing companies*. Hii itasaidia Serikali katika kuongeza pato la Taifa na kuongeza ufanisi kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kuishauri Serikali kuona haja ya kuanzisha Gridi ya Taifa ya Nishati ya Gesi Asilia ya kupikia majumbani, lakini sehemu za biashara, pamoja na viwanda vidogo ili kuwasaidia wajasiriamali kupunguza gharama ambazo sasa hivi wanaingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa kwa mfano sasa hivi Mheshimiwa mjasiriamali unampa mtungi, anapata mtungi leo atapewa mtungi ukishaisha mtungi kwenda kujaza ule mtungi mdogo gharama ni 25,000 lakini akirudi akienda ule mkubwa gharama ni 50,000. Kwa hiyo, unaweza ukakuta faida yote anayoipata inashia kwenye ile mitungi ya gesi na dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha gesi asilia inawanufaisha wajasiriamali wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri pia Serikali kutokana na Gridi ya Taifa kupata *break down;* kwa mfano juzi Gridi ya Taifa ilipata *break down* wasafiri wa treni walishindwa kusafiri, treni ilisimama abiria wengi walishuka kwenye ile treni kusubiria *stabilization* ya umeme ili waanze na safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishauri Serikali yangu sikivu kuona namna ya kupeleka *power back up* kwenye hivi vituo vya gesi ili ikitokea tena tatizo kama hilo ili wasafiri waweze

kuendelea, lakini hata kwenye yale maeneo muhimu yanayotoa huduma, huduma zisikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah na Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya ajiandae.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii muhimu Wizara ya Nishati ambayo ni tegemeo kubwa kwa nchi, ni tegemeo ambalo sisi Watanzania ni Wizara ambayo ni kiunganishi katika taasisi zote za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana waandaaji wa mpango wa bajeti hii. Jambo kubwa la msingi na la maana na katika historia ya nchi hii ni pale ambapo umeandika trilioni 1.6 zinatoka mfuko wa ndani, lakini tegemezi ni bilioni 800 na *something* kidogo, ni jambo kubwa na ni jambo la kujivunia, hongera sana watalam, Katibu Mkuu na watendaji pamoja na Waziri mwenye dhamana na msaidizi wake. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba nishati hii inaenea katika maeneo ambayo tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mpango wa *REA*, ninaamini katika trilioni 1.6 baadhi ya maeneo kwenye Mkoa wetu wa Simiyu niwapongeze sana Wizara, wameleta ujenzi wa kujenga Kituo cha Kupozea Umeme pale Imalilo na baada ya kuona wakandarasi wanasuasua *TANESCO* kupitia wataalam wao wameleta na mradi unakwenda vizuri sana, ninawapongezeni sana kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo sisi Wabunge tukiwa tunazungumza kwamba kila wizara itumie ufanisi katika watalam tulionao kwenye Wizara ili waweze kunusuru maendeleo ya Taifa letu na kazi hiyo *TANESCO* wameifanya. Mradi uko 47%, hongera

sana na Mungu awabariki waendelee kuongeza maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikibidi Mheshimiwa Waziri waendelee kuwapeleka vijana wapate ufanisi zaidi kwenye mataifa yaliyoendelea ili kusudi tupate wataalam ndani ya maeneo yetu. Fedha nyingi tunaitoa, lakini tuna vijana wako ndani ya nchi wanaweza wakasimamia, wakafanya kazi nzuri hata tatizo likitokea tunaweza tukawahoji na tukawauliza ni jambo ambalo Wizara hii wameonesha uthubutu wa hali ya juu. Bila kusahau kwamba Mheshimiwa Rais ndiyo amewapa majukumu makubwa kama haya na ndiye mtoa dira, mbeba maono ya nchi. Hapa walipofikia ndiyo mahali penyewe, ni jambo la kuwashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, lakini jambo lingine, Mkoa wetu wa Simiyu ninadhani ni mkoa mkubwa na unaokua kwa kasi. Kwenye suala la *REA* Vijiji, Wizara inafanya kazi kubwa na *REA* lakini bado kuna changamoto, wakandarasi wanaowapa hizo tenda wao wanaangalia maeneo ambayo hata kama kuna taasisi ya kiserikali ambayo inahitaji umeme kulingana na mikataba na utaratibu wanaowekeana inakuwa ni changamoto kubwa, kuna shule au kuna zahanati hapa inarukwa kwa sababu *scope* ile haijafika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri na niwaombe, maeneo yote ambayo yako kimsingi na yako kwenye jambo ambalo tunategea kuwa na teknolojia ya sasa, basi wawaruhusu ili kusudi maafisa waliopo kwenye maeneo ya mikoa ile, wawape dhamana ya kuhakikisha kwamba wanachangisha mawazo mazuri kupitia ngazi za halmashauri. Ili kusudu umeme maeneo yote yaweze kupata umeme wa *REA* ili kusudi tufikie kule ambako tunapokufikilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninataka nizungumzie suala la *EWURA;* tunawapongeza wanafanya kazi kubwa na nzuri, lakini Taifa linakua na linaongezeka, mahitaji ni makubwa, pikipiki watu wananunua kila siku, zamani kule usukumani tulikuwa tunatumia baiskeli. Hii dhana Mheshimiwa Waziri ya kwamba kibali tu cha mtu apate leseni ya kuweka kituo

katika Kijiji X mpaka Bodi ikae ni jambo ambalo limeshapitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi inatakiwa ishughulike na mambo makubwa, hicho ni chombo kikubwa sana waachieni *management* watoe hizi leseni kwenye wilaya kule wanakojenga na hiyo inasababisha nini? Inasaidia kuwa na *control* ya mafuta kwenye nchi, inasaidia kupunguza gharama kwa watumiaji maana kwenye eneo ambalo hakuna kituo cha mafuta, mnunuzi anaweza akauza bei yoyote anayoona anajisikia kwa sababu hakuna *control.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kadogo tu unaambiwa Bodi ikae, haijaruhusu wakati kule kuna Serikali, kuna Mkuu wa Mkoa, kuna Mkuu wa Wilaya, kuna Wakurugenzi, kuna viongozi. Ninadhani Mwenyekiti ifike sehemu wafanye mabadiliko maamuzi mazuri, bodi zishughulike na mambo makubwa makubwa, ujenzi wa mabomba ya gesi hayo, *LNG* basi hata Bodi ikikaa inajadili vitu vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kituo cha pampu mbili Bodi hivi ikae inatumia thamani ya shilingi ngapi kukaa kwenye hilo jambo. Hilo nalo halihitaji yaani linahitaji tu maeneo mafupi kutoa kibali, *management* ifanye hizo kazi maisha yaendelee na watu waendelee kufurahia na kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, *TANESCO* sasa hivi tunapanuka, zamani tulikuwa tuna viwanda vichache na tulikuwa tukiamini kwamba uhitaji wa umeme ulikuwa ni mkubwa na gharama ilikuwa kubwa kuliko uhitaji ulioko sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye wawekezaji wote anapokata kile kiwanda malighafi ikiisha anabidi alipe miezi mitatu 75%. Niiombe Serikali kulingana na hali ya sasa ilivyo uwekezaji unapanuka unaenda kwa kasi na tuna-*compete* na nchi zingine tukiendelea na mfumo huu na uzalishaji wetu ni mdogo. Tukiendelea na mfumo huu wawekezaji wa ndani wataendelea kunyong'onyea, wataendelea kurudi nyuma kwa sababu bili ya mwisho inaweza ikaja labda milioni mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua 75% yake kwa miezi mitatu hazalishi ni suala tu la kitaalam, wakae waangalie ku-*review* kuangalia namna gani itakayokuwa bora ili na hawa waweze ku-*complete* na mataifa mengine kwenye biashara ambazo wanazifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana jambo hili ni muhimu sana wakatusaidia ili kusudi kila ambacho tunakitarajia kiweze kufikiwa katika malengo husika na watu waendelee kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwapongeza sana Wizara ya Nishati, kwa maamuzi makubwa ambayo wameyafanya ya kuhakikisha chombo cha ndani kimetajwa na Mbunge aliyemaliza kuzungumza *TPDC* kukijengea uwezo wa kuweza kuagiza mafuta hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kidogo ni gumu na linahitaji uthubutu ukigusa mafuta ndiyo mataifa makubwa kule duniani, tunasikia sisi sote tulioko humu ndani. *TPDC* akipata ni chombo chetu cha ndani, chombo ambacho tunaweza tukaki-*regulate* na kukisimamia na tunapozungumzia usalama wa nchi ni pamoja na mafuta, hakuna jambo lolote linaweza likafanikiwa bila kuwa na mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali iweze kuwajengea uwezo na hawa *TPDC* wajiendeshe kibiashara siyo kutengewa fedha, wafanye kama ni miaka miwili inayofuata waanze kuendesha biashara kama Makampuni mengine wa-*compete,* watengeneze faida ili walete faida walipe kodi Serikalini na waajiri watu katika maeneo ambayo tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo Serikali ya CCM, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tutaanza kuona mabadiliko makubwa; na niwaombe wataalam niliangalia Hotuba ya Mheshimiwa Rais alipokuwa akifungua mradi wa kuweka mafuta pale *TPA,* alieleza kwamba sasa tumekuwa na *storage* za kutosha. Maana yake Rais alikuwa na masikio, alikuwa

anamaanisha kwamba tuwe na *storage* za kutosha, tuwe na mafuta ya kutosha ndani ya miezi miwili yalitokea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Taifa lisingekuwa na watu wenye uweredi leo hata tusingefika humu ndani na magari yetu hata shughuli zingine zote zingekuwa zimesimama. Sasa niombe watumishi wa umma wajenge uzalendo wa kusimamia kile ambacho tunakitarajia katika Taifa letu. Tukifanya hivyo ninaamini tutapiga hatua na *TANESCO* – Wizara ya Nishati wameanza vizuri, lakini ninaomba wafanye maamuzi ambayo yatakayosaidia Taifa na kuhakikisha Dira ya Mwaka 2025 - 2050 inafikiwa kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo tutakuwa tumefanya vizuri zaidi. Niendelee sana kuwaomba katika mkoa wetu na katika Jimbo langu la Itilima bado vitongoji 229 havijapata umeme. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii ya trilioni 1.6, atakapokuja atuambie zinazokwenda kwenye *REA* ni kiasi gani na anazobakinazo huku ni kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, *focus* kubwa katika wizara hii ni wizara ambayo inaunganisha wizara zote na wao wakilala tu wizara zingine zote tunasimama. Ukizungumza mafuta wako nayo, ukiizungumza umeme wako nao, ni jambo la kushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni waliotembelea Bunge jioni hii. Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 55 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Jijini Dodoma. Ahsante na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, atafuatiwa na Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. AISHA M. MDUYAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ikiwa mara yangu ya kwanza kuchangia katika Bunge hili Tukufu, ningependa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyeniwezesha kufika siku hii ya leo, nami jina langu limeandikwa katika Orodha ya Wabunge wa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninapenda kumshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, ambaye ni Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na vikao vyake vyote vilivyopita vya kuniteua mimi kugombea, lakini pia kuniteua kuwa Mbunge wa Viti Maalum ninayewakilisha watu wenye mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuwasahau nipende kuwashukuru wanawake wote ambao ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa UWT – Taifa chini ya Mwenyekiti wetu, mama yetu kipenzi, Mary Pius Chatanda kwa kunikopesha imani yao ndani ya hii miaka mitano 2025 - 2030 na ninachoweza kuahidi kwao ni ushirikiano uliotukuka katika utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niishukuru familia yangu pamoja na marafiki zangu ambao wamehakikisha kwamba ndoto zangu haziwezi kukwama mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa ninaelekea katika kuchangia hotuba hii, ninapenda kuipongeza Wizara ya Nishati: Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Menejimenti ya Wizara, pamoja na taasisi zote zilizoko hapo chini ya Wizara ya Nishati kwa juhudi kubwa wanazoziweka katika kuhakikisha kwamba Taifa letu linasonga mbele kwenye sekta ya nishati. Tunaona *REA* wanavyoweka juhudi zao kubwa katika kuhakikisha kwamba vitongojini pia tunapata umeme na wameweza kuanza na vitongoji 9,009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona pia Serikali yetu namna ambavyo hailali usiku na mchana kuhakikisha kwamba mafuta siyo kikwazo katika nchi yetu na kuhakikisha pia masuala ya kiuchumi na kijamii hayakwami kwa kigezo cha mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kuipongeza Wizara yetu kwa kuendelea kuibua vyanzo mbalimbali vya nishati. Tunaona nishati ya jua, nishati ya umeme wa maji, lakini pia gesi asilia na joto ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa ninaelekea katika kuchangia hotuba hii nikianza na suala la nishati safi, sisi kama Taifa kwanza tunajivunia kuwa na kinara wetu wa masuala ya nishati safi ambaye ni Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata jana tu tumeona akitoa mitungi ya gesi kwa mama lishe na baba lishe Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ninaipongeza pia Wizara kwa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi, lakini pia kutoa majiko banifu yenye bei ya ruzuku na kuhakikisha kwamba nishati safi inamfikia kila mwananchi. Ninaomba tu waendelee kutoa elimu hii na kuhakikisha kwamba kila mwananchi aliyeko mjini na pembezoni mwa mji anajua umuhimu wa kutumia nishati safi, kwani tukiongelea kuhusu masuala ya athari za mabadiliko ya tabianchi, basi wanawake, watoto, na watu wenye ulemavu huathirika zaidi. Hata takwimu zinatuambia kwamba watu wenye ulemavu wanaathirika mara mbili zaidi kukitokea athari zozote ikiwemo mafuriko, ukame na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kupendekeza kwamba tuwe na *National Clean Cooking Energy Coordination Framework*. Leo hii unaweza ukafika ndani ya nyumba moja ya mwananchi ukakuta ana mitungi hata mitano hadi sita ambayo amepewa na watu kadhaa. Amepewa mitungi hii na Mbunge wake wa jimbo, akaja Mbunge wa Viti Maalum akampatia, wakaja *STAMICO* kupitia mkaa wao mbadala wakampatia na wadau wengine wa nishati safi pia wakampatia, hali ya kuwa jirani yake hana hata mtungi mmoja wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kukiwa kuna huu mfumo wa uratibu tunahakikisha kwamba wananchi wote wanapata nishati safi, lakini pia upatikanaji wake unakuwa nafuu na pia inawezesha hata wale waliopo pembezoni wanaweza kuji-*coordinate* kuweza kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii pia niweze kupendekeza kwamba fursa hizi kama tunavyoona Wizara ya Nishati inavyotoa mikopo, vituo vya mafuta vinajengwa pembezoni mwa miji, basi itoe pia mikopo hii kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hasa waliopo pembezoni mwa miji waweze kupata mikopo hii na kuweza kuuza nishati hii kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ninapenda kuongelea kwenye suala la *Local Content*. Sisi kama Taifa tunajivunia kuwa na sera hii, lakini pia ni Watanzania wachache sana ambao wanafahamu hivyo. Kwa hiyo, ninapendekeza Wizara iweze kuelezea zabuni ambazo ziko chini yake, ambazo ni *specific* kwa ajili ya Watanzania. Pia, ihakikishe kwamba wakandarasi hawa wa sekta ya nishati wanahakikisha kwamba zabuni hizo zinaenda kwa Watanzania pekee. Hali hii itafanya uchumi wetu uzidi kukua kwa Mtanzania mmoja mmoja, lakini pia Taifa kiujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwisho, ninapenda pia kuipongeza Wizara ya Nishati kwa kuhakikisha kwamba vijana wanaendelea kupata ujuzi. Tunaona vijana wengi wanaji-*engage* na miradi ya mikakati ikiwepo wa *ECO* ambapo wanaenda kupata *skills* kutoka kwa wakandarasi ambao wako nje. Ninatoa tu wito kwa vijana wenzangu kuendelea kupata ujuzi kwenye sekta ya nishati safi, vijana wote ikiwemo watu wenye ulemavu, kwani tunatambua kwamba mnyororo wa thamani ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwatia moyo, kwa ni mimi pia hali ya kuwa nina ulemavu, lakini nimesomea Uhandisi wa Mafuta na Gesi. Kwa maana hiyo, vyote vinawezekana kwa vijana wenzangu hasa wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango huu mchache nilioutoa na kwa moyo wa dhati, ninaomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, atafuatiwa na

Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo ajiandae.

Mheshimiwa Onesmo Mnkondya hayupo, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo na Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hii hotuba ya Waziri wa Nishati. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais aliyekuwa mwingi wa fadhila kwa kuwateua Mawaziri wazuri, Manaibu na Makatibu wazuri kwenye Wizara ya Nishati. Rafiki yangu Mheshimiwa Ndejembi, leo nilikuwa na mambo mengi mengi, sasa ninamwona kama vile ananiangalia, lakini ukweli ni kwamba kazi anafanya na hata waliokuwepo kazi walikuwa wanafanya kwenye Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, sisi Wabunge tuliorudi hapa Bungeni na moja ya hatua kubwa zilizopigwa ni pamoja na kuweka umeme vijijini na kwenye vitongoji. Maeneo mengi sasa hivi wananchi wameshakuwa na wivu. Kitongoji A kikikosa umeme Kitongoji B kinasema sisi kwa nini hatukupata. Tatizo tulilonalo sasa ni usambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaiomba sana Wizara; sasa hivi ni kipindi cha kushauri. Taasisi zetu sisi, sekta kwa mfano shule za msingi zote, vituo vya afya vyote, zahanati zote, sekondari zote, sasa ninashindwa kuelewa mambo mengine. Hivi Wizarani kwenu huko hamna *data*? Kwamba Bunda kuna zahanati tano hazina umeme, kuna vituo vya afya sita havina umeme, kuna shule za msingi tano hazina umeme, kwa nini hawana *data* hizo? Kwa nini shule moja inaweza ikakaa miaka mingi haina umeme? Wanajenga vituo vya afya havina umeme, tunajenga shule mpya hazina umeme, tunajenga hospitali za wilaya hazina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupeleka umeme pale wanaenda *TANESCO* wanaambiwa shilingi milioni 38. Sasa ni mambo gani haya? Kwa hiyo, ninaomba wawe na *data* za kuweka umeme kwenye sekta maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Bunda; ninaomba hii ieleweke, maana yake tunaenda kwenye Dira yetu ya 2050, ieleweke Mheshimiwa Waziri. Ieleweke wewe ni kijana, ieleweke wazi kwamba, ni kweli Serikali tumepeleka umeme kwenye vijiji, ni kweli Serikali imepeleka umeme kwenye vitongoji, lakini uhalisia ni kwamba kitongoji ni nini na kijiji ni nini? Kijiji ni muunganiko wa vitongoji. Maana yake kama tumepeleka umeme, tunapeleka kwenye *centre* ya kijiji fulani, ambacho kijiji hicho kina kaya 300 na umeme uliokwenda ni kaya 25 au kaya 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huko tunakokwenda kwenye dira yetu tufikirie namna ya kusambaza umeme kwenye nyumba za watu, siyo kuweka idadi ya vijiji na kuweka idadi ya vitongoji. Kwa hiyo, ninaomba huko tunakokwenda kwenye dira yetu tufikirie mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la mafuta ninaomba Waziri, ninajua hiyo *Bulk Procurement System* ni nzuri, imelinda mfumo wa kuwa na mafuta nchini. Hatuwezi kuikataa, nzuri sana; kwa sababu wenzetu kuna wengine wana hela, hawana mafuta. Ni nzuri sana lakini huko tunakokwenda kama hali itakuwa mbaya, ndugu zangu turuhusu watu binafsi kuingiza mafuta. Vinginevyo tunataka twende kupunguza fedha au tozo za mafuta kwenye maeneo mbalimbali ya kimaendeleo. Kama tunaona ni vipi turuhusu watu binafsi ili ushindani uwepo ili tuweze kupata mafuta ambayo yanaweza kutusaidia kwenye hali zetu za kawaida hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hili lieleweke. Miaka yote ambayo *REA* imekuwepo, walitwambia kwamba kijiji kinapelekewa nguzo 60 na kitongoji kinapelekewa nguzo 40, miaka yote. Toka tumeanza *REA* kijiji nguzo 60 wananchi wamekaririshwa wamejua. Saa hizi simu zinapigwa. Juzi wamesambaza nguzo, wamepeleka nguzo 30 kwenye kitongoji. Wananchi walishaelimishwa kwamba kitongoji ni nguzo 40 na kwenye kijiji ni nguzo 60. Kwa nini nguzo zimeenda 30? Ninajua inawezekana kwamba wameona labda kahela walikonako (kasungura) ni kadogo, lakini ni bora pale ambapo tungepeleka vitongoji vitano tukapeleka vitongoji vitatu, lakini kwa nguzo 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hizi nguzo kwenye maeneo ya huko kwetu, kutoka nyumba moja kwenda nyumba nyingine ni nguzo 18. Sasa, sisi ambao tuna maeneo makubwa kiasi hicho unakuta hizo nguzo 30 zinaenda miji mitatu tu. Ndugu zangu hii inatuletea shida. Kwa hiyo, pale ambapo waliona kuna mapungufu ya nguzo 10, kama kuna uwezekano wa kupata hela mahali turudishe. *System* ieleweke kwamba kitongoji ni nguzo 40 na kijiji ni nguzo 60. Mheshimiwa Waziri kazi wanafanya kubwa sana, kubwa ya umeme, lakini huwa ninajiuliza, hivi *system* ya umeme ya *REA* ikifa au siku tukiacha *REA*, *TANESCO* itafanya nini? Sijui kama kuna *TANESCO* saa hizi, maana yake huko kijijini ni *REA REA, REA*. Hivi sasa *TANESCO* wako wapi? Wanafanyaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sasa kama kuna mafungu ya *TANESCO* na ninaomba Waziri, mimi sielewi na kwa nini sijui mimi sielewi. Kwa nini tusianzishe wale watu wenye uwezo wa kupata umeme hata kwa kukopa tuwakopeshe kwa dhamana ya Serikali watakuwa wanakatwa humo humo ndani, hivi hilo haliwezekani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Ninataka kumpa tu taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Getere inawezekana *REA* anaiona kwa wingi sana kwa sababu ya *nature* ya jimbo lake. Ninataka nimpe tu taarifa kwamba, *REA* wakikamilisha kazi inakuwa *handled* na *TANESCO thereafter*, lakini *TANESCO* pia kuna maeneo wanafanya hasa kwa sisi ambao tuko kwenye majimbo ya mjini ambayo hayana programu za *REA*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere taarifa ya Mheshimiwa Esther unaipokea?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa utaikataaje tena taarifa ya mdogo wako? Unaipokea tu hivyo hivyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli lazima tupunguze gharama za umeme. Hivi kweli, maana ninauliza hili swali nikiwa na mantiki moja. Kwamba, kijijini tukiacha shilingi 27,000 na wakati *TANESCO* ni shilingi 320,000/370,00 ni mwanakijiji gani ataingiza umeme? Ataingizaje? Kwa hiyo, ni lazima hata kama *REA* itakufa, *system* ya kuweka umeme kwa shilingi 27,000 au hata kwa shilingi 40,000/= itengenezwe na Serikali ili watu wa vijijini waendelee kuweka umeme. Vinginevyo kama tunaleta *system* ya mjini, kupeleka umeme kwa mtu shilingi 320,000/370,000 mwanakijiji hawezi kuweka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ninawashukuru sana watu wanafanya kazi kubwa. Watu wa *REA* ninawashukuru sana wanafanya kazi kubwa, Mkurugenzi wa *REA* na watu wote wa *REA*. Kweli mimi *REA* ndiyo ninawaamini wanafanya kazi kubwa sana, *TANESCO* tutakutana huko baadaye tukiwa mji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ambayo imewasilishwa na Wizara ya Nishati na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na ninakiri kupokea umeme kwangu kule vitongoji 39, japo nina vitongoji 80 vimebaki, lakini kwa mpango wa Serikali nina uhakika kuelekea mwaka 2030 kama ambavyo Ilani ya chama chetu inasema vitakuwa vimekamilika. Kwa hiyo, sina shaka na Mheshimiwa Waziri, nimeona mipango yake kwenye Wizara kwamba vitongoji vyote vinakwenda kufikiwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama leo hii kwanza kwa sababu kuu ambayo inatupata sisi watu wa Songwe. Watu wa Songwe hatuna umeme wa uhakika. Hivi nilivyosimama hivi leo umeme Mkoa wa Songwe ni mara nyingi sana unakatika katika na umekuwa ni maarufu kwa Mkoa wetu wa Songwe. Yaani unaweza ukasema tuko gizani sasa. Hili jambo sisi kama Wabunge kwa kweli limeleta shida sana kwa mkoa wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewaambia wananchi wetu kwamba muwe na subira. Sisi ni wawakilishi wenu tutakwenda Bungeni kuwasemea na ikiwezekana hivi nimesimama Mheshimiwa Waziri, unapokwenda kuwasilisha hotuba yako (kumaliza) ninakuomba tu; kwa namna ambavyo tuna tatizo Mkoa wa Songwe la katikakatika ya umeme. Hii inatokana na kwamba sisi watu wa Songwe tunachukua umeme kutoka pale Mbeya. Kuna kituo kimoja kinaitwa Mwakibete cha kupozea umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimuuliza hata mtoto mdogo leo ukimuuliza Mwakibete ni nini, atakuambia ndiye anayetukatia umeme. Yaani hiki kituo cha kupozea umeme kimekuwa ni maarufu mno. Kwetu imekuwa ni kero. Matangazo yote yanayokuja na watu wa *TANESCO*, tatizo Mwakibete. Ni kweli, sasa kama mtu mwingine anatu-*control* sisi Watu wa Songwe, tutashindwaje kukosa umeme? *Control* zote zipo kwao, wakiwa na jambo lao lolote lile watakata tu umeme Mkoa wa Songwe tunakosa umeme. Laini yote tunakosa umeme, tena siyo Mbozi tu peke yangu, wilaya zote za Mkoa wa Songwe majimbo yote ya Mkoa wa Songwe, Wabunge wako hapa wanajua hilo, kwamba kelele ni umeme Mkoa wa Songwe. Tunakosa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wakulima kuna uzalishaji wa hali ya juu kule. Wafanyabiashara, viwanda vidogovidogo haviendelei wajasirimali wadogo hawawezi kufanya kazi kwa sababu umeme haupo, siyo wa uhakika. Ninaamini atakuja na mpango wa dharura wa kutusaidia watu wa Songwe wakati tunasubiri huu Mradi wa *TAZA* unaokwenda kukamilika. Kwa kweli umeme Mkoa wa Songwe hauridhishi. Hatuko salama kwenye umeme. Ninaomba Mheshimiwa Waziri alichukue hili na atusaidie

tupe majibu. Hivi wananchi wa Mkoa wa Songwe wanasubiri Serikali inakwenda kusemaje. Sina shaka na Waziri anakwenda kuwajibu na kutuma wataalam huko wakatuangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana ndiyo, toka tuchukue hii laini mpaka sasa, wakati tunaanza na hii laini ya kutoka Mbeya kuja Songwe ilikuwa na watumiaji 68,000. Sasa watumiaji wameongezeka kwenda 144,000. Ni pongezi kwa Serikali kuongeza watumiaji, ndiyo hivyo vitongoji vimeshapata umeme na ongezeko ni watu 80,000. Sasa, bado tunatumia laini ile ile na miundominu ile ile. Hapana, Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ninataka nishauri sasa, kupitia mradi ambao unaelekea kutukomboa sisi watu wa Songwe wa *TAZA*. Mradi huu ni mzuri, ni mpango mzuri wa Serikali, lakini mradi huu ulikuwa umepangwa ukamilike tarehe 21 Mei, 2026, bado mwezi mmoja. Hivi ni kweli unakwenda kukamilika? Tatizo linakuja kwa wakandarasi wanaotekeleza huu mradi. Inawezekana hawawasimamii vizuri. Sasa, Mheshimiwa Waziri hawa wakandarasi wasimamiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe Waziri mfano wa wakandarasi hawa; mkandarasi kutoka Iringa kuja Kisada amekamilika hana tatizo. Mkandarasi kuja hapa Kisada sijui panaitwa Sasada, kuja Mbeya…

**MBUNGE FULANI:** Kisada.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Kisada *yes,* kuja Mbeya yuko *slow* mno, yuko taratibu sana. Mpaka hivi ninavyozungumza, kati ya nguzo 495 amesimamisha nguzo 199, bado nguzo 296, atamaliza? Huyu ndiye atakayechelewesha. Mpango mahsusi uende kwa huyu mkandarasi, kama ni kusimamiwa asimamiwe. Atatuchelewesha sisi watu wa Songwe kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka hapo mkandarasi wa kutoka Mbeya kuja kwetu Songwe hadi Nkangamo, Kituo cha Kupozea Umeme yuko vizuri, bado nguzo sita tu. Huyo hatuna shaka naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine litakalochelewesha mradi huu ni kile Kituo cha Kupozea Umeme Nkangamo, mpaka sasa mkandarasi hajaanza kusafirisha zile *transformer* kutoka bandarini kwenda Songwe na tunajua zile *transformer* zilivyo na uzito, sidhani kama ana gari za kwenda kusafirisha zile *transformer* kwa wakati. Ninaamini hatakuwa na uwezo huo. Sasa, nini cha kufanya ili kumsaidia na *transformer* moja ya kusafiri ni kati ya siku 28 na kuendelea? Ili kumsaidia Serikali yetu, ninaamini ina uwezo mkubwa tu, ipeleke gari zenye uwezo wa kubeba mizani mizito ili aweze kusaidiwa huyu mkandarasi, aweze kuleta *transformer* akamilishe mradi wake pale Nkangamo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye uwasilishaji wa Mheshimiwa Waziri, kwa kweli ninampongeza sana. Wakati ninaendelea kutafakari namna gani tutakavyopokea huu umeme sisi Watu wa Songwe, kama sasa tuna changamoto na Kituo cha Kupooza Umeme cha Mwakibete Mbeya na sasa wameturuka vilevile kituo cha kupooza umeme kutoka Mbeya kimeenda mpaka wapi? Nkangamo!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninawaza hivi umeme huu utatoka Nkangamo uanze kurudi tena Songwe. Makao Makuu ya Songwe jamani yako Mbozi. Tunapaswa kuwa na *substation* mahali hapa tu-*control* wenyewe ule umeme. Sasa uende kule urudi huku, hivi inawezekana? Itakuwa ni hali ile ile. Kitakachotokea kule Nkangamo ndicho kitakachotuathiri huku. Mpaka tuje tu-*solve* hilo tatizo muda ushakwenda. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kutoka Mbeya tatizo lilikuwa lile lile. Waje watuwekee *substation* Mbozi Makao Makuu pale, watu wa-*control* pale ili tusipate shida ambayo tunaipata sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kule Nkangamo ni mahsusi kwa ajili ya Zambia, ni mahsusi kwa ajili ya wenzetu wa Rukwa na kuendelea, lakini kwetu hatutapata manufaa. Wakati kengele ya kwanza inagonga, ninaomba nimalizie kwa kusema kwanza ninampongeza sana Meneja wa *TANESCO* Mkoa, ni kijana mzuri, kijana mdogo kama mimi tu. Kazi anayoifanya, pamoja na kukatikakatika umeme ni nzuri, anaitwa *Engineer* Chonya. Anafanya kazi nzuri usiku wote, kwanza anatoa ushirikiano mzuri,

ila anazidiwa na wenzetu wa kule kwenye kituo ambacho kinatuletea shida hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huyu Meneja, Mkoa wetu wa Songwe hatuna Ofisi ya *TANESCO*. Hivi ninavyozungumza anatoka kwenye nyumba ya kupanga ndio ofisi, jengo la kupanga ndio ofisi. Kweli kwa mkoa wenye hadhi kabisa, kesho kutwa tu tunaenda kupata Manispaa, tuendelee kutumia ofisi ya kupanga, kweli? Hawa watu wana kiwanja. Mheshimiwa Waziri wajengee ofisi, ili kuwanusuru na wenyewe angalau wawe na uwezo wa kufanya kazi, wawe na ofisi yao badala ya kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, meneja huyu ndiye anayefanya kazi pia, kama meneja wa wilaya yetu, lakini kazi yake ni nzuri, wamjengee ofisi. Ninaomba sana Serikali ichukue jambo hili la umeme kukatikakatika kwa Mkoa wetu wa Songwe, kama jambo la dharura kwa Wanasongwe tuondokane na giza ambalo tuponalo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi ambayo umenipa na mchango ambao nimeutoa kwa rafiki yangu Mheshimiwa Waziri. Ninaamini Wanasongwe wanakwenda kunufaika kuanzia kesho na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Onesmo. Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay. Mheshimiwa Haran Sanga, ajiandae.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii tena ya kuchangia Wizara yetu ya Nishati. Kwanza kabla sijaenda mbele ninaomba nimwambie ndugu yangu Waziri kwamba, shida ya ukatikaji wa umeme pia, katika jimbo langu imekuwa ni jambo la kawaida, hasa Kata ya Gongo la Mboto, Kata ya Pugu Station na Buyuni, imekuwa inajitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana peke yake imejitokeza mara mbili kwa hiyo, ninaomba kwa umuhimu wake, Mheshimiwa Waziri, aone namna ya kumalizia hili tatizo ambalo ukiliunganisha linaweza likachukua zaidi ya miezi miwili sasa. Kwa hiyo, imekuwa ni karaha na hasa ukizingatia kwamba, jimbo langu lina wafanyabiashara wengi, machinga na kadhalika na umeme ndiyo sehemu pekee sasa hivi ya ukombozi wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua, ili tuweze kuvuka ni lazima tutumie umeme. Katika Jimbo langu la Ukonga yapo maeneo ambayo kwa sura ya kawaida ya kimipaka yanaonekana kwamba, ni maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, lakini kiuhalisia ni kama tupo kijijini; Kata kama ya Zingiziwa, Chanika, Buyuni na Pugu Station. Hizi ni kata ambazo, kama unapita kwenye barabara ya lami kila siku unaweza ukahisi huko nyuma ndiyo maisha yalivyo, lakini huko nyuma kuna misitu, Msitu wetu maarufu wa Zingiziwa, ukitembelea maeneo yale utakuta zaidi ya mita na 100 hakuna miti mikubwa, hii maana yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kuwa wananchi wa pale wanajikimu kwa kutumia miti ile kufanya kuni. Katika mazingira hayo ninaamini inatokana na hali ya uchumi wa wananchi wa jimbo lile, katika hayo maeneo, wanashindwa kubeba gharama za malipo ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatolea mfano kwa bei za *TANESCO,* kuanzia mita sifuri hadi mita 30 ni shilingi 321,000 na kwa mita sifuri hadi mita 70 ni shilingi 515,000 na mita sifuri hadi mita 120 ni shilingi 796,000 na kidogo. Pia, ukienda vijijini huko ambako kuna huduma ya *REA* utakuta nako mita sifuri hadi 30 ni shilingi 27,000, lakini ikizidi hapo gharama zinafanana, kama hizi ambazo nimetaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hali ya kawaida ya wananchi wetu pesa hizi ni nyingi sana, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri na *cabinet* yake na Serikali waangalie mpango wa makusudi. Huko nyuma tulikuwa na utaratibu wa mwananchi asiyekuwa na *cash* anaruhusiwa kulipia kidogo kidogo, bahati mbaya ule utaratibu sijui ulifutwaje, ambapo sasa haupo, lakini yapo maneno ambayo yamekuwa siyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, mimi ni mtaalam wa umeme kwa hiyo, haya mambo nayajua. Kumekuwa na taarifa zisizo rasmi kwamba, kumekuwa na baadhi ya wananchi waliodhaminiwa kulipa kidogokidogo wakawa hawalipi, lakini ninaamini kwamba, inawezekana pia, kwenye shirika letu kulikuwa kuna uzembe wa kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunaona kodi za majengo zinalipwa kwa ufanisi kupitia bili za umeme tunapowenda kununua *units*. Sasa kwa kuwa, sasa hivi tupo kwenye hali ya tahadhari na mazingira na kata hizo nilizozitaja, kama zinavyojulikana kijiografia zipo kandokando ya misitu yetu, ninaomba sasa kwa umuhimu wa pekee kwa jimbo langu na majimbo mengine kwamba, Serikali irudi kwa utaratibu ule wa wananchi kuchangia 25% angalau ya gharama halisi ya kuvuta *service line*, halafu gharama inayofuata wachangie asilimia mbili kila wanapoenda kununua zile *units*. Hakika ndio njia sahihi, ambayo itakwenda sambamba na kunusurisha misitu hasa kwetu Kazimzumbwi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa umakini, tukiondoa uvivu wa baadhi ya watendaji wa shirika, tunaweza kujikuta tunafanya vizuri. Hivi tunavyozungumza habari ya Mradi wa *REA* ninashukuru na baadhi ya Wabunge wenzangu hapa wanazungumzia umuhimu wa Miradi ya *REA* na umuhimu wa bei, wanazungumzia jinsi bei za *TANESCO* zilivyo juu. Ili tutoke ni lazima tuweke utaratibu ambao utawawezesha wananchi wetu kulipa kidogokidogo, kama ambavyo tunalipa kodi za majengo, tulipe hivyohivyo na ninaamini inawezekana kwa sababu, umeme ndiyo kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma, ili uweze kupika, uwe na jiko na uweze kutumia umeme; ilikuwa inahitajika uwe na matumizi ya wastani wa *current* inayoanzia 15 kwenda hadi 45, wakati wa majiko yale ya plate, enzi za *coil,* lakini kwa sasa tumepata teknolojia mpya, tuna majiko madogo yanayotumia *current* ndogo kati ya tano hadi 12. Kitendo hiki maana yake ni kinakuja kutupunguzia gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni gharama sana kutumia gesi kwa sasa kuliko kutumia umeme kwa kupikia. Ni gharama sana kutumia mkaa na kuni kuliko kutumia majiko ya kisasa. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri ni ndugu yangu, jamaa yangu wa karibu, aangalie hili jambo kwa umuhimu wa namna hiyo. Siyo mara zote tufanye uwekezaji wa kulipa leo, tumeona uwekezaji mzuri na mkubwa tunaoufanya kule kwenye Viwanja vya *AFCON*, uwekezaji mkubwa sana Arusha na viwanja vingine vidogovidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawekeza kule tukiwa na maana tutapata baada ya kuwa viwanja vimekamilika kwa hiyo, *style* hiyo hiyo tuitumie pia, kuwekeza kwa wananchi wetu kuhusu suala la umeme. Kwa hiyo, tusione ubaya kuweka mabilioni kuwawezesha wananchi wetu kupata huduma ya umeme kwa lengo la kuondokana na uchafuzi wa mazingira na pia afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua ndugu zangu, watani zangu Wasukuma, wakati wanatumia yale mabaki ya maji ya chakula cha ng'ombe, akinamama wengi wamekuwa wanapata shida ya macho mekundu, lakini pia, hata kwangu kwenye jimbo langu, matumizi ya kuni yanaleta sababu ya macho kuwa mekundu. Ile ni athari kiafya kwa hiyo, tuondokane na hiyo hali hasa ukizingatia kwamba, tunatakiwa tubadilike kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye suala ambalo ndiyo linaonekana lipo kimjini sasa hivi. Tuna ombwe kubwa la bei ya mafuta, bei ya mafuta inasababishwa na wababe duniani na Waswahili wanasema wapambanapo fahari wawili, ziumiazo ni nyika. Sisi tunakubali tunakwenda kuumia, lakini ninaiomba Serikali, kwa makusudi kabisa kwamba, sasa ifike wakati ipunguze tozo, angalau kwa shilingi 300, wakati huo iweze kuongeza ruzuku kwa shilingi 300, utakuta tunakuwa tumeokoa karibu shilingi 600. Kwa mwananchi wa kawaida huko tunakotoka utakuwa ni msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua siku zote, baba kwenye mji ndiyo anabeba gharama za uendeshaji wa maisha ya familia yake nyumbani, ama kama mama ni mwenye mji ndiyo

anabeba gharama zote za uendeshaji wa familia nyumbani. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla, kwa jambo hili, ikubali tu kulivaa kama bomu tuweze kuvuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana wababe wakaendelea kupigana ikasababisha ongezeko la bei zaidi, lakini siyo maana yake tuogope, tupambane kadri ya hali itakavyokuwa, lakini Serikali iangalie katika hayo mazingira. Katika mtazamo wetu huu na kwa kuwa tupo hapa kwa malengo yanayofanana, pamoja na majukumu ya Wabunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali na kadhalika; Serikali pia, yenyewe ina majukumu ya kuangalia watu wake. Ukifanya tathmini ya Wabunge tulio wengi humu ndani tumechangia tukizungumzia habari ya hizi bei na upatikanaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri yake ni kwamba, wawakilishi wa wananchi walio wengi tunawakilisha shida ambayo ndiyo maisha tunayoishi nayo kule kwetu. Kwa hiyo, ninaomba kabisa Wizara kwa makusudi kabisa ichukulie hata uchangiaji wa Wabunge tulio wengi juu ya hoja ya kurahisisha masharti ya wananchi kupata umeme iwe ndio dira na uelekeo wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishie hapo. Ninaomba kuwasilisha hoja yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bakari Bakari. Mheshimiwa Zacharia Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Haran Sanga na Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kupata wasaa huu. Ninachukua nafasi hii kwanza kwa namna ya pekee sana kuungana na Wabunge wenzangu na Watanzania kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa baraka zake mbalimbali katika Taifa letu na jamii kwa ujumla. Hatua hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa iliyofanyika ya usambazaji wa umeme katika majimbo yetu nchini. Kwa kweli, kwa namna ya

pekee Wizara hii au Serikali kwa ujumla imefanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, 2015 baadhi ya majimbo hapa nchini tulikuwa tunapokea umeme wa jenereta ama wa mitambo ya kuzalisha kwa mashine. Tulipofanya ziara maeneo mengine, kuna eneo tulikwenda wakati huo 2015 tukaambiwa ikifika saa nne usiku umeme utazimwa; leo walau kwa sehemu kubwa Serikali imepeleka umeme kwenye maeneo mengi. Hii ni hatua kubwa sana na hasa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini pia, upelekaji wa umeme kwenye maeneo yetu yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii pia, kumpongeza sana Waziri, ndugu yetu Mheshimiwa Ndejembi, Naibu Waziri, Wizara nzima na watendaji wote, kazi kubwa imefanyika na Wizara hii ni muhimu. Kila Mbunge hapa atakumbuka maswali na maoni mengi yaliyoulizwa na wananchi wakati ule wa uchaguzi; tulikuwa tunadaiwa sana usambazaji wa umeme, ufikishwaji wa umeme, kwenye maeneo yetu na sasa kwa ujumla, vitongoji vingi vimepelekewa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni hatua kubwa sana kwa Tanzania. Ni hatua kubwa sana kuwa na umeme wa uhakika katika nchi yetu kwa sababu, Bwawa hili la Mwalimu Nyerere lisingekuwepo nchini, umeme huu tungeupata wapi? Tulishakuwa na kadhia ya umeme kukatika mara kwa mara. Kwa kweli, kwa namna ya pekee tunampongeza Mheshimiwa Rais na wale wote watangulizi wa Taifa letu waliotangulia mbele za haki, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kwa namna ya pekee kuipongeza sana Kamati yetu ya Nishati, imefanya kazi kubwa sana. Imechakata taarifa, imerahisisha kazi ya Wabunge kwa namna ya kuchangia na kutoa maoni yetu kwa Serikali. Kwa namna ya pekee wameleta taarifa ambayo imeonesha mafanikio, changamoto na pia, namna ya kuyafanyia kazi, kwa namna ya pekee, kwa maonesho ya Wizara, imekuwa kivutio na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa eneo hili ni kwamba, tutumie *media* zetu kupeleka maonesho yale kwa Watanzania, ili waone fursa zilizopo pamoja na mafanikio na hatua iliyofikiwa na Taifa letu. Hatua hii ni kubwa sana kwa sababu, yale maonesho yanatuonesha Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unatuonesha jinsi umeme unavyozalishwa na fursa nyingi zinazokuwepo nchini. Hongera kwa Wizara kwa namna ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaeleza pia, umuhimu wa Serikali kuiomba ipeleke bajeti ya Wizara hii. Kweli, kama Wabunge, tunalo deni kubwa la umeme vijijini, deni la kila Mtanzania kuhitaji umeme; maeneo ni mengi, lakini fedha tunazopata Serikali inajitahidi sana kupeleka ingawa bado maeneo ni mengi sana. Mfano ni Jimbo langu la Mbulu Mjini, tunasura mbili, sura ya mji na sura ya vijiji; nina kata 10 zipo vijijini na kata saba zipo mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale mjini kati kuna nyumba ambazo hazijaunganishwa na umeme, kutokana na gharama kubwa ya uunganishaji wa umeme kwenye eneo hilo. Ninaamini miji mingi ipo hivyo, unakuta nyumba zilizo ndani ya mita 30 ni nyingi, pengine 70% kuliko zile ambazo zimeunganishwa na umeme. Wananchi wanaoishi mjini siyo kwamba, wote wana uwezo wa kulipa shilingi 300,000 na zaidi katika kuingiza umeme, wengi wao ni wakazi wa kawaida, ni wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naiomba sana Serikali ije na utaratibu ambao, kama mpango mahususi wa muda mfupi wa maeneo hayo ya mji kuunganishwa hasa nyumba zote zilizo ndani ya mita 30, mita 25, ziunganishwe kwa shilingi 27,000 ili Watanzania waweze kunufaika na umeme. Pia, kwa namna ya pekee huu umeme tunaouita wa ziada uende kwa Watanzania walio wengi, ili waweze kunufaika na umeme na kupata fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mbulu Mjini kuna mitaa 58, takribani mitaa nane ni mwaka wa 11 haijafikiwa na umeme japokuwa umeme una miaka 14 katika Jimbo la Mbulu Mjini. Kwa hiyo, hali hii inasababisha wale wananchi wanapenda kuingiza huo umeme kwenye majengo yao, lakini namna ya

kupata shilingi 360,000 na namna ya kufanya *wiring* kwa shilingi laki tatu pengine na kitu, jumla shilingi 700,000, fedha hizi ni nyingi sana kwa mwananchi wa kawaida. Shilingi laki saba siyo elfu sabini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali, iangalie utaratibu huu, Mheshimiwa Waziri ikimpendeza, nimemwomba mara nyingi aje atembelee Jimbo la Mbulu Mjini. Ni mji unaopakana na halmashauri nne; yaani kila Waziri aliyekuja kwenye jimbo langu alikuwa ananiuliza na huku ni mjini? Wale Mawaziri wote waliokuja kutoka 2015; lakini nikwambie kweli, ni mji gani unapakana na halmashauri kama nne nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu sasa wale waliopo kule pembezoni wanaonekana wapo mjini katika tamko lile la Serikali. Ushauri wangu ni kwamba, maeneo hayo yafanyiwe tathmini, eneo la mji tuorodheshe majengo yote, ambayo yana sifa ya kuunganishiwa umeme tuone utaratibu wa umeme, tunatafuta programu ama mpango wa muda mfupi utakaokuwa unaleta marejesho hata kwa watumiaji baadaye, ili wananchi hawa ambao kwa muda mrefu wamesubiri umeme waweze kuunganishiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Programu ile ya UMETA, katika jambo hili wala tusifichane, kuna majengo ama kaya ndani ya hata miaka 15 hawajafikiwa na umeme kwa sababu, unakuta kwenye jiografia yetu tunavyoishi tuna milima na tuna umbali wa jengo hadi jengo. Majengo haya yapo mbali sana ambapo nyumba moja inahitaji nguzo 40 wakati sisi kwenye kitongoji tuna nguzo 20, hawa hawatafikiwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni tutafute mpango wa kupata kile chombo cha UMETA, ili kwenda kuwawekea. Sasa hivi wananchi wengi vijijini wanatumia *solar,* kwa ajili ya kukodisha ama kukopa. Serikali ione fursa hii ya kupeleka hivi vyombo ama kile chombo cha UMETA kwa kila jengo ambalo linaonekana umbali uliopo hatuwezi kufikisha umeme kwa haraka, halafu tumkate kwenye matumizi wakati anatumia, mwananchi anaendelea kutumia umeme. Kwa nini ninazungumza hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu, nguzo 20 pengine zinaisha kwenye nyumba kama tano kwa mjini. Kwa sababu, nyumba moja itahitaji nguzo tatu ama nne hadi kufikiwa, lakini tukiwa na UMETA hiki chombo tulichotumia zamani, sasa hivi sijui kama tumebadilisha kwa jina lingine, lakini kina msaada mkubwa sana, kwa ajili ya kuwasaidia wananchi ambao wanalipa gharama kubwa katika kukodisha *solar* kutoka kampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni, haya maeneo yanayohitaji ujazilizi yaainishwe, yapewe kipaumbele kwa kuzingatia majengo mengi na kwa kuzingatia ukaribu wa majengo, ili kuona kama zile nguzo 40 katika ujazilizi zinafikisha pengine hata nyumba 80 ama pengine hata nyumba 100 kulingana na jiografia ya majengo yalivyokaa. Ninaiomba Serikali yangu kwa namna ya pekee kuchukua hatua za kuainisha maeneo yenye fursa ya uwekezaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo lenye uwezo wa kuzalisha umeme kule Mbulu ambalo linaitwa Maporomoko ya Mto Hhayno. Kampuni nyingi zimeenda, ninadhani ni kwamba, wakienda wakaona gharama ni kubwa wanaacha, lakini ninaona lile eneo ni fursa. Timu ya Wizara iende Mbulu Mjini ikatembelee Maporomoko ya Hhayno ione jinsi ambavyo ina fursa ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkondo wa Mto Hhayno maji yake yanatiririka mpaka katika Tarafa za Babati, lakini kwa kule juu kuna fursa ya kuzalisha umeme. Tuweze kuona maeneo kama haya na mengineyo, pamoja na umeme wa joto jua na wa upepo kwa maeneo haya, ili tuone fursa hizi Watanzania wanazishika na zinatoa mchango kwa Serikali na kuongeza uzalishaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote niliyoyazungumza, Serikali ifanye utaratibu wa kufanya mapitio ya shule zetu. Tathmini inaonesha nyumba nyingi za walimu hazina umeme nchini na uwezo wa *REA*, mwananchi kupata shilingi 330,000 au yule Mwalimu kutoa shilingi 330,000. Mchango huu wa shilingi

330,000 au aongeze na sabini, ili afanye *wiring,* kwa Mwalimu ni shilingi 700,000 hataweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta Mwalimu anakaa kwenye jengo ambalo halina umeme lakini *REA* imeshafika miaka mitatu. Maeneo hayo yawe na programu maalum na Waziri akija atoe maelekezo mahsusi ili nyumba zote za walimu, zahanati zote na makanisa pamoja na nyumba za watumishi wengine na yale majengo mengine ambayo kwa namna moja au nyingine yana fursa ya kutumia umeme kwa wingi na kwa mahitaji muhimu yaweze kuunganisha ili umeme wetu uwe na tija na Watanzania wanufaike kwa namna ya pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda ninaomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia. Mheshimiwa Haran Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Alan Thomas Mvano.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo imebeba maono ya mapinduzi ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Waziri wa Nishati, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya toka amepewa jukumu hilo kubwa la kusimamia Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo nikiwa ninatoa na ushahidi kabisa, mimi ni Mbunge labda inaweza kuwa ni wa kwanza toka huyu amepewa majukumu haya kufika kwa haraka sana pale ambapo Jimbo langu la Kigamboni lilipata tatizo la *low voltage,* alifika na kuhakikisha ametoa maelekezo. Ninawashukuru wale wataalam waliweza kuyapokea yale maelekezo na kuyafanyia kazi, mpaka sasa tuna umeme mzuri, wananchi wanafurahia na wanaendelea kuisifu Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme kwenye kitabu chetu cha dira imeainishwa kama ni kichocheo namba mbili cha kuleta mapinduzi ya uchumi wa Tanzania kuelekea 2050. Sekta hii ya nishati ndiyo ambayo imebeba jukumu kubwa la kuleta mapinduzi ya kiuchumi. Pia nimpongeze Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza hela nyingi katika sekta hii ili kuhakikisha maono yake ya mapinduzi ya kiuchumi Tanzania yanaenda kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuangalia kwa mifano, ujenzi wa *SGR* unategemea kiwango kikubwa sana cha *supply* ya umeme na Mheshimiwa Rais ameanza hatua kwa hatua, amesimamia ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo mpaka leo hii tunavyoongea linatoa megawati 2,145, kiasi kwamba inasaidia kwa kiasi kikubwa uendeshwaji wa treni yetu hii ya umeme ya *SGR*. Hii ni hatua kubwa sana katika Taifa la Tanzania, *East Africa* pamoja na Afrika kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama hapa kupongeza kwa sababu Jimboni kwangu kule Kigamboni umeme umesambaa kila mahali, lakini Mheshimiwa Waziri kuna vitongoji vichache pale Pemba Mnazi na Kimbiji ambavyo vinahitaji jicho la ziada la Waziri ili viweze kupata umeme na tatizo la umeme kule Kigamboni libaki kuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali yangu iweze kuongeza nguvu ya umeme kwa kujenga Kituo cha Kupooza Umeme kingine pale Kisarawe II, tuliongea Waziri nina imani hili analijua na hii bajeti tunayoichangia sasa hivi mradi huu nina imani kabisa utakuwemo. Kwa hiyo, niombe sana, kwa sababu Kigamboni kwa sasa hivi inakua kwa kiasi kikubwa cha ujengaji wa viwanda vikubwa na hatua hii ina mahitaji makubwa sana ya umeme. Kwa hiyo, nimwombe Waziri kile kituo asikiache katika miradi yake ambayo atakuwa ameshaipanga ili wafanyabiashara na wawekezaji waweze kufurahia Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza na kujenga imani katika uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme imeleta mchango mkubwa sana wa kibiashara katika pato letu la Taifa.

Ukiangalia katika ile randama ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba Tanzania pia katika *East Africa,* sisi pia tunauza umeme nje ya nchi, tunauza umeme Kenya, tunauza umeme Rwanda, tunauza umeme Zambia. Hizi zote ni fedha za kigeni ambazo zinaingia kwenye pato letu la Taifa. Ninaomba nimwambie Mheshimiwa Waziri achape kazi, sisi Waheshimiwa Wabunge tunaangalia na tutamsaidia na tutam-*support* kwa asilimia zote kuhakikisha malengo yote ya Wizara yanaenda kukamilika bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta hii ya nishati, imeimarisha ukuaji wa sekta ya madini namna gani? Ukianza kuangalia migodi mikubwa ya dhahabu, *nickel, graphite* sasa inatumia umeme, zamani walikuwa wanatumia majenereta, walikuwa wanatumia makaa ya mawe. Haya yote ni maendeleo ya sekta hii ya nishati na mipango madhubuti ya Wizara kuhakikisha wameleta mapinduzi ya uchimbaji kwa kutumia umeme, ambapo wanatumia muda mfupi na uwezekano wa upataji wa dhahabu unakuwa ni mkubwa, ambao unaleta mapato kwa Taifa kwa maana ya ile *royalty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa tu tahadhali au ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, Kigamboni ni Wilaya pekee Tanzania inayotunza nishati ya mafuta, matenki yote ya mafuta kasoro matenki sita ambayo yako Mtwara, yapo Kigamboni, lakini Kigamboni hatujaweka miundombinu rafiki ya *fire*. Ninamwomba sana ashirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ili tuweze kuwekeza kituo kikubwa cha *fire* kwa maana ya kuhakikisha yale matatizo ya moto yanapotokea kunakuwa na *rescue* ya karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake tumeshapata matatizo kama haya mara mbili, lakini *fire* mpaka itoke kule Geza mpaka ije ifike huku inakuwa imeshachelewa na unajua ile ni sehemu ya mafuta yanakuwa yameshapotea kwa kiasi kikubwa sana. Nimwombe sana Waziri jambo hili alizingatie na alifanyie kazi, kwa sababu hata Rais mwenyewe anaendelea kufanya uwekezaji. Juzi ametoka kuzindua matenki sita ya *storage* ya mafuta, lakini haya yote yanakwenda kuwa na tija pale ambapo

tunaweka na vitu ambavyo vinaweza kusaidia pale ajali zinapokuwa zinajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimechangia kwa maana ya kumpongeza Waziri na kwa niaba ya wananchi wangu wa Kigamboni wananisikia sasa hivi wanampongeza katika ma-*group* mbalimbali kwa namba ambavyo anafanya kazi. Ninamshukuru sana kwa sababu aliridhia lile ombi langu ambalo nilimwomba kwamba Kigamboni imekuwa kubwa na akaamua kuniletea Mameneja wa Wilaya wawili. Hivi sasa ninaomba nimpe taarifa, wamefika wako *site* wote wanafanya kazi na mmoja leo hii Meneja wa Mkoa amekuwepo hapa Dodoma kwa ajili ya maonesho ya nishati safi ya umeme. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ina dhamira ya kweli ya dhati kuweza kuleta mabadiliko katika Taifa letu la Tanzania. Pamoja na haya mambo yote, niwaombe Wabunge tufike hatua ya kuishauri Serikali yetu vizuri. Pia tutakuwa tunamsaidia Mheshimiwa Rais kama kila Mbunge wa hapa ndani akibeba yale yote ambayo yakifanyika katika Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuyapeleka kwa wananchi kisawasawa, wananchi wakapata uelewa, ninadhani dhana ya umoja katika Taifa hili itakuwa ni kubwa na itakuwa na tija na italeta mapinduzi na morali ya wananchi wa Tanzania kuweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, ninaomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Haran Sanga. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo ni Mheshimiwa Alan Thomas Mvano.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kutujalia afya sisi sote. Nitumie vilevile nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya na niwapongeze

sana Waziri wetu wa Nishati, Naibu Waziri wa Nishati na timu yote ambayo inamsaidia majukumu. Kwa kweli, kazi kubwa inafanyika na mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine yote ninayoweza kuyasema ni kwamba lazima nianze na pongezi kwa sababu mimi ninatokea Kakonko katika Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Kigoma hapa tunavyozungumza tayari umekwishaunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Ndiyo maana tunaona katika Mkoa wa Kigoma viwanda sasa vinajengwa. Ukienda Kigoma Mjini utaona Kiwanda cha *Cement,* utaona Kiwanda cha Nondo, utaona Kiwanda cha Kuchakata Asali, kuna Viwanda pale vya Kusindika na Kuchakata Samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye Wilaya ya Kasulu utaona Kiwanda cha Sukari. Tunaamini mpango mzuri wa Serikali hii kwamba Kiwanda cha Kuchakata Zao la Muhogo katika maeneo ya Kakonko na Kibondo tunaamini hili nalo litafanikiwa kwa sababu tayari tunao umeme wa uhakika. Hizi ni pongezi kubwa sana na lazima tuziseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Wilaya ya Kakonko ina vijiji 44 na vitongoji…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alan, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Festo Sanga.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu ni fupi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mbunge anachangia hapa pia Watanzania wakumbuke kwamba Mkoa huu ulikuwa unatumia *diesel* ya takribani shilingi bilioni 21 kwa mwaka, lakini kwa juhudi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuunganisha gridi ya Taifa, tumeokoa shilingi bilioni 21 kwa mwaka kwa matumizi ya *diesel. (Makofi)*

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaipokea taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge subiri, taarifa ya Mheshimiwa Sanga, unaipokea? *(Kicheko)*

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaipokea taarifa. Kimsingi Watanzania watambue kwamba Mkoa wa Kigoma unatambua sana jitihada kubwa zinazofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengi ningeweza kuyasema, lakini kwa sababu ya muda niseme hivi, Wilaya ya Kakonko pekee vijiji vyote 44 hivi tunavyozungumza vina umeme, kati ya vitongoji 355, vimebakia vitongoji takribani 50 tu, vingine vyote vina umeme. Kwa hiyo, lazima nitoe shukrani nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jitihada za Serikali, tarehe 17 ya mwezi Januari ulisainiwa mkataba wa shilingi trilioni 1.2 ambapo vitongoji 9,009 vilikuwa vinakwenda sasa kunufaika na umeme vijijini. Kwenye mpango ule Serikali hii njema imesema Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Katavi vitongoji vyote vinakwenda kupata umeme kupitia kwenye mkataba huo. Ninaomba kwa niaba ya wananchi wa mikoa hii nifikishe shukurani hizi nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizo, yapo mapendekezo. Jambo la kwanza ambalo ninapendekeza ni kwamba, tunatamani sana kuona kazi kubwa inaendelea na tayari mipango mizuri tumeiona, jambo la umuhimu ni kwamba umeme umeshakwishafika kwenye vitongoji vingi, hamu ya wananchi sasa ni kuona umeme unasambaa ndani ya vitongoji. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu na wananchi wanatamani sana kuliona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni vitendea kazi. Wakati Wizara inapeleka vitendea kazi katika maeneo yetu, ni muhimu sana kuangalia jiografia za maeneo yetu, maeneo ambayo yana milima mikubwa na mabonde, yapelekewe

vitendea kazi kwa uharaka na yaangaliwe kwa jicho la pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, tunashukuru sana katika Wilaya ya Kakonko tumepata gari dogo jipya upande wa *TANESCO,* lakini tunaomba pia kupitia nafasi hii tuweze kupata lori kwa sababu ya jiografia tuliyonayo ili wananchi wetu waweze kupata huduma nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu sana, ni kwamba tutakubaliana kwamba umeme sasa tunao, lakini matumizi ya umeme tuliyonao walio wengi wanatumia umeme kuwasha taa majumbani na kuchaji simu. Sasa kama Taifa tunahitaji kufanya mageuzi ya matumizi ya umeme wetu, tunahitaji kuufanya umeme utumike kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kupendekeza kwamba Wizara itengeneze timu izunguke katika nchi hii kupitia viongozi na waliopo katika mikoa waangalie watu wanahitaji umeme ambao wanahitaji kuutumia kwa ajili ya kuzalisha ili watu hawa wapewe kipaumbele. Ninatoa mfano, Wilayani Kakonko kuna mwekezaji anafuga ng'ombe kisasa, anafanya uwekezaji mkubwa kabisa pale, lakini ili afikishiwe umeme kwenye eneo lake anatakiwa alipie shilingi 65,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji Wizara iliangalie eneo hili kwa jicho la pekee kwa sababu hawa watu wenye viwanda, taasisi za Serikali, shule, viwanda tunahitaji wafikishiwe umeme, hawa ndiyo watumiaji wakubwa. Huyu mtu akifikishiwa umeme kwenye kiwanda chake hiki kwenye biashara yake kama hii ataweza kuajiri watu. Unaona kwenye biashara kama hii ndugu yetu huyu analazimika kukamua ng'ombe kupata maziwa mara moja kwa siku, badala ya kupata lita 12,000 za maziwa analazimika kupata lita 6,000 pekee kumbe angekuwa na umeme angeweza kukamua mara mbili kwa siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mchango wangu wa leo unajikita katika eneo hili, Wizara iangalie na itenge fedha, tuzunguke katika nchi hii ili kuona zile taasisi zote ambazo zinahitaji umeme, zifikishiwe umeme. Viwanda vyote vinavyohitaji umeme

wafikishiwe umeme ili hawa watumiaji wakubwa waweze kuwa na manufaa makubwa na vilevile manufaa hayo yaweze kushuka katika jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mchango huo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Alan Mvano ambaye umekuwa mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii ya leo.

Ninatumia nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia na kutoa maoni na mapendekezo, tukianza na Kamati yetu ya Kisekta ya Nishati na Madini, chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Subira na Wajumbe wa Kamati yako tunawapongeza kwa maoni mazuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wote mliopata nafasi ya kuchangia pia tunawapongeza. Kwa upande wa Serikali Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wanaendelea kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho Saa 3.00 Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 12.56 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 23 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*